

**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI NA MBILI**

**Kikao cha Arobaini na Saba – Tarehe 18 Agosti, 2008**

*(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

**MHE. WILSON M. MASILINGI - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE (K.n.y. MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA):**

Taarifa ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na maoni ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 407

### **Malipo ya Watendaji Katika Uandikishaji wa Wapiga Kura**

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura lilianzishwa nchini kote na Walimu pamoja na watendaji ndio waliohusika katika zoezi la uandikishaji na kwa kuwa kazi ilifanyika kwa mwezi mmoja lakini malipo yalitolewa nusu (laki nne tu) na kwa kuwa baadhi ya watendaji waliendelea tena na kazi ya kufanya masahihisho kwa mwezi mmoja lakini hawakulipwa:-

- (a) Je, fedha iliyobaki italipwa lini?
- (b) Je, fedha ya malipo ya mwezi mmoja italipwa lini?
- (c) Kama kazi iliyoongezwa ya mwezi mmoja ilikuwa ni ya kujitolea kwa nini Serikali isiwaambie wahusika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijajibu swali, naomba kutoa neno la shukrani kwa Wabunge wenzangu hasa baada ya kuondokewa na Mama yangu mpendwa, Mama Lucia Deaisile Mwanri, wakati nilipopata tatizo hili Ofisi yako pamoja na Wabunge wenzangu walismama imara na walihakikisha kwamba wanifaraji katika hali hii ngumu ambayo ilinipata.

Kwa niaba ya familia napenda kuchukua nafasi hii kusema ahsante kwako, kwa Spika mwenyewe, kwa Waziri Mkuu, viongozi wote pamoja na Waheshimiwa Wabunge wenzangu. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sijapata Fadhili Nkayamba, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba watumishi Walimu pamoja na watendaji walishiriki katika mchakato wa kuandaa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Katika zoezi hilo Wakurugenzi wa Halmashauri ndiyo waliokuwa wasimamizi katika Halmashauri zao na kila Mtendaji wa Kata alikuwa ndiye msimamizi mkuu katika Kata husika. Baadhi ya Waratibu Kata Elimu pia walishiriki kama wakufunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kwamba, zoezi hilo linafanyika kwa ufanisi kila mdau aliyeshiriki alitakiwa kutekeleza wajibu wake kwa makini. Ilipotokea kasoro mwandikishaji kwenye kituo husika pamoja na Afisa Mtendaji walitakiwa kufanya marekebisho kwa kuzingatia viwango vilivyokubaliwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi ili hatimaye walipwe staili zao.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka kwa Mkuu wa Wilaya ya Kigoma wahusika wote walilipwa haki zao na kama wapo baadhi ambao hawakulipwa naelekeza kwamba wawasilishie vielelezo vyao kwa Mkuu wa Wilaya ya Kigoma kwa ajili ya uhakika. Iwapo itabainika kwamba ni kweli hawakulipwa baadhi ya posho zao watalipwa mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu waandikishaji ambao waliendelea tena na kazi ya kufanya masahihisho ilipotokea kasoro ya uandikishaji kwenye kituo husika ilikuwa ni wajibu wa mwandikishaji kusahihisha, hivyo walioendelea na kazi kwa kufanya masahihisho walikuwa wanatimiza wajibu wao ili kuboresha palipokuwa na kasoro.

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa watumishi hao walifanya kazi yao kwa mujibu wa sheria lakini katika malipo Halmashauri ya Kigoma Vijiji walilipwa laki nne, Kigoma Mjini walilipwa laki nane.

Je, kwa kuwa wote walifanya kazi moja wao walilipwa nusu na wengine wakalipwa taslimu. Je, ilikuwakuwaje wao walipwe nusu na wengine walipwe taslimu na ni vigezo gani vilivyotumika?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili...

**NAIBU SPIKA:** Wengine walilipwa *cheque* wengine taslimu au? (*Kicheko*)

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Wengine walilipwa laki nne na wengine walilipwa laki nane. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kwa kuwa watumishi hao walipokuwa wanakwenda kumdati Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi wa Mkoa aliwaambia kuwa

wapeleke barua ya mkataba. Je, ina maana Tanzania nzima wale walioandikisha daftari la wapiga kura walikuwa na mkataba?

**NAIBU WAZIRI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyoeleza hapa, tumewasiliana na wenzetu kule Kigoma na wao *records* zao zinaonyesha kwamba wale wote ambao walitumika katika zoezi la kuandaa hili daftari walilipwa na kama nilivyojibu hapa kama kuna vielelezo vyovyyote vile ambavyo vinathibitisha na kuonyesha kwamba hawa watumishi walitumika lakini hawakulipwa kama ilivyostahili. Tumeagiza hapa kwamba walipwe mara moja na tunachohitaji ni huo ushahidi na wala hakuna haja ya ku-doubt hayo anayosema Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kwamba hawa ambao walikuwa wamedai hiyo nusu iliyobakia kwamba wametakiwa kutoa mkataba, nadhani ni katika ule mchakato tu wa kutaka kupata huo ushahidi na vitu vingine. Hapa kinachotakiwa ni kwamba kama waliingizwa katika orodha ya watu waliofanya zoezi hili na kama kweli walitumika kama inavyozungumzwa watalipwa. Ambao tunasema hawastahili kulipwa ni wale ambao walikuwa wameandikisha hili daftari lakini wakawa wamekosea, sasa kile kipindi cha kusahihisha ndicho tunachosema hawawezi kulipwa.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa tatizo la mapunjo kwa hawa walioandikisha hili daftari la wapiga kura linaelekea kuwa ni tatizo kubwa ambapo hata mapunjo mengine yanababisha hata Walimu kutaka kuandamana katika nchi hii. Walimu wanataka kuandamana kwa ajili ya mapunjo yao na kwa nini sasa Serikali isifanye utaratibu wa kuhakiki mapunjo ya Walimu hao pamoja na watumishi wengine haraka ili kuzuia hali hii?

**NAIBU SPIKA:** Mapunjo ya uchaguzi au mapunjo ya nini?

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mapunjo ya uchaguzi ni sawasawa tu na malipo ambayo Walimu wanalamikia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Luhahula, siyo sawa. Ahsante. Tunaendelea.

Na. 408

#### **Uuzaji wa Nyumba za Serikali**

**MHE. SAID A. ARFI (K.n.y. MHE. MHONGA S. RUHWANYA)** aliuliza:-

Kwa kuwa utaratibu wa uuzaji wa nyumba za Serikali nchini umeliingizia Taifa hasara kubwa na kusababisha matumizi yasiyo ya lazima kwa kuwalipia gharama za malazi watendaji wake wanapohamishiwa katika vituo vipyta kazi Mikoani:-

(a)Je, Serikali inafahamu kuwa Majaji watatu wa Kanda ya Tabora wameishi kwenye Hoteli ya *Orion* Tabora Hotel kwa kipindi kirefu kutokana na kukosa nyumba za Serikali?

(b)Kutokana na hadhi zao umuhimu na unyeti wa kazi zao Majaji hutakiwa kufanya kazi na kuishi mazingira yaliyo tulivu na *comfortable* hivyo kupelekea Serikali kuwalipia chumba chenye hadhi ya *suit* ambacho ni shilingi 120,000/= kwa siku. Je, Serikali imetumia kiasi gani kulipa hoteli kwa kipindi chote?

(c)Je, ni hasara kiasi gani imesababishwa na uuzaaji wa nyumba nchi nzima?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa Majaji watatu wa Mahakama Kuu Kanda ya Tabora katika nyakati tofauti kuanzia mwaka 2006 waliwahi kuishi Hoteli ya *Orion*. Hata hivyo, kwa sasa hakuna Jaji yeoyote ambaye bado anaishi hotelini Mkoani Tabora. Mheshimiwa Jaji aliyekuwa amebaki hotelini hapo aliondoka na kuhamia kwenye nyumba ya Serikali mwezi wa Agosti, 2007.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hadhi za Waheshimiwa Majaji kutakiwa kupata chumba cha *suit* jumla ya fedha iliyotumika kulipia malazi ya Waheshimiwa Majaji watatu katika Hoteli ya *Orion*, kuanzia mwaka 2006 hadi Julai, 2007 ni Sh. 22,063,950=/. Aidha, gharama ya chumba kimoja kilichokodishwa ilikuwa Sh. 42,000/= na siyo Sh. 120,000/= kama ilivyosemwa na Mheshimiwa Mbunge.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa, hatua ya Serikali kuuza baadhi ya nyumba zake imekuwa na faida na manufaa yafuatayo:-

(i) Watumishi wa umma waliouziwa nyumba hizo sasa wanaishi katika nyumba zao, nyumba ambazo ni bora kuliko nyumba walizokuwa wanapanga awali.

(ii) Uuzwaji wa nyumba za Serikali umeweza kuokoa kiasi kikubwa cha fedha zilizokuwa zinatumika kugharamia matengenezo ya nyumba hizo ambazo sasa zinalipwa na waliozinunua.

(iii) Kutokana na mapato yaliyotokana na kuuzwa nyumba hizo, Wizara yangu kupitia Wakala wa Majengo imeweza kujenga nyumba mpya 967 katika maeneo

mbalimbali nchini. Nyumba hizo zimeingizwa kwenye mpango wa kuwauzia na nyingine kuwapangisha watumishi wa umma.

**MHE. AMOUR S. ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa katika majibu ya swali la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri anasema kwamba, imepatikana faida kubwa sana katika kuuza nyumba za Serikali na kuokoa fedha nyingi lakini wakati huo huo Serikali imelazimika kuwaweka watumishi wake katika mahotelii.

Je, sasa hivi Serikali ina mpango gani wa kujenga nyumba za watumishi hasa Majaji, Madaktari katika maeneo ya Mikoa na Wilaya?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi hili la kuuza nyumba za Serikali kwa kweli lilikuwa limekusudia kupatikana kwa fedha ili kuweza kujenga nyumba zingine. Kama nilivyokuwa nimeeleza katika jibu langu la msingi jumla ya nyumba mia tisa sitini na saba sasa hivi zimejengwa nchini kote na mgawanyo wake naweza kumpatia Mheshimiwa Mbunge hapo baadaye kwa kila Mkoo lakini zoezi hili linaendelea na kama nilivyo sema kwamba kwa sasa hivi watumishi wengi wa Serikali hawawezi kuishi tena katika mahotelii kwa sababu nyumba hizi zinawahifadhi watumishi hawa ikiwa ni pamoja na nyumba ambazo sasa hivi zinahifadhi baadhi ya Waheshimiwa Wabunge hapo Dodoma.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, swalii moja la nyongeza. Katika majibu yake Mheshimiwa Waziri amesema kwamba nyumba mia tisa zimejengwa kutokana na fedha zilizopatikana kutokana na mauzo. Je, Mheshimiwa Waziri ana hakika na hiyo *statement* yake na kwamba kama ni kweli hivyo anaweza kutuambia nyumba mia tisa zilizojengwa ni kila moja iligharimu kiasi gani na malipo waliyolipa hawa waliouziwa nyumba ni kiasi gani ili kuthibitisha kauli yake? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema hizi nyumba 967 zimejengwa nchini kote, sasa mchanganuo wa gharama zake itakuwa si rahisi kuzieleza isipokuwa tu nieleze kwamba katika zoezi hili la uuzaji wa nyumba za Serikali ilikusudiwa kukusanya mapato ya Sh. 57,965,241,000/=, kati ya hizo zimeshakusanya Sh. 38,961,116,234/= ambayo ni sawa na asilimia 67.81. Sasa kutokana na fedha hizi ndiyo nyumba hizi zimeendelea kujengwa. Kama nilivyo sema kwamba pengine mchanganuo wake kwa haraka haraka hapa isingekuwa rahisi lakini kiasi cha fedha kilichokusanya ndicho nilichokisema hapa.

**NAIBU SPIKA:** Kwanza haiwezekani kwa sababu kama ni mkopo wanalipa polepole na haziwezi kuwa zimekusanya siku hiyo hiyo na kujengewa. (*Makofii*)

### **MHE. GODFREY W. ZAMBI aliuliza:-**

Kwa kuwa kumekuwa na ajali nyingi ambazo wakati mwingine husababisha vifo katika Miji ya Vwawa na Mlowo katika Wilaya ya Mbozi barabara kuu iendayo Zambia na kwa kuwa uongozi wa Wilaya ya Mbozi ulishaomba kupitia vikao vya Bodi ya Barabara Mkoa kwamba, maeneo hayo yawekewe matuta (*speed hump*) lakini majibu ya Serikali kupitia *TANROADS* yamekuwa ya kukatisha tamaa:-

(a) Je, Serikali itakuwa tayari kuruhusu ujenzi wa matuta katika maeneo hayo ili kudhibiti mwendo kasi wa magari na hivyo kuepusha ajali na vifo vya raia?

(b) Je, ni vigezo gani vinavyotumika kuruhusu uwekaji wa matuta (*speed humps*) katika baadhi ya maeneo na kuzuia ujenzi huo kwenye maeneo mengine?

### **NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu itafanya tathmini katika maeneo aliyoainisha Mheshimiwa Mbunge ili maeneo hayo yaweze kuwekewa matuta kwa lengo la kupunguza ajali kwa watembea kwa miguu katika maeneo hayo na lengo hapa ni kuokoa maisha ya wananchi.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu swalii namba 289 tarehe 25 Julai, 2008 la Mheshimiwa Mwaka Abdulrahman Ramadhani, vigezo vinavyotumika kuweka matuta barabarani ni kama ifuatavyo:-

1. Hali ya barabara katika eneo husika. Mfano, karibu na madaraja ambayo magari hayawezi kupishana kwa usalama yakiwa katika mwendo wa kawaida, karibu na kona kali, karibu na vizuizi na kadhalika.

2. Maeneo yenye matukio ya ajali za mara kwa mara.

3. Maeneo yenye watu wengi kama vile shule, nyumba za ibada, hospitali na kadhalika.

4. Maeneo yenye msongamano wa wanyama kama kwenye mbuga ama hifadhi za wanyama.

Aidha, napenda kurudia tena kwamba dhamira ya kuweka matuta katika barabara ni kulinda maisha ya watu kutokana na ajali zinazosababishwa na kutozingatiwa kwa sheria, kanuni na taratibu za matumizi sahihi ya barabara.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza. La kawanza, kwa sababu vigezo

alivyovitaja Mheshimiwa Naibu Waziri tayari vipo katika maeneo yangu kwa maana ya Mji wa Mloo na Vwawa na tayari suala hili tulishalipeleka *TANROADS* muda mrefu sana zaidi ya mwaka sasa. Sasa Mheshimiwa Waziri anaweza kutuambia ni kwa haraka namna gani tathmini hiyo itafanyika ili tuokoe maisha ya watu katika maeneo hayo niliyoyataja?

Mheshimiwa Naibu Spika, swal la pili, matuta ambayo yanawekwa katika barabara mbalimbali za lami yanatofautiana, mengine ni makubwa sana na mengine yamekuwa ndiyo chanzo cha ajali zenyewe. Ni kwa nini matuta mengine yanawekwa makubwa sana kuliko kawaida hasa ukiangalia sehemu za Morogoro na sehemu zingine kwa nini yasiwe na *standard* moja ili magari yaweze kupita kwa usalama zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza hapa kwamba maeneo ambayo tunayafanya tathmini tayari tumeshakamilisha kazi hiyo na tumeshayaainisha maeneo hayo kwa mfano, katika barabara hii ambayo Mheshimiwa Zambi anaizungumzia.

Kwa hiyo, wakati wowote matuta haya yanaweza kuanza kujenga na maagizo yameshatolewa kwa *Regional Manager* wa *TANROADS* Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili,nataka nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba matuta haya sasa hivi yanavyojengwa yanajengwa bila mpangilio wa kuonyesha kwamba yanafanana nchi nzima. Sasa hivi ilichofanya Serikali imeshatoa maelekezo kwa wakandarasi wote amba wanapewa kazi ya ujenzi wa barabara ili matuta haya yasiwe yanapishana viwango katika Mikoa na Mikoa au Wilaya na Wilaya. Kwa hiyo, zoezi hilo tutaendelea nalo lakini kuanzia sasa barabara zinazojengwa matuta yatakuwa yanajengwa katika kiwango kinachofanana ili kuepusha ajali zaidi.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kuuliza swal moja la nyongeza. Pamoja na dhamira nzuri ya Serikali ya kuruhusu kuwekwa matuta katika barabara nyingi hapa nchini lakini bado kuna tatizo kubwa sana la watumiaji wa matuta hayo kwamba hawana elimu yoyote ile kuhusu matumizi ya matuta hayo.

Je, Serikali ipo tayari kutoa elimu ya kutosha hasa kwa madereva lakini vilevile wananchi kufahamu kwamba kuna matuta na kwamba wafuate kanuni za matumizi ya matuta hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kwamba tunapoweka matuta barabarani suala la kuelimisha watumiaji wa barabara ni la muhimu na ndiyo maana katika ujumla wake Serikali ina kipindi kile cha usalama barabarani ambacho hutolewa katika vipindi vyta redio lakini pia kuna wiki ya usalama barabarani, vyote hivi vinalenga katika kuelimisha watumiaji wa barabara pamoja na waendeshaji wa magari. Kwa hiyo, nakubaliana naye kwamba zoezi la kuelimisha litakuwa ni la kudumu.

**NAIBU SPIKA:** Singida kuna ajali nyingi, Mheshimiwa Msindai swal la nyongeza. (*Kicheko*)

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Kwa sababu hizi ajali karibu nchi nzima huwa zinatokea na Mkoa wa Singida karibu kila wiki tunapata ajali hizi.

Je, Waziri yuko tayari kutoa agizo kwa Mameneja wote akiwemo wa Singida kutengeza matuta kuanzia Chikuyu, Ikungi, Iguguno, Mlima wa Sekenke na kuendelea?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimeeleza hapa kwamba maagizo yameshatolewa nchi nzima kwamba ujenzi wa barabara sasa hivi uwekwe na hayo matuta ya barabara ili kuweza kuokoa maisha ya watu.

Kwa hiyo, katika agizo hilo ni pamoja na katika maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge.

Na. 410

#### **Barabara ya Minjingu – Dodoma – Iringa**

**MHE. FELISTER A. BURA** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Minjingu – Dodoma – Iringa ni muhimu sana kwa maendeleo ya kiuchumi kwa wananchi wa Mikoa ya Arusha, Manyara, Dodoma na Iringa na kwa kuwa katika mwaka wa fedha wa 2007/2008, Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya upembuzi yakinifu kwa barabara hiyo:-

Je, upembuzi yakinifu huo umeshakamilika?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felister Aloyce Bura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Minjingu – Dodoma – Iringa ni kati ya barabara zilizopo kwenye mipango ya Serikali kujengwa kwa kiwango cha lami. Utekelezaji wa ujenzi wa barabara ya Minjingu – Dodoma – Iringa unaendelea katika ngazi tofauti kwa sehemu tatu za barabara hiyo kama ifuatavyo:-

(i) Sehemu ya Minjingu – Babati. Sehemu hii imefanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na Kampuni ya Ushauri wa Kihandisi ya *Carlbro* ya Denmark ndani ya mradi wa Singida – Babati – Minjingu. Mhandisi Mshauri ameshakamilika usanifu wa kina wa barabara hiyo na kuwasilisha ripoti na nyaraka za zabuni.

Zabuni kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Singida – Babati – Minjigu zilifunguliwa tarehe 6 Juni, 2008 na mchakato wa kuwapata Wakandarasi kwa ajili ya kazi za ujenzi unaendelea.

(ii) Sehemu ya Babati – Dodoma. Sehemu hii imefanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na Kampuni ya Ushauri wa Kihandisi ya *Carlbro A/S* ya Denmark ikishirikiana na *M-Konsult Limited* ya Tanzania. Mhandisi Mshauri ameshakamilisha kazi ya usanifu wa kina na nyaraka za zabuni.

Serikali imetenga fedha kiasi cha Sh. 12.01bn/= kwa ajili ya kuanza ujenzi wa sehemu katika mwaka huu wa fedha wa 2008/2009.

(iii) Sehemu ya Dodoma – Iringa. Sehemu hii inafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na kampuni ya Ushauri ya Kihandisi ya *COWI AS* ya Denmark ikishirikiana na *COWI Consult* ya Tanzania.

Mhandisi Mshauri ameshawasilisha rasimu ya upembuzi yakinifu. Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina inatarajiwa kukamilika mwezi Februari, 2009.

Sambamba na kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi kutoka kwa wahisani mbalimbali. Kwa sasa Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) imeonyesha nia ya kufadhili ujenzi wa barabara hii.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa Bajeti ya Wizara hii ilipita pasipo kupunguzwa hata senti tano na kwa kuwa Serikali imetenga fedha za ujenzi wa sehemu ya Babati - Dodoma, naomba kuuliza kwamba Serikali inafikiraje kuweka wakandarasi wawili mmoja aanzie Babati na mwagine aanzie Dodoma kutokana na umuhimu wa barabara hii ili barabara hii ikamilike haraka iwezekanavyo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri alioutoa Mheshimiwa Mbunge ni mzuri na kusema kweli umeweza kuharakisha sana ujenzi wa barabara hiyo isipokuwa nataka nimwambie sasa hivi kwamba hatua ambazo zinafuata sasa hivi ni kwamba, zabuni zinaandaliwa kwa ajili ya kuanza kazi hii na ujenzi ambao nafikiria utaanza ni ujenzi wa madaraja katika barabara hiyo na kazi nyingine zitaendelea hatua kwa hatua lakini ushauri wake utazingatia kadri fedha zitakavyokuwa zinaendelea kupatikana.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa barabara hii ya kutoka Arusha mpaka Iringa ni kati ya barabara kadhaa zilizopewa kipaumbele sana kujengwa katika kipindi cha miaka mitano.

Kwa nini barabara hii kati ya barabara zote hususan kipande cha kutoka Dodoma mpaka Iringa ndicho kinachopewa *very low priority* katika ujenzi wa barabara hizo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kipande cha Dodoma – Iringa kusema kweli hakijapewa *low priority*.

Katika mipango yetu kwa mfano kipindi cha mwaka wa fedha uliomalizika hivi karibuni, kipande hiki kilitengewa kiasi cha Sh. 900m/= kwa ajili ya upembusi yakinifu na mwaka huu zimetengwa Sh. 574m/= ili kukamilisha tu kazi hiyo na kama nilivyosema kwamba baada ya kazi hii kukamilika, utaratibu wa kuwapata wahisani ili barabara hii iweze kuanza nao utakuwa umeshakamilika. Kwa hiyo, si kweli kwamba barabara hii inapewa umuhimu mdogo, inapewa umuhimu mkubwa sambamba na barabara nyingine ambayo inaunganisha Babati na Dodoma.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika majibu yake mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba barabara hii ya kutoka Babati kuja Dodoma inaandaliwa kuanza ujenzi. Sasa nataka nifahamu ni lini hasa ujenzi huo utaanza?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika maandalizi niliyoyaeleza hapa kwamba fedha zimekwishatengwa, na sasa hivi maandalizi ya kutafuta wazabuni ndiyo yanaendelea. Kwa hiyo, kwa kifupi ninaweza kusema kwamba kwa sababu kazi yoyote inaanza kwa maandalizi, naweza kusema kwamba kazi hii sasa imekwishaanza maadam fedha zimekwishatengwa, na kazi za awali zimekwishaanza barabara hii imekwishaanza kutengenezwa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaenda Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, swali namba 411, mkiangalia *Order Paper* pamoja na utangulizi lakini hilo swali lina sehemu (a), (b) na (c), lakini nadhani lilipelekwa vibaya kwenye Wizara inayohusika ya Habari, Utamaduni na Michezo, sehemu (c) haipo. Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri atajibu sehemu (a) na (b), na sehemu (c) itakuwa hajibidiwa kwa sababu hawakupelekewa, nadhani lilitokea tatizo la mawasiliano.

Na. 411

### **Mauaji yanayohusishwa na Imani za Uchawi**

**MHE. JAMES P. MUSALIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa, kwa muda mrefu kumekuwa na matukio ya mauaji ya watu yanayohusishwa na imani za kichawi hapa nchini; na kwa kuwa, Serikali haiamin dhana ya uchawi:-

- (a) Je, Serikali ina tafsiri gani ya maneno kama vile ushirikina, nguvu za giza, wanga, misukule na kadhalika?
- (b) Je, ipo nchi yoyote duniani inayoamini kwenye dhana hii ya uchawi, na kama ipo/zipo ni ipi/zipi nchi hizo?
- (c) Je, ni matukio mangapi ya mauaji yanayotokana na imani za uchawi yametokea kwenye Mikoa ya Shinyanga, Mwanza, Kilimanjaro na Arusha (kwa takwimu) kati ya kipindi cha Januari, 2000 na Desemba, 2007?

**NAIBU SPIKA:** Nimesema sehemu (c) haitajibiwa kwa sababu majibu yake hayakuandaliwa.

### **NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa James Philip Musalika, Mbunge wa Nyang'hwale, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Naibu Spika, tafsiri ya maneno aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge nitaitoa kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Toleo la mwaka 2004 lililochapishwa tena mwaka 2005 na 2006 kama ifuatavyo:
  - (i) Ushirikiana ni tabia ya kuamini mambo ya uchawi , mizimu na kadhalika.
  - (ii) Nguvu za giza ni uwezo wa kufanya jambo au msukumo mkali unaotokana na ushirikiana.

(iii) Wanga ni hali inayosadikiwa kuwa inaweza kuwadhuru watu kwa kuwaroga, ulozi na ukuhani.

(iv) Misukule (msukule) haimo kwenye kamusi niliyoitaja hapo awali lakini utafiti umeonyesha kuwa ni imani inayosadikika jamii kuchukuliwa kwa mtu (hasa mtoto) na kwenda kutumikishwa au kufanyiwa kazi mahali kusikojulikana. Inaaminika kuwa baadhi wanafanyishwa kazi usiku na wanapoamka wanajisikia wachovu sana na wengine wanatoweka kabisa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, itakuwa vigumu kujua iwapo kuna nchi yeyote duniani inayoamini dhana ya uchawi kwa sababu kama nilivyosema hapo awali kuwa, mambo ya uchawi yanatokana na itikadi zinazosadikisha jamii kuamini matokeo ya matukio fulani.

Mwisho, Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe wito kwa wananchi wote kwamba kwa kweli tuachane na imani za uchawi katika nchi yetu.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili mdogo ya nyongeza.

(a)Kwa kuwa imani hii ya uchawi ipo siku nyingi na hapo nyuma watu wenye vipara walikuwa wanatafutwa na baadaye kuchuna ngozi za watu, na sasa hivi ni mawazo ya maalbino; na kwa kuwa hii tabia au dhana hii huenda ikabadilika watahitaji sasa pengine kiungo cha mwili wa Singa singa au pengine Spika, Serikali haioni sasa kuna haja ya kuunda kikosi maalum cha kupambana na kuzuia mauaji yatokanayo na imani za uchawi yakiwemo mauaji ya albino, vikongwe pamoja na waganga wanaotoa kinga au hirizi kwa majambazi? (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Kupata kichwa cha Spika atapata kazi kweli! (*Kicheko*)

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** (b) Kwa kuwa sehemu ya (c) ya swali langu haijajibiwa, Naibu Waziri anaweza kuniambia ni lini ataijibu sehemu hiyo (c) ili nipate kuuliza swali la pili la nyongeza?

**NAIBU SPIKA:** Jibu la sehemu ya (c) litajibiwa kwa maandishi kwa sababu hata lenyewe kwa *nature* lilitaka *data* kutoka 2000 mpaka 2007 za wachawi wote waliopatikana katika Mkoa wa Shinyanga. Kwa hiyo, litajibiwa kwa maandishi kwa vyo vyote vile. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kama alivyosema ni kweli kwamba limezuka tatizo la imani potofu kwa wananchi wetu. Lakini naomba niipongeze Serikali, niipongeze Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, viongozi wetu Wakuu, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Rais kwa hotuba zao ambazo wanazitoa lengo ni kutoa elimu kwa

Watanzania wote kwamba imani hizo za uchawi za kufikiria kwamba ukipata kiungo cha Spika kwa sababu ana upara au ukipata mtu ambaye ana nywele ndefu ama albino kwa kweli ni suala ambalo sisi Watanzania wote tulipige vita kwa nguvu zetu zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana nilisoma gazeti linaelezea masikitikio makubwa sana. Kuna walimu fulani katika Mkoa wa Shinyanga wameajiriwa waende kule, lakini wamejikuta wote wanalala nje baada ya siku tatu. Sasa vitu kama hivi vinatia woga na havipendezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kusema kwamba waachane na tabia hiyo haileti maana nzuri kwa Taifa letu na ni aibu, nawaomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru swal lake la pili umelijibu, tutalitafutia takwimu nzuri na tutamjibu Mheshimiwa Mbunge atakapolileta tena upya ili Wizara ilifanyie kazi vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mbunge hatalileta tena upya, mnatakiwa mumjibu kwa maandishi na majibu yake myasambaze. Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, swal la nyongeza.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kumwuliza kama ifuatavyo:-

Je, anayo habari kuwa katika nchi yetu ipo Sheria ya Uchawi, na kama hivyo ndivyo haoni kuwa wakati sasa umefika kwa sababu tupo katika karne ya Sayansi na Teknolojia kwanza kuifuta hiyo Sheria yenyewe, lakini la pili, mtu ye yeyote atakayejaribu kutenda hivyo vitendo na akikamatwa dhahiri achukuliwa hatua kali?

**NAIBU SPIKA:** Sasa akifuta sheria, hatua kali zinatoka wapi sasa? (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kufuta sheria peke yake haitoshi, lakini kikubwa hapa ni elimu, na kama ambavyo sasa hivi Serikali imepania kulishughulikia hili. Naomba nilitoe wasiwasi Bunge kwamba tutaendelea kuweka mkakati kuhakikisha kwamba vitendo hivi tunavikomesha katika nchi yetu.

Na. 412

### **Uchimbaji wa Madini Nchini**

**MHE. DORA H. MUSHI** aliuliza:-

Kwa kuwa, nchi ya Tanzania imezagaa madini ya kila aina kama vile dhahabu, Almasi, *Tanzanite, Green Ginet Surphire, Spinal Ruby*, Chama na kadhalika:-

Je, tunapowaleta wawekezaji ni kwamba wanakuja kufanya utafiti, au utafiti unakuwa umeshafanywa na kwamba kazi yao ni kutengeneza mipango mizuri ya kuwekeza?

### **NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Dora Heriel Mushi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti wa madini katika nchi yetu umefanywa tangu enzi za ukoloni wa Wajerumani na Waingereza. Wakati wa karne ya 19 na mwanzoni mwa karne ya 20 sehemu nyingi zenyе madini hapa nchini ziligunduliwa na taarifa na ramani za kujiolojia ziliandaliwa. Kuanzishwa kwa *Geological Survey of Tanganyika* kama Idara ya Serikali mwaka 1925 Mjini Dodoma kuliongeza kasi ya ugunduzi wa madini kwa njia ya kitaalam hapa nchini. Hivyo kufikia miaka ya 1950 nchi yetu ilikuwa inauza madini mbalimbali kama vile dhahabu, almasi na ulanga katika soko la dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti wa madini kwa nchi nzima au baadhi ya maeneo ya nchi yetu umekuwa ukifanywa na Serikali na pia kwa ushirikiano na taasisi za ndani na nje ya nchi na pia kampuni binafsi za ndani na nje ya nchi. Matokeo ya utafiti wa madini hutoa takwimu, taarifa na ramani za kitaalamu ambazo hutumiwa na wawekezaji katika kuchagua maeneo ambayo watayaombea leseni ili kuyafanyia utafutaji madini, na iwapo yataonekana kuwa na mashapo ya kutosha kuchimbwa kwa faida na kuanzishwa migodi.

Mhesimiwa Spika, Wakala wa Jiolojia Tanzania (*GST*) imeendelea kufanya utafiti wa awali wa kijiolojia, kijiokemia na kujifizikia katika maeneo mbalimbali nchini ikishirikiana na taasisi mbalimbali kutoka nchi za nje. Matokeo ya utafiti huo ni ramani na taarifa zinazoonyesha miamba, udongo na madini yaliyoko kwenye maeneo husika na pia takwimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wawekezaji wanapokuja kuwekeza katika Sekta ya Madini hukuta utafiti wa awali umeshafanywa na Serikali hivyo huanza kwa kutumia taarifa, ramani na takwimu zilizopo kama miongozo katika kuchagua maeneo ya kufanyia utafutaji wa madini na kupanga kazi watakazofanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti wa madini katika maeneo tofauti ya nchi upo katika hatua tofauti. Wakati maeneo mengine yamefanyiwa utafiti wa awali kuna maeneo mengine ambayo yameshafanyiwa utafiti wa kina ikiwemo uchorongaji wa miamba na hata kufahamika kwa kiasi na wingi wa madini yaliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, tunapowapokea wawekezaji hapa nchini wanakuja kufanya utafiti hata kama maeneo hayo yalishafanyiwa utafiti wa awali au wa kina miaka ya nyuma. Utafiti utakaofanyika kwa upande wao ndio utakaonyesha kama eneo lao lina madini ambayo yanaweza kuchimbwa kwa faida na kwa

kutegemeana na vigezo vyao. Matokeo ya utafiti huo ndio utawafanya waamue kuanzisha migodi au la.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize kama ifuatavyo:-

La kwanza, kwa kuwa, wawekezaji hao wanapokuja hapa nchini wanakuta maeneo yale yalikwishafanyiwa utafiti na wao wanaingia kuchimba tu, na hata hivyo huwa wanapata madini mengi sana. Pamoja na kwamba Serikali inawasamehe kodi, na wanapoingiza vifaa nya uchimbaji wanasekehewa ushuru pamoja na kodi. Je, yale madini wanayochimba na wanayopata kwa wingi sana kwa kipindi kile cha miaka mitano inakuwa ni kwa faida ya nani? Je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa hivyo vivutio ambavyo wamepewa kwa sababu Serikali yetu ndiyo inayopata hasara kwa muda wote ule wa miaka mitano wanapokuwa wanachimba na wanapata madini, na wanayasafirisha nje na sisi tunabakia na mashimo hatubaki na faida yoyote? Naomba Serikali iondoe vivutio hivyo mara moja? (*Makofii/Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Hilo swali la pili liwe fupi.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** La pili, kwa kuwa wachimbaji wadogo wadogo wamekuwa wakichimba madini hayo kwa hali ngumu sana kutokana na zana za uchimbaji kuwa ghali. Naomba basi Serikali iwape nao vivutio nya kusamehewa kodi ya kuingiza zana za uchimbaji katika nchi yetu? Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema wawekezaji wanapokuja wanakuta utafiti umefanyika, lakini utafiti huo kusema kweli unakuwa ni utafiti wa awali sana, hakuna mwekezaji mkubwa anayekuwa anakuja kuwekeza anaamua kufanya maamuzi ya kuwekeza kwa kutegemea utafiti ule ambao sisi tumeufanya. Kusema kweli kwa misingi ya viwango nya utafiti, utafiti ule bado unakuwa ni tafiti wa awali sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, isipokuwa utafiti huu kama nilivyosema ni miongozi tu ya kumwelekeza mwekezaji kwamba maeneo haya yana madini ya namna gani na kadhaa. Lakini bado yeye inabidi afanye utafiti wa kina na wa gharama kubwa sana ambao unamwezesha kubaini kama viwango nya madini na *quality* na kadhalika vinamwezesha kufanya uwekezaji ule anaoutaka yeye. Kwa sababu hata huo uwekezaji bado una viwango, kuna uwekezaji wa chini, na wa kati, na uwekezaji mkubwa kama ule ambao unaingiwa mikataba na Serikali na wawekezaji wakubwa kama ule wa Bulyankulu, Buzwagi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani hili suala la kusamehewa kodi na ushuru wanawenza kulieleza vizuri zaidi wenzetu wa Wizara ya Fedha na Uchumi.

Lakini nadhani nia yetu na nadhani kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge mwenyewe ni kuweka vivutio vya kuwaleta wawekezaji hao. Tumekuwa na misingi hii kwa miaka kumi tangu Sheria ya mwaka 1998 ilipokuja, na sasa naamini kwamba Sheria mpya ikija itazingatia ushauri wa Kamati mbalimbali ambao tumekuwa tukiupokea katika kufanya marekebisho ya sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swal la pili la nyongeza, tulipokuwa tunawasilisha Makadirio ya Wizara yetu tulisema kwamba tunafanya mikakati ya makusudi kwanza ya kuboresha Sheria ya Madini ambayo itazingatia nafasi ya wachimbaji wadogo katika Sekta ya Madini ambayo pia itafikiria pia kuongeza vivutio na namna ya kuwawezesha kupitia mfumo ulio rasmi. (*Makofit*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anne Malecela, swal lingine la nyongeza kwa kifupi.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi hii ya kuuliza swal moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa madini ni chanzo Kikuu cha mapato ya nchi yetu kama tukiwa makini sana, lakini kwa kuwa, katika kipindi hiki cha utandawazi, wawekezaji ni Mataifa yale makubwa sana ambayo yana teknolojia ya kisasa, na ni rahisi sana tusipowaangalia wawekezaji vizuri wao wakafaidi kwenye rasilimali yetu hii ya madini kuliko sisi. Je, Serikali ina mkakati hasa na imejizatiti vipi kuhakikisha kwamba Watanzania wanafaidi kutokana na madini haya kuliko ambavyo Mataifa makubwa yanafaidi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri sasa hivi nataka majibu kwa kifupi kabisa.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyosema katika miaka 10 ambayo tume-*liberalize* Sekta ya Madini na tumekuwa tukipokea wawekezaji, na tumekuwa tunatumia kipindi hiki kuliangalia sheria na *experience* tuliyokuwa tunapata. Kwa hiyo, ni matarajio yangu kusema kweli kwamba katika kipindi hiki kama tulivyoeleza katika Bunge lako Tukufu ambapo tunataka kutumia kipindi hiki kupitia upya *experience* ya miaka 10, na haya yote yaliyopita tukija na sheria mpya kama tulivyoahidi Bunge lako Tukufu mwakani itakuwa imezingatia nafasi ya madini katika uchumi wa Tanzania, na namna ya kuboresha nafasi ya madini katika kuongeza mapato ya uchumi wa Tanzania na manufaa zaidi kwa wananchi kwa ujumla. (*Makofit*)

Na. 413

#### **Watumishi wa Mashirika ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa, mwaka 1981 Serikali ilianzisha Mashirika ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo yaitwayo *TARO* na *TALIRO*, ambapo watumishi wa Serikali waliokuwa kwenye Taasisi ya utafiti wa mifugo walihamishiwa kwenye Shirika la Utafiti wa Mifugo (*TALIRO*) ambalo lilidumu kwa miaka minane (8) kabla ya kuvunjwa na watumishi wake kurejeshwa Serikalini:-

(a) Je, Serikali inafahamu kuwa, Muswada wa kuvunjwa kwa Shirika hilo unatambua kuwa, watumishi wote walihidiwa kuwa haki zao zote za kiutumishi zitahifadhiwa ikiwa ni pamoja na mafao yao baada ya kustaaful?

(b) Je, Serikali inafahamu kuwa, watumishi waliokuwa kwenye Shirika la Utafiti wa Mifugo wanapostaafu wanakosa malipo ya miaka minane ya utumishi wao?

(c) Je, Serikali ina sababu gani za msingi za kutolipa malipo ya miaka minane kwa watumishi hao baada ya kustaaful?

#### **NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Utafiti wa Mifugo (*TALIRO*) lilivunjwa kwa Sheria ya “*Tanzania Livestock Research Organization*” (*Dissolution*) Na. 6 ya mwaka 1989 na katika kifungu cha 4 imetamkwa bayana kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itachukua majukumu yote ya Shirika hilo, yakiwemo madeni na mafao ya watumishi.

Hivyo, Serikali inafahamu na inatambua kuwa watumishi wote waliokuwa *TALIRO* walihidiwa kulindwa na kuhifadhiwa kwa haki zao zote za kiutumishi, ikiwa ni pamoja na mafao yao baada ya kustaaful ikijumuisha miaka minane waliotumikia Taifa hili chini ya *TALIRO*.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, *TALIRO*, likiwa Shirika la Umma lilijiunga na Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma (*PPF*) kama mwanachama Januari mwaka 1982 na kuendelea kuwachangia wafanyakazi wake 852 mpaka Shirika lilipovunjwa mwezi Mei, 1989. Aidha, kipindi cha utumishi wa wanachama hao kilihesabiwa tangu walipoajiriwa Serikalini.

Jumla ya wafanyakazi 709 wamekwishalipwa stahili zao na mafao yaliyolipwa yapo katika makundi yafuatayo:-

- Mafao ya kujitoa (*surrender value benefit*) yaliyolipwa kwa wafanyakazi 134 ambao ajira zao zilikoma kwa kuachishwa, kuacha au kufukuzwa kazi na walilipwa kwa mkupuo mmoja.

- Michango iliyorejereshwa (*refund of contributions*) kwa wafanyakazi 21 ambao hawakutimiza vigezo vya kuwa wanachama wa Mfuko kwa kuwa na umri mkubwa.
  - Mafao ya kifo (*Death Benefit*) yaliyolipwa kwa wategemezi wa wafanyakazi 5 waliofariki wakiwa kazini.
  - Mafao ya kiinua mgongo (*gratuity*) yaliyolipwa kwa wanachama 492 ambao utumishi wao Serikalini na *TALIRO* ulikuwa chini ya miaka 10.
  - Mafao ya uzeeni (*Old Age Benefit*) yaliyolipwa kwa wanachama 47 ambao utumishi wao Serikalini na wakiwa *TALIRO* miaka 10 wanaendelea kupata malipo yao ya pensheni ya kila mwezi hadi sasa.
- (c) Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya watumishi 143 waliohamishiwa Serikalini kutoka *TALIRO* bado hawajastaaifu na wanaendelea kuwa wanachama wa mfuko wa pensheni na kila mmoja atalipwa mafao yake atakapostaaifu kama nilivyoeleza hapo juu, ikiwa ni pamoja na miaka minane walijotumikia *TALIRO*.

Hivyo, ni nia ya Serikali kuhakikisha kuwa kila mtumishi, hususan mstaafu analipwa mafao yake kwa wakati muafaka na wala haina nia ya kumnyima ama kumsababishia usumbufu mstaafu yeoyote.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hivi karibuni Mheshimiwa Naibu Waziri alipotembelea taasisi ya utafiti wa mifugo Mpwapwa na kituo cha uchunguzi wa malazi ya mifugo *VIC* Mpwapwa watumishi walimlalamikia kwamba baadhi yao walikuwa hawajalipwa mafao yao, kwa kipindi cha miaka minane (8).

(a) Je, sasa Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba iko haja sasa ya kuandika waraka kwa watumishi wote ambao wamestaafu kwamba Serikali itawalipa?

(b) Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kunipa orodha ya watumishi wote ambao wamelipwa na ambao hawajalipwa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumshukuru Mheshimiwa George Lubeleje kwa namna anavyofuutilia mambo yanayohusu taasisi zake zilizoko Mpwapwa na sehemu nyingine kwa sababu mara ya kwanza alikuja wakati tunaandaa Bajeti kwenye kamati yetu akatetea na mambo yakaenda vizuri.

Pili, alishatualika kwenda huko. Sasa kuhusu kuandika waraka ili tuandike haraka hatuna matatizo kwa sababu sisi tumelifuutilia hili jambo mpaka huko Serikalini na tuna majina ya watu wote waliolipwa na wamelipwa kiasi gani. Sasa kama kuna mstaafu yoyote ambaye hajalipwa sisi tutaandika waraka ili aweze kufuutilia na sisi tupo tayari kumsaidia.

Kuhusu majina ili aweze kwenda nayo akakae nayo na kuhakiki kwamba anapomwuliza anapata majina ninayo hapa na nitamkabidhi kila mtu ameodorodheshwa haki yake aliyopata. (*Makofi*)

Na. 414

### **Washauri wa Kilimo**

**MHE. ANNA R. LUPEMBE (K.n.y. MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, kazi kubwa ya Washauri wa Kilimo ni kuwafikishia wakulima vijijini maarifa juu ya kanuni za kilimo bora cha mazao wanayolima na elimu juu ya hifadhi ya udongo:-

- (a) Je, washauri hao wa kilimo wanawezeshwaje kuwafikia wakulima?
- (b) Je, ni kwa nini Washauri wa Kilimo kumi (10) wa Manispaa ya Mtwara wanapewa lita 2.5 tu za mafuta kwa wiki kwa ujumla wao?
- (c) Je, utendaji wa kazi kwa wataalam hao utapimwa vipi endapo Washauri wa Kilimo watashindwa kuwafikia wakulima wengi?

### **NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kupitia programu ya kuendeleza sekta ya kilimo (*ASDP*) Serikali inatoa ruzuku kwa ajili ya kuzijengea uwezo Halmashauri na Manispaa ili ziwashudumie wakulima na wafugaji waliopo katika maeneo yao kwa ufanisi zaidi.

Uvezeshaji huo hutolewa kupitia ruzuku ya kilimo ya ugani (*A-EBG*) na ruzuku ya kujenga uwezo katika kilimo. Kwa mantiki hiyo katika mwaka 2007/2008 Serikali ilipeleka katika Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara jumla ya shilingi 160,161,385/=.

Kati ya hizo shilingi 50,672,258/= zilikuwa kwa ajili ya ruzuku ya kilimo ya ugani na shilingi 38,653,000/= kwa ajili ya ruzuku ya kujenga uwezo katika kilimo. Kwa kutumia fedha hizo, mwaka 2007/2008, Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara ilinunua gari moja na baiskeli 11 kama sehemu ya kuwajengea uwezo watalaam wa ugani kuwafikia wakulima kwa ufanisi zaidi.

(b) Kama nilivyoeleza katika sehemu (a) mwaka 2007/2008, Serikali imepeleka fedha kwa ajili ya kugharamia programu ya kuendeleza sekta ya kilimo jumla ya shilingi 160,169,385/= katika Halmashauri ya Mtwara. Halmashauri huruhuswa kutumia asilimia sita ya fedha za *ASDP* kwa ajili ya usimamizi na utaratibu ikiwa ni pamoja na kununua mafuta. Wizara itaendelea kuzishauri Halmashauri kutenga fedha za kutosha za mafuta

kwa ajili ya kuwawezesha watalaan wa ugani kuwahudumia wakulima na wafugaji kwa ufanisi zaidi.

(c) Utendaji wa kazi wa watalaan wa ugani hufanywa kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo ya usimamizi wa utumishi wa umma kama ilivyoainishwa katika sheria ya Utumishi wa umma Na. ya mwaka 2002. Mtalaam wa Ugani wa kijiji husimamiwa na mtalaam wa ugani wa Kata ambaye naye anawajibika kwa mtaalam wa ugani wa Wilaya. Upimaji wa makazi wa watalaan hao unapofanya utazingatia pia malengo yaliyowekwa na kiwango cha uwezeshaji kilichotolewa.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mkoa wa Mtwara pamoja na Mkoa wa Rukwa ndiyo mikoa ambayo inayolima sana na wakulima wengi wako maeneo hayo. Na kwa kuwa hawa washauri wa kilimo ni wachache sana katika nchi yetu ya Tanzania. Na kwa kuwa sasa hivi nchi yetu tunaweka mikakati ya kilimo kwa hali na mali na kwa kuwa sasa hivi wananchi wengi wakiwa vijiji hawana watalaan wale watalaan wako kwenye Kata chache. Je, Serikali ina mikakati gani ya kuwapa hawa washauri wa kilimo usafiri ili waweze kuwafikia wananchi vijiji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri swali lilikuwa usafiri tu. Naibu Waziri jibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla ni kwamba kilichoua huduma za ugani pamoja na wale watumishi wa ugani/maofisa wa ugani (*extension officers*) kutopata vitendea kazi. Sasa katika programu hii tumepanga kwamba watajengewa nyumba, watanunuliwa magari kama nilivyotoa mfano wa kule Manispaa ya Mtwara wameshapata gari, wale *extension officers* wa kwenye Kata na Tarafa watanunuliwa pipipiki kwa kutumia fedha ASDP na wale wenye ngazi ya vijiji watapewa baiskeli.

Na. 415

#### **Hali ya Kilimo - Sumbawanga**

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wilaya ya Sumbawanga ni moja kati ya Wilaya zinazotoa chakula kingi nchini hasa Jimbo la Kalambo; na kwa kuwa, Jimbo hilo limekuwa halipati huduma za Serikali kama mbolea ya ruzuku, dawa za kuuwa wadudu zinazotakiwa na Maafisa Ugani kama inavyotakiwa:-

(a) Kwa kuwa, Maafisa Ugani hawatoshi katika vijiji vya Jimbo la Kalambo. Je, ni lini watapangwa kwenye kila kijiji?

(b) Je, ni lini Serikali itaweka vituo vya usambazaji wa mbolea, dawa za mimea na nafaka katika miji midogo ya Matai, Mwazye na Mwimbi?

## **NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ludovick John Mwananzila, Mbunge wa Kalambo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inatambua tatizo la upungufu wa Maafisa Ugani katika Wilaya nyingi nchini. Ili kuondokana na tatizo hilo Serikali imeandaa mpango wa kuimarisha huduma za ugani wa 2007/2008 hadi 2010/2011 kwa lengo la kuhakikisha kwamba kunakuwepo na Maafisa Ugani wa kila kijiji, Kata na Tarafa. Lengo ni kuajiri watalaam wa Ugani wapya 11,703 ifikapo mwaka 2011 na hivyo kufanya idadi ya watalaam kufikia 15,000.

Katika mwaka 2007/2008 wameajiriwa Maafisa Ugani 309. Aidha, katika mwaka 2008/2009 Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga itaajiri Maafisa Ugani 10. Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI itaendelea kuweka kipaumbele katika kuwapanga Wilayani Sumbawanga watalaam wanaofuzu katika vyuo vya kilimo.

(b) Jukumu kubwa la Serikali katika kufikisha pembejeo kwa wakulima ni kutoa motisha msaada wa ruzuku ambaa unawezesha mkulima kupata mbolea kwa bei nafuu. Aidha, Serikali inashirikiana na kuhamasisha Makampuni binafsi ambayo yanasaambaza mbolea kupeleka mbolea karibu zaidi na wakulima kuitia kwa Mawakala wa pembejeo vijijini. Ili kuhamasisha Makampuni ya mbolea kufikisha mbolea karibu zaidi na wakulima, kuanzia msimu wa 2008/2009 ruzuku itatolewa moja kwa moja kwa mkulima ambaye atakuwa huru kununua mbolea iliyokaribu zaidi na ya bei nafuu zaidi. Kwa hiyo, Makampuni ya mbolea yatahindana kuwa karibu zaidi na wakulima.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa Serikali imeelekeza Kiwanda cha Minjingu ndicho kiweze kusambaza mbolea nchi nzima na tunaelewa jinsi nchi yetu ilivyo kubwa na kiu ya wakulima kupata mbolea hii mpaka sasa hatujaweza kutosheleza nchi nzima. Je, Serikali itahakikishaje kwamba mbolea hiyo inafika pembe zote za nchi hii Kigoma, Rukwa, Ruvuma, Mtwara pamoja na katika jimbo langu la Kalambo?

Swali la pili, kwa kuwa Makampuni yaliyokuwa yanasaambaza mbolea yapo Makampuni ambayo hayakuwa na uaminifu na yamesababisha hasara kubwa sana kwa wananchi kwa sababu wamewanyonya wananchi kwa kuwauzia mbolea kwa bei kubwa. Je, Serikali inachukua hatua gani kwa kipindi cha mwaka huu ili wananchi wangu katika jimbo la Kalambo wasiweze kununua mbolea kwa bei ambayo sio ya ruzuku kama ilivyokuwa mwaka jana?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme ili mbolea iweze kuwafikia wananchi na wakulima kwa uharaka zaidi ni kuanza mapema.

Kwa hiyo, Serikali kwa kipindi hiki imejipanga kuanza mapema na kwa kiasi kikubwa mbolea inayotoka *Minjingu Phosphate* itakuwa inasambazwa na *Tanzania Fertilizer Company (TFC)* ili iweze kufika mapema huko maana ndio wameonyesha kuwa *effective* kuliko Makampuni mengine.

Pili, kuhusu uaminifu kama nilivyosema kwamba sasa hivi ruzuku itakwenda moja kwa moja kwa mkulima. Mkulima anapewa *coupon* anatumia ile *voucher* anakwenda kwa msambazaji wa mbolea ambaye anaona anauza mbolea kwa bei rahisi na ambaye anayo mbolea anayohitaji. Kwa hiyo, hakutakuwa na suala tena la Makampuni yale kutokuwa maaminifu.

Na. 416

#### **Kituo cha Polisi – Kibakwe**

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE** aliuliza:-

Kwa kuwa, Kituo cha Polisi Kibakwe kimejengwa vizuri sana ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa nyumba ya Mkuu wa Kituo:-

- (a) Je, kwa nini kituo hicho hakijawekewa umeme licha ya kwamba umeme upo mita chache toka kituoni hapo?
  
- (b) Je, Serikali ina mipango gani ya kukipatia kituo hicho usafiri hata wa pikipiki ili kufanikisha ufanisi wa kazi kwa Askari kuweza kufika katika matukio ya uhalifu yanayofanyika sehemu za milimani kama Kata za Wotta, Ipera na Mbuga za Luhundwa ambako si rahisi kutumia usafiri wa balskeli?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI (K.n.y.  
WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa George B. Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe, lenye sehemu (a) na (b) napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 6 Februari, 2008 wakati wa Mkutano wa Kumi, Kikao cha Saba, Waziri wa iliyokuwa Wizara ya Usalama wa Raia alijibu

swali Na. 92 liloulizwa na Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mbunge wa Jimbo la Kibakwe, kuhusu kuboresha Kituo cha Polisi Kibakwe. Swali hili linafanana kabisa na Swali hili la leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mbunge wa Jimbo la Kibakwe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kujibu swali Na. 92 Serikali ilimhakikisha Mheshimiwa Mbunge kwamba itafanya kila liwezekanalo kuhakikisha kwamba umeme katika kituo cha Kibakwe unapatikana.

Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa Bajeti inayotengwa kila mwaka kwa ajili ya shughuli za Maendeleo ukilinganisha na mahitaji makubwa ya ujenzi wa vituo vya Polisi, Makazi ya Askari na Miundombinu ikiwemo umeme katika vituo vya Polisi imekuwa vigumu kutekeleza mahitaji yote kwa wakati mmoja. Lakini nia ya Serikali ya kuweka umeme katika vituo vya Polisi hapa nchini kikiwemo cha Kibakwe ipo pale pale na tutaendelea kutekeleza kwa awamu.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilikipatia kituo kidogo cha Polisi cha Kibakwe pikipiki mpya Na. PT 1371 aina ya Yamaha mnamo tarehe 4 Februari, 2008. Pikipiki hiyo imesaidia sana kuwawezesha Askari Polisi kufanya doria, misako na kuwahi kwenye matukio ya uhalifu mara inapotokea katika sehemu alizozitaja Mheshimiwa Mbunge. Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda kumshukuru Mheshimiwa Simbachawene kwa kufutilia kwa karibu sana maslahi na vitenda kazi katika kituo cha Polisi cha Kibakwe na Wizara yangu itaendelea kushirikiana naye ili kukamilisha kazi iliyobaki.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii kuuliza swali dogo tu la nyongeza. Kwanza nishukuru kwa kuleta pikipiki katika kituo cha Polisi cha Kibakwe. Lakini tangu Serikali ilipoahidi kuweka umeme katika kituo cha Polisi Kibakwe, katika Mkutano wa 10 mpaka leo hii hakuna hatua zozote zile au Maendeleo yoyote ambayo yamechukuliwa.

Je, Serikali inaweza kutuhakikisha maana ahadi yake hiyo ilitolewa na wananchi wakisikia ni lini wanaweza wakaanza utaratibu wa kuweka umeme katika kituo cha Polisi Kibakwe?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Serikali kutoa ile ahadi hatua zimekuwa zinachukuliwa tayari tathmini ya kazi ya kuweka umeme katika kituo hicho imeshafanyika inaonyesha kwamba zinatakiwa kama shilingi 2,900,000 ili kazi ikamilike. Fedha zinatafutwa na wakati wowote zikipatikana hiyo kazi itafanyika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali yamekwisha na muda umepita, sasa tunao wageni katika Bunge letu hili. Kwanza kabisa ninaye mgeni wa Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Jackson Makwetta ambaye ni Mheshimiwa Edgar-Maokola Majogo, huyu alikuwa Mbunge waliingia siku moja katika Bunge hili Mheshimiwa Majogo, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Makwetta waliingia siku moja na wote wakawa Mawaziri na ni marafiki wote hao.

Kwa hiyo, tunakukaribisha sana Mheshimiwa Majogo na mimi mwaka 1975 alikuwa mpiga debe wangu Bungeni humu. Halafu tuna wageni wengine Bungeni, wageni wa Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Naibu Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ambao ni binti yake Rahma Juma Omar, yuko wapi Bi Rahma? Halafu yupo na Salma Abdallah Ally, karibuni sana. (*Makofī*)

Halafu tuna wageni wa Mheshimiwa George Malima Lubeleje, hawa ni Mheshimiwa Diwani wa Kata ya Mlali Kongwa Ndugu Sina Munde, Mheshimiwa Diwani yuko wapi? Karibu sana tuna Mheshimiwa Diwani wa Kata ya Godegode, Mpwapwa Kinyaka Omar Kinyaka, tuna Katibu Mwenezi wa CCM wa Kata ya Chunyu Ndugu Anthony Chonya, tuna Katibu wa CCM Kata ya Chunyu Ndugu Jonas Silanga, tuna Mchungaji kutoka Kanisa la *Anglican* Dayosisi ya Mpwapwa Mchungaji Michael Luhaha, karibu sana wageni wa Mheshimiwa Lubeleje.

Halafu tuna wageni wa Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga ambao ni Ndugu Biswalo Bernard na Ndugu Kileo Buhero wote wanatoka TUWASA Tabora wako wapi? Karibuni sana. Halafu tuna wageni wa Mheshimiwa Alhaj Mohamed Missanga hawa ni Mwenyekiti wa Kata ya Ikungi, Luteni Joseph Mkuki, kuna Mwenyekiti wa Kata Isanga Isuna Jonas Jingu.

Halafu na Mheshimiwa Diwani wa Isuna Mheshimiwa Stephen Missai na Mheshimiwa Diwani wa Ikungi Mheshimiwa Haji Mkandi. Yupo Katibu Kata Isuna Emmanuel Gwao na yupo Katibu Kata Ikungi Ndugu Abdallah Mujengi. Karibuni sana katika Bunge letu, ahsante sana. Tuna wanafunzi 45 na walimu 3 kutoka Shule ya Sekondari ya Ruvu wasimame na walimu walipo. Aah!! Karibuni sana. Ahsante. Tuna wanafunzi wengine 30 kutoka Shule ya Msingi Ipagala B wasimame na walimu walipo hili ni kundi lingine walikuja Jumatatu. Ahsanteni sana tunafurahi kuwaoneni. (*Makofī*)

Waheshimiwa Wabunge kuhusu Kamati kwanza kabisa Kamati ya Uongozi na Tume ya Bunge walikuwa wakutane leo kikao kimeahirishwa mpaka kesho saa 7.00 mchana tutaeleza tena. Kwa hiyo leo hakuna kikao mpaka kesho. Halafu Mheshimiwa George Lubeleje, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuwa kutakuwa na kikao leo hii tarehe 18 Agosti, 2008 Saa 5 asubuhi katika Ukumbi Na. 219.

Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii Mheshimiwa Omar Kwaangw' yeze anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake, Kamati ya Kudumu ya Huduma za Jamii kuwa kutakuwa na kikao leo Saa 5 pia katika ukumbi Na. 23. Halafu napenda

kueleza kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko safari badala yake Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano anashikilia shughuli hizi za Serikali hapa Bungeni. Mpaka leo nafikiri leo ndio siku yake ya mwisho kwa maana hiyo. Juzi kulikuwa na Mashindano ya Michezo ya Kirafiki baina ya Mtwara *Veterans* na Bunge kwa *football*. Sasa *Veterans* wa Mtwara walipata goli moja na *Bunge Sports Club* timu ya Mpira ilipata magoli 3. Kwa hiyo, waliwashinda wa Mtwara *Veterans* nadhani wale walikuwa wametoka mbali walichoka labda. Halafu kulikuwa na timu nyingine ya *netball* hii ilikuwa kati ya Dodoma *Veterans* na *Bunge Netball Sport Club*, Dodoma *Veterans* walipata magoli 20 Bunge *netball team* ilipata magoli 23. Kwa hiyo, Bunge walishinda, sababu za kwanza hapa hazipo sasa.

Waheshimiwa Wabunge pia napenda kuwaarifu kwamba jana tarehe 17 saa 11.30 Mheshimiwa Dr. Haji Mwita alipata ajali eneo la Kibaigwa akiwa na familia yake akitokea Dar es Salaam. Tunamshukuru Mungu kwamba ye ye mwenyewe Dr. Haji ameumia, lakini mke wake ndio ameumia zaidi na amelazwa katika hospitali hii ya hapa Mkoani Dodoma na hali zao zinaendelea vizuri. Kwa hiyo, tunamshukuru Mungu kwamba haikuwa zaidi ya hapo.

## HOJA ZA SERIKALI

### **Makadirio ya Matumizi ya Serikali Kwa Mwaka 2008/2009 Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia**

(*Majadiliano yanaendelea*)

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wote wa Wizara, kwa kuandaa na kuwasilisha hutoba hii mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, nina mambo machache ya kuchangia:-

Mheshimiwa Spika, msingi mkubwa wa kujenga Chuo cha Mbeya cha Sayansi na Teknolojia (*Mbeya Institute of Science and Technology (MIST)*, ulikuwa ni kuzalisha wataalam katika fani hizo. Lengo lilikuwa ni kukifanya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia, lakini jambo la kusikitisha ni kwamba, hadi leo chuo hicho bado hakijapewa hadhi ya kuwa Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Spika, naomba nimkumbushe Waziri kwamba, suala la kukifanya *MIST* kuwa Chuo Kikuu ni ahadi iliyotolewa na Muasisi wa Taifa hili (Baba wa Taifa), Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa Kwanza wa nchi yetu. Mwalimu Nyerere, aliwaomba Warusi waisaidie Tanzania kujenga Chuo hicho. Urusi ilikubali kujenga Chuo hicho.

Mheshimiwa Spika, michoro yote ya kukijenga chuo hicho ni ya ngazi ya Chuo Kikuu, eneo lililotolewa kwa chuo ni kwa mipango ya Chuo kikuu. Hivi ni nani huyo ambaye alichukua maamuzi ya kutoendelea na kukipa hadhi chuo kuwa chuo kikuu? Je, kufanya hivyo si kudharau ahadi na mtazamo wa Muasisi wa Taifa hili Mwalimu Julius Kambarage Nyerere?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nchi yetu bado ina vyuo vichache (Vyuo Vikuu), hasa vyta fani ya Sayansi na Teknolojia; na kwa kuwa bado tunahitaji kuwa na Vyuo Vikuu vingi; na kwa kuwa ni heshima kubwa zaidi kumuenzi Muasisi wa Taifa letu na Rais wa Kwanza wa nchi hii aliyeahidi kukifanya chuo hicho kuwa na hadhi ya Chuo Kikuu; nashauri Wizara ione umuhimu wa kukifanya chuo hicho kuwa Chuo cha Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu kulikuwa na mgogoro wa umiliki kati ya *T.T.C.L* na Celtel Tanzania; naomba kujua je, mgogoro huo uliisha, kama uliisha uliishaje?

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Celtel wamebadilisha jina na kuitwa Zain; nataka kujua je, taratibu zote za kubadilisha jina na mambo mengine zimezingatiwa?

Mheshimiwa Spika, kampuni zote za simu za mkononi hulipia gawio (*divident*) serikalini. Hata hivyo, kwa sababu ambazo mimi sizielewi, Kampuni ya Vodacom kwa muda mrefu sana imekuwa hailipi gawio serikalini, huku wote tukijua kwamba, Kampuni hii inafanya biashara yake kwa mafanikio makubwa sana. Sasa naomba Waziri atueleze ni sababu gani zinazofanya Kampuni hiyo isilipe gawio kwa serikali? Je, sasa si muda/wakati muafaka, Kampuni hiyo ikaanza kulipa gawio ili serikali ipate fedha kwa maendeleo ya nchi yetu?

Mheshimiwa Spika, mimi pamoja na kwamba ni Mjumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, ambayo inasimamia Wizara hii, sitaunga mkono bajeti ya Wizara hii, kama sitapewa maelezo ya ni nani hasa aliyeamua *MIST* isiwe Chuo Kikuu na kama huko siyo kudharau tamko la Muasisi wa Taifa hili aliyetaka *MIST* kuwa Chuo Kikuu. Ahsante.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, kama ninavyopenda mara kwa mara kuchangia Wizara hii kuhusu mkoa wangu. Kuhusu Wizara hii nina uchungu sana, sitachoka mawasiliano ni muhimu sana tena sana. Mapori yetu ya Kasindaga hadi Biharamulo katikati humo ni pabaya sana. Naomba kuishauri au kuwashauri wenyewe mitandao yote, mapori hayo nitakayoyataja Kimisi hadi Karagwe, Uzuri wa Kondoo hadi Kyanga; matatizo ni makubwa sana. Kwanza, wananchi wanaosafari katika mapori yote hayo kama ilivyotokea juzi Kimisi pabaya sana tena sana.

Simu za mkononi wanasema kwamba, zina madhara; je, ni kweli? Tumeshaanza kuziogopa; je, mionzi ina matatizo na tufanyeje ili kupingana na tatizo hilo?

Kuhusu matumizi ya simu inatokea tatizo gani unaweka pesa kwa mfano Sh. 100,000 eti unaongea kwa sekunde hazimalizi muda; je, huo sio wizi? Kuna matatizo mengine, wanatuma ujumbe kwamba, umeshinda milioni moja weka vocha za elfu themanini, halafu tuma namba yako ya akaunti yako tukuwekee pesa na si mara moja ni mara nyingi tu; je, hiyo ni nini; ukipiga simu mko wapi mara Nairobi mara wanaongea lugha isiyofahamika; je, ni kitu hicho?

Naomba ufanuzi mpana mimi nimeshachoka nilitaka kuchangia kwa kuzungumza lakini bado sijawa sawa. Inaniumisa sana na kunikera; simu za mezani umeitumia au hukuitumia utalipa; je, unalipa nini?

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, nitaomba ufanuzi mpana. Nawataki Bajeti njema.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Nawaomba waendelee hivyo hivyo kwa faida ya taifa letu.

Mheshimiwa Spika, napenda nikukumbushe Mheshimiwa Waziri, ahadi ya Kampuni za Zain, *Tigo* na *Vodacom* ya kujenga minara ya simu Iramba Mashariki. Huu ni mwaka wa saba toka Wizara hii itoe ahadi ya kujenga mnara wa *Celtel* sasa *Zain*, Kijiji cha Nkungi, Iramba Mashariki; hatua inayofanya wananchi kukosa imani kwa ahadi za serikali.

Mheshimiwa Spika, *Tigo* walishatembelea maeneo ya Iramba Mashariki na kuchagua maeneo ya kuweka minara yake. Nawaomba Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, wakumbushe ili watekeleze ahadi. Wananchi wa Iramba Mashariki, wanao uwezo sana wa kujua gharama za mitandao hii.

Mheshimiwa Spika, *Vodacom* walihidi kujenga mnara Gumanga, nao naomba Mheshimiwa Waziri awakumbushe.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, naomba kwa niaba ya Wana-Iramba Mashariki, kuipongeza sana serikali kwa kuwashawishi mashirika ya simu kujenga minara kama ifuatavyo: *Celtel (Zain)* Iguguno, Nduguti na Ibaga; *Tigo* – Iguguno; na *Vodacom* – Iguguno.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja yako mia kwa mia.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri na yenye ufanuzi wa kina kuhusu Wizara yake.

Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Kwa kuwa mawasiliano ya simu za kiganjani (mkononi) ni muhimu sana kwa maendeleo ya uchumi wa nchi yetu; na kwa kuwa serikali ilikuwa na mpango wa kupeleka huduma ya mawasiliano ya simu za kiganjani sio mijini tu bali hata vijijini; je, mpango huo umefikia wapi?

Je, serikali ina mpango gani wa kujenga minara ya simu za kiganjani katika Kata ya Mima, Mkanana, Tambi, Mlembule, Majami, Matomondo, Berege, Nana, Lupeta, Godegode, Kiborian na Igoji Kaskazini, Wilayani Mpwapwa ili kuboresha mawasiliano ya simu katika vijiji hivyo.

Kwa kuwa mnara wa *Celtel (Zain TZ)*, ulijengwa kati ya Vijiji vya Chiseyu, Mzase na Lukole, Wilayani Mpwapwa na kwa kuwa mnara huo tangu ujengwe sasa ni miaka miwili lakini haufanyi kazi hadi sasa. Je, kwa nini mnara huo haujafunguliwa kutoa huduma ya mawasiliano katika vijiji hivyo; na je, utafunguliwa lini?

Kwa kuwa simu za kiganjani zina madhara. Je, serikali imeweka mkakati gani wa kudhibiti hali hiyo ili simu hizo zisilete madhara kwa watumiaji?

Kwa kuwa Jengo la Posta ya Mpwapwa linahitaji ukarabati; je, ni lini serikali italikarabati Jengo hilo na kuongeza watumishi na kuwapatia vitendea kazi vya kutosha?

Je, serikali ina mpango gani wa kuboresha huduma ya Kampuni ya Simu ya *TTCL* ili kupeleka huduma ya mawasiliano hadi vijijini?

**MHE. HEMED MOHAMMED HEMED:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuijalia nchi yetu kuwa na amani na kuwafanya Watanzania waishi kwa amani kama vile ndugu. Vilevile napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, kwa umahiri wao na utendaji wao ambao umeweza kuwaunganisha Watanzania ndani na nje ya chini. Mwenyezi Mungu, awape fikra zitakazowasaidia kusukuma mbele mahitaji ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hayo, sasa naomba nitoe mchango wangu katika Wizara husika.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mawasiliano ni miongoni mwa sekta zilizoweza kuiletea nchi yetu mabadiliko makubwa. Wizara hii imeweza kuboresha mtandao na huduma za simu nchini na kuimarisha uwezo wa kutabiri hali ya hewa nchini kwa kutumia vyombo vya kisasa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada za Wizara, kuna mambo ambayo bado hawajaweza kuyatekeleza kwa kiasi.

Mheshimiwa Spika, bado upo upungufu wa simu za mezani na simu za mikononi kupanua huduma zake vijijini na wananchi wetu wanahitaji huduma hizi kwani kuna baadhi ya maeneo mawasiliano hayapatikani. Naiomba Wizara iangalie maeneo hayo ili kuondokana na tatizo hili. Pia gharama za utumiaji wa simu ni kubwa sana, hali ya watu

wetu ni ya umaskini. Ni vyema Wizara itoe msaada wake ili iwawezeshe wateja wa simu, waweze kuwa na mategemeo ya kazi zenu. Ongezeko la ushuru wa forodha, ndio unaompeleka mtu wa chini kushindwa kumiliki simu na huduma kiujumla.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada ya taasisi maalum ya kuzuia bidhaa bandia hapa nchini, bado uingiaji wa simu bandia unaongezeka siku hadi siku, jambo ambalo husababisha kuwatia hasara wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia ya Wizara kutayarisha Muswada wa Sheria itakayowezesha kupata simu kadi (*Sim Card*), kwa vitambulisho na kuwezesha kuwachukulia hatua za kisheria wale wote watakaobainika kuwa na matumizi mabaya ya simu hizo. Mimi napata wasiwasimkubwa juu ya nia ya Wizara kufanya haya, simu kadi. Kufanya hivi si kugema siri za watu? Jambo ambalo linaweza kupunguza watumiaji wa simu.

Mheshimiwa Spika, ongezeko la mawasiliano ya simu limeathiri matumizi ya Posta kwa njia ya barua. Hivyo, Wizara ibuni mbinu ya ziada ili kuziongezea Posta zetu kipato.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hayo nasema ahsante.

**MHE. GIDEON A. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kutumia nafasi hii, kumpungeza Mheshimiwa Waziri, pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuteuliwa kuiongoza Wizara hii muhimu.

Aidha, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Watendaji wote wa Wizara, kwa maandalizi ya bajeti na uwasilishaji mzuri Bungeni.

Mheshimiwa Spika, katika kuunga mkono hoja hii, naomba kuchangia machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza serikali kwa kuendelea kuiboresha Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya. Kwa kuwa kilio kikubwa cha Wananchi wa Mkao wa Mbeya ni kuiwezesha Taasisi hii kutoa mafunzo hadi ngazi ya shahada na kuendelea kuiboresha Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya.

Kwa kuwa kilio kikubwa cha Wananchi wa Mkao wa Mbeya ni kuwezesha Taasisi hii kutoa mafunzo hadi ngazi ya Shahada na kuendelea, tunafarijika kusikia kwamba, taratibu za kuanzisha Shahada ya Kwanza katika fani zilizotajwa katika aya ya 38 ya Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, zitakamilishwa katika mwaka wa 2008/2009. Tunaomba taratibu hizo zikamilike kwa muda muafaka ili Taasisi hiyo iweze kufikia hadhi ya juu iliyokusudiwa. Aidha, ni muhimu Taasisi hiyo iweze kutambuliwa na mamlaka zote zinazosimamia Elimu ya Juu na Ufundu nchini ili shahada zake ziweze kutambuliwa.

Mheshimiwa Spika, makampuni binafsi ya simu za kiganjani, yanaendelea na jitihada zao za kusambaza huduma zao sehemu mbalimbali nchini. Simu za kiganjani

siyo suala la anasa tena, bali ni vitendea kazi muhimu katika Sekta ya Mawasiliano. Kwa hiyo, ni muhimu kwa serikali kuendelea na jitihada za ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na kushawishi na kushirikisha sekta binafsi kuwekeza katika Sekta ya Mawasiliano. Simu za kiganjani zinahitajika mijini na vijiji na kwa hiyo, serikali iendelee kuweka mazingira mazuri ya miundombinu hususan vijiji, ili makampuni binafsi yaweze kufikisha huduma zao bila ya vikwazo.

Mheshimiwa Spika, nikirejea kwenye Jimbo langu la Ileje, nayapongeza makampuni binafsi ya simu ya ZAIN, TIGO na VODACOM, ambayo yamefikisha huduma zao katika baadhi ya maeneo ya Wilaya yetu. Naomba Wizara itusaidie kuyashawishi makampuni haya, kuelekeza huduma zao sasa katika maeneo ya Tarafa ya Bundali. Sasa hivi makampuni hayo yote, yamejikita maeneo ya Tarafa ya Bulambya ambako ndiko yalipo Makao Makuu ya Wilaya. Kiuchumi, Tarafa ya Bundali ina hali nzuri zaidi na kuna uhakika wa biashara nzuri ya simu za kiganjani. Aidha, kuna Hospitali Teule ya Wilaya katika Tarafa hiyo na barabara ni nzuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huo mfupi, naomba kuunga mkono hoja na kuwatakitia mafanikio mema.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii, kuwapongeza kwa dhati Waziri, Mheshimiwa Profesa Mosolla, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari, Katibu Mkuu, Viongozi, pamoja na Wataalam wote wa Wizara hii na taasisi zake. Nawapongeza kwa hotuba nzuri na jitihada kubwa sana katika kutekeleza sera, mipango na mikakati kuhusu majukumu ya Wizara hii katika mazingira magumu ya ufinyu wa bajeti, uhaba wa wataalam na vitendea kazi na ushindani mkubwa wa utandawazi duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi maalum kwa jinsi uchambuzi na mipango ulivyozingatia maelekezo ya Ilani ya uchaguzi ya CCM ya 2005, mfumo wa Wizara na vipaumbele kwa mahitaji mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada za kueneza mtandao na huduma za simu hadi vijiji, zinastahili pongezi maalum. Nachukua fursa hii, kutoa shukrani zangu kwa niaba ya Wananchi wa Wilaya ya Mkinga, kwa matumaini mema tuliyopatiwa na Wizara hii, kupitia jibu lao kwa swali langu Na. 274 hapa Bungeni tarehe 23 Julai, 2008. Ninaahidi kushirikiana ipasavyo na Wizara, pamoja na Kampuni za Simu za ZAIN, TTCL, TIGO na ZANTEL kuhakikisha mafanikio ya kuwepo mawasiliano ya kutosha na bora Wilayani Mkinga kote. Matumaini yangu ni kwamba, Wizara itatoa ushirikiano na msukumo mkubwa katika kufanikisha azma hiyo. Hata hivyo, TCRA iimarishe udhibiti wa bei za huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefarijika kwa azma ya Wizara kuboresha na kuimarisha huduma za Shirika la Posta. Ni matumaini yangu kwamba, zaidi ya kulikwamua Shirika hili kuondokana na ukwasi na kuboresha miundombinu, kuna umuhimu mkubwa wa kuendeleza ufanisi wa Shirika hili hasa kwa huduma nyeti kama vile EMS.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Mkinga bado ina kiu kubwa ya huduma za posta. Tunasubiri kwa hamu kubwa kupatiwa huduma za posta katika Wilaya hii mpya kama tulivyoahidiwa miaka miwili iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukamilishaji wa uendeshaji wa mtandao wa *TEKNOHAMA* kufikisha *internet* hadi vijijini, utakuwa na manufaa makubwa ya kuboresha mawasiliano, elimu, huduma nyingine za jamii na kuisimamia biashara na shughuli nyingine za uzalishaji vijijini. Mfuko wa *UCAF* sio tu usaidie kuwapatia ruzuku wawekezaji walio tayari, bali pia usaidie kuelimisha na kuamsha ari ya wanavijiji kuhusu manufaa ya programu, jinsi wanavyoweza kufaidika na jinsi wanavyoweza kushiriki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna umuhimu mkubwa kwa kuchukua hatua thabiti kutekeleza mpango wa kuifanya Tanzania kuwa kiungo kikuu cha mawasiliano kikanda na kimataifa kupitia *UHURUNET* na *UMOJANET*, kwa kuzingatia ushindani mkubwa ambao baadhi ya nchi jirani hujianaa kuipiku Tanzania, licha ya itifaki ya *NEPAD* kuilenga Tanzania kuwa *ICT hub through marine optic fibre systems*.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli za Utafiti na Maendeleo (*R&D*) ni muhimu sana kwa uvumbuzi na maendeleo ya teknolojia, uongezaji tija na uendelezaji bidhaa bora, vifaa bora na michakato bora. Shughuli hizi ni muhimu sana kwa kuzingatia kwamba, ndilo chimbuko kuu la kuongeza ufanisi na kupiku ushindani mkali katika dunia hii ya utandawazi; hali inayofanya matokeo ya utafiti wa kisayansi kuwa siri ya nchi au taasisi husika na kuhifadhi na kulinda kwa hataza (*patent*). Kwa maoni yangu, kiwango cha *MTUSATE* na tengeo la serikali kwa ajili hii bado ni dogo sana kwa kulinganisha na umuhimu na uzito wa shughuli za “*R&D*”. Naishauri serikali iongeze kipaumbele kwa *MTUSATE* na tengeo lake, kwa shughuli hii ni muhimu ili ifanyike kwa mafanikio makubwa zaidi na hivyo kuongeza kasi ya mchango wake kwa maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii, kumpongeza sana Waziri na Wizara kwa ujumla, kwa maandalizi ya hotuba nzuri na yenye kuzingatia zaidi malengo ya MKUKUTA.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa ili uchumi wetu ukue, basi suala hili la Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ni la msingi sana. Hivyo, namwomba Waziri ahakikishe kila lililoandikwa katika hotuba hii nzuri linatekelezeka (*implementation of all the stated plans*).

Mheshimiwa Spika, nasema hivi baada ya kuona udhaifu uliopo kwa sasa kwenye Wizara zetu nyingi.

Mheshimiwa Spika, binafsi ningependa Waziri atutolee ufanuzi wa sababu za msingi zilizopelekea *Celtel* kubadili jina na sasa kuitwa *ZAIN*. Ningependa Waziri pia

atueleze kama wabia; ni faida na hasara zifi ambazo nchi yetu imezipata kutokana na mabadiliko hayo?

Mheshimiwa Spika, vilevile ningependa kujua ni kwa nini mchezo huu wa *VUNA PESA* humsababishia mwananchi kutumia Sh. 1000 kwa kila anapotuma SMS moja kwenda kwenye simu namba 15550, pesa ambayo ni nyingi sana ukilinganisha na viwango vingine vya utumaji wa *SMS*?

Mheshimiwa Spika, mchezo huu wa *VUNA Pesa* umeonyesha utapeli mkubwa na umekuwa kama njia mojawapo ya kuiba pesa za wananchi.

Mheshimiwa Spika, ningependa Waziri atujibu ni kwa nini mchezo huu na mingine minge ambayo ni utapeli mtupu iruhusiwe katika taifa letu?

Mheshimiwa Spika, katika suala zima la Posta, napenda kuishauri Wizara iongeze kwa wingi matumizi ya simu, *internet* na *telefax* katika maeneo ya mijini na pia kuongeza matumizi ya masanduku ya posta katika maeneo yetu ya vijijini ili kuboresha mawasiliano katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Wizara iboreshe zaidi matumizi ya *SIM Card* hasa katika eneo la upatikanaji au manunuzi ya hizi *SIM Card*.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa matumizi ni mabaya sana, maana watu wametumia mwanya huu kuzifanya *SIM Cards* hizo uharamia wa kila aina.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hali hii imekuwa kero kubwa kwa wananchi; hivyo ni muhimu Wizara ibuni mikakati ya kudhibiti uharamia ufanewao na haya matumizi mabovu ya hizi *SIM Cards*.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naomba kuwasilisha.

**MHE. FELIX N. KIJKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuunga mkono hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa hoja nzima imejitosheleza. Nawapongeza sana Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na Wataalam wote, kwa kuandaa hotuba nzito, yenye kuonyesha mwelekeo wa Wizara hiyo ambao kwa hakika ni changa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo ambazo zinanifanya niunge mkono hoja kwa asilimia zote, ninapenda kuchangia katika vipengele vifuatavyo:-

Mkoa wa Kigoma unayo makambi mengi na makubwa, ambayo yamekuwa yakinuwa na wakimbizi ambao si muda mrefu wataondoka wote. Ninaomba katika jitihada za kuuendeleza Mkoa wa Kigoma zinazofanya na serikali, basi Wizara hii

changa ichukue kambi moja na kuiendeleza kwa ajili ya kuwa na Chuo cha Kufundisha Utaalamu wa Sayansi. Ni dhahiri kwamba, ili kuanza kwa chuo gharama kubwa huwa ni miundombinu kama majengo na huduma muhimu, vitu ambayo vyote viro. Ni kwa mantiki hiyo, kutakuwa na unafuu wa kuanzisha chuo hicho kwa kuokoa fedha za serikali.

Nayapongeza mashirika ya simu za mkononi kwa jitihada zinazofanywa na mashirika hayo, kwa kujenga minara. Hata hivyo, katika Wilaya ya Kibondo, bado mawasiliano hayafiki baadhi ya maeneo kutokana na maeneo hayo kukosa minara. Nilishatoa maombi na kuahidiwa kujengewa minara mitatu, lakini hadi sasa hakuna hatua ambazo zimechukuliwa. Maeneo yasiyo na mawasiliano ni Kata za Murungu, Kigina na Kabingo. Ninaomba kupatiwa maelezo ya kuwasaidia wananchi hawa wakati Waziri akijibu.

Kwa muda wote, Kampuni ya Posta Kibondo imekuwa ikiendeshea shughuli zake kwenye jengo la mtu binafsi, ambalo limepangishwa. Usalama wa mitambo na mali za kampuni umekuwa hatarini kuibiwa wakati wowote kwa maana ya jengo kutokuwa na uimara. Hotuba ya Waziri, imeeleza kuhusu kujengwa kwa ofisi hiyo Kibondo, lakini fedha zake hazikuonyeshwa na hata muda wa kuanza kujenga. Kwa uchungu na huruma kubwa waliyonayo Wananchi wa Kibondo, wameshatoa kiwanja cha kujenga. Naomba wananchi hao waliota kiwanja, wapate maelezo ya Waziri kuhusu kuanza kwa ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni changa kabisa, wakati inayagusa maisha ya Watanzania na hasa Wanasyansi. Ninashauri Wizara hii, iongezewe fedha kwa sababu fedha zilizoombwa ni kidogo mno. Nina hakika, Wizara itashindwa kukamilisha miradi iliyopangwa.

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa niaba ya Wananchi wangu wa Hai, kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji wengine wote hapo Wizarani. Hii ni hotuba nzuri na inayoashiria kuwa, labda taifa letu sasa tunaanza kuwa *Digital Country*. Hongereni sana na tuongeze bidii.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika kuwa, dunia ya leo bia sayansi tena ya vitendo, kufikia malengo ya milenia ni ndoto. Ninachomaanisha hapa ni lazima tuwe *serious* na tuthubutu kuwekeza kwa wingi sana na kuwa tayari kuyapongeza mabadiliko yaliyopo na yanayotarajiwaa duniani.

Kuna kila sababu ya kuliboresha zaidi Shirika letu la Posta, kwani pamoja na kuwepo huduma za simu na *internet*, bado mahitaji ya posta yapo na yataendelea kuwepo mathalani usafirishaji wa vifurushi na *registers*. Umuhimu wa *New Addressing System and Post Code* ni wa juu sana na wa haraka, kwani dunia yote ndio ipo huko hivi sasa ikiwa ni pamoja na faida zake lukuki.

Niipongeze serikali kwa kuanzisha Mfuko wa Huduma za Mawasiliano Nchini (*Universal Communication Access Fund*), huu ni ukombozi hasa kwa wananchi wetu kule vijiji (*TEKNOHAMA*).

Mawasiliano ya simu za mikononi yanakwenda vizuri, lakini tunahitaji uangalifu mkubwa sana kwani pamoja na maendeleo yake, madhara pia ni makubwa. Uwekaji minara yao; kutokudhibitiwa kwa *lines* zao kwani hata hapa Bungeni jana tuligawiwa bure *line za Zantel*, sasa hapa udhibiti utakuwaje? Vilevile ughali wa bei za mawasiliano, kwani *tariffs* zinatisha. Je, tumeweka utaratibu mzuri wa kukusanya kodi kutoka kwa haya makampuni ya simu za mikononi? Bado hatupati cha kutosha. Tuzidishe juhudi katika masomo ya sayansi na sayansi kwa matendo. Kule Wilayani Hai pia tunalima Zao la Artemisia, kwani hatukutajwa.

Mheshimiwa Spika, nashauri tuongeze *tele centres*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, nakumbushia kuhusu maombi yangu kwa barua kwa Naibu Waziri, kuhusu kuwashamasisha wawekezaji wa simu za mikononi, kuangalia uwezekano wa kupeleka mawasiliano katika Tarafa ya Mwambao, Wilayani Ludewa, nyuma ya Milima ya Livingstone angalau kutoka Kata za Lupingu na Makonde kunako zaidi watu 10,000

Nashukuru tuna huduma ya Posta pale Ludewa Mjini, lakini barua na vifurushi kutoka au kwenda Njombe vinasafirishwa mara moja tu kwa juma. Naomba hali hii irekebishwe na kuongeza kasi ya usafirishaji.

Tunashukuru kuwa Ludewa kumeanzishwa Kituo cha Mawasiliano, ukurasa wa 15, kifungu cha 25 kwenye kitabu. Ningependa kujua makusudi na mategemeo ya kuwa na kituo kama hicho.

Sayansi na Teknolojia, kwa sehemu kubwa inahu utafiti. Mimi sijaona mpango au mkakati wa utafiti elekezi unaoelekeza jinsi taifa letu litakavyotoka kutoka ngazi hii tuliyonavyo ya kunakiri matokeo ya tafiti za wenzetu na kuanza kutegemea matokeo ya tafiti zetu wenywewe. Wataalam tunao lakini hatuna *political will* ya kuanza utafiti katika maeneo fulani fulani ili kelekeza maendeleo ya nchi. Tunaendelea kupuuza utafiti na hasa wa sayansi katika nchi hii.

**MH: RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Napenda kuipongeza Wizara/Serikali kwa mahusiano mazuri iliyofanya na kampuni za simu kama *TIGO*, *VODA* na *CELTEL* (*Zain* sasa), kuweza kufikisha mawasiliano ya simu katika maeneo mengi ya jimbo langu na kutupatia usikivu wakati wote. Nawaombea baraka za Mwenyezi Mungu ziwafunike.

Mheshimiwa Spika, vijiji vifuatavyo sasa vina usikuvu tofauti na mwaka jana; Kata ya Izigo Vijiji vya Kabale na Kimbugu; Kata ya Mayondwe Kijiji cha Bugasha;

Kata ya Kagoma Vijiji/Kitongoji cha Rwazi na mwambao wote wa Ziwa Kata; Kata ya Rushwa Vijiji vya Buhuma, Bihija, Rushwa, Omurunazi, Kanoni (Kitongo) na Kyanshege; Kata ya Bulyakashaju Vijiji vya Kizinga, Ruganda, Nyakahama na vitongoji vyote vya Kata hii; Kata ya Ngenge Vijiji vya Kishuro (bado kidogo), Ngenge, Rwigembe na Rutoro (bado maeneo machache). Kwa ujumla, usikivu umeongezeka hadi kufikia kiasi cha 85 – 90% ya jimbo kutoka 40 – 45% hivi. Nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na shukrani hizi, bado naomba serikali isichoke kuniangalia ili tupate usikivu katika jimbo zima. Maeneo yaliyobaki sasa ni yale yenye hatari kwa maana ya umbali na mazingira magumu; hayana maji. Kwa sasa tatizo limebaki kata moja ambayo ni ya visiwani kama ifuatavyo; Kata ya Goziba Kijiji cha Kelebe (eneo lilioelekea Mwanza linapata mawasiliano), Kijiji cha Goziba hakina kabisa mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, vijiji hivi vilivyobaki ni vile vinavyochangia sana katika uchumi wa Wilaya ya Muleba, kwa maana ni vijiji vya wavuvi wa dagaa, samaki na aina zote zinazopatikana Ziwa Victoria. Tatizo lao hali hii nzuri ya uchumi inayoambatana na ugumu wa mazingira, wanavamiwa sana na majambazi na kukosa msaada wa haraka, maana mionganoni mwa matatizo mengi ni kukosa mawasiliano ya simu.

Mheshimiwa Spika, naiomba serikali iiangalie Kata hii na kuona jinsi ya kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, vilevile naiomba serikali iangalie uwezekanao wa kutupatia vyombo vya usafiri wa maji katika Ziwa Victoria, hasa unaoviunganisha visiwa vyangu vikiwemo hivi vifuatavyo: Kata ya Bumbire kuna Vijiji Iroba, Mahaiga, Kutua, Kinagi na Nyaburo.

Aidha, Kata Goziba Vijiji vya Makibwa, Kelebe na Goziba. Hata hivyo, mtandao huu unaunganisha na fukwe za nchi kavu zikiwemo Kyamkwikwi, Bugasha, Rwazi na Kimbugu. Naiomba serikali ikumbuke ahadi ya kuboresha gati la Kyamkwikwi, ahadi iliyosahaulika! Aidha, ieleteke kuwa bila magati, uchumi wetu unaporwa na majambazi na watu wasio waaminifu wanavusha mali yetu kwenda nchi jirani kupitia ziwani.

Mheshimiwa Spika, naomba serikali ishirikiane kati ya Wizara na Wizara ili ipate boti ziendazo kazi, kudhibiti uporaji na kuweka mazingra ya amani katika ziwa. Boti zetu hizi za *engine*, haziwezi kupambana na matatizo niliyoyataja.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, narudia kuunga mkono hoja.

**MHE. EMMANUEL J. LIHAHULA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa ulinzi wake ambao anaendelea kutulinda na kutupa uhai tulionao siku ya leo.

Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote, kwa hotuba nzuri, pamoja na kuwa hii ni Wizara mpya. Tunaomba Mungu awatie nguvu na kuwapa hekima katika utumishi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie maeneo yafutayo:-

Kampuni ya simu (*TTCL*) ni msaada mkubwa sana kwa wananchi, kwani hata gharama zake ni ndogo. Naomba mfanye utaratibu wa kutupatia simu hizi za *TTCL* katika Wilaya ya Bukombe. Ni muda mrefu sana tangu wapate kiwanja bila kuendelezwa.

Makampuni mbalimbali ya simu za mkononi kama vile *VODACOM*, *ZENTEL*, *TIGO* na *ZAIN* nayapongeza kwa kufikisha huduma zao Wilayani Bokombe. Hii inaonyesha jinsi gani wanavyofuutilia utekelezaji wa Ilani ya CCM 2005.

Naomba Kampuni ya *TIGO*, wafunge mawasiliano haraka kwenye mnara waliojenga Ushirombo (Makao Makuu ya Wilaya). *VODACOM* na *ZAIN* naomba wakamilishe uwekaji wa minara katika maeneo ya Lugunga au Nyasato Mlimani, Bulega na Namonge; ni maeneo yenye msongamano mkubwa wa watu.

Serikali iingilie kati suala la gharama za muda wa hewani ni mkubwa mno. Wananchi wetu wanashindwa kumudu gharama hizi, wakati mawasiliano sio starehe bali ni lazima.

Nashauri serikali ishauri makampuni haya yachangie shughuli za maendeleo katika wilaya. Utaratibu wanaofanya wanasubiri waombwe. Matumaini yangu ni kwamba, lazima wajue kwamba, kila eneo wanapofanyia kazi linahitaji maendeleo mfano, katika Wilaya ya Bukombe hakuna Kampuni hata moja iliyochangia maendeleo Wilayani Bukombe.

Shirika la *TCRA* linafanya kazi nzuri sana katika usimamizi. Nashauri serikali isiingilie sana matumizi yake, kwani kwa kufanya hivyo, uendeshaji wake unakuwa mgumu. Hii inatokana na maelekezo wanayoyapata ama toka Wizara Mama au Wizara ya Fedha. Utaratibu huo unaweza kusababisha matumizi mabaya ya shirika.

Shukrani za dhati ziende kwa Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, jinsi alivyoweza kutoa msukumo wa makampuni haya kuleta/kujenga minara katika Wilaya ya Bukombe.

Nawashukuru *VODACOM* kwa kuleta ajira 20 kwa Wananchi wa Bukombe, pamoja na kutoa huduma ya mawasiliano kwa bei nafuu kwa wananchi. Nia yao ya kuanzisha *VODACOM* Simu ya Watu (T) na *Vodafasta* waliyoizindua tarehe 14 Juni, 2008 ni nzuri.

Nashauri Makampuni ya *ZAIN* na *TIGO* nao wajifunze kutoka *VODACOM*, ili kuwepo ushindani wa punguzo la bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri sana ya Wizara hii, naomba kushauri yafuatayo:-

Maeneo ya sekta binafsi kama Mabenki, wamejithidi sana kwenye huduma hii ya mawasiliano, sayansi na teknolojia. Natarajia Wizara iboreshe huduma hizi katika Wizara zote za Serikali. Bado watu wanapohitaji mafao yao ngazi ya serikali za mitaa, masuala ya mirathi wanaambiwa wapeleke mafaili toka Ludewa, Iringa mpaka Hazina Dar es Salaam halafu lirudishwe.

Je, Wizara ina mpango gani wa kuboresha huduma hii ndani ya Wizara za Serikali, maana muda mwangi sana unapotea kwa mtu kusafiri na muda ni fedha?

Nayapongeza pia mashirika binafsi ya mawasiliano kwa kazi kubwa wanayofanya; mashirika kama *VODACOM, CELTEL, TIGO, ZENTAL* na kadhalika; kwa kuelimisha na shughuli za michango ya maendeleo kama elimu/afya. Waendelee hivyo hasa wilaya za pembezoni kwa kaka zangu, Mheshimiwa Profesa Mwalyosi na Mheshimiwa Dr. Mahenge.

Nawashukuru vile vile Vodacom kwa ujenzi wa wodi ya *maternity* pale Ludewa. Mawasiliano kwa njia ya sayansi yanaokoa muda na fedha nyingi sana; utafiti umeonyesha. *Access to Information is deemed crucial to development during this era of a global economy supported by electronic communications.* Changamoto za mawasiliano zinategemeana na *education level location*.

Aidha, makampuni ya simu yaanzishe viwanda vya *handset* hapa nchini badila ya kuagiza nchi za nje; hii itasaidia ajira na kukuza uchumi.

Masomo ya Sayansi na Teknolojia (*theoretically*), yaanze kufundishwa shule za sekondari hata kama vitendea kazi havipo yaanze *theoretically*.

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kuapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri wanayoitekeleza katika Wizara yao.

Mheshimiwa Spika, napenda nichangie katika hoja hii katika nyanja moja ya mawasiliano ya simu za mkononi. Kutokana na utandawazi uliopo, tumefikia kiwango cha juu katika mawasiliano ya simu, lakini tatizo kubwa hasa kwa wananchi wa kipato cha chini ni kutoweza kumudu au kuweza kupata nafasi ya kununua chombo cha mawasiliano (*handset*), ambacho ni ghali kutokana na VAT. Vile vile gharama za muda wa maongezi (*airtime*) ni kubwa sana kutokana na VAT.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Wizara husika iliangalie suala hili, kwa kuhakikisha inawasiliana na mashirika husika ili waweze kupunguza gharama hizo. Mashirika hayo yanapata faida kwa kiwango cha juu sana na kuwakamua wananchi.

Mheshimiwa Spika, nayapongeza mashirika ambayo yameweza kujenga minara katika maeneo mbalimbali mijini na hasa vijijini. Pamoja na juhudhi hizo, lakini bado kwa wananchi wa vijijini, inaonekana wameongezewa mzigo. Kwanza, gharama ya *airtime* ni kubwa sana; hivyo, anapowasiliana na watu wa maeneo mbalimbali kuhusu kilimo au ufugaji anakuwa katika hasara kubwa. Tatizo lingine, simu hizo zinatumia betri ambayo inahitaji kuchajiwa kwa kutumia umeme ambaa haupo.

Mheshimiwa Spika, umeme unahitajika na vijiji ni vingi havina umeme. Je, Wizara ina mkakati gani wa kuyashirikisha mashirika hayo yaweze kupeleka huduma ya umeme hata wa *solar*?

Je, ni lini Wizara italeta sheria ya kuzuia uuzaaji holela wa *SIM Card* ili kuwe na utaratibu mzuri? Naomba jibu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. MZERU O. NIBUKA:** Mheshimiwa Spika, naomba na mimi niungane na wenzangu waliotangulia kuchangia hoja ya Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kuwapongeza Waziri na Naibu wake, kwa umahili wao katika utendaji kazi zao za kila siku, ambaa pia ni watu makini sana katika shughuli zao. Ninaamini watainua kiwango cha uwezo wa uzalishaji katika Wizara hii muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono hoja hii, lakini yako mambo ambayo ningependa aidha kuulizia au kutoa ushauri kwa serikali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, muda wa maongezi wa simu zetu (*air time*), hasa hizi za mgononi ni gharama kubwa mno ukilinganisha na wenzetu nchi za nje kama Uingereza na kadhalika. Ukizingatia kule wenzetu wameshaendelea na vipato vyao ni vikubwa, lakini bei yao ni ya chini mno, ukilinganisha na sisi maskini wa kutupwa.

Mheshimiwa Spika, simu sio kitu cha anasa bali ni uchumi; ni kuharakisha maendeleo. Sasa kwa kadiri gharama zinavyokuwa kubwa, maana yake ni kuwadumaza watu na kuchelewesha maendeleo ya wananchi na taifa zima. Kwanza, gharama zikiwa ndogo watumia huduma wataongezeka na hivyo mapato yataongezeka.

Mheshimiwa Spika, kusamehe kodi kwa makampuni au kuwaongezea muda wa msamaha ni kujichimbia wenyewe kaburi la umaskini. Kama tulifanya hivyo kwa ajili ya kuwavutia wawekezaji, tayari wameshawekeza; hivyo, nashauri hakuna haja tena ya kufanya hivyo kwa vile wao wanatunyonya sana na bado bei yao ipo juu.

Hapa sawasawa na kumtunza mtoto wa mwenzio na kumwacha wa kwako akifa. Sasa huoni ni ujanja au kinyume chake? Halafu Makampuni haya yanachukulia mwanya huo, kubadilisha majina ya Kampuni kwa ujanja kwamba yameuzwa kwa mwekezaji mwingine ili waendelee na msamaha hata baada ya muda wa msamaha wa miaka kumi

kwisha. Hapa lazima serikali ikodolee kwa macho yote mawili, la sivyo, tutaendelea kulala usingizi wakati wenzetu wanaendelea.

Mheshimiwa Spika, utabiri wa hali ya hewa unanipa wasiwas kwa vile mara nyingi tu hauendani na ukweli na hii ni hatari kwa maendeleo. Kwa mfano, wakulima wanaambiwa hizi ni mvua za kupita tu (yaani za muda mfupi), kumbe zikianza ni nzito na hazishi upesi, kitu ambacho wakulima wameacha kupanda kwa kujuia sio mvua za kupanda kumbe ndizo hizo.

Mheshimiwa spika, hapa kuna mifano mingi tu; hata kwa wavuvi na sekta mbalimbali. Jambo la hatari litatokea lakini wananchi hawajui ili wajiandae. Sasa hapa sijui ujenzi ni mdogo au vifaa ni duni?

Naomba mlichunguze kwa undani jambo hili, maana ni muhimu kwa maendeleo ya nchi au kuepusha maafa wakati mwengine.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, naomba majibu kwa yafuatayo:-

(a) Kuongeza minara ya simu kutoka Mgandu kwenda Kujimbo, Kirumbi, Mwamagembe, Kintanula, Rungwa, Kambi Katoto (Chunya). Tunahangaishwa sana na wananchi wa maeneo haya kwamba, wametengwa na wenzao kwa kukosa mawasiliano ya haraka kuwawezesha kuwasiliana na maeneo ya nchi.

(b) Kampuni za *Vodacom*, *Celtel* na *Tigo* zinapata faida lukuki. Naomba wachangie shughuli za maendeleo pale ambapo minara inapita vijijini kama umeme, maji, shule na barabara. Vijiji vya Kamenyanga, Njirii, Gurungu na Sanjaranda, viangaliwe na vipatiwe misaada kama hiyo.

(c) Kampuni ya Posta ipatiwe mtaji wa shilingi bilioni 24 ilizoahidiwa; lilipwe Sh. 8.26 bilioni za pensheni ya wafanyakazi; na ipunguziwe deni lake na ahadi ya kufutiwa madeni yake itimizwe.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Watumishi na Wataalamu wote wa Wizara na Mashirika yaliyo chini ya Wizara, kwa hotuba nzuri na mafanikio makubwa katika mawasiliano ya simu.

Naunga mkono hoja ya Wizara, lakini ningependa kutoa ushauri ufuatao:-

(i) Serikali kuitia Wizara hii ijiepushe na ugonjwa wa *degree* badala ya yale ya ufundi au uwezo wa kuumba vitu kwa mikono. Hata kama Watanzania wote watapata digrii Tanzania haitasonga mbele bila sayansi na teknolojia (ufundi).

(ii) Tunaishi katika ulimwengu wa sayansi na teknolojia, lakini zaidi ya asilimia 70 ya wakulima wetu bado wanatumia jembe la mkono; lini watajitoa katika hali hii?

(iii) Tujenge vyuo vikuu vipywa badala ya kubatiza au kugeuza vyuo vilivyoko kuwa vyuo vikuu (*Mbeya Technical College, Dar es Salaam Technical College, Arusha, Dar es Salaam Business College* na kadhalika). Tanzania inahitaji mabingwa au wanayansi wenyewe digrii, mafundi wa kati na mafundi mchundo (*VETA*), kwa uwiano wa 1:5:45+. Leo tunaua vyuo vya wataalam na wasomi wa kati kwa sababu ya matakwa ya walimu na wanafunzi wa vyuo hivyo badala ya kujali mahitaji ya nchi na wananchi. Serikali inashindwa kupanga mambo na kuzuia mwelekeo wa watu kupata *degree* bila kujuwa inataka kutatua tatizo gani kwa kutoa *degree* hizo. Mwelekeo huu hausaidii nchi.

(iv) Serikali kwa makusudi iamue kujenga vyuo vya ufundi walau chuo cha ufundi kimoja katika kila mkoa. Wahisani hawataki kusaidia eneo hili, wala wananchi hawana uwezo huo. Wananchi waachiwe kujenga shule za sekondari na siyo vyuo vya ufundi. Wahisani pia waombwe kufanya hivyo.

(v) Vyuo vya Ufundu Dar es Salaam, Arusha na Mbeya, vitakiwe kutoa zaidi ya asilimia 70 ya wanafunzi wake kiwango cha kati na asilimia 30 wawe wanafunzi wa *degree* kama ni lazima.

(vi) Nashauri kongamano lifanyike kuhusiana na suala hilo.

(vii) Vijana wanapenda kusoma lakini wengi hawachukui masomo ya sayansi; tufanye nini? Tuwe na mkakati na programu kubwa ya kutatua tatizo hili kama nchi.

(viii) Tuwaombe Wachina, Wajerumani, Wajapani, Waswideni na wengine watujengee vyuo vinne nchini.

(ix) Tutenge fedha kila mwaka kwa ujenzi na vyuo vya ufundi kama tunavyotenga za barabara.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo kwa biashara huria na ushindani, lakini kama nchi ni lazima tuangalie mashirika ambayo yana maslahi na taifa yanalindwa na kusaidiwa kwa makusudi kabisa.

Mheshimiwa Spika, mimi ninayo hofu kubwa sana kwa namna iliyoruhusiwa kusafirisha pesa kuititia njia ya simu, ambayo kwa sasa hutangazwa sana. Je, udhibiti wake ukoje? Je, njia hii haiwezi kuwa ni njia ya kuitisha na kutorosha fedha; na ile sheria yetu ya kudhibiti fedha haramu ina nafasi gani katika kudhibiti usafirishaji huu wa fedha holela?

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nafikiri kwamba, usafirishaji wa fedha ubakie katika mabenki au posta.

Mheshimiwa Spika, najua Shirika la Posta lipo katika ushindani mkubwa sana na kwa jitahada za Wizara na Serikali kulisa idia shirika hili; sasa linaweza kukopesheka;

hivyo ni kuandaa na kupata *overdraft* toka benki kwa kiwango fulani ili kila anayetuma *money fax* yake, basi kituo cha kulipa kimlipe mteja bila usumbufu. Kutohana na uwezo wa Shirika la Posta kuwa mdogo, kumekuwepo na usumbufu; hivyo njia nyingine zimeanza kujitokeza kama hii ya kusafirisha pesa kwa simu.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa pia napenda kushauri kwamba, mawasiliano ya simu ni muhimu. Kama watu tunavyofahamu; ni vyema sasa tuangalie maeneo ambayo hayajaunganishwa kwa simu, kwa mfano, toka Mpanda hadi Sikonge Tabora ni karibu kilomita 320. Njia hii haina namna yoyote ya kupata msaada wa mawasiliano, isipokuwa simu ya Kituo cha Polisi Inyonga.

Mheshimiwa Spika, Inyonga ni eneo muhimu sana kwa maana ya mahali ilipo, kuna harakati nyingi za kibiashara kati ya Mpanda na Tabora hivyo ipo haja ya makusudi kupelekwa kwa huduma hiyo katika Kijiji cha Inyonga, Tarafa ya Inyonga, Jimbo la Mpanda Mashariki.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILINGATI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kutoa pongezi kwa kazi nzuri na hotuba nzuri ya bajeti inayoleta matumaini.

Pamoja na pongezi hizi, ninayo maoni na ushauri katika mambo yafuatayo:-

(a) Kupanua mtandao wa simu za mkononi Manyoni. Maeneo mengi ya Manyoni Mashariki, wananchi tayari wanazo simu (*handsets*), lakini mawasiliano hakuna. Hali ni mbaya katika Tarafa ya Nkonko hususan maeneo ya Sanza, Nkonko, Heka na Chikola.

Maeneo yote hayo yamewahi kutembelewa na Naibu Waziri wa Wizara hii, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari. Alifanya mikutano ya hadhara kila sehemu, ambayo ilihudhuriwa na watu wengi na wengi wao wakiwa na simu za mkononi ila mawasiliano hakuna hadi waende Mjini Manyoni.

Mheshimiwa Naibu Waziri, aliahidi kuyashawishi makampuni ya simu waje kujenga minara ili mawasiliano yapatikane, lakini tangu wakati wa ziara hiyo, mwaka mmoja umepita bila kuona hatua.

Aidha, mwezi Mei, 2008, Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, alipotembelea maeneo hayo alipata kilio hicho, naye aliahidi kuyafanyia kazi maombi hayo. Baada ya ziara, alikutana na baadhi ya makampuni ya simu (*Vodacom, Zain* na *TTCL*) na aliwaeleza kuwapo kwa soko la biashara hii. Wananchi wanasubiri matunda ya jitihada hizi.

Kwa hiyo, napenda kuiomba Wizara iyakumbushe na kuyahimiza makampuni haya ili walete huduma hii, wateja wapo na wengi zaidi watatumia mawasiliano hayo yatakapoletwa.

(b) Napongeza hatua inayoandaliwa na Wizara kuhusu kuanzisha mtambo wa *Central Equipment Identification Register (CEIR)*, ili kudhibiti matumizi mabaya ya simu za mikononi.

Wakati Wizara inatekeleza kazi hii ni vizuri ishirikiane na wataalam wa kudhibiti makosa yanayohusika na teknolojia ya kisasa (*cyber crime*) ili kuwadhibiti wakati wanapotumia simu za mikononi.

Mwisho, narudia tena kuishukuru Wizara kwa mwelekeo na mwanzo mzuri katika kulihudumia taifa letu.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Prof. Peter Msolla, Waziri wa Wizara hii, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Naibu Waziri wa Wizara hii, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Wataalamu mbalimbali, kwa kazi nzuri wanayofanya na kwa kuandaa hotuba nzuri, ambayo ninaamini ikitekelezwa ipasavyo, nchi yetu itapiga hatua kubwa katika sayansi na maendeleo ya mawasiliano na teknolojia.

Pili, huduma mbovu za upatikanaji wa fedha katika Posta ya Korogwe kutokana na fedha chache zinazotolewa kwa Posta ya Korogwe. Upo usumbufu wa muda mrefu wa kukosekana fedha za kutosheleza kuwapatia wateja waliotumiwa fedha zao. Mji wa Korogwe una shule nyingi za sekondari, mfano, Korogwe Girls Secondary School. Shule hii ni ya bweni na ina wanafunzi zaidi ya 1000 kuanzia *form one* hadi *form four*.

Korogwe kuna Chuo cha Ualimu, kuna Chuo cha Uuguzi na taasisi mbalimbali, mfano ya Malaria ya Kanda. Sekondari za Mjini Korogwe zaidi ya tano. Wanafunzi na wafanyakazi mbalimbali, wanatumiwa fedha na familia, ndugu na jamaa. Kwa hiyo, huduma ya Posta Korogwe kuwa na fedha za kutosha kukidhi haja ya kulipa wanafunzi hawa ni muhimu sana.

Ni jambo la kusikitisha sana kwa wanafunzi na wananchi wa Korogwe kushinda Posta kusubiri fedha au kuambiwa fedha zimekwisha. Jambo hili ni tatizo sugu na la muda mrefu. Ninaomba sasa nipatiwe jibu la kudumu. Ninaomba wananchi wa Korogwe wahakikishiwe jibu la kudumu.

Gharama za simu za mikononi *Vodacom, Tigo, Zain* na *Zantel* ni ghali sana. Hali hii ikiachiwa kuendelea hivi hivi huduma hizi wananchi watashindwa kabisa kuzitumia. Ni lazima tukubali kwamba, kwa maendeleo ya dunia ya leo, huduma hii ya simu imesaidia sana kufanya wananchi waweze kuwasiliana kwa urahisi. Aidha, pia tija kwa wananchi imeongezeka kwa kupunguza gharama za usafiri. Ninashauri sana Wizara ijitahidi kumaliza mkongo ya taifa ili pawepo uwezekano wa kupunguza gharama.

Minara mbalimbali ya simu kusambaa nchi nzima. Hali hii sio nzuri, ningeomba kushauri Wizara iyashauri makampuni haya ya simu za mkononi kuweka minara yao katika eneo moja badala ya kusambaza minara nchi nzima.

Mfano ni Mji wa Korogwe; Mji huu peke yake una minara 12. Huu ni uharibifu wa mazingira na kuharibu mandhari ya Mji; inashindikanaje kuwa na *centres* mbili au tatu tu? Ninashauri suala hili lipatiwe ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, kwa mazingira ya dunia ya leo ni lazima kuwe na mtaalamu Somo la *IT* mashulenii kuanzia darasa la kwanza hadi juu. Teknolojia ya leo, bila wanafunzi wetu kuelewa kutumia *computer* tutakuwa tumepitwa na wakati. Ninapenda kusisitiza suala hili lipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii muhimu sana.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, kwa hotuba yenye mlolongo mzuri.

Mchango wangu utakuwa hasa kwene mawasiliano ya simu. Kwanza, napenda binafsi nimshukuru Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, ambaye amekuwa msaada mkubwa katika jimbo langu kila nilipomwomba kupata huduma za mtandao wa simu. Asilimia 75 ya eneo la Wilaya yangu tunawasiliana kwa simu.

Ombi langu ni Kata mbili ambazo zimesalia na kuongeza ufanisi sehemu tatu katika Vijiji vya Idete na Namwawala (Kata ya Idete). Kata ambazo zimesalia ni Kata ya Taweta – Vijiji vya Ipinde, Taweta na Tanganyika; Kata ya Uchindile – Vijiji vya Udundile na Kidete; Kata ya Utengule – Vijiji vya Utengule na Ngalimila; na Kata ya Idete - Vijiji vya Idete, Namwawala na Kisegese.

Kwa vile katika Kijiji cha Namwawala kuna mpango wa kujenga kiwanda kipyaa cha sukari katika Bonde la Mto Ruipa, uwekezaji katika eneo hilo utakuwa na manufaa makubwa kwa makampuni ya simu.

Mnara wa *Celtel* umejengwa muda mrefu katika Kijiji cha Mpanga, Kata ya Utengule, lakini mpaka hivi leo haujazinduliwa. Wananchi wanaiomba Kampuni ya Celtel iwafungulie huduma hiyo.

**MHE. MATHIAS M. CHIKAWE:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na Watumishi wote wa Wizara hii, kwa bajeti nzuri, iliyowasilishwa vizuri sana.

Naomba kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri, kwa kuwasilisha ombi moja tu kwa Mheshimiwa Waziri. Kule Nachingwea katika Tarafa ya Kilimarando, zipo Kata nne za Mbindo, kilimarondo, Matekwe na Kiegei, ambazo hazipati kabisa huduma ya simu za mkononi. Wakazi wa Tarafa hii ni wakulima wazuri sana wa korosho, ambao wana uwezo wa kununua na kuhudumia simu za mkononi.

Tafadhali sana, naomba Mheshimiwa waziri, ayashawishi makampuni ya simu yaweke minara yake Kilimarando, wananchi wa kule waanze kupata huduma zao na kufaidi matunda ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza kwa dhati kabisa, Mheshimiwa Prof. Peter M. Msolla, Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, kwa hotuba yake nzuri sana, yenye maelezo ya wazi na aliyoisoma kwa ufanisi. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Kwa upande mwengine, nawapongeza sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Katibu Mkuu, Dr. Naomi Katunzi, Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi chini ya Wizara hii na Wafanyakazi wote, kwa mshikamano na ushirikiano wa dhati ambao umemuwezesha Waziri kuwasilisha Bungeni hotuba hii nzuri. Hongereni sana.

Hata hivyo, ninalo suala moja tu ambalo ninaomba litolewe maelezo, nalo ni kuhusu *Celtel* kufikisha masafa ya simu katika Tarafa ya Mgwash, Jimbo la Bumbuli – Lushoto. Ahadi ya kutekeleza hili ilitolewa na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, tarehe 14 Juni, 2007 wakati akiijibu swalı langu Na. 23 kuhusu huduma za mawasiliano ya simu za *Celtel* (*Zain* sasa). Nanukuu Taarifa Rasmi ya Bunge (*Hansard* ya tarehe 14 Juni, 2007): “*Celtel...* ina mpango wa kufikisha huduma zake katika Tarafa ya Mgwash ifikapo mwezi Juni, 2008 ili Wananchi wa Tarafa hiyo waweze kunufaika na huduma za *Celtel*.” Hadi tarehe 15 Agosti, 2008, yaani leo, bado wananchi hao hawajafikishiwa huduma hii.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuyapongeza mashirika yenye kutoa huduma ya simu za mkononi, lakini bado kuna sehemu nyingi hasa vijijini, huduma hii haijafika na kama imefika bado mawasiliano ni mabovu sana. Kunahitaji minara zaidi katika huduma hizi za simu za mkononi. Kunakuwepo na uholela wa kuuza *line* za simu hizi, matokeo yake watu wanunua *line* hizo na wanazitumia vibaya kuwapigia watu wengine na kuwatukana.

Nashauri iwekwe *system*; hakuna mteja yejote kuuziwa *line* ya simu (*Sim Card*) bila kuwa na kitambulisho cha uhakika, kikiambatana na barua ya kijiji na ikiwezekana watu wanunue *card* kutoka kwenye maeneo yao ambako wakitoa vitambulisho watajulikana. Kwa njia hii, wale wenye kununua *line* hizo na kuzitumia vibaya watajulikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, bei za simu za mkononi ni ghali sana, wakati mitambo yote ipo kwenye *satellite*. Ni sababu zipi zinafanya bei hizi kuwa ghali kiasi hicho? Kampuni za simu *zicharge* kwa dakika na mtu ajue ametumia kiasi gani kama nchi za Ulaya zifanyavyo. Mtu unajua umetumia kiasi gani. Isipofanyika hivi na maisha yamekuwa ghali sana badala ya kuwa kitu cha maendeleo badala yake itakuwa hizi simu ni kichocheo cha kuzidisha umaskini na wasichana wenye simu kwa sababu hawawezi kununua vocha, itabidi warubuniwe na hizi vocha mwisho tunarudi pale pale, madhara ya UKIMWI na kadhalika.

Nchi zote duniani kwa sasa hivi, yaani dunia ya leo zinatumia *computer* kwa kazi zake zote. Tukizingatia matumizi ya *computer* yanahitaji umeme na sehemu nyingi Tanzania hasa vijijini mpaka wa leo bado umeme haujafika na hata kama upo ni mdogo, hauna nguvu ya kuwasha *computer*.

Hivyo, hapa kuna changamoto kubwa kwa nchi yetu katika matumizi haya ya *computer*. Kuna haja ya serikali kuhakikisha kuharakisha upatikanaji wa umeme wa uhakika ili nchi yetu iweze kuwa katika teknolojia hii.

Vile vile serikali iangalie ni jinsi gani ya kuongeza wanafunzi wa sayansi, kwa kuwapa motisha zaidi hata wakipata *Division III* kuendelezwa, ukizingatia tuna uhaba sana ya wanasayansi tena hawa watafiti.

Huu ni wakati muafaka sasa kwa serikali kuangalia ni jinsi gani Shirika la Posta litakuwa na *address* zenye jina la barabara, itasaidia kutambua *address* za watu na pia tukiwa tumeingia kwenye *database information* ya mtu ni rahisi kujulikana kila mtu alipo.

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja na pia niwapongeze Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, kwa kazi nzuri ya maandalizi ya bajeti hii, pamoja na kuwa Wizara hii bado ni changa.

Mheshimiwa Spika, makampuni mengi hapa nchini yakiwemo ya simu na hoteli, yamekuwa yakibadilisha majina yao baada ya miaka michache yanapoanzishwa. Hivi katika mikataba, makampuni huruhusiwa kubadilisha majina mara ngapi na baada ya kipindi gani?

Mheshimiwa Spika, Waziri haoni kuwa kubadilibadili kwa majini ya makampuni haya ni moja ya njia ya kukwepa kulipa kodi na pia kuleta usumbufu kwa wateja wake? Serikali inasema nini kwa Kampuni ya *CELTEL* kubadilisha jina na kuwa Zain na Kampuni ya Simu ya Mobitel ambayo hadi sasa imebadilisha majina yake mara tatu (Mobitel, Buzz na sasa Tigo)? Serikali imepata faida au hasara gani kwa makampuni haya kubadilisha majina yake katika kipindi kifupi tangu kuanzishwa?

Mheshimiwa Spika, kuna majengo yaliyojengwa na hayakuwahi kutumika huko Upenja, Mkoa wa Kaskazini Unguja. Majengo haya yalijengwa na lililokuwa Shirika la Posta na Simu Tanzania.

Baada ya Shirika hilo kuachanishwa, naamini kuwa, majengo hayo ni mali ya Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL*). Kwa kuwa majengo hayo hayajawahi kutumika na wala hakuna dalili ya kutumiwa hadi sasa; je, serikali ina mkakati gani wa majengo hayo ambayo yanazidi kuharibika?

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza kwa dhati serikali, kwa hatua iliyodhamiria kuichukua ya kudhibiti matumizi mabaya ya simu za kiganjani kwa kuanzisha *CEIR* kwenye mitambo yote ya simu Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, wasiwasи wangu ni vipi wananchi wa vijijini watakavyoweza kufikiwa ili kupatiwa huduma ya kuwaelimisha taratibu zitakazohitajika kufuatwa wakati mwananchi huyo anaponunua *Sim Card*? Aidha, suala la kuwa mtu na kitambulisho nalo linahitaji ufanuzi kwani kuna vitambulisho vya aina nyingi kwa baadhi ya wananchi wetu. Sasa nataka nifahamishwe ni kitambulisho gani hasa kitakachotumika wakati mteja wa simu anapojiandikisha kununua *Sim Card*; na je, kutakuwa na kiwango au idadi maalum ya *Sim Cards* ambazo mtu mmoja atakuwa nazo?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa taasisi zilizoko chini ya Wizara, hasa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (*DIT*) na ile cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (*MIST*), ndiyo wakombozi wetu; Serikali izitengee fedha za kutosha ili ziweze kufanya tafiti zake kama zilivyojipangia ili kuviwezesha kutoa *products* za matokeo ya tafiti ambazo zitazalishwa kwenye viwanda vyetu hapa nchini, ambavyo vitasaidia katika nyanja mbalimbali za uzalishaji kama vile mashine za kilimo, vinu vya umeme, taa za barabarani, majiko yanayotumia mionzi ya jua na kadhalika. Fedha inayotengwa kwa sasa, hazikidhi haja hata kwa taasisi moja. Hakuna lisilowezekana panapo nia.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na kuunga mkono hoja kwa mara nyingine.

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninapenda kuunga mkono hoja hii ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchukua fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Prof. Msolla, kwa hotuba yake nzuri. Vile vile nampongeza Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, kwa kuonyesha uwezo mkubwa katika kazi zake na kwa kumsaidia Waziri kwa upeo mkubwa. Aidha, napenda kumpongeza Katibu Mkuu wa Wizara hii, pamoa na Watendaji wote ambao kwa namna moja au nyingine, walihusika katika uandaaji wa Bajeti hii ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Nanyumbu ni mpya baada ya kuigawa Wilaya ya Masasi, kwa maana hiyo haina Posta. Wananchi wa Wilaya ya Nanyumbau, tunategemea kupata huduma za posta katika Posta ya Masasi Mjini. Mathalani, kutoka Lumesule Kijiji kilichopo mpakani na Tunduru ni kama kilomita 80 kufika Masasi Mjini na kama kilomita 120 kufika Tunduru Mjini. Kutokana na hali hii, Wananchi wa Nanyumbu tunapata tabu sana katika kupata huduma za posta.

Hivyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, aliagize Shirika la Posta litujengee Posta pale Mangaka, ambapo ni Makao Makuu ya Wilaya ya Nanyumbu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuyapongeza makampuni ya simu za mkononi kwani yamejitahidi kwa kiasi Fulani, kusambaza huduma kwa kujenga minara kwenye maeneo mbalimbali Wilayani Nanyumbu. Hata hivyo, kuna maeneo mengi Wilayani hayana huduma hizi. Ninaomba kuititia Wizara hii, kuyaomba makampuni haya yajenge minara katika Kata za Napacho, Chupuputa, Lumesule na Mkonona.

Mheshimiwa Spika, niliwahi kumwandikia Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii, kuchukua hatua kwa Kampuni ya Simu ya Tigo, kwani wamejenga minara katika Vijiji vya Chungu katika Kata ya Nanyumbu na Mtambaswala katika Kata ya Masuguru, bila ridhaa ya Uongozi wa Vijiji husika. Mpaka sasa sijapata taarifa ya jibu la kutoka *TIGO*. Hili ni jambo ambalo wananchi wa vijiji husika wanahoji na kutaka taarifa. Hivyo, ninaiomba Wizara, itakapofanya majumuisho inipe ufanuzi wa ujenzi wa Posta Mangaka, ambapo ni Makao Makuu ya Wilaya ya Nanyumbu; na ujenzi wa minara uliofanywa na Kampuni ya *Tigo* katika Vijiji vya Chungu na Mtambaswala bila idhini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuunga mkono hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii. Wizara hii ni mpya, lakini kutokana na mwelekeo wa bajeti hii na kama mambo yote yaliyoandikwa kwenye kitabu yakitekelezwa, kuna uwezekano mkubwa wa Wizara hii kuweza kuleta ufanisi mkubwa na maendeleo ya nchi yanaweza kupatikana.

Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia hotuba hii kwa kuzungumzia suala la ofisi/jengo la *TTCL* la Kibiti. Jengo hili ambalo wamelikodi ni dogo sana, kiasi cha kushindwa hata watu watatu kuweza kuhudumiwa kwa wakati. Ni vizuri sana, kama kuna uwezekano, shirika hili liweze kujenga jengo lake ambalo litakuwa ni kubwa. Kwa kufanya hivyo, kunaweza kuvutia wawekezaji.

Suala la pili ni kukosekana kwa mawasiliano katika baadhi ya maeneo kwenye Jimbo la Rufiji. Maeneo hayo ni yale ya Delta (Tarafa ya Mbweri). Nayaomba mashirika haya ya *TIGO*, *ZAIN* au *VODACO* M waende wakaangalie uwezekano wa kujenga mnara katika Vijiji vya Mtanga au Ruma. Vijiji hivi viro kilomita 19 toka Muhoro/Rufiji na vinafikika bila matatizo yoyote kwa kutumia gari. Mnara huo utaleta mawasiliano mazuri sana eneo hilo ambalo lina wateja wengi.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine linalotakiwa kupelekewa huduma hiyo ni Kata ya Mahege katika Kijiji cha Kivinja A. Kuweka mnara eneo hilo, kutasaidia sana kuboresha mawasiliano katika maeneo hayo ambayo pia yana wateja wengi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuitumia nafasi hii, kwa njia ya maandishi, kuwapongeza Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Prof. Peter Mahamud Msolla, Naibu Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji wote, walioshiriki kuandaa bajeti hii mahiri yenyewe mwelekeo wa kuboresha Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza kipekee Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Naibu Waziri, kwa jithada zake kubwa katika Wizara hii, ambayo ameitumikia kwa muda mrefu sasa. Nazitambua juhudzi za kufanya ziara mikoani, ukiwemo Mkoa wa Singida na kufanikisha huduma nydingi ikiwemo simu za viganjani.

Mheshimiwa Spika, juhudzi za Mheshimiwa Dr. Maua Daftari ni nydingi sana, pamoja na uwezo mkubwa wa kujibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Ningekuwa na nafasi ya kumshauri Mheshimiwa Rais, anapoteua Baraza lake la Mawaziri, ningemshauri ampe Wizara yake kuiongoza kwani uwezo wake ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizi, ninawatachia kheri katika kutekeleza yote waliyoyaainisha katika hotuba hii. Mwenyezi Mungu, awaties nguvu, afya, uwezo na mshikamano, waweze kufikia malengo yao. Napenda kukiri kuwa, ninaunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, ninaendelea kutambua juhudzi za serikali, juu ya usambazaji wa simu za viganjani Mkoani Singida. Hivyo basi ni maeneo machache sana ambayo yamebaki nayo ni Wilaya ya Iramba, Tarafa ya Kirumi, Kata ya Tulya, Kata ya Urughu, Wilaya ya Manyoni Kata ya Sanza, Kata ya Rungwa na Kata ya Iseke.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba sana serikali ijitahidi kupeleka mawasiliano ya viganjani maeneo haya. Nitashukuru endapo Waziri atatupa matumaini tutapata lini, ili wana-Singida ambao wanaendelea na harakati ya kutafuta maendeleo wapate mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, napenda kukiri huduma nzuri iliyokuwa inatolewa na TTCL miaka mingi iliyopita, lakini huduma hiyo sasa inashuka kwa kiasi kikubwa. Baada ya kufanya utafiti, nimegundua kinachochelewesha au kushusha huduma ya Shirika la Simu ni Teknolojia yake kupitwa na wakati.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri serikali kuboresha huduma hii ili iende na wakati kwa kubadili huduma yake kutumia teknolojia ya sasa; mfano, *money fax* iwe kama zinavyofanya benki zetu, kwani wakati mwingi mteja husubiri fedha zikusanywe ndipo apewe fedha alizotumiwa na ndugu yake. Vile vile uzalishaji wake ni mdogo sana baada ya simu za viganjani kuwa nydingi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sasa kuna simu za *TTCL* za viganjani, ninaiomba serikali kupeleka simu hizi hadi vijijini, pamoja na vocha zake.

Mheshimiwa Spika, ninakiri kuwa, wataalamu wa fani ya sayansi ni wachache sana, kwa sababu wanafunzi au wanachuo wengi hawachukui masomo ya sayansi, kwa sababu walimu wapo wachache sana, pia michepuo ipo michache nchini.

Vile vile wataalam hawa wanapohitimu na kupata ajira, mishahara yao bado midogo sana kulingana na gharama kubwa wanazotumia kusomea fani hii. Ninaishauri serikali, kuongeza mishahara ya wataalam wa fani hii, pamoja na marupurupu ili kuwavuta wengi wasomee fani ya sayansi. Ninategemea wakati wa majumuisho, Mheshimiwa Waziri, atatoa maelezo yenye kuwatia moyo wataalam wa fani ya sayansi.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wanafurahia sana huduma inayotolewa na makampuni mbalimbali ya simu za viganjani zikiwemo *Celtel* (*Zain*), *Vodacom*, *Tigo*, *Zantel*, *TTCL* na kadhalika. Tatizo ambalo wateja wengi wanalizungumza kila mara ni gharama za juu za matumizi karibu kwa simu nydingi, ingawa *Tigo* kwa kupitia *Extreme* kuna unafuu sana. Ninaiomba serikali, ambayo ndiyo yenye mamlaka, iyashauri makampuni haya kupunguza gharama ili wateja wengi waweze kumudu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudhi za mashirika haya kupeleka huduma ya simu za viganjani hadi vijijini, bado kuna tatizo la *network* kukosekana baadhi ya maeneo; mfano, mabondeni, nyumba zenye ghorofa *groundfloor* ni tabu. Ninayashauri makampuni haya, kuangalia tatizo ambalo linafanya *network* kukosekana baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuipongeza sana Wizara hii, kwa jinsi ambavyo inatekeleza kwa vitendo kupambana na Ugonjwa wa UKIMWI. Hotuba imeonyesha jinsi ambavyo huadhimisha siku hii kila mwaka, vile vite hutoa ajira siku hiyo ya maadhimisho. Napenda kufahamu ajira hizo hutolewa kwa waathirika au kwa watu wote. Nitashukuru Mheshimiwa Waziri, wakati wa majumuisho yake akitoa maelezo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ugonjwa huu asilimia kubwa hupatikana kwa njia ya zinaa; na kwa kuwa wapenzi wengi huwasiliana kwa njia ya simu; na kwa kuwa kila simu kumi anazopiga mtu lazima moja hadi tatu ni za mapenzi; ninaiomba serikali iyashawishi mashirika yote kutoa elimu kwa njia ya *message* kama wanavyofanya *Tigo* kwa baadhi ya mambo tena itolewe bure. Mheshimiwa Waziri, atoe ufanuzi.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango wangu ambao nategemea kabisa Waziri atatoa ufanuzi wakati wa majumuisho yake, napenda kurudia tena kuwa, ninaunga mkono hoja hii mia kwa mia.

**MHE. MANJU S. MSAMBYA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, natamka kuwa, naunga mkono hoja. Katika mchango wangu wa maandishi, nitazunguzia maeneo yafuatayo:-

Napenda niishukuru sana Wizara kwa juhudzi za kutendaza huduma ya simu za mgononi nchini. Huduma hii pia imetandazwa Mashariki mwa Jimbo la Kigoma Kusini.

Nashukuru maeneo ya Nguruka, Mtegowanoti, Mganza, Uvinza na Kandaga, kupatiwa huduma ya karibu toka Zain, Tigo na Vodacom. Hata hivyo, napenda nieleze masikitiko yangu kwa jinsi ambavyo huduma hii imetolewa kwa eneo dogo sana karibu. Karibu robo tatu ya eneo la Kigoma Kusini, haipati huduma ya mawasiliano ya simu hizi.

Maeneo ya mwambao wa Ziwa Tanganyika, kusini mwa Mkoa wa Kigoma yametelekezwa. Eneo hili lina shughuli nyingi za kiuchumi ambazo kama zingepewa nguvu kuitia kuwepo mawasiliano ya simu za mgononi; maeneo ya kuanzia Kata za Sunuka, Sigunga, Igalula, Buhingu na Kalya yanajishughulisha na shughuli za kilimo, uvuvi, utalii (Mbuga ya Mahale), usafiri na usafirishaji hususan majini. Maeneo haya kwa bahati mbaya sana yanatengwa, pengine kwa makusudi katika nyanja ya mawasiliano. Pamoja na uzalishaji mkubwa uliopo, tunasikitika mawasiliano ya simu za mgononi hayapo.

Kutokana na hali ilivyo sasa, pamoja na kuwa nilikwishaandikia Wizara na Makampuni kuhusu adha yetu hii, nachukua fursa hii, kuitia mchango huu wa maandishi, kuomba Wizara iyahimize makampuni ya simu za mgononi ili yatazame upande wa Kigoma Kusini, mwambao wa Ziwa Tanganyika.

Napenda niihakikishie Wizara kuwa, huduma hii haitayapa hasara makampuni haya. Wateja wa kutosha wapo na watumiaji wa kutosha kuleta tija kwa makampuni wapo sana. Naamini, Wizara itayaelekeza makampuni haya kwenda huko, kwani huko serikali itakuwa inaimarisha ulinzi, huduma za jamii kama vile elimu, afya na kadhalika.

Michango ya wachangiaji kadhaa hususan Mheshimiwa Mwananzila, kuhusu huduma ya Shirika la Posta, naiunga mkono. Kwa bahati, mimi nimekuwa muajiriwa wa Shirika la Posta na Simu Tanzania, nikiwa nimetokea Shirika la Reli la Afrika Mashariki kabla ya 1997.

Kwa hiyo, naelewa umuhimu wa huduma za Shirika hili. Hata hivyo, naomba sana Wizara iliangularie Shirika lipeleke huduma vijiji na hasa wale wa Kigoma Kusini. Naiomba sana tupatiwe huduma za usafirishaji wa barua na vifurushi.

Pamoja na yote hayo, napendekeza Wizara isimamie upatikanaji wa mtaji kwa Shirika hili. Napenda ifahamike kuwa, Shirika hili linapambana na ushindani mkubwa. Hivyo, kupewa nguvu kifedha ni muhimu ili liweze kutoa huduma maridhawa. Matarajio

ya Watanzania ni kuona shirika hili linasimamiwa ili hapo litakapowezeshwa, lijiendeshe kibashara na kihuduma.

Napenda niiombe serikali, itupe maelezo ni kwa namna gani inaondoa mgogoro wa kiuongozi unaofukuta katika Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL*). Inashangaza kusikia kuwa, kampuni iliyokabidhiwa kuendesha kampuni hii, inawalaumu wataalam wazalendo eti kwa nini wameweza kuiingiza kampuni kwenye biashara ya simu za mkononi. Mbaya zaidi, waendeshaji hawa wageni wanadiriki hata kutoa tuhuma kuwa, hawa wataalam wazalendo wanakwamisha upatikanaji wa mikopo ya kuiendesha kampuni.

Mimi nilidhani kuwa, kampuni hii itakuwa imekuja na mikakati ya kupata fedha za kuendesha kampuni. Vinginevyo, kutakuwa hakuna haja ya kuingiza utaalamu wao.

Naomba Wizara ituletee maelezo ya hali ya uongozi *TTCL*.

**MHE. ALHAJ DR. JUMA A. NGASONGWA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa afya na uwezo wa kufika hapa Bungeni leo na kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

Nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara, kwa kuiandaa vizuri sana hotuba hii.

Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Mawasiliano ni nyenzo muhimu sana kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya nchi yetu; hivyo, tunapaswa tuyape kipaumbele. Mkazo katika kupanua matumizi ya simu za kiganjani ni sahihi.

Mfuko wa Mawasiliano sasa uanze na upewe fedha za kutosha, vinginevyo *the urban bias* katika matumizi ya simu za mkononi, utakuwa wa kudumu.

Lakini ili tufikie lengo hili, lazima sasa tuiimarishe *TTCL* kwa kuingia katika teknolojia za kisasa, pamoja na ya simu za kiganjani. Ndoa kati ya *TTCL* na Huawei ni nzuri.

Kampuni hii ya Kichina, ina ujuzi na uzoefu mkubwa katika eneo hili la **TEKNOHAMA**. Tukichangamkia hili, tunaweza kupiga hatua kubwa, pamoja na kuipa uwezo mkubwa *TTCL*.

Suala la Mkongo wa Taifa, pamoja na Mradi *EASSY Cable*, lipewe kipaumbele. Matumizi ya *Optic Fibre* ni mkombozi, kama tunataka kushusha gharama na bei za simu za kiganjani. Gharama za juu za huduma hii ni kikwazo katika kueneza huduma hii nchini hasa vijijini.

Suala la *R & D* sasa lipewe kipaumbele. Ilani ya CCM imeelekeza kuwa, ifikapo 2020 tuwe na kiwango cha asilimia moja ya Pato la Taifa itumike kwa *R & D*.

Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia bila uwekezaji mkubwa, haitafikia viwango vinavyostahili.

Juhudi za *e-government* ni muafaka. Tuendelee na juhudi za kushirikiana na *CILICORP* na *IBM* kupitia Dr. Leunard Tenende (*leunard.tenende@cilicorp.com*), pamoja na Dr. Mark Dean, Vice President wa *IMB*.

Mradi huu aliuanzisha Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Kikwete na kuratibiwa na *MPEE*. Nakuomba Mheshimiwa Waziri, uendeleze juhudi hizi.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Spika, Kwimba kama Wilaya, inatajwa mara moja tu katika kitabu chote cha bajeti.

Bajeti hii itapitishwa bila wasiwas. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, akubali kuja hadi Kwimba aitembelee Tarafa ya Mwanashimba, ashuhudie wananchi wanavyosukumana mitini kupata mitandao.

Ziara yake imfikishe hadi Ngudu kwenye Ofisi za Posta na Kampuni ya Simu. Akiyaona hayo, nitakachokuwa ninamwomba atakuwa anakielewa; hasa akiitembelea Magu na Misungwi, Wilaya mpya zilizotokana na Kwimba (Wilaya Kongwe).

Mheshimiwa Spika, ninawatachia kheri.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wa Wizara.

Naipongeza Wizara kwa utendaji. Naomba yafuatayo Waziri anisaidie kwa wawekezaji wa makampuni ya simu za mikononi:-

Nawaomba wawekezaji watoe huduma ya simu kwa maeneo ya Kata za Ntwike, Tulya na Mtekeute, kwani ndizo Kata pekee ambazo hazina mawasiliano ndani ya jimbo langu.

Naomba Mheshimiwa Waziri, ayahamashe makampuni ya *Vodacom*, *Zain*, *Tigo* na *Zantel*, kwani idadi ya wateja inatosheleza sehemu hizo.

Kampuni ya Vodacom kutotimiza ahadi ya mkataba na Kijiji cha Nguvu Mali au Ndago kwa kushindwa kulipa gharama za eneo la ardhi inayomilikiwa na kijiji walikowekeza mnara, eneo la Magila, gharama za kila mwezi.

Naomba Mheshimiwa Waziri, anisaidie walipe deni lao. Kadhalika, Zain zamani *Celtel*, nayo ilipe deni la mwaka 2006/2007 Kijiji cha Mselembwe na Mseko, ikiwa gharama ya kuwekeza mnara kati ya vijiji hivyo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Kabla hatujaendelea na shughuli zetu, napenda kuwafahamisha kuwa Mheshimiwa Mabina amefiwa na kaka yake na ameruhusiwa kwenda kufanya maandalizi ya mazishi.

Tulipomaliza Siku ya Ijumaa tulikuwa tumemaliza wachangiaji wote walioorodheshwa, walikuwa wamechangia na tukasema tutaanza na Mawaziri kuanza kujibu hoja zenu. Kwa hiyo, kwanza nitamwita Mheshimiwa Naibu Waziri, halafu Waziri mhusika mtoa hoja.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kuchangia hoja iliyoko mbele yetu leo hii. Namshukuru Mwenyezi Mungu kutujalia uzima na afya njema na leo hii tuko hapa kujadili hoja yetu ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Napenda kwanza nimshukuru Rais wangu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kunithea nimsaidie katika Wizara hii. Naahidi kama ilivyo kawaida yangu nitajitahidi kwa nguvu zangu zote kwa uwezo na maarifa kuona natekeleza majukumu yangu ipasavyo na namwomba Mwenyezi Mungu anisaidie. Aidha nampongeza Mheshimiwa Mizengo Pinda kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri Mkuu, uwezo na juhudi zake umekamilika. Naahidi kumpa ushirikiano wa dhati. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana kipindi kama hiki cha bajeti na siku kama leo ya bajeti yangu nilipokuwa Wizara ya Miundombinu nilibahatika kupata *support* na busara za marehemu mume wangu. Namshukuru Mola kwa kunipa moyo na stahamili kuhimili kifo chake na namwomba *Allah* aiweke roho yake mahali pema peponi. (*Amin*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru ndugu zangu, Viongozi wangu wakuu wote, Waheshimiwa Wabunge wote na wapendwa wote kwa kushiriki kikamilifu katika maziko na hatimaye arobaini ya mume wangu. Nawashukuru wote walionifariji kwa kunitembelea, kunipigia simu na kuniletea barua. Lakini shukrani za pekee ziwaendee familia yangu kwa mshikamano wao, mapenzi yao na kwa kunifariji. Napenda nimshukuru Waziri wangu Professa Peter Msolla kwa ushirikiano, mawazo na miongozo mbalimbali anayonipa ya kunisaidia utekelezaji wa majukumu yangu. Aidha, sitoweza kumsahau Katibu Mkuu wangu na Wakurugenzi wote wa Wizara, viongozi mbalimbali wa Taasisi na vyuo vilivyo chini ya Wizara hii na wafanyakazi wote.

Nakiri muda mfupi nilioanza kufanya kazi nao nimepata msaada wa kutosha kutoka kwao, nimejifunza mengi sana kwa muda huu mfupi na naamini hawatosita kuendelea kuniruhusu niendelee kuchota hazina ya busara, elimu na mawazo yao mazuri ya kuendeleza Wizara yetu. Umoja wao na mshikamano wao ni nguvu tosha ya kuturusha na kutufanya tusonge mbele. Kazi iliyoko mbele yetu ina changamoto nydingi ambazo bila ya umoja na mshikamano hatuwezi kuzikamilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Spika, Wenyeviti wote na hasa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuendelea kushirikiana nami katika kusukuma kero za wapiga kura wao zinazotokana na sekta zilizo chini ya Wizara yetu na kuona zinapata ufumbuzi ipasavyo. Naamini Waheshimiwa Wabunge wote

watakulaliana nami kuwa kwa namna moja au nyingine tumeweza angalau kwa kiasi fulani kukidhi kiu ya shida zao katika mawasiliano yao angalau kwa asilimia fulani. Mimi naamini kwamba kero zao ni kero zangu na daima nitakuwa tayari kuwapa msaada wangu.

Tuko katika karne ya 21, karne ya Sayansi na Teknolojia, karne ambayo haimsubiri mtu, karne ambaye inatutaka tukimbie badala ya kutembea, karne inayohitaji mbinu mpya za kisasa za kufanya kazi. Karne hii na zinazokuja mbele ni karne ambazo hazina huruma katika ushindani hivyo katika ushindani ni lazima ukazane uende na wakati na ufuate upopo unapokwenda ukizubaa utaachwa nyuma au upopo utakuangusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa Mawasiliano na Sayansi unaonekana wazi na hakuna anayeweza kubisha ulimwenguni kote. Haya yanajitokeza katika malengo ya *Millennium* katika *vision* yetu tuliyoiweka 2025, sera zetu zote za sekta na vipaumbele vya nchi yetu tulivyojiwekea. Sekta ya mawasiliano inawakomboa Watanzania wengi mijini na vijijini inaleta ajira tele, imemsaidia mkulima, mvuvi, mfugaji na mfanyakazi popote alipo. Hakuna atakayebisha kwa mawasiliano si chachu ya maendeleo na ukuaji wa sekta nyingine.

Hivi sasa vijijini baadhi yetu tumekuwa wajasiriamali wazuri kwa kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano. Vijijini japo hatupendi kupiga simu basi suala la mtu ku-beep tu kwa yule anayetaka ampigie simu basi kumefanywa kwa ni mradi mzuri kwa baadhi ya wajasiriamali kwani tozo ya shilingi 100/= kwa kila anapo-bip unamfanya mwenye simu kuongeza kipato chake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ninavyosema umuhimu wa mawasiliano teknolojia, habari ni chachu katika shughuli za maendeleo inawawezesha wananchi kupata taarifa na kubadilishana taarifa na mawazo, inababalishana mawazo na ujuzi kukabiliana na changamoto za maisha, katika biashara masuala ya *ICT* ambayo Mheshimiwa Waziri atayazungumzia yanasaidia kukuza biashara, biashara ndogo ndogo kuwa za kati na zile za kati kuwa za Kimataifa chini ya hali ya ushindani kwa lengo la kukidhi matakwa ya wateja wa nchini kwa huduma ambazo wanaweza kumudu kulipia.

Katika Serikali *ICT* inachochea Utawala Bora na kuwa na Serikali imara kwa kuwafanya wananchi wake kutumia mitandao kupata huduma na kuondosha rushwa. Yako mengi yaliyofanyika na kuboresha mawasiliano, kuingiza ushindani kwa kuruhusu Makampuni mengi kuja kutoa huduma na kumpa nafasi mtumiaji kuwa na utashi wa kuchagua. Kufikisha simu vijijini na mijini na hivyo kurahisisha mawasiliano. Upatikanaji wa mawasiliano umewasaidia wakulima kupata taarifa za hali ya hewa, upatikanaji wa pembejeo, taarifa za masoko na kadhalika. Kwa wafanyakazi wasomi na elimu zimewasaidia kujifunza zaidi, kuboresha taaluma na utendaji kazi, kubadilisha taarifa kwa kujifunza kwa kupitia *e-learning* na *e-services* mambo haya Mheshimiwa Waziri atayaelezea. Serikali imeanza mchakato wa kuanza *e-government* ili kuleta Utawala Bora na kupunguza vitendo vya rushwa na pia itasaidia mawasiliano baina ya Wizara na Wizara nyingine, mazungumzo haya zaidi Mheshimiwa Waziri ataaelezea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la utalii uko mpango wa *e-tourism* wenye lengo la kuboresha utalii katika elimu tuna *e-education* itasaidia sana wanafunzi haya yote Mheshimiwa Waziri atayaeleza. Lakini pia Serikali imesaidia sana Makampuni, imeondosha kodi za Makompyuta kitu ambacho kitaongeza tija kwa elimu. Ujenzi wa mkongo wa ndani na ule wa baharini, maandalizi yako hatua mbalimbali Mheshimiwa Waziri ataaelezea. (*Makofii*)

Ushirikishwaji wa sekta binafsi katika utoaji huduma umefanyika vizuri na nadhani sote tu mashahidi baada ya kuingia sekta binafsi katika masuala ya mawasiliano simu zimesambaa maeneo mengi mijini na vijijini. Lakini pia kuna sheria na taratibu za kusimamia maendeleo ya mawasiliano. *TCRA* inafanya kazi vizuri na mfumo wa leseni waliouweka sasa, unahuru teknolojia yoyote ya mawasiliano kuingia na kutumika nchini. Lakini pia zaidi tuna wataalam wenye ujuzi wa kuendeleza fani hii. Sera zote zinazohusika zimetayarishwa na hivi sasa tunazihusisha kwa pamoja. Kulikuwa vile vile kuna suala la Mfuko wa Huduma za Mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wangu sasa naomba nichangie kwa kujibu hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge katika maeneo yafuatayo. Masuala ya Mawasiliano hii pamoja na *TTCL*, simu vijijini, *Tele-centers*, masuala yatokanayo na udhibiti wa mawasiliano, athari za simu za viganjani na minara, matumizi mabaya ya simu na kadhalika.

Kwenye masuala ya *TTCL* wachangiaji Kamati ya Miundombinu, Waheshimiwa Wajumbe wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Anthony Diallo Mbunge wa Ilemela, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mbunge wa Masasi, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mbunge wa Bukombe, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Abdul Jabiri Marombwa, Mbunge wa Kibiti, Mheshimiwa Alhaj Dr. Juma Ngasongwa, Ulanga Magharibi, Mheshimiwa Dianna Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum.

Hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla wao walipenda kujua mambo kadhaa kuhusu Kampuni ya Simu ya *TTCL* ikiwa ni pamoja na hali ya Kampuni kifedha, uendeshaji, uwekezaji, uhusiano kati ya *CELTEL* na Serikali Tanzania na *CELTEL INTERNATIONAL* ndani ya *TTCL* na *CELTEL Tanzania Limited* na utendaji wa Meneja Uendeshaji wa *SKASTEL INTERNATIONAL*.

Aidha kuna maombi kadhaa ya Waheshimiwa Wabunge juu ya *TTCL* kupeleka huduma katika majimbo yao. Uendeshaji wa Kampuni na utendaji wa Meneja.

Kampuni ya Simu Tanzania iachane na teknolojia iliyopitwa na wakati na kwa nini *TTCL* inaanlisha *mobile* kwa kutumia teknolojia ya *CDMA* ambazo haziingiliani na simu nyiningine.

Je, Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano ililiona hili, hili alilisema Mheshimiwa Diallo. *TTCL* inapaswa kuingia katika soko la ushindani kwa nguvu sawia na

Makampuni mengine yanayotoa huduma kama hiyo kuna mkakati gani wa Shirika hili katika kujiongeza kipato katika kutoa huduma mfano wa *internet* na kadhalika.

Lingine lililojitokeza ni kwa nini uendeshaji wa Kampuni ya *TTCL* wanaenda kufanya majadiliano Mabenki huku Bodi ikiwa haiwakilishwi kikamilifu.

Kuna majengo yaliyojengwa kule Upenja Kaskazini Unguja hayakuwahi kutumika, majengo yaliyojengwa lililokuwa Shirika la Posta na Simu awali na baada ya Shirika hili kuachana na *TTCL* majengo yale yakabaki je, Serikali ina mkakati gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye hoja kulikuwa na maombi vile vile na ushauri kwamba hakuna mtandao simu za viganjani *TTCL* katika Wilaya ya Masasi, Wilaya ya Bukombe ipatiwe simu za *TTCL* kwa gharama ndogo na kwa kuwa Ofisi za *TTCL* Kibiti ndogo sana kiasi cha kushindwa kuhudumia watu watatu kwa wakati mmoja kwa hivyo Mbunge anaomba uwezekano wa Shirika kujenga jengo lake ambalo litakuwa na uwezo wa kuhudumia wateja wengi kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uwekezaji Wizara inatambua fika kwamba *TTCL* ni Kampuni ambayo inamilikiwa na Serikali ya Tanzania kwa asilimia 65 kwa ubia na Kampuni ya *CELTEL INTERNATIONAL* ya *Netherlands* tangu ilipobinafishwa hapo tarehe 22 Februari, awali ubia huu ulianishwa katika mkataba wa uuzwaji wa hisa yaani Subscription and shareholders agreement mwaka 2001 fedha za mauzo wa hisa hizo kiasi cha dola milioni 60 zilitumika kuanzisha *CELTEL TANZANIA* ambayo ilikuwa Kampuni Tanzu ya *TTCL*.

*CELTEL TANZANIA* ilitenganishwa kutoka utanzu wa *TTCL* mwaka 2005 kwa makubaliano mapya ya wabia baadhi ya fedha zilizotumika kuanzisha *CELTEL TANZANIA* ni *US Dollar* milioni 40 zilirudishwa kwa Serikali pamoja na fedha za mauzo ya hisa asilimia 25 za Serikali kwa *CELTEL INTERNATIONAL* zipatazo *US Dollar* milioni 28, fedha zote hizi zilitumika katika maendeleo ya *TTCL*.

Serikali ya Tanzania sasa inamiliki hisa asilimia 40 katika *CELTEL Tanzania* badala ya 65 za awali na *CELTEL INTERNATIONAL* inaendelea kumiliki hisa asilimia 35 ndani ya *TTCL*.

*TTCL* imefanya mabadiliko makubwa kiteknolojia, mitambo ya zamani yote ya *analogy* na ile ya njia ya kuuza mawasiliano kwenye mtandao wake imebadilishwa na kuwa *digital*.

Aidha, *TTCL* imeanza kutumia teknolojia ya *CDMA* na inatoa huduma mbalimbali za kisasa kabisa ikiwa ni pamoja na simu za mezani, za viganjani na takwimu ili kukabiliana na ushindani. Mpango Mkakati wa Biashara ya Kampuni ya *TTCL* unaboresha na kufikisha huduma zake nzima vijijini.

*TTCL* ilianza huduma ya simu za viganjani kwa kutumia *CDMA* kwa sababu ni teknolojia ya kizazi cha tatu ambayo ni ya kisasa zaidi kuliko ile *GSM* ambayo ni ya

kizazi cha pili, chaguo hili linaiwezesha *TTCL* kutoa huduma zaidi zinazoendana kutoa za teknolojia habari na mawasiliano.

Aidha teknolojia ya *CDMA* na *GSM* hazina matatizo katika uunganishaji wake kupitia mitambo ya mawasiliano ya aina hiyo yote.

Hata hivyo chaguo la *CDMA* inakidhi matakwa ya udhibiti wa *TTCL* kwani leseni zinazotolewa na *TCL* ni *technology neutrally* zinaruhusu teknolojia mbalimbali ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa makubaliano ya wana hisa yaani *Shareholders Agreement* ya mwaka 2005 tarehe 1 Julai utendaji wa *TTCL* ulikabidhiwa

Meneja Uendeshaji wa *SKASTEL INTERNATIONAL* kwa mkataba wa miaka mitatu liliaanza mwaka 2007 mpaka 2010. Mwendeshaji huyo anasimamiwa na Bodi ya Wakurugenzi ya *TTCL* ambao Wajumbe wake wote ni Watanzania akiwemo mjumbe mmoja mwakilishi wa *CELTEL INTERNATIONAL*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba huu wa *SKASTEL INTERNATIONAL* sio wa uwekezaji bali ni wa uendeshaji yaani Menejimenti ya *TTCL*.

Baada ya kupokea malalamiko mengi kuhusu utendaji wa Mwendeshaji huyu wa *TTCL* Wizara imeunda Kikosi kazi kupitia utendaji na shughuli zote za *TTCL*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikosi kazi tayari kimeanza kazi na kitakamilisha kazi yake Septemba, 2008. Baada ya hapo ripoti ya kikosi kazi itawasilishwa Wizarani, tutaandaa waraka wa kuishauri Serikali namna ya kuimarisha kampuni hii na kuhakikisha kwamba *TTCL* inajиendesha kibiashara na kupata faida. (*Makofi*)

Kuna suala la kuhusu hoja ya *Celtel* kuwa *Zain*. Jina la *Celtel* lilibadilishwa kuwa *Zain* Agosti mwaka huu, Serikali ilishirikishwa kupitia wajumbe wake ndani ya Bodi ya Wakurugenzi wa *Celtel Tanzania Ltd*. *TCRA* nayo ilijulishwa kabla ya mabadiliko hayo. *Zain* yaani *Celtel* ya zamani ni chaguo la jina la kimatangazo au kimasoko yaani *brand name*. *Brand name* tu ndiyo iliyobadilika lakini *legal entity* au *legal name* haijabadilika bado ni *Celtel Tanzania Ltd*. (*Makofi*)

Aidha, mfumo wa ubia ndani ya *Celtel Tanzania Ltd*. haujabadilika nikiwa na maana kwamba muundo wa wanahisa. *Share Holding Structure* ni 65% kwa 35% ndani ya *TTCL* na 40% kwa 60% ndani ya *Celtel Tanzania*. Kwa hiyo, sisi tunatumia jina tu, lakini hili jina limerahisisha sana kwa sababu ni nchi kama 22 sasa zinatumia jina hili kwa ajili ya mawasiliano.

Kuhusu hisa 35 za *Celtel International* na *TTCL* ikiwa ni pamoja na zile 60 ndani ya *Celtel Tanzania* zinaendelea kumilikiwa na *Celtel International* ya Netherlands ila sasa *Celtel International* inamiliikiwa na *Mobile Telecommunication Company* ya Kuwait ambayo kibiashara inajulikana kama *Zain Group*. Kibiashara badiliko kama hili linakubalika kibiashara.

Kwa mfano tulipotoka tulikuwa na *MIC Tanzania* ambayo ilikuwa na simu zikiitwa *Mobitel* baadaye wakabadilisha jina lao likawa *Buzz* na hivi sasa *Tigo*. Hakuna athari zozote kutokana na badiliko hili, hakuna hasara yoyote ile aidha, nchi yetu ambayo inapata kwa kampuni ya *Celtel* kubadilishwa jina na kutumia jina la kibashara la *Zain*. Aidha, kubadilisha jina la kibashara hauyawezeshi Makampuni haya kukwepa kodi kwani kodi zao hutozwa kwa majina yao ya kusajiliwa ambayo ni *Celtel International*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi, Mheshimiwa Raynald Mrope ombi lako tutatafuta pesa kusambaza *CDMA* kule kwako, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula Mbunge wa Bukombe, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum tutapeleka ushauri *TTCL* ili maeneo hayo yashughulikiwe. Lakini niseme tu Waheshimiwa Wabunge wale wote ambao wameleta malalamiko yao ya masuala ya mawasiliano napenda niwahakikishie kwamba nitayashughulikia ipasavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na suala la *Telecenter* kwa sababu ya muda. Waliochangia ni Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, Mheshimiwa Herbert Mntangi na Mheshimiwa Gosbert Blandes, wanasema nini maana ya uanzishwaji wa *Telecenter* nchini, hatua za utekelezaji wa mradi wa *Telecenter* zikoje?

Mheshimiwa Naibu Spika, *Telecenter* ni vituo vinavyotoa huduma za mawasiliano katika maeneo ya watu wenye kipato cha chini ambao hawana uwezo wa kumiliki vifaa na kumudu gharama za huduma za teknolojia ya habari na mawasiliano. Baadhi ya huduma zinazotolewa na vituo hivyo ni pamoja na *computer internet*, barua pepe, huduma za *photocopy*, nukushi, vifaa vya utangazaji vya jamii na magazeti. (*Makofi*)

Uanzishwaji wa *Telecenter* ni utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Teknolojia ya Habari ya Mawasiliano ambayo tulipitisha hapa mwaka 2003 na kupeleka huduma katika maeneo yote nchini kwenye maeneo hususan ya vijiji yenye shida ya mawasiliano. *Telecenter* zinategemewa kufanya kazi nzuri na kwa wenzetu walioko Sengerema wanaweza kutuambia wamefaidika nini. Vituo vya *Telecenter* kikawaida huongozwa na menejimenti yenye wajumbe waliochaguliwa pamoja na Kamati ya Utendaji yenye wajumbe muhimu katika eneo husika, maana hawapangiwi, wenyewe kule wanachagua uongozi wa kuendesha kituo, fedha za uendeshaji zinapatikana kwa upigaji wa simu za mikononi, za mezani, barua pepe, huduma za *photocopy*, huduma za *secretariat* na huduma za luninga na kadhalika. Vituo hivi lazima viweze kuijendesha vyenyewe. Baadhi ya vituo hivyo ambavyo ni vya majiribio ni Sengerema, Geita, Songea, Kasulu, Ngara, Kinampanda, Singida, Ikungi, Mpwapwa, Mtwara, Ludewa, Lugoda Lufilo na vituo vingine vitaanzishwa mwaka huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na suala la matumizi mabaya ya simu na uuzwaji wa *Sim Card* kiholela.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga hoja mkono. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tuliongeza dakika tano juu ya zile kumi na tano ambazo alikuwa amepewa Waziri wake na akamwambia achukue na tano nyingine.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kipindi cha maswali na matangazo, ameingia Mama Maria Nyerere. Mama tunaomba tukusimamishe kidogo. Tumefurahi kuwa na wewe na una afya njema ya kuja kututembelea katika Bunge letu. Karibu sana. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nitamwita mtoa hoja, dakika za kusoma majina hazihesabiwi. Kwa hiyo ni dakika 55. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele yenu na kutoa mchango wangu katika hoja hii. Kwa mara nyingine tena nachukua fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Kilolo kwa imani kubwa waliyonayo kwangu, nawashukuru hasa kwa njia ya kipekee kwa ushirikiano waliyonionyesha katika ujenzi wa shule za sekondari chini ya uongozi wa Halmashauri ya Wilaya na hatimaye kudahili asilimia 100 ya wanafunzi wote waliofaulu darasa la saba na hatimaye kujiunga na kidato cha kwanza. (*Makofi*)

Napenda nikukushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa umakini mkubwa mnaoonyesha katika kuliendesha Bunge letu. Nichukue nafasi hii pia kumpongeza kwa dhati, Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, Waziri Mkuu kwa umakini wake wa kusimamia shughuli za Serikali. (*Makofi*)

Aidha, napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliopata nafasi ya kuchangia hoja yangu niliyoiwasilisha hapa Bungeni siku ya Ijumaa tarehe 15 Agosti, 2008 kwa michango yao mizuri na ya kina. Kumetolewa changamoto nyingi na hii ni dalili ya dhati ya mwamko mkubwa kwa upande wa kuendeleza maeneo ya sayansi, teknolojia na ubunifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika michango hiyo imedhihirika wazi juu ya mahitaji makubwa ya mawasiliano ya simu kama ilivyo huduma za usafiri wa reli, barabara, bandari kuwa ni nyenzo muhimu ya maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya Wabunge 58 walichangia katika Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, kuititia Hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Fedha na Uchumi na Wizara yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo sasa napenda kuwatambua Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja mbalimbali kuhusu sekta hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja ya hotuba ya Wizara hii kwa kuzungumza kuititia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni hawa wafuatao, Mheshimiwa Samwel Chitalilo, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, Mheshimiwa

Susan Lyimo, Mheshimiwa Janet Kahama na Mheshimiwa Mwinchoum Msomi.  
(*Makofî*)

Waliochangia kwa kuzungumza kupitia hotuba ya Waziri wa Fedha na Uchumi ni Mheshimiwa Mohammed Amour Chomboh na Mheshimiwa Ibrahim Sanya. Waliochangia kwa kuzungumza kwenye hotuba yangu ni hawa wafuatao, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge, Mheshimiwa Abdasalaam Issa Khatibu, Mheshimiwa Dr. Luka Siyame, Mheshimiwa Anthony Diallo, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Benson Mpesa, Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia, Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Richard Ndassa na Mheshimiwa Maua Abeid Daftari. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mheshimiwa Mbarouk Mwandoro, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandoza, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Zaynab Vullu, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa *Captain* John Chiligati, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Castor Ligalama, Mheshimiwa Mathias Chikawe, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Dastan Mkapa, Mheshimiwa Abdul Marombwa, Mheshimiwa Manju Msambya, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Paul Lwanji, Mheshimiwa Dr. Mzeru Nibuka, Mheshimiwa Juma Killimbah na Mheshimiwa Bujiku Sakila. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, michango ya Waheshimiwa Wabunge niliyowataja ilikuwa ni mizuri sana, aidha, si rahisi kujibu kwa kina na kutosheleza hoja zote za Waheshimiwa Wabunge kwa muda huu mfupi tuliopewa. Naahidi kwamba hoja zote tutazijibu kwa maandishi na kuwapatia Waheshimiwa Wabunge wote. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri na maoni ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu na Kambi ya Upinzani umezingatiwa. Hata hivyo napenda nitumie muda uliobaki kujibu hoja mbalimbali ambazo zimejitokeza wakati wa kujadili hoja niliyoiwasilisha hapa Bungeni. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ambalo ningetaka kuuliza ni juhudzi zinazofanywa kujenga Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Jambo hili limechangiwa na Kamati ya Bunge ya Miundombinu, Kambi ya Upinzani na Waheshimiwa Wabunge mbalimbali. Hoja zilizotolewa kwa ujumla wake ni kwamba tutuoetarifa ya maendeleo ya ujenzi wa mkongo na kwamba mkongo huu ni muhimu sana, utapunguza gharama za matumizi ya simu za mkononi na vilevile kuweza kufikisha mawasiliano vijijini. Maelezo ni kwamba bei kubwa ya huduma za mawasiliano huchangiwa na gharama za uwekezaji katika miundombinu, mitambo, usambazaji huduma na uendeshaji. Serikali inachukua

hatua mbalimbali za kuhakikisha kuwa huduma za mawasiliano nchini zinaboreshwu pamoja na kuwafikia wananchi wote nchini hadi vijijini. Utekelezaji wa ujenzi wa mkongo upo katika hatua zifuatavyo:-

Kwanza mchakato wa ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ulianza mwaka 2004. Mkongo unaotarajiwa kujengwa utakuwa na urefu wa takribani kilometa 7,000 na utaunganishwa na Makao Makuu ya Wilaya zote nchini, yaani Tanzania Bara na Visiwani. Mkongo huu utatumia teknolojia ya kissasa kupitisha taarifa, takwimu, ripoti, picha, makala, machapisho sauti na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya mkongo huu kama ilivyoelezwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya kuweza kufikisha mawasiliano hata vijijini ni kuwezesha yafuatayo, kwanza kuwezesha wawekezaji na watoa huduma za mawasiliano kufikisha huduma za mawasiliano nchini kote kwa gharama nafuu, pili, kurahisisha utekelezaji na utoaji wa huduma za elimu, afya, utalii, utawala bora na kadhalika, tatu, kufikisha huduma ya mawasiliano katika maeneo mengi nchini hususah vijijini, nne, kurahisisha ujenzi wa jamii habari kama ilivyoainishwa kwenye dira ya maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025, kwenye MKUKUTA na Malengo ya Mileniamu ya mwaka 2015 ili kupambana na umaskini, ujinga na maradhi na tano, kuongeza ajira ya takribani kati ya watu laki tatu mpaka laki tano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mkongo huu utakapokamilika unatarajiwa kuunganishwa na mikongo ya baharini ili tuweze kuunganishwa na ulimwengu mzima. Hatua zilizofikia katika ujenzi wa Mkongo, ni kuwa ujenzi wa mkongo utaanza mwaka huu wa fedha yaani 2008/2009, Serikali imeshatenga kiasi cha shilingi bilioni 17 kwa ajili ya mradi huu na taratibu za kupata fedha za nje zipo katika hatua za mwisho. Mkongo huu katika ujenzi wake utagharimu jumla ya shilingi bilioni 170. Wajenzi wa mkongo wameshaanza kuwasili nchini na hao ni *Chinese International Telecommunication Cooperations*. Wizara ipo kwenye maandalizi ya utaratibu wa kuanza kutumia mitandao iliyojengwa na Taasisi za Umma kama vile *Tanesco*, *Songas*, Reli na kadhalika katika mwaka huu wa fedha. Naomba Waheshimiwa Wabunge waendelee kuvuta subira wakati Serikali inaendelea na juhudzi za kuhakikisha ujenzi wa Mkongo wa Taifa unaanza na unakamilika mapema iwezekanavyo. Lengo la kukamilisha ni kufikia Desemba, 2010. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo lilizungumzwa ni kuanzishwa Mfuko wa Huduma za Mawasiliano. Hili lilichangiwa na Kamati ya Miundombinu ya Bunge, Kambi ya Upinzani na Waheshimiwa Wabunge nisingependa kuwataja majina kwa sababu itachukua muda mwingi. (*Makofi*)

Hoja zilizotolewa ni kuhusu uharaka wa ujenzi wa kuanzisha mfuko huo na vilevile kueleza hatua ambazo tumefikia kwani simu za viganjani si suala la anasa tena hata mtu wa vijijini anahitaji. Kwa hiyo, mfuko wa *UCAP* uanzishwe mapema na upewe fedha za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo juu ya kuanzishwa kwa mfuko huo ni kama ifuatavyo, hatua za kuanzisha Mfuko wa Huduma ya Mawasiliano ni sehemu ya utekelezaji ya Sera ya Taifa ya Habari na Mawasiliano ya mwaka 2003. Lengo lake ni kusaidia kufanikisha azma ya kuwekeza kwenye miundombinu na kusamabaza huduma ya mawasiliano nchini kote hadi maeneo ya vijijini na sehemu ya mijini zenyekosefu wa huduma hizo kwa gharama nafuu. Kuwepo kwa huduma hizo kutafanikisha jitahada za kueneza matumizi ya TEKNOHAMA, kuibua na kutumia fursa zilizopo kuiwezesha jamii kutekeleza shughuli za kijamii na kiuchumi sanjari na kupambana na umaskini na kuharakisha maendeleo yao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uundaji wa sheria ya mfuko. Mwenzi Novemba, 2006 Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilipitisha Sheria namba 11 ya mwaka 2006 ya kuanzishwa kwa Mfuko wa Huduma ya Mawasiliano yaani *Universal Communication Access Fund* ili kufikia malengo yaliyoelezwa kwenye utangulizi nilioutambua sasa hivi. Hatua zilizofikia ni kama zifuatazo, rasimu ya kanuni za sheria za mfuko wa mawasiliano kwa wote zimekamilika na zimejadiliwa kwenye vikoa vya wadau tarehe 22 Julai, 2008. Barua ya ombi la kutangazwa kwa sheria ya kuanzisha mfuko kwenye Gazeti la Serikali ilikwishatumwa kwenye Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali tarehe 4 Julai, 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, rasimu ya kanuni itawasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali tarehe 23 Agosti, 2008 kwa hatua zaidi. Nne, taratibu wa kuteua Wajumbe wa Bodi ya Mfuko na Meneja zitafanywa baada ya tangazo kutoka kwenye Gazeti la Serikali, sita, mfuko utaanza mwezi Desemba, 2008 na kwa kuanzia zitatumika fedha shilingi milioni 900 kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano amba ni wachangiaji wa mfuko huo. Serikali ya Sweden kupitia Benki ya Dunia inakusudia kuchangia dola za Kimarekani milioni 30 kwenye mfuko. Juhudu za kupata fedha hizo kupitia taratibu za Benki ya Dunia zinaendelea. Aidha, kwa utaratibu wa Benki ya Dunia hatua zifuatazo zimekamilika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *expression of interest* imekamilika Agosti, 2007, taratibu za uchambuzi za waombaji kwa kazi hiyo umekamilika Oktoba, 2007, waombaji walitumiwa *request for proposal* Januari 2008, kupokea *request for proposal* kutoka kwenye Makampuni yaliyoomba na kufanyiwa tathmini imefanyika mwezi Machi, 2008. Kupata *order no objection order* ya Benki ya Dunia na kupitishwa na *Ministerial Tender Board*. Hili limefanyika Julai, 2008. Kufungua *financial proposal* na taratibu za kumpata mtaalam muelekezi ili kuingia mkataba na Benki ya Dunia zinaendelea. Vyanzo vya fedha za mfuko huu kwanza ni Serikali yenye, Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania, Benki ya Dunia na wadau wengine. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo lilichangiwa na Waheshimiwa Wabunge ni kuimarisha matumizi ya huduma ya Serikali elektroniki yaani *e-government*. Hili lilichangiwa zaidi na Waheshimiwa Wabunge wawili, Mheshimiwa Pindi Chana na Mheshimiwa Gideon Cheyo. Hoja zilizotolewa ni kwamba kuna umuhimu wa Serikali kuharakisha matumizi ya Serikali elektroniki na vilevile huduma za simu za viganjani zisambazwe hadi kufikia vijijini. Maelezo katika hili ni kwamba huduma za Serikali

elektroniki zinategemea sana uwepo wa miundombinu na mkongo madhubuti ili kuwezesha mawasiliano nchini kote hususan mawasiliano kati ya Makao Makuu ya Wizara na Ofisi zingine na Ofisi zilizoko Mikoani, Wilayani hadi vijijini. Aidha, Serikali katika awamu ya pili ya mpango wa urekebishaji wa utumishi wa umma, moja ya malengo ni kuanzisha Serikali elektroniki; hivyo matatizo ya kuhamisha mafaili kutoka Makao Makuu ya Wilaya hadi kwenda sehemu nyingine itapungua au kumalizika kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo lilizungumziwa na Waheshimiwa Wabunge ni eneo la Sayansi na Teknolojia. Hoja ilitolewa kwamba kwanza ilitolewa na Kamati ya Miundombinu ya Bunge, Kambi ya Upinzani na Waheshimiwa Wabunge ambaao *list* yao ni ndefu.

Hoja hizo ni pamoja na kwamba wanafunzi wanaosoma masomo ya sayansi ni wachache, kuna mkakati gani wa kuongeza idadi ya wanafunzi hao? Hivi sasa kuna uhaba mkubwa wa wataalam wa Sayansi na Teknolojia nchini na Bajeti inayopangwa kwa Wizara hii ni ndogo na hasa kwa vyuo vya *DIT* na *MIST* na kwamba Serikali ione umuhimu wa kuingiza masuala ya Sayansi na Teknolojia na TEKNOHAMA katika mitaala kuanzia shule za msingi hadi vyuoni. Wizara iandae walimu na wataalam wa masomo ya sayansi ili waweze kusaidia katika kufundisha. Serikali iweke juhudzi za kuongeza Idadi ya wataalam wa sayansi na kwamba Wizara ishirikiane na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu katika kuhimiza wanafunzi kupenda masomo ya sayansi. Serikali iangalie ni jinsi gani ya kuongeza wanafunzi wa sayansi kwa kuwapa motisha mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo katika hili ni kama ifuatavyo, kwanza, Serikali kwa kushirikiana na Taasisi za Mafunzo imeanza kutekeleza yafuatayo, kuendesha mafunzo maalum yaani *pre-entry programme*, kwa wanafunzi wa kike kwa kozi za ufundu na sayansi. Hivi sasa baadhi ya vyuo vimeanza kutoa kozi kama hiyo hata kwa wanafunzi wakiume, kutoa mikopo kwa wanafunzi wote wa elimu ya juu wanaochukua masomo ya sayansi, kutoa ufadhili kwa wanafunzi wote wanaochukua kozi ya udaktari wa wanadamu, kutoa tuzo kwa wanafunzi wa kike wanaofanya vizuri katika masomo ya sayansi katika mitihani ya sekondari na vyuo vya ufundu. Aidha, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu na Wizara yangu tumeunda Kamati ya pamoja ambayo inashughulikia jitihada za kufufua masomo ya sayansi tangu shule za msingi hadi vyuo vya elimu ya juu. Pamoja na mambo mengine Kamati hii inaangalia kwa undani sababu zinazofanya wanafunzi wasipende kusoma masomo ya sayansi na itatoa mapendekezo kwa Serikali nini kifanyike, pia itapitia upya mitaala ya masomo ya sayansi kuanzia shule za msingi ili kukidhi mahitaji ya Taifa na itawasiliana Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ili wahitimu wa masomo ya sayansi wapate mishahara inayowavutia. Serikali inafanya jitihada ya kuboresha mazingira ya mafunzo kwa kuimarisha na kujenga maabara, karakana na kuboresha maktaba. (*Makofi*)

Vilevile upo utaratibu kwa wanafunzi wanaofaulu masomo ya sayansi kwa kiwango cha *division three* ili mradi kati ya masomo aliyofaulu ni sayansi ikiwemo somo

la hisabati kupata udahili katika taasisi za teknolojia kupitia *pre-entry programme*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali inahamasisha wanafunzi kusoma masomo ya sayansi na TEKNOHAMA kuanzia shule za msingi kwa kuweka masomo haya katika mitaala yao kama ifuatavyo, kwanza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundisimeunda sera maalum ya TEKNOHAMA ikiwa ni juhudzi za kufanikisha utekelezaji wa sera ya Taifa ya TEKNOHAMA na pili, Taasisi ya Elimu Tanzania imeandaa mitaala kama ifuatavyo, mtaala wa Teknolojia na Habari yaani TEHAMA kwa shule za msingi nchini, mtaala wa *computer information study* kwa shule za sekondari kidato cha kwanza mpaka cha nne, mtaala wa *computer studies* kwa Kidato cha Tano na Sita. Aidha, *ICT* hufundishwa katika vyuo vya elimu ya juu na vya ualimu nchini. (*Makofi*)

Kuhusu *DIT* na *MIST* kutengewa fedha kidogo, hili limezungumzwa na Kamati ya Bunge ya Miundombinu, Kambi ya Upinzani na Waheshimiwa Wabunge mbalimbali. Hoja zilizotolewa ni kwamba Taasisi hizi hazikupewa fedha za kutosha na kule *MIST* hawakupata fedha kwa ajili maendeleo. Maelezo ya hali hii ni kama yafuatayo, Wizara imetengewa na Hazina fedha za Maendeleo kiasi cha shilingi bilioni mbili tu kwa ajili ya taasisi zote zilizo chini yake. Kutokana na kiasi hicho ilionekana kuwa ni vyema kukamilisha miradi iliyokuwa inaendelea. *MIST* kwa mwaka 2008/2009 imetengewa kiasi cha shilingi bilioni 2.9. kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambalo ni ongezeko la asilimia 89.13 tofauti na kiasi cha shilingi bilioni 1.5 walizopewa kwa mwaka jana. Kati ya fedha hizo Wizara imeagiza *MIST* kwa barua kwamba kiasi cha shilingi bilioni moja kitumike kwa ajili ya ukarabati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inalenga kuboresha mazingira ya taasisi ili iweze kudahili wanafunzi wengi zaidi na nyingi ya kazi hizo ni *civil works* kama kupaka rangi, kubadilisha sakafu na vitu vingine. *DIT* kwa upande mwingine katika mwaka wa fedha 2008/2009 wametengewa kiasi cha shilingi milioni 60.8 kwa ajili ya maendeleo. Katika mwaka wa fedha 2007/2008 walitengewa shilingi bilioni 1.3 pamoja na fedha hizi walitengewa kiasi cha shilingi bilioni 2.7 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, huku *DIT* fedha zilizotengwa ni katika kukamilisha michoro, kuangalia sampuli za udongo katika eneo ambalo litajengwa *Multipurpose Block*, kwa upande wa *COSTECH* wametengewa kiasi cha shilingi 474,000/= hii ni kumalizia ukarabati wa jengo ambalo ulianza tangu mwaka jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine lilikuwa ni upungufu wa fedha za utafiti. Hili limezungumzwa na Kamati ya Bunge ya Miundombinu, Kambi ya Upinzani na Waheshimiwa Wabunge kadhaa. Hoja zilizotolewa ni kwamba Serikali iangalie uwezekano wa kuongeza tengeo la fedha katika masuala ya utafiti na maendeleo na kwamba shughuli za utafiti na maendeleo ni muhimu sana kwa uvumbuzi na maendeleo ya teknolojia. Uongezaji tija na utengenezaji wa bidhaa bora, vifaa bora na michakato bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli hizi ni muhimu sana kwa kuzingatia kwamba ndio chimbuko kuu la kuongeza ufanisi na kupiku ushindani mkali katika dunia hii ya utandawazi, hali inayofanya matokeo ya utafiti wa kisayansi kuwa siri ya nchi au taasisi husika na kuhifadhi na kulinda kwa hatadhi (*patents*). Kwa maoni ya Mbunge, kiwango cha fedha za Mfuko wa Utafiti ni kidogo mno, anaishauri Serikali iongeze kipaumbele ili shughuli za utafiti na maendeleo ziweze kuwa na mafanikio zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya hoja hii ni kama ifuatavyo, Wizara imepokea ushauri wa Mbunge. Wizara yangu itawasiliana na Wizara ya Fedha na Uchumi ili kuona namna ya kuongeza tengeo hilo ili lifikie angalau asilimia moja ya Pato la Taifa kama ilivyokubalika kwenye Azimio la Lagos (*Lagos Plan of Action*). Hata hivyo, Wizara yangu inaendelea kuchukua hatua mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha kwamba masuala ya utafiti yanatengewa fedha za kutosha kila mara hali inaporuhusu. Hatua hizo ni pamoja na kuimarisha Mfuko wa Utafiti *any fast* kwa kuutengea shilingi bilioni moja kwa mwaka huu wa fedha 2008/2009 kutoka shilingi milioni 600 kwa mwaka 2007/2008 ambapo ni ongezeko la asilimia 67 ya fedha katika Mfuko huu, kuhuisha Sheria Na. 7 ya COSTECH ili iipe uwezo zaidi wa kutekeleza majukumu yake ikiwemo kupata takwimu kutoka Taasisi za Utafiti ambazo zipo chini ya Wizara nyinezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali imeandaa Rasimu ya Sera ya Taifa ya Utafiti na vile vile kwa kushirikiana na UNESCO, Serikali inapitia upya Mfumo wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu nchini. Aidha, Wizara imeandaa Benki ya Takwimu za Utafiti na kuandaa ajenda za Taifa kuhusu Utafiti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo lilizungumzwa kwa urefu na watu wengi sana, ni lile linalohusu utendaji kazi wa Posta. Hoja zilitolewa na Kamati ya Bunge, Kambi ya Upinzani na Wabunge wengi. Hoja ya kwanza ilikuwa Serikali itoe mtaji wa kutosha kwa Shirika la Posta Tanzania ili kuliwezesha kuwekeza katika maeneo yenye kuboresha miundombinu, mtandao, vifaa na mitambo ili kuinua viwango vyta huduma za Posta kwa wateja.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ni kwamba, Wizara yangu inaishukuru Serikali kwa uamuzi wa kufuta na kuchukua madeni ya Shirika la Posta, kuchukua jukumu la kulipa pensheni ya wafanyakazi ambao ajira yao zilitokea Shirika la Posta la Afrika na kurejesha jengo la Posta ya Zamani kurudi tena kwenye Shirika la Posta. Wizara imeunda Kamati ya Watalaam ambayo itakutana kuanzia mwezi ujao kuandaa taarifa yenye mchanganuo wa mahitaji halisi ya mtaji. Kamati inahusisha wadau kutoka Hazina, Posta, *Consolidated Holding Corporation* na wengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili ilikuwa kuna mipango gani ya Shirika la Posta itakayoliwezesha Shirika kuingia katika soko la ushindani wa kibiashara na kuboresha huduma zake kwa kutumia teknolojia ya kisasa? Maelezo ni kwamba kuongezeka kwa ushindani wa maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano ni changamoto kwa Shirika la Posta. Aidha, teknolojia inalipa Shirika la Posta fursa ya

kuboresha na kuanzisha huduma nyingine mpya ili kuongeza kasi na ufanisi wa utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Posta limetayarisha na linatekeleza Mpango Mkakati wa kibiashara wa miaka mitatu kuanzia mwaka 2008 hadi 2010 ambao umezingatia maswali ya kuboresha biashara, kutumia teknolojia mpya katika kuongeza hadhi na huduma za siri, kuanzisha huduma mpya ili kukidhi mahitaji mapya ya wateja na kukabiliana na ushindani. Maeneo muhimu ambayo yamezingatiwa katika mpango huo ni pamoja na yafuatayo, kuanzisha na kutekeleza mradi wa kutuma fedha kwa kutumia mtandao (*Electronic Money Transfer*), kuboresha huduma ya kutuma vifurushi na barua kwa haraka (*EMS Courier*) kwa kutumia *Bar Code* na teknolojia mpya katika kufuutilia usafirishaji na uwasilishaji wa vipeto (*Track and Tress*), kupanua wigo wa kuendesha shughuli za Taasisi nyingine kama Wakala ambapo Shirika linapokea na kulipa fedha kuitia huduma ya *Post JAILO* kwa mfano, kuuza hisa, kulipa gawiwo kwa wanahisa, kulipa pensheni na kadhalika.

Pia kufanya mapitio ya majengo yake yote nchini ili kuhakikisha kuwa yanatumika kibiashara na kikamilifu. Majengo hayo ni pamoja na jengo linalotumika kama Makao Makuu ya Shirika (*Posta House*) pamoja na jengo la Posta ya Zamani lililoko mtaa wa Sokoine na Mkwepu Dar es Salaam ili yatumike kama vitega uchumi wa Shirika hili, kushirikiana na Mamlaka ya Mawasiliano (*TCRA*) kubuni na kuanzisha Mfumo Mpya wa Anuani za *symbol* za Posta (*New Addressing System and Post Code*) ili kuboresha shughuli za kiuchumi na kijamii, kuwasilisha ofisini na nyumbani nyaraka za haraka katika Jiji la Dar es Salaam (*City Agent Mail*) na mashauriano yanafanywa kati ya Posta na *TTCL* ili kubuni na kutekeleza mradi wa kufikisha huduma za mawasiliano yanayotumia teknolojia ya kisasa (*TEKNOHAMA*) kwenye ofisi na vituo vya Posta vilivyoko Wilayani na vijijini. Lengo ni kuviwezesha vituo vyote vya Posta kutoa huduma zote za mawasiliano na upashanaji habari (*Universal Communication Access Fund*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani ilihoji je, ni kwa kiasi gani malengo ya Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005/2010 yametekelezwa na Sekta ya Posta kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita? Maeleo ni kwamba Wizara kupitia Shirika la Posta Tanzania imejiwekea malengo ya kuhakikisha kuwa huduma za Posta nchini zinapanuliwa hadi vijijini ili kuongeza kasi ya usambazaji wa barua, vifurushi, huduma za kifedha pamoja na kuendeleza na kupanua matumizi ya teknolojia mpya ya habari na mawasiliano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Julai, 2008 idadi ya ofisi kamili za Posta zilifikia 161 ambalo ni ongezeko la asilimia 3.8. Ofisi zinazoendeshwa na Mawakala ni 260, Vituo ni 32 vya kusambaza barua na Mawakala wanaouza bidhaa za Posta ni 3,306. Masanduku ya kupokelea barua kwa nchi nzima ni 173,800. Ofisi zinazotoa huduma ya *EMS Courier* ni 136, *Money Fax* 124 na Vituo vya *Internet* ni 14, tofauti na mwaka 2005 ambapo Shirika la Posta lilikuwa na kituo kimoja kinachotoa huduma za *internet*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya muda mrefu ni kuhakikisha kuwa Makao Makuu ya Wilaya zote yanakuwa na ofisi kamili za Posta zenye hadhi ya Wilaya na ofisi zote za Posta zitatoa huduma zote za Posta ikiwa ni pamoja na *EMS Courier, Money Fax, Internet* na nyinginezo.

Aidha, Shirika la Posta halikuweza kujenga majengo mapya katika Wilaya na kuanzisha ofisi katika kila kijiji kutokana na hali mbaya ya kifedha. Hata hivyo mtandao wa Posta unaendelea kupanuliwa kutumia majengo ya kukodi na kutumia utaratibu wa Mawakala kuendesha baadhi ya Posta ndogo kwenye maeneo ya kibashara kwa lengo la kupunguza gharama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa nini hatma ya jengo la Posta ambalo tunataka lirezeshwe kwa Shirika la Posta. Je, Serikali imetua mtaji kwa ajili ya kuliwezesha Shirika la Posta kujiendesha? Maelezo ni kwamba, Jengo la Posta la Zamani limerezeshwa kuititia barua ya Katibu Mkuu Kiongozi ya tarehe 11 Agosti, 2008 na barua hii imenakiliwa kwa Katibu Mkuu, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Wizara inashukuru Serikali kwa kulirudisha Jengo hilo Posta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeunda Kamati ya Watalaam ambayo itaanza kazi Septemba, 2008 kama nilivyoeleza hapo awali kuanda taarifa ya mchanganuo wa mahitaji halisi ya mtaji wake. Kamati inahusisha wadau kutoka kama nilivyoeleza, Hazina, Posta, *Consolidated Holding Company* na Wizara ya Katiba na Sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyotolewa ni kwa kuwa Jengo la Posta la Mpwapwa linahitaji ukarabati, je, ni lini Serikali itakarabati Jengo hilo ili kuongeza watumishi na kuwapatia vitendea kazi? Maelezo ni kwamba, Jengo la Posta la Wilaya ya Mpwapwa ni moja kati ya Majengo ya Shirika ambayo yako kwenye mpango wa kukarabatiwa katika kipindi cha mwaka 2009/2010. Aidha, Shirika litaendelea na kuboresha vitendea kazi katika ofisi hii hali ya fedha inaporuhusu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa ni kuhusu ongezeko la mawasiliano ya simu limeathiri matumizi ya Posta kwa kutuma barua, Wizara ni vyema ikabuni mbinu ya kuliongezea kipato. Kama nilivyoeleza hapo awali, maelezo ni kwamba pamoja na ukweli kwamba ongezeko la mawasiliano ya simu limepunguza uandikaji wa barua, teknolojia mpya ya habari na mawasiliano imelipa Shirika la Posta fursa ya kuanzisha huduma nyingine mpya. Shirika la Posta limetayarisha na linatekeleza Mpango Mkakati kama nilivyoeleza na majukumu mengine ambayo litachukua ili kujiwezesha kupata kipato kikubwa zaidi. Jambo la msingi ni kuliwezesha Shirika la Posta liweze kutoa huduma zake kwa kasi na ufanisi zaidi sambamba na kutumia TEKNOHAMA ili kupanua wigo wa huduma zake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ilikuwa ni hoja, kwa nini fedha za ujenzi wa Jengo la Posta Kibondo hazikuonyeshwa katika Bajeti ya Wizara ikiwa ni pamoja na muda wa kuanza ujenzi huo, je, ni lini ujenzi huo utaanza? Maelezo ni kwamba ujenzi wa jengo la Posta Kibondo utafanywa kwa kutumia mapato ya kawaida ya Shirika la Posta lenyewe. Aidha, ujenzi huo utaanza mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa kuna kila sababu ya kuliboresha zaidi Shirika la Posta kwani pamoja na kuwepo kwa simu na *internet* bado mahitaji ya Posta yapo na yataendelea kuwepo kwa usafirishaji wa vifurushi na *register*. Maelezo ni kwamba Wizara inakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa kuna kila sababu ya kuboresha Shirika la Posta. Serikali imeshaanza kuchukua hatua ambazo ni pamoja na kuchukua na kufuta madeni kama nilivyoeleza hapo awali, kuliondolea Shirika mzigo wa pensheni na kurudisha Jengo la Zamani la Posta. Hatua hizo zimelenga kuliwezesha Shirika la Posta kuboresha huduma zake, kuanzisha huduma mpya, kutumia teknolojia mpya na kupanua mtandao wake ili kufika kwa wananchi walio wengi zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine katika eneo hili ilikuwa ni barua na vifurushi kutoka Ludewa kwenda Njombe hufanyika mara moja tu kwa wiki. Hali hii ya kazi ya usafirishaji inafaa iboreshwe. Maelezo ni kwamba Shirika la Posta linaendelea kuboresha usafirishaji wa barua na vifurushi kati ya Ludewa na Njombe, huduma hii sasa hufanyika mara tatu kwa wiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa je, Sheria yetu ya kudhibiti fedha haramu ina nafasi gani katika usafirishaji huu wa fedha wa holela? Wakatoa ushauri kwamba usafishaji wa fedha ubakie katika mabenki na posta kwa kuzingatia kwamba Shirika la Posta halitakuwa na matatizo ya fedha baada ya Serikali kulisadia kukopa fedha kutoka kwenye mabenki. Maelezo ni kwamba ushauri wa kudhibiti huduma ya kutuma fedha umepokelewa na hivyo suala hilo litawasilishwa kwenye mamlaka inayohusika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa kwa kuwa kwa muda mrefu pamekuwa na huduma mbovu za upatikanaji wa fedha katika Posta Korogwe, je, tatizo hili sugu litapatiwa lini utatuzi wa kudumu? Maelezo ni kwamba, boda ya kuondolewa mzigo wa madeni, Shirika la Posta litakuwa na uwezo wa kupata fedha na mtaji kwa njia ya mkopo toka kwenye mabenki na hivyo kuweza kuwekeza katika huduma za kifedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa ni wakati muafaka sasa wa Serikali kuangalia jinsi gani ya kuwa na *address* zenye jina la barabara kusaidia kutambua *address* za watu wakiwekwa kwenye *database*, *Information* ya watu na ni rahisi kujulikana. Maelezo ni kwamba Wizara kuititia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania na Shirika la Posta imeanza kutekeleza mfumo mpya wa anuani za *symbol* (*New Address System and Postal Code*) ambao utawezesha kuwa na anuani za makazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine kuhusu Posta ilikuwa Wizara iliagize Shirika la Posta kujenga Posta pale Mangaka ambapo ni Makao Makuu ya Wilaya mpya ya Nanyumbu kwani Wilaya hii haina Posta na wananchi wake wanategemea Posta ya Masasi Mjini ambayo ina umbali wa kilometra 80 hadi 120. Jibu ni kwamba Shirika la Posta Tanzania limetayarisha mpango wa muda mrefu wa ukarabati na ujenzi wa majengo mapya ya posta. Ujenzi wa jengo la Posta katika Mji wa Mangaka Wilayani

Nanyumbu umeingizwa kwenye mpango ambao utekelezaji wake utazingatia upatikanaji wa fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa Serikali iliambie Shirika la Posta lipeleke huduma vijiji hasa Kigoma Vijijini, Shirika la Posta lipewe mtaji ili liweze kujiendesha kibashara. Maelezo ni kwamba Wizara imepokea ushauri huu na itaufikisha katika Shirika la Posta ili ufanyiwe kazi na pili, Kamati imeundwa ya kutathmini mahitaji halisi ya mtaji wa Posta ili Serikali iweze kutafuta fedha hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa Serikali ichukue hatua ya kuliokoa Shirika la Posta, kwa nini *Money Fax* hulipwa baada ya kibali kutoka Makao Makuu, Shirika la Posta lirezeshesha ubora wa huduma zake za huko awali. Maelezo ni kwamba Serikali inatambua matatizo yanayolikabili Shirika la Posta na tayari hatua zimeshaanza kuchukuliwa na Serikali ili kutatua matatizo kama ifuatavyo, kama nilivyoeleza hapo awali, kufuta na kuchukua madeni ya Posta, kulirudisha jengo, kuchukua dhamana ya kuwalipa wale watu wa pensheni na kwamba Serikali inafanya tathmini ya mahitaji halisi ili Shirika la Posta liweze kujiendesha lenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Posta kwa upande wake limetayarisha mpango mkakati ambao una lengo la kujijengea uwezo, kuboresha, kuongeza na kukuza huduma na kuongeza mapato. Mpango huo pia una lengo la kuliwezesha Shirika sambamba na maendeleo ya teknolojia katika kutoa huduma. Moja ya malengo ya mpango mkakati wa Shirika la Posta ni kuongeza na kuboresha ubora wa huduma zake. Huduma kwa wateja (*customer care*) ni moja ya eneo linalotiliwa mkazo sambamba na kutumia teknolojia ya kisasa katika kutoa huduma. Shirika limeweka utaratibu wa kutoa vibali vyta kuchukua fedha kwa sababu ya kiusalama kwani kuna uwezekano watu wasio waaminifu kuingia kwenye mtandao na kutumia hati za kughushi, hivyo ni muhimu kufanyika uhakiki wa kutosha kabla ya malipo kufanyika. Hata hivyo utaratibu huu utabadilika baada ya Shirika kukamilisha mradi wa *Counter Automation* ambao una udhibiti wa kutosha. Utaratibu unaotumika kuendesha huduma za *Money Fax* umeweka viwango vyta malipo yanayopaswa kutolewa kibali na Makao Makuu ya *EMS* na viwango vitakavyolipwa bila kibali. Aidha, vibali hivyo vinapaswa kutolewa bila uchelewesho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa Serikali ikubali kuharakisha kuboresha Shirika la Posta, haya nimeishayatolea maelezo.

Kuhusu kulipwa pensheni kwa wastaafu, Serikali kutafuta shilingi bilioni 24, Serikali ione umuhimu wa kujenga Posta Itigi. Haya yote nimekwishayatolea maelezo isipokuwa jengo la Itigi. Jengo la Posta la Itigi linalotumika hivi sasa ni mali ya kampuni ya Reli na ni dogo. Shirika litaangalia uwezekano wa kujenga jengo lake katika Mji mdogo wa Itigi hali ya fedha itakaporuhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa nyuma ya Dodoma hoteli liko jengo refu la miaka mingi, je, jengo hilo ni la nani na kwa nini limetelekezwa kwa muda mrefu? Maelezo ni kwamba jengo hilo siyo mali ya Shirika la Posta bali lilikuwa la

Benki ya Posta ambao wameliuza kwa iliyokuwa Wizara ya Maji na Mifugo mwaka 2004. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nije kwenye eneo ambalo lilizungumziwa sana kuhusu *MIST* na ambao kwa miaka karibu mitatu sasa tumekuwa tukilizungumza. Ningependa kuchukua nafasi hii kueleza kwamba mimi vile vile ni mdau katika hili na siyo kwamba nalitekeleza nikiwa kama mtu niliyeko nje. Lakini katika kulitolea maelezo hili, napenda kuanza na utangulizi ufuatao, kwanza, ni dira ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ambayo ndiyo muongozo wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, dira ya Wizara ni kuwa na jamii yenyе maarifa yaliyojengwa katika misingi thabiti yenyе kuipa uwezo, ustadi na umahiri ili kuweza kunufaika na sayansi, teknolojia na ubunifu katika kuleta mageuzi yatakayotupa uchumi endelevu wenye kuhimili ushindani wa Kimataifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, dhima ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ni kuwezesha upatatikanaji wa rasilimali watu (*human capital*) na uibuaji wa maarifa mapya ili viweze kusaidia katika kuleta utajiri wa nchi uliojengwa juu ya misingi imara na endelevu inayotokana na sera zenye kutoa fursa ya kuiendeleza sayansi, teknolojia, habari na mawasiliano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya Wizara ni kama ifuatavyo, kuratibu na kusimamia uandaaji na upatikanaji wa watalaan wa ndani katika fani za sayansi na teknolojia na kusimamia maendeleo ya sayansi na teknolojia nchini kwa kuweka uzito unaostahili kwa taasisi za teknolojia za *Dar es Salaam Institute of Technology (DIT)* na *Mbeya Institute of Science and Technology* ambazo zina dhamana ya kutekeleza sera za Wizara kuhusu ukuaji wa sayansi na tekinolojia nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, historia ya *MIST*. Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya (*MIST*) ilitokana na kupandishwa hadhi kwa Chuo cha Ufundı Mbeya (*Mbeya Technical College*) kwa Azimio Namba 5 la mwaka 2004 lililopitishwa na Bunge hili Tukufu tarehe 21 Aprili, 2005. Kwa hiyo, Chuo cha Ufundı Mbeya kikabadilishwa kuwa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia (*MIST*) kuanzia tarehe 1 Julai, 2005. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Ufundı Mbeya kilianzishwa na Serikali mwaka 1986 kwa msaada ya Serikali ya Umoja wa Nchi za Jumuiya za *Soviet (USSR)*. Ujenzi wa Chuo uliendelea hadi pale Umoja wa Nchi za Jumuiya za Kisoviet uliposambaratika mwaka 1990. Tangu wakati huo, Serikali ya Tanzania iliendelea na ujenzi kwa kasi ndogo kutokana na uhaba wa fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilipoamua kwa kupitia iliyokuwa Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kukipandisha hadhi kilichokuwa Chuo cha Ufundı Mbeya, iliomba Mshauri Mwelekezi (*Bureau of Industrial Cooperation – BICO*) kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 2003 kufanya tathmini ya kutoa mapendekezo juu ya hatua za kuchukua kuhusu kukipandisha hadhi kutoka kuwa Chuo cha Ufundı Mbeya na kuwa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia. Washauri walifanya kazi hiyo na maoni

yao waliyotoa ni kama ifuatavyo, waliona ni vyema tukatenganisha kujua tofauti ya Chuo Kikuu na Taasisi. Vyuo ambavyo vinatoa tuzo ya *Degree* na zisizo za *Degree* katika Uhandisi, teknolojia na ufundi ni Taasisi za Teknolojia (*Polytechnics*).

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa taasisi za sayansi na teknolojia dhidi ya Vyuo Vikuu umefafanuliwa zaidi katika ripoti hiyo. Napenda hapa niyaeleze kwa makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Elimu ya Chuo Kikuu imeelezwa kama ifuatavyo naomba uniruhusu nitumie Kiingereza; “*a University whether of science or technology or otherwise, is characterized by its ability to advance knowledge and search for new frontiers of knowledge. Universisty training imparts knowledge and understanding of methods, principles and concepts and emphasizes on research. A Universities main pre-occupation in training is training at a Degree level. Any training below Degree level at a University level is normally secondary.*” (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu itolewayo katika Taasisi za Sayansi na Teknolojia kinyume na yale yaliyoelezwa kwenye *University* ni kama ifuatavyo; “*Any Institute of science and technology (IST) is characterized by its competence in the application of knowledge. Institute of science and technology and training imparts skills in the translation of knowledge into tangible results. Research undertaken by an Institute of science and technology is more inclined towards the application of knowledge and scientific principles. Under normal circumstances an Institute of science and technology is more practice oriented than a normal University. Degree graduates from such an Istitution are trained to exhibit competence in application of knowledge and skills in a wide and unpredictable variety of context with substantial personal responsibility.*” End of quote. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya maelezo hayo, mambo mengine muhimu katika ripoti hiyo ya watalaam, kwanza ilikuwa hadidu za rejea alizopewa Mshauri Mwelekezi (*BICO*) na *College of Engineering and Technology* ya *University of Dar es Salaam*, zilimtaka kupendekeza njia za kuboresha, kupanua na kupandisha hadhi ya Chuo cha Ufundi Mbeya kuwa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia. (Makofi)

Mheshimiaw Naibu Spika, baada ya kufanya tathmini ya hali halisi, Mshauri Mwelekezi aliona kwamba kuna uhaba mkubwa wa Mafundi Sanifu zaidi ya tatizo la uhaba wa wahandisi (*Engineers*) hapa nchini Tanzania. Mshauri Mwelekezi aliona kuwa kupandisha hadhi Chuo cha Ufundi Mbeya kuwa Chuo Kikuu itafanya hali ya ukosefu wa mafundi sanifu kuwa mbaya zaidi. Mshauri Mwelekezi alipendekeza kwamba Chuo cha Ufundi Mbeya kipandishwe hadhi na kuwa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya (*MIST*) na kipanue ufundishaji katika ngazi mbalimbali za mafundi sanifu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa kuwa hadidu za rejea zilitaja kupandisha hadhi ya Chuo hicho kuwa Chuo Kikuu, Mshauri Mwelekezi alishauri pia ifanyike tathmini baada ya miaka 10 yaani kuanzia mwaka 2003 kuona kwanza kama wastani wa wahandisi ikilinganishwa na mafundi sanifu na mafundi stadi yaani *ratio* kati ya *Engineer, Techinician and Artisans*. Wakati ule ilikuwa 1:2:14 yaani *Engineer* mmoja,

*technicians* wawili na mafundi sanifu 14 kwamba *ratio* hiyo tuone kama kama itakuwa imekaribia *ratio* ya Kimataifa ambayo ni 1:5:25. Kwa hali ya sasa ya hiyo *ratio* ya 1:2:14, sasa ni mbaya zaidi kwa sababu Vyuo Vikuu vinatoa wahitimu wengi zaidi kwa *Degree level za Engineering* pale *College of Engineering and Technology*, vile vile Chuo cha Ardhi, vile vile *DIT*. Kwa hiyo, *ratio* hiyo imekwishashuka tayari. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ilisema kwamba iangalie kama idadi ya vyuo vya kufundishia mafundi sanifu vimeongezeka na idadi ya mafundi sanifu imeongezeka, ili ihalalishe Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya kutolewa kwenye kufundisha mafundi sanifu. Wakati huo tulikuwa na Chuo hicho hicho cha Mbeya, tulikuwa na *DIT* na *Arusha Technical College*. Vyuo hivyo bado vimebakia pale pale, havijaongezeka wakati mahitaji ya hao wahitimu bado ni makubwa. Ilipendekezwa kwamba kupandishwa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya kuwa Chuo Kikuu kufanyike tu pale ambapo masharti yaliyotolewa na niliyoyasoma hapa juu, hiyo *ratio* na idadi ya vyuo kama imeongezeka. Mshauri elekezi alishauri Serikali ikijengee uwezo kilichokuwa Chuo cha Ufundî Mbeya hatua kwa hatua ili kiweze kutoa wataalamu wengi zaidi, hivyo mapendekezo yaliyotolewa kwa misingi kwamba mara Chuo kikipata hadhi ya Chuo Kikuu, huanza kukilinganisha na Vyuo vingine vya zamani na lengo kubadilika kwa kutoa wahitimu wa Shahada ya kwanza na Uzamili, mafunzo ya ufundî sanifu huwekwa pembeni na hunyimwa rasilimali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zilizochukuliwa na Wizara ni kwamba, mwaka 2004 Serikali ilichukua hatua zifuatazo, kwanza kukibadilisha kilichokuwa Chuo cha Ufundî Mbeya na kuwa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia (*MIST*), pili, iliendelea kujenga uwezo wa rasilimali watu kwa kuwapeleka watumishi katika masomo ya Uzamili na Uzamivu na kuajiri watumishi wapya kukidhi mahitaji, idadi ya walimu imeongezeka kutoka 50 mwaka 2003 hadi kufikia 122 ikiwa ni pamoja na Mkuu wa Chuo hicho akiwa ni Profesa wa *Engineering*, tatu, imeendelea kuboresha miundombinu ya *MIST* kwa kununua vifaa vya maabara na karakana na kujenga mabweni ya wanafunzi, mne, imepanua eneo la Taasisi kwa ajili ya mahitaji ya baadaye, mwaka 2007/2008 rejea *Hansard* ya tarehe 20 Julai, 2008 ukurasa wa 110, ambapo nilieleza kama ifuatavyo; “Lengo lililopo ni kwa taasisi ya *MIST* ni kutoa *Certificates, Diploma* ya Juu, Shahada ya Kwanza, Shahada ya Pili na Shahada ya Uzamivu sawa na Chuo Kikuu, jambo la muhimu kwa sasa ni kuimarisha taasisi hii na kujenga uwezo kwa wataalamu wa kutosha, kuweka karakana, maabara, miundombinu na vifaa vingine ili viweze kutoa elimu bora kwa vitendo yaani *skills development*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, hivyo basi kuna tofauti kuna msisitizo kati ya Vyuo Vikuu na taasisi ya sayansi na teknolojia (*IST*). Lengo letu ni kutoa wataalamu wenye uwezo wa kufanya kazi kwa vitendo katika ngazi zote na wanaoweza kutatua matatizo ya nchi yetu hawa ni wahitimu wanaoweza kujiajiri moja kwa moja na pia kuongeza ajira. Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, zilianzishwa kwa utaratibu tofauti na ule uliotumika kuanzisha vyuo vikuu kwa lengo la kukidhi mahitaji ya rasilimali watu katika ufundî na teknolojia, wahitimu wa aina hii wanahitajika sana ili lengo la nchi yetu kuwa nchi ya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2020 - 2025 iweze kufikiwa. Kutokana na maelezo hayo na kama nilivyosema

katika hotuba yangu napenda kutamka ya kwamba mchakato unaendelea ili kuzifanya taasisi za *DIT* na *MIST* kuwa na hadhi ya vyuo vikuu kwa kutoa mafunzo ya Stashahada, Shahada ya Kwanza, Shahada ya Uzamili na Uzamivu. Taasisi hizi kama ilivyo kwenye Taasisi nyingine kama vile *MIT*, *ITT*, *KIST* (Korea), *IIS* (India) na kadhalika zipatiwe hati idhini (*charter*) na ithibati yake itatolewa na chombo kinachotoa ithibati ya vyuo vikuu (*Tanzania Commission of Universities - TCU*). (*Makofi*)

*Mist* inatarajia kuanza kutoa shahada ya kwanza kuanzia mwezi Oktoba, 2008. Aidha, Serikali imeanza mchakato wa kuzipatia taasisi hizi hati ya idhini (*charter*) na kupata ithibati ya Tume ya Vyuo Vikuu. Aidha mipango ya Wizara ni kuanzisha vyuo vya ufundi katika kila kanda ili kupata mafundi wengi. Wahitimu wa vyuo hivi watakaofanya vizuri wataweza kijiungu na Taasisi za DIT na MIST ili kuchukua shahada za kwanza, Uzamili na Uzamivu. Wizara itaufanyia kazi ushauri wa kuhakikisha kuwa DIT na MIST zinatoa mafunzo ya ufundi sanifu kwa angalau asilimia 60 ya udahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

**NAIBU SPIKA:** Hoja hiyo imeungwa mkono, nilikuwa nataka aweke nukta kwanza. (*Kicheko*)

## **KAMATI YA MATUMIZI**

### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

#### **Fungu 68 – Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia**

Kifungu 1001-Administration and General..... Shs. 2,960,202,403/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Anthony Diallo, Mheshimiwa Godfrey Zambi na Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye. (*Makofi*)

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, ninaomba niende *Vote 68, programme 10, subvote 1001* Kifungu 250100 kuhusu mshahara wa Waziri, ninalo jambo moja. (*Makofi*)

Kwa muda mrefu sana hata Mheshimiwa Waziri tumekuwa tukiwasiliana, tumefungua sasa hivi mpaka wa Tanzania na Msumbiji katika Kata na Kijiji cha Mhukulu eneo la Mkenda na mawasiliano ya simu kule hayapatikani kabisa ukizingatia kwamba ni mpakani na wenzetu kule Msumbiji tayari wao wameshamaliza kazi kabisa, halafu pia nimekuwa nikizungumza sana na Mheshimiwa Waziri suala la msingi la kituo cha *SGR* cha kununulia mazao katika Kijiji cha Mgazini na vijiji vinavyozunguka huko hakuna mawasiliano, halafu liko eneo la Ifinga kule ninakosema hakifikiki kabisa,

hakuna barabara na vitalu vya uwindaji ni vingi, ulinzi wa wanyamaporu tunashindwa kwa sababu hakuna mawasiliano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri aniambie yale mawasiliano tunayowasiliana kila siku nakuomba sasa miaka mitano inakwisha yatakelezwa lini?

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa maelezo kuhusiana na swali la Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tumekuwa na mawasiliano naye ya mara kwa mara kuhusu upelekaji mawasiliano katika maeneo aliyoyataja, tumeshazungumza na makampuni yanayohusika ili kusudi waweze kupeleka mawasiliano katika maeneo hayo na wao wametujulisha kwamba wako katika juhudhi za kufanya utafiti ili kuweza kujua maeneo kamili ya kuweza kuweka hayo mawasiliano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda vile vile nimuongezee maelezo ya ziada kwamba kama nilivyoeleza katika ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa mawasiliano ambao utasaidiwa na mfuko wa *UCAF*, ambao malengo yetu ifikapo mwaka 2010 uwe umekamilika, kilichochelewesha ni makubaliano tu katika mkataba na natarajia kwamba kama nilivyotoa maelezo kwamba utakamilika mapema na nafikiri tarehe 2 ama 3 Septemba, 2008 makubaliano yatatiwa saini, kwa hiyo, kwa nchi nzima jambo la simu baada ya kama kipindi cha mwaka mmoja ninauhakika tutakuwa na maendeleo mazuri zaidi. (*Makofi*)

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru, kwanza napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa maelezo yake mazuri, nilikuwa na mambo mawili nikuwa nataka nipate ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri *programme 10, Subvote 1001*, kwa sababu Wizara imekuwa ikikutana na Kamati ya Bunge ya Kisekta kabla ya kuwasilisha Bajeti yake hapa haikupata hata mara moja kueleza kama inashirikishwa katika mpango wa kubadilisha jina la matumizi kutoka *Celtel* kwenda *Zain*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kuleta taarifa hizo kwenye Kamati ya Kisekta ya Bunge ili ijiridhishe kwamba hakuna ambacho kitakuwa kimepotea yaani Taifa litakuwa limepata hasara kutokana na kubadilishwa kwa jina kutoka *Celtel* kwenda *Zain*, jambo hili limehojiwa na kambi ya upinzani, aidha, pia Kamati ya mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhitimisha hapa Mheshimiwa Waziri hajatueleza lolote kuhusu hoja ya misamaha ya kodi kwa makampuni ya simu na ongezeko la ushuru kwenye *air time* kutoka asilimia saba kwenda asilimia 10 ambayo sisi tunahisi kwamba atakayeumia kutokana na ongezeko hili ni mwananchi wa kawaida ambaye anahitaji kuitumia simu kwa ustawi na maendeleo yake, naomba ufanuzi.

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujibu maswali madogo matatu ya Mheshimiwa Said Amour Arfi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kubadilisha jina kwamba je, Wizara itakuwa tayari kupeleka maelezo kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ili kusudi kuwe na rekodi halisi, jibu ni ndiyo na madhara ya kwamba je, kubadilisha hilo jina kuna madhara yoyote nafikiri Naibu Waziri amelieleza kwa kina sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ametaka kujua hoja ya misamaha ya kodi kwa haya makampuni ya mawasiliano, Misamaha ya kodi ipo tu kwa vile vifaa vinavyoletwa kwa ajili ya ujenzi na sikumbuki ni kwa *percent* gani lakini vinginevyo hakuna misamaha mingine yejote wanalipa kodi zao kama kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swal la tatu ilikuwa juu ya *airtime*, gharama za *air time* zinatokana na gharama za ujenzi wa miundombinu yenyewe, uendeshaji wa miundombinu hii na kwa kutumia minara hii bila shaka mnaona kila mahali kunakuwa na *generator*, kunakuwa na mafuta, kunakuwa na mfanyakazi ni taratibu ambazo kwa kweli zinatakiwa kuboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ongezeko la kodi hii inatokana na kodi zetu ambazo zinatozwa, nafikiri Watanzania ni wa pili kutoka Uturuki ambayo kodi zake za mawasiliano zinafikia asilimia 45 na sisi ni asilimia 30, Bunge hili lilipitisha hili ongezeko la kodi la *airtime* wakati wa mwanzo wa kikao cha kupitisha Bajeti ya Serikali, hata hivyo imani yangu ni kwamba baada ya kuujenga huu Mkongo wa Taifa na kupeleka mawasiliano hadi vijijini, Mkongo huu utapunguza bei za mawasiliano kwa sehemu kubwa sana, hata sasa japokuwa haionekani sawa sawa sasa hivi zinazidi kupungua lakini baada ya kukamilisha mradi huu gharama za mawasiliano zitakuwa zimepungua. (*Makofi*)

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niulize maswali ya ufanuzi tu, katika mchango wangu nilitaka kufahamu kuna mnara umejengwa kati ya kijiji cha Kiseyu, Mzase na Lukole miaka miwili sasa haujafunguliwa, je, Mheshimiwa Waziri atanihakikishia kwamba ni lini mnara huu utafunguliwa na kuanza kufanya kazi na mimi ninahakika mnara huu utasaidia sana wananchi wa Nzase, Berege na Chitemo. (*Makofi*)

Hoja yangu ya pili ilikuwa ni kwamba kulikuwa na mpango wa kuujenga mnara Kata ya Matomondo pale Majami, ili wananchi wa Tambi, Mlembule na Mwenzele waweze kupata mawasiliano na ujenzi wa mnara Godegode, je, Mheshimiwa Waziri ana maelezo gani kwa minara hiyo mitatu.

**MWENYEKITI:** Naomba nikuulize uliadika hayo maneno unayosema?

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Ndiyo Mheshimiwa Mwenyekiti.

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa George Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mnara uliojengwa miaka miwili kati ya Mzese na Lukole, alishatuleta barua na tumewasiliana na kampuni inayohusika, naomba atupe muda ili kusudi tufuatialie tuweze kumpa jibu la uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kulikuwa na maombi ya kujenga minara mingine miwili katika maeneo aliyoyataja moja ikiwa ni Matomondo. Tumepokea ombi hilo lakini tutalifuatilia na kampuni inayohusika ili tuweze kumleteaa jibu ambalo lina uhakika zaidi. (*Makofi*)

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swalii dogo tu la ufanuzi kwa Mheshimiwa Waziri, mwaka jana niliuliza swalii langu hapa Bungeni juu ya upanuzi wa simu za viganjani katika ngazi ya vijiji na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa sababu analifahamu sana Jimbo langu na vijiji vyenyewe alikiri kwamba kuna matatizo makubwa ya usikivu katika maeneo mengi ya Jimbo langu la Chambani, hasa katika vijiji vya Matele, Chwale, Kekewani, Maambani, Mapape, Tumbini, Nteng'ombe, Maweni, Nkenya, Ngezi, Ngagadu na kadhalika na akaahidi kulifuatilia na kulipatia ufumbuzi lakini kwa bahati mbaya hadi leo hatujaona hatua yoyote.

Mimi nilikuwa nafikiri labda eneo langu halivutii sana kibiashara ndiyo sababu yenye na ni kweli kwa sababu eneo langu ni moja katika maeneo ambayo yako nyuma sana kimaendeleo hasa mawasiliano ya barabara na simu, hata wakati mwingine wanapotaka kuomba gari la Mheshimiwa Mbunge kuchukua wagonjwa inakuwa ni mgogoro, nimefarijika kuona kwamba Bajeti ya mwaka huu kumeundwa mfuko wa huduma za mawasiliano kwa wote (*Universary Communication Access Fund - UCAF*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumuuliza Naibu Waziri je, sisi tupo katika mpango huu wa *UCAF* mwaka huu au tupo mpango gani?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimjibu Mheshimiwa Salim Hemed Khamis kwamba ni kweli nafahamu sana Chambani na maeneo yote ambayo anayazungumzia pamoja na kule Kwahala ambako mimi na yeye tunakufahamu vizuri zaidi, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mradi huu wa simu vijijini na Zanzibar ikiwamo Unguja na Pemba napo watakuwepo, hatua za awali zinazofanywa sasa hivi ni kuwapo na mawasiliano na Wizara husika na kuona ni maeneo gani hasa wanahisia tuenze, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hivi karibuni tu tumewaomba watu wa *Vodacom* kwa sababu kule Pemba sehemu nyingi tu haijafika na sehemu nyingine ni lazima upande juu ya mti au juu ya nyumba ndiyo uweze kupata mawasiliano, kwa hivyo na wao wamenihakikishia kwamba watakwendwa muda siyo mrefu ili angalau kuona ni namna gani kuweza kuboresha, lakini ukiacha hivi hivi tu na wao wamenihakikishia

kwamba watakwenda muda siyo mrefu ili angalau kuona ni namna gani wanawenza kuboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiacha hivi hivi tu kama mradi ya *ICT* ambao ni Mkongo tunaozungumza kuna mpango wa kupitisha mkongo wa bahari kwenda Zanzibar na ninahakika hilo likifanikiwa mawasiliano nyumbani Pemba yatakuwa mepesi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira lakini shughuli hizi zinafuatiliwa ipasavyo. (*Makofi*)

**MHE. SALIM HEMED KHATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba atafuatilia na atachukua hatua ili ufumbuzi upatikane, kinachonivunja moyo sasa hivi ni kwamba yale maeneo ambayo yalikuwa na minara sasa hivi kwa mfano Chanjamjawili unayafahamu vizuri umeondolewa, sasa taabu imekuwa zaidi badala ya kupungua kwa nini wanafanya hivi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri naona haya maswali ya mtu kwa mtu haya. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimjibu Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama atakubaliana nami kwamba asilimia 90 kama nilivyosema ya mawasiliano ya simu tunapata kutumia mtandao wa *Zantel* Pemba kuliko sehemu nyinge yoyote hapa Tanzania, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama mnara umeondolewa utakuwa umeondolewa kwa sababu au labda unaleta matatizo kwenye masuala ya usafiri wa anga kwa sababu unatakiwa mnara ule saa 24 taa iwake na inawezekana *location* ya mnara siyo nzuri lakini mimi nitafuatilia njue ni sababu gani zilizofanya mnara wa Chanjamjawili uondolewe lakini ninavyoelewa eneo la Chanjamjawili lina kilima kidogo inawezekana *level* ya mnara ilipowekwa haileti sura nzuri kwa ajili ya wasafiri wa anga. (*Makofi*)

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana, mimi nina-*issue* ambayo nimezungumza kwa mdomo na nimechangia kwa maandishi, Jimbo la Manyoni Magharibi kutoka Itigi kwenda Mgandu watu wa *Celtel* waliweka mtambo lakini katikati ya Itigi na Mgandu ni kilometra 70 watu hawapati mtandao kwa hiyo, inaonekana kwamba inatumika Itigi na *at the end* kule, tatizo hili tumejaribu kuwaeleza wahusika hatujapata majibu, pia kutoka Mgandu wamefanya *survey* muda mrefu ya kupeleka minara kwenda Kalangari, Kiombo, Kirumbi, Mwamagembé mpaka Rungwa kuunganisha na Chunya ni muda mrefu, kwa kweli tunapofika maeneo hayo tunasumbuliwa sana na wananchi kana kwamba sisi ndiyo tuna wajibu wa kupeleka minara hiyo, sasa ningependa kupata ufanuzi juu ya hilo. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa John Lwanji kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa John Lwanji si peke yako mwenye matatizo kama haya, matatizo kama haya pia yanamkumba Mheshimiwa John Chiligati ambaye yeye mwenyewe hapa hawesi kujisemea, yapo maeneo ambayo tayari tumeshafanya ziara na wenyewe makampuni haya, wako wananchi ambao wana simu za mikononi tayari lakini mawasiliano bado hawapati, kuna sehemu ambako Mheshimiwa Mbunge wa Longido na Mbunge wa Loliondo katikati mawasiliano vile vile hayapatikani kutokana na msitu mnene ambao uko pale ni lazima utumie teknolojia inayofaa kwa kila sehemu, si teknolojia yoyote ya mawasiliano inafaa kila pahala, kuna sehemu zingine ambazo huwezi kupata kama sehemu zingine vile vile za Mheshimiwa Ali Tarab Ali, msitu wa Ngezi huwezi vile vile kupata mawasiliano ni lazima upitie baharini, lakini nimhakikishie Mheshimiwa John Lwanji tutaendelea kuwaomba tena wenzetu kwa sababu tunawaandikia, tunawaambia na ninawahakikishia wananchi wa Jimbo la Mheshimiwa John Lwanji wampe raha na mvumilie suala hili si la kwake ni suala la makampuni ambalo sisi Wizara ya mawasiliano tutalishughulikia. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, kuna kukosa kura kwa sababu ya simu?  
(*Makofi/Kicheko*)

**MHE. ANTHONY M. DIALLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mchango wangu wa maneno na wa maandishi nilizungumzia suala la uhamishwaji wa hisa za *Celtel Tanzania*, lakini maelezo ambayo tumeepata kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri ni mambo ya *brand change* ambayo si tatizo ni *domain* ya kampuni yenyewe kubadilisha majina ya *product*, mimi nilichokuwa nauliza *TTCL* ilikuwa na *share* na *in-share* *Celtel Tanzania*, mbia wao mwingine alikuwa *Celtel International* sasa *Celtel International* akaamua kuuza *Celtel* ambayo *ina-include* ndani ya *Celtel Tanzania* na katika mauzo hayo aliuza ile *value* ya *share* karibu mara mbili ya *share* za *Celtel International* wakati ule ambayo inaungana pamoja na *Celtel Tanzania*, sasa *for that particular transaction definitely share* za *TTCL* kwenye *Celtel* zilitakiwa kuongezeka na zenyewe *in value* hiyo ni *normal* duniani kote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliuliza kwamba tulipata *share* zetu *TTCL* kwenye *Celtel Tanzania* ziliongezeka kwa kiwango gani na kama hazikuongezeka kwa nini ile *benefit* ya *transaction* hiyo haiku-*benefit* *TTCL* kama *shareholder* wa *Celtel Tanzania*, hilo ndilo lilikuwa swali langu na sikujibiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili Waheshimiwa Wabunge hapa tumewaomba kuwe na *registration* ya *simcard* na tukakubaliana kweli, lakini kwenye mpango wangu wa maandishi nikawauliza sheria najua italetwa kama itahitajika au taratibu ambazo *TCRA* wangeziweka tutatumia vitambulisho gani kwa sababu Tanzania hatuna vitambulisho, nikauliza tutatumia hivi vyeti vyaya kupigia kura? Na kama ni hivyo watoto wasio na umri zaidi ya miaka 18 ina maana hawatahusika ku-*own* simu za mikononi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikaomba zaidi kwamba teknolojia iko *in place* sasa hivi kwamba nikiibiwa simu naripoti kwa *operator*, kwa sababu unapoweka *simcard* inapotoa ripoti kwenye ile namba kwa *operator* huwa inapeleka *specific* namba ya ile *handset which means* nikiripoti simu imeibiwa wana uwezo wa kuiua ile simu, hili tatizo linasababisha wizi kuwa ndiyo mchezo *as a result* tunaharibu mila na tunaharibu Watanzania kwa nini teknolojia hii isitumike kuzuia wizi wa *handset* hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Anthony Diallo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nianze na lile la pili la *registration* ya *simcard*, kama nilivyokuwa najibu hapa Bungeni kwamba tutatumia vitambulisho vifuatavyo, kama *passport* zetu, *bill* za maji, vitambulisho vya benki, lakini cha msingi ni kwamba sisi tunategemea sheria hii au *bill* hii imalizike Bunge lijalo ili tuwe na sheria madhubuti ambayo itasaidia *TCRA* kusimamia masuala haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba iko mitambo ambayo ni *programu* zimo ndani ya makampuni ya simu kwamba ukiibiwa simu ukibonyeza namba siwezi kukumbuka vyema lakini ni kama \*006# ukibonyeza itatoka ile namba ya namba ya simu yenewe na wametuambia wataalamu sina uhakika kama ni kweli sitaki niwe *quoted*, kwa upande mwengine hii simu ni ya nani ina *registration* namba na tunauhakika tukianza shughuli hizo makampuni ya simu yote yatapaswa *ya-switch on* hiyo mitambo ili iweze kufanya kazi ya *registration*, lakini *at present* vile vile mtu akiibiwa simu akienda kupeleka mawasiliano kwamba simu yangu imeibiwa kama anaijua ile namba yake wanaweza kui-block ile simu lakini faida nyingine katika zile namba kumi na tano wanasema wataalamu kwamba namba saba na ya nane inasema maneno mengi, ikiwa ina sifuri, sifuri, ni kwamba simu zile zimetengenezwa katika viwanda, kama ina sifuri moja simu zile zimetengenezwa kwenye maeneo ambayo yanajilikana ni *reputable* lakini ikiwa na namba tatu - nne, tatu - sita, nane-sita ni kwamba hizo hazieleweki sana sitaki niseme zinaeleweka halafu nikapelekwa mahakamani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hii ni faida kwa wananchi unaponunua simu ni vizuri ubonyeze hizo namba zilizokuambia utazame je, hii simu ni kweli ni nzuri na hiyo pia itakusaidia wewe kwamba una *quality handset* ya kukusaidia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili napenda nimwambie Mheshimiwa Anthony Diallo tunalishughulikia ipasavyo. Lakini sisi tulipouza ile *share* yetu ya asilimia 25 tuli-realize shilingi bilioni 28 lakini hilo hilo la *details* tunalifanyia kazi na tutakujibu ipasavyo. Kikosi kazi kinafanya *details* hizi pamoja na *details* za mwekezaji tuliomweka sasa hivi mwendeshaji wa *TTLC* anaendesha hivi sasa pamoja na bodi ya *TTCL* namna inavyofanya shughuli zake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anthony Diallo nadhani ameridhika. Mimi Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa aliposema mngeleta kwenye Kamati nilifikiria angeleta kitu kama hiki. Kusema jina kutoka *Celtel to Zain* sidhani kama muhimu sana. Lakini hili ni muhimu. Kwa sababu itawasaidia Wabunge kuelewa kwa undani kabisa. (*Makofi*)

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niulize mambo mawili ya ufanuzi.

Kwanza, naomba niseme kwamba kumekuwa na dhana ambayo pengine siyo nzuri sana hasa kwa Mbunge wa Mbeya anaposimama na kuzungumzia suala la Chuo Kikuu Mbeya (*MIST*) kwamba inawezekana kuna masuala ya kisiasa. Mimi naomba dhana hiyo iondoke kwa sababu tunazungumzia chuo hicho kwa maslahi ya Watanzania wote. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Hiyo dhana ameleta nani?

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Kuna mambo ya kufikirika ya namna hiyo.

**MWENYEKITI:** Basi hayapo katika Bunge, hakuna kufikirika, uhuru wa kusema unao. Kwa hiyo, sisi hatuna hiyo. (*Makofi*)

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama historia ambavyo Mheshimiwa Waziri amesema na mimi naomba nirejee hapa kwamba kumekuwa na matamko mengi ya viongozi wakuu wa nchi waliotangulia, moja ni Mheshimiwa muasisi wa Taifa hili Marehemu Mwalimu Julius Nyerere na Mungu amrehemu alipolala. Alishawahi kutoa tamko kwa maana ya kukifanya chuo hicho kuwa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia. Lakini pia Mheshimiwa Jakaya Kikwete alipokuwa anazungumza kwenye Uwanja wa Samora mwezi wa tano mwaka 2005 alizungumza nia yake ya kuona kwamba tunakuwa na vyuo vikuu vingi sana pamoja na Mkwawa kukifanya chuo kikuu, tayari Mkwawa imekuwa *constituent college* ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, lakini pia alizungumza na Chuo cha Mbeya kuwa Chuo Kikuu cha Ufundi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni viongozi wengi na hususan Waziri Mkuu wa sasa alikuwa anasisitiza sana kuwa na shule nyingi za sayansi kuanzia shule za sekondari na kwa maana hiyo kuna umuhimu hata wa kuwa na Vyuo Vikuu vya Sayansi na Teknolojia. Sasa pamoja na haya yote ambayo Mheshimiwa Waziri ametueleza hapa kwamba kulikuwa na *Biko* ambao ni washauri waelekezi ambao walitoa mapendekezo mbalimbali. (*Makofi*)

Lakini nadhani bado kuna sababu ya kuwa na vyuo vikuu vya sayansi na teknolojia vingi maana ya kwamba Mbeya, *DIT* na vyuo vingine kwa sababu bado tuna shida ya mafundi na nia yetu siyo kwamba vyuo hivi viache kuwafundisha hawa *mathematicians* siyo azma hiyo, ni kwamba vinaweza vikafanyakazi ya kutoa shahada lakini pia kutoa *degree* katika maeneo hayo. Waziri anatueleza nini katika hiyo, anatoa ufanuzi gani zaidi katika jambo hilo?

Lakini jambo la pili, kuna taasisi mbili hapa ambazo zinashughulikia na ithibati za Vyuo Vikuu. Kuna *Tanzania Commission for Universities (TCU)* na *NACTE*. Sasa *NACTE* ndiyo inayosimamia vyuo hivi vya ufundi, lakini *TCU* inasimamia vyuo vikuu. Ni mahali gani duniani ambako taasisi mbili ambazo zinasimamia uendeshaji wa vyuo vikuu yaani kwa maana ambazo zinatoa ithibati ya uendeshaji wa shahada hizi hapa duniani? Kuna tatizo gani sasa la kufanya ithibati ya elimu ya shahada ikatolewa na taasisi moja kwa maana ya *TCU* Waziri anaona kuna tatizo gani, naomba ufanuzi. Ahsante. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa ufanuzi kwa maswali mawili yaliyoletwa na Mheshimiwa Godfrey Zambi kama ifuatavyo, kwa bahati mbaya nilipokuwa natoa taarifa yangu sikufikia mwisho ambako kungekuwa kumemuelewesha baadhi ya masuala anayoyaaulizia. (*Makofi*)

La kwanza, ningependa kusema kwamba kauli ya muasisi Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na kauli alioitoa Rais wetu wa awamu ya nne alipokuwa kwenye kampeni Mkoani Iringa, zote zinaheshimika na ni misingi imara ambayo tunajenga hoja hii. Nilimalizia kwa kusema kwamba napenda kutamka ya kwamba mchakato unaendelea ili kuzifanya Taasisi za Dar es Salaam yaani *DIT* na *MIST* kuwa na hadhi ya Vyuo Vikuu kwa kutoa mafunzo ya Stashahada, Shahada ya Kwanza, Shahada ya Uzamili na Uzamivu. Taasisi hizi kama ilivyo katika taasisi nyingine duniani kama vile *Mastisearch Institute of Technology, The Indian Institute of Technology, The Korean Institute of Science and Technology, The Indian Institute of Science* na kadhalika ziko nyingi, zitapewa hati idhini yaani zitakuwa *licensed, zitakuwa charted.* (*Makofi*)

Lakini pili, ithibati yake itatolewa na chombo kinachotoa ithibati ya Vyuo Vikuu sikutamka jina. Maana yake ni nini huku katika uratibu wa *NACTE* nao wana madaraka. Lakini kwa kweli sijawahi kuona nchi yoyote ambako mnakuwa na vyombo viwili vya kutoa shahada. Kama kweli tunataka ubora lazima tuunganishe hizi mbili ili ziweze kufanyakazi mojawapo. Kwa upande wa *NACTE* tutashauriana na Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundu kwa sehemu zote hizi kwa sababu zinamhusu ili kusudi ile ya *NACTE* iishie *diploma* ya juu. Lakini unapokwenda kwenye *degree we want quality* watu ambao akisema ana *degree* fulani siyo ya Tanzania tu lakini atakwenda hata nchi nyingine yoyote lazima tuwe na chombo kimoja cha ithibati. Nilisema kwamba *tendency* mara nyingi kusema Chuo Kikuu na nimeshatoa *definition* pale kati ya *Institute* na Chuo Kikuu. Pamoja na kwamba vyote vina hadhi sawa na kweli *institute* zingine duniani ni bora kabisa kuliko Chuo Kikuu. (*Makofi*)

Lakini shida yetu vile vile tunahitaji hawa watalaam wanaoweza kutoka chuoni na kwenda kufanyakazi. Wameshapata mafunzo ya kutosha ya vitendo kuna maabara, kuna karakana na vifaa mbalimbali. Tukisema ukiacha tu hivi vyuo vikienda hivi hivi nalo hilo linaweza kuwa tatizo. (*Makofi*)

Lazima tu- *prescribe ratio* kwa sababu nia yetu ni kutoa hawa watalaam ni vyema tukasema angalau 60% watakuwa hawa ngazi za kati na 40% ndiyo wanaweza kuendelea kwenda juu mpaka kwenye *degree*. Vinginevyo tutaendelea hivi hivi, leo hii tuna vyuo vikuu karibu 34 hapa Tanzania pamoja kule *college* zake hata kama Watanzania wote tungekuwa na *degree* lakini kama hakuna ujuzi wowote ambao unaweza kuutumia kwa kuigeuza nchi hii tutakuwa tunatwanga maji katika kinu. (*Makofi*)

Mimi nashauri huu mkazo tuuveke na Wizara yangu italeta mpango wa kuanzisha vyuo vya ufundi katika kila kanda, hivi vyuo vyenyewe vitaishia *higher diploma*. Lakini hivyo ndiyo vitakuwa ndiyo chanzo cha wanafunzi watakaoingia kwenye vyuo hivi kama *MIST* na *DIT*. Vinginevyo kwa hali ya sasa ambapo tunachukua vijana waliotoka *form six* anakwenda *DIT*, anakwenda *MIST* ni sawa na yule anayekwenda *College of Engineering and Technology University of Dar es Salaam*, huyu hujapata hata *back ground* ya mambo ya ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani tulikuwa na *secondary school* za ufundi, kulikuwa na *secondary school* za kilimo lakini tumefuta yote hiyo kwa hiyo sasa hivi tunaowapeleka wanasema yuko *MIST*, yuko *DIT*, pengine tofauti kati ya hao na wale wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ama Ardhi ni ndogo sana, kwa hiyo, nilifikiri kwamba tuweke msisitizo huu ili kusudi tuweze kutoa hao wahitimu. Sasa hili nafikiri limejibu na ithibati ambayo Mheshimiwa Mbunge ameliuliza. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya mwisho katika kuchangia katika hoja hii ya Waziri.

**MWENYEKITI:** Siyo ya mwisho, tuko kwenye Kamati ya Matumizi.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Ahsante, lilinigusa sana suala la *accreditation*, ambalo Mheshimiwa Waziri sasa hivi amelizungumzia vizuri. Kwa jumla kwa kweli maelezo yake ya leo tofauti na mwaka jana leo yametupa ufanuzi zaidi na hasa kuhusu suala la *MIST Mbeya*. (*Makofi*)

Nimefurahi vile vile kwamba amesema yeye ni mdau katika suala hili la *MIST Mbeya*. Kwa hiyo, ieleweke kwamba ni wadau sisi wote siyo mdau mtu mmoja wala halimhusu mtu mmoja ni suala la Kitaifa. Kwa hiyo, mimi napenda nimpongeze katika hilo na kwamba amelifafanua zaidi kwa mwaka huu na naamini kabisa kwa sababu ni mdau basi tutaona mabadiliko ambayo yatafanyika kuhusu suala zima la uendeshaji wa *DIT* pamoja na *MIST Mbeya*.

Naomba vile vile nimkumbushe kwamba fedha hii ya uendeshaji hasa hasa katika *development* kwa upande wa *MIST Mbeya* na vile vile upande wa *DIT* hajajionyesha vizuri katika vitabu naomba atakapokuja safari ijayo atueleze namna gani fedha hiyo imetumika, lakini kuweka mpango thabiti kwa sababu ya ahadi aliyoitoa hapa katika maelezo yake na katika maazimio yake aeleze mwaka ujao je, vyombo hivi au taasisi hizi zitapewa fedha ya kutosha ili ziweze kufanyakazi ya maendeleo badala ya kusisitizia tu suala la matumizi ya kawaida.

Je, Waziri anatoa ufanuzi gani au maelezo gani kuhusu suala hili? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Nashukuru sana naomba Waziri asijibu kwa sababu sasa hivi tunashughulikia Bajeti ya mwaka 2008/2009 kama atakuwa na uwezo wa kuzungumzia mwaka 2009/2010 sidhani na halafu mengine nadhani ni maoni tu kwamba umeridhika na majibu aliyotoa kwa swali la Mheshimiwa Godfrey Zambi. Kwa hiyo, naomba Waziri asijibu. (*Makofi*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1002 – <i>Finance and Accounts</i> ...	Sh. 562,660,646/=
Kifungu 1003 – <i>Policy and Planning</i> ...	Sh. 1,135,747,389/=
Kifungu 2001 - <i>Communication Division</i> ...	Shs. 606,381,693/=
Kifungu 3001 - <i>Higher Education</i> ...	Sh. 0
Kifungu 3002 - <i>Technical Education</i> ...	Sh. 0
Kifungu 3003 – <i>Science and Technology</i> ...	Sh. 16,027,981,869/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo vilipitishwa na Kamati ya Matumizibila mabadiliko yoyote*)

#### **Fungu 68 – Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia**

Kifungu 1001- <i>Administration and General</i> ...	Sh. 640,000,000/=
Kifungu 1003 – <i>Policy and Planning</i> ...	Shs. 215,167,000/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 2001 – *Communication Division* ... Sh. 17,212,842,000/=

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *vote 68 sub vote 2001 item 4208 na 4283* kwa pamoja katika *item hizi ambazo zinazungumzia suala la ICT* hakuna fedha za nje na katika Bajeti Mheshimiwa Waziri katueleza kwamba hiki ni kitengo muhimu sana kwa maendeleo ya nchi na bila shaka inatakiwa mambo mengi hapa yafanyike ili kukamilisha vitengo hivi muhimu. Kilichonishangaza hapa ni kuwa katika vitengo vingine kwa mfano *research and education for democracy in Tanzania* kuna fedha za kigeni sasa swali hapa hazikuombwa au zimeombwa hazikutolewa au kwa nini haukutunishwa mfuko huu wa kitengo hiki cha *ICT*?

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salim Hemed Khamis kama ifuatavyo, ni kweli hapa hazionekani fedha za nje, fedha hizi shilingi bilioni 17 zinazoonyeshwa ni fedha za ndani ambazo zinatumika katika matayarisho na kulipa *compensation* za mahali ambapo mkondo wa mawasiliano utapita. Lakini fedha za ujenzi kama nilivyotamka katika taarifa yangu kiasi cha shilingi bilioni 170 ziko katika mchakato wa kupatikana kwa mkopo wa riba nafuu kutoka Uchina kulikuwa na kipengele kidogo kilikuwa kinashughulikiwa kwa kisheria lakini hicho nacho kimefikia

kwa karibu mwishoni na kama nilivyosema kati ya tarehe 3 na 4 mwezi Septemba, makubaliano yatatiwa sahihi na kazi kuanza mara moja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, ni *the national ICT infrastructure*. Ile nyingine 4208 *ICT Development* maeleo ni hayo hayo? Katika kifungu hiki kina *items* mbili.

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho kinatumika kwa ajili ya kununua vifaa na hasa kompyuta kwa ajili ya maofisi.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 3001 – *Higher Education* ... ... .... ... ... ... ... ... ... Sh. 0  
Kifungu 3002 – *Technical Education* ... ... .... ... ... ... ... ... Sh. 0

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 3303 - *Science and Technology*... ... Sh. 3,534,833,000/=

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *sub-vote 3003* kifungu namba 4384 Dar es Salaam, *Institute of Technology* nimeona imepangiwa shilingi milioni 60. Nilitaka tu nijue ni kwa ajili ya kufanya kazi gani maana naona ni fedha ndogo sana ukilinganisha na *institute* yenyewe ilivyo muhimu katika uchumi wa nchi yetu. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Peter Serukamba kama ifuatavyo, kwanza, nilikwishatoa maeleo nilipokuwa nahitimisha hapa hoja yangu, lakini ni kwamba fedha hizi zimetengwa kwa ajili ya kuanza kazi za awali, kwa ajili ya kupima udongo, kupata michoro kwa ajili ya jengo ambalo linatarajiwa kujengwa pale *DIT*. (*Makofi*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

(*Bunge lilirudia*)

## TAARIFA

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka 2008/2009 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo basi, naliomba Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. (*Makofi*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)  
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa 2008/2009 yalipitishwa na Bunge*)

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia imepitishwa makadirio yake. Kwa hiyo, naomba niwapongeze Waziri na Naibu Waziri wake na wataalam waliopo katika Wizara hii. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kama mlivyoomba Wizara hii ni ya kisayansi sana na kuna watu waliokuwa wamesema ni vizuri mkaitangaza vizuri kwa sababu inaelekeea hata ndani ya Bunge bado inatupa shida. Kwa hiyo, bidii ya kutueleza Wizara hii sasa hivi mipaka yake ni ipi na shughuli zake ni zifi nadhani mkifanya itatoa elimu nzuri zaidi kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi wanaohusika. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, elimu haina mwisho. Tukikaa kwenye Kamati ya Matumizi pale tunapitisha matumizi, mkiniletea habari yoyote ndefu, mimi siwezi kuisoma. Kwa sababu nikisoma sitasikiliza hoja zinazozungumzwa na sababu yake kubwa ni lazima usikilize kwa sababu hapo ndipo tunapofanya maamuzi. Kwa sababu itakuwa kosa kabisa kwa kitu kuendelea kusoma barua zinazotoka kwa Waheshimiwa Wabunge halafu ukaacha kusikiliza hoja zinazotolewa na yule anayeuliza, halafu unafanya uamuzi wakati hapa ndipo tunapofanya maamuzi. Kwa hiyo, kuna walioandika barua samahani sikuzijibu wala sikuziona ndiyo ninaziona sasa. Kwa hiyo, naomba wakati wa Kamati ya matumizi msiletie barua, kwa sababu hazisomeki zile barua. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, lakini la pili, hoja ya Mheshimiwa Cynthia Ngoye kwa nini nimeomba Mheshimiwa Waziri asijibui. Kwa sababu mtoa hoja alikuwa anaomba fedha na kabla hatujampa fedha na alikuwa anazungumzia fedha ya mwaka 2009/2010 haiwezekani. Katika kipindi hiki tunafikiria matumizi ya fedha zilizopo ndani ya kitabu. Angezungumza wakati wa kuchangia tu huko hayo yangetuwa mawazo yake kama mnavyosema fedha hizi hazitoshi na nini na nini. Lakini tukiwa kwenye Kamati ya Matumizi hawezi kusimama mtu kusema kwamba naomba kutoa hoja ziongezwe fedha ama nini haiwezekani ndiyo hizi zilizopo. Kwa hiyo, ndiyo maana nikamwambia kwamba hiyo ninamwomba Waziri asijibui kwa sababu ilikuwa haifiti katika kazi tuliyokuwa tunafanya.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, jioni kama mtatambua nadhani hamjapewa tumefanya mabadiliko ya ratiba yetu ya Bunge kuanzia sasa mpaka

tutakapomaliza Bunge. Jioni Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa itawasilisha hotuba yake ya Bajeti, lakini watamaliza kesho asubuhi tarehe 19 Agosti, 2008 na kesho jioni watawasilisha hotuba yao Wizara ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira watalimaliza tarehe 20 Agosti, 2008. Halafu tarehe 21 Agosti, 2008 asubuhi tutakuwa na ugeni, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atalihutubia Bunge. Kwa maana hiyo Wizara itakayowasilisha hotuba yake ya Bajeti tarehe 21 Agosti, 2008 jioni ni ya Mambo ya Nje na kumaliza tarehe 22 Agosti, 2008 mchana. (*Makofi*)

Halafu tarehe 22 Agosti, 2008 jioni itawasilisha hotuba yake Wizara ya Fedha na Uchumi wao watamaliza tarehe 25 Agosti, 2008 siku ya Jumatatu jioni. Kwa sababu asubuhi ya tarehe 25 Agosti, 2008 Rais wa Comoro atalihutubia Bunge. Kwa hiyo, hivyo ndivyo tutakavyoendelea, nadhani mtagawia hiyo ratiba mchana. Lakini jioni tutakuwa na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(*Saa 6.25 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

*Hapa Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alikalia Kiti*

## **HOJA ZA SERIKALI**

### **Makadirio ya Fedha za Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama ambavyo mnaona ratiba yetu ilibadilika na kwa hiyo, Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, imebidi ianze kwa jioni hii. Tutaendelea Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa atahitimisha hoja yake mchana ikikaribia saa 7 mchana halafu ndiyo tutaingia katika Wizara nyingine. Kwa hiyo, sasa naomba kumwita mtoa hoja Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. (*Makofi*)

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na uzima na hivyo kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu leo ikiwa ni Bunge la Bajeti ya Tatu kwa Serikali ya awamu ya nne. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuchukua nafasi hii kwa moyo wa dhati kumshukuru Rais, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuniamini na kunteua kuongoza Wizara hii nyeti ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa mara baada ya kuundwa kwa Baraza jipya la Mawaziri. Naahidi kufanya kazi hii kwa bidii, uaminifu na uadilifu mkubwa katika kufanikisha malengo ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, kutokana na Taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kuititia na kisha kuitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2008/2009. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mbunge wa Muleba Kusini, kwa kazi nzuri ya kuchambua mapendekezo na kutoa ushauri katika maeneo mbalimbali wakati wa kuititia Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Ushauri wa Kamati hii umesaidia sana katika kuboresha Bajeti inayowasilishwa leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008 Bunge lako Tukufu lilipata msiba wa Marehemu Salome Mbatia, aliyekuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Marehemu Benedict Losurutia aliyekuwa Mbunge wa Kiteto. Aidha, wakati Bunge lako Tukufu likiendelea na Mkutano huu, lilipata msiba wa Marehemu Chacha Zakayo Wangwe, aliyekuwa Mbunge wa Tarime. Kama wenzangu waliotangulia, napenda kuchukua fursa hii kuwapa pole ndugu, jamaa, marafiki, familia na wananchi wote wa majimbo ya Marehemu hao. Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, nami naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Mpanda Mashariki, kwa kuteuliwa kwake na Rais na kisha kuthibitishwa na Bunge lako Tukufu kwa kura nyingi kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia nampongeza kwa Hotuba yake ya kina ambayo imeelezea mafanikio ya utekelezaji wa shughuli za Serikali katika mwaka 2007/2008. (*Makofi*)

Aidha, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wenzangu kwa kuteuliwa na Rais kuwemo kwenye Baraza la Mawaziri na kwa Hotuba zao walizokwishawasilisha na kuitishwa na Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008 Bunge lako lilipata Wabunge wanne wapya amba ni Mheshimiwa Benedict Ngalamu Ole-Nangoro, aliyechaguliwa kuwa Mbunge wa Kiteto, Mhe. Dr. Christine Gabriel Ishengoma, Mheshimiwa Mchungaji Dr. Getrude Rwakatare na Mheshimiwa Al-Shymaa John Kwegyr, walioeteuliwa kuwa Wabunge. Wote nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa malengo ya Bajeti ya mwaka 2007/2008, wakati wa kufunga mjadala kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2007/2008, Mwenyekiti wa iliyokuwa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Ulinzi na Usalama, kwa niaba ya Kamati yake na Waheshimiwa Wabunge, katika kuchangia mjadala huo, walitoa maelekezo na ushauri wa jinsi ya kuboresha zaidi utekelezaji wa majukumu ya Wizara yetu.

Naomba kutoa taarifa kwamba tulizingatia maelekezo na ushauri huo kulingana na uwezo kwa kadri Bajeti ilivyoruhusu. Hivyo, pamoja na kutoa maelezo kuhusu mapitio ya utekelezaji wa malengo ya Bajeti ya mwaka 2007/2008, taarifa rasmi ya utekelezaji wa ahadi tulizotoa hapa Bungeni imeandaliwa na Waheshimiwa Wabunge wamepatiwa nakala kama sehemu ya Hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, shabaha kuu za ulinzi wa Taifa letu ni hizi zifuatazo, kwanza kuwa na Jeshi dogo, lenye vifaa vya kisasa, madhubuti na lenye utayari na utimamu kivita kwa ajili ya majukumu ya ulinzi wa nchi, ambayo ni pamoja na haya yafuatayo:-

- (i) Kulinda uhuru na usalama wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania dhidi ya adui.
- (ii) Kushiriki katika majukumu ya kulinda amani duniani.
- (iii) Kusaidia Mamlaka za Kiraia katika kukabiliana na maafa ili kuokoa maisha na mali za wananchi.
- (iv) Kuandaa na kuongoza umma wa Watanzania katika jukumu la ulinzi wa Taifa dhidi ya adui.

Mheshimiwa Spika, pili, kuwa na Jeshi la Kujenga Taifa lenye uwezo wa hali ya juu na kuwa chuo cha kujenga uzalendo na ulinzi kwa vijana wa Kitanzania, kuwaandaa vijana hao katika uzalishaji mali na ufundi na kuimarisha usawa na umoja wa Watanzania, chimbuko la ajira kwa vyombo vya ulinzi na usalama hapa nchini na chombo cha kuzalisha mali.

Mheshimiwa Spika, tatu, kuwa na uwezo wa kujitegemea katika bidhaa na teknolojia ya kijeshi na nne, kuishi kwa amani na utulivu na nchi nyingine duniani, hasa nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, jukumu la Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni kuhakikisha shabaha hizo zinafikiwa kwa kufanya mambo yafuatayo:-

- (a) Kuajiri askari wa kutosha wenye sifa zinazohitajika kwa ajili ya ulinzi wa nchi na kuwapatia mafunzo na mazoezi ya kijeshi na kutoa mafunzo ya mgambo kwa umma wa Watanzania.
- (b) Kulipatia Jeshi la Wananchi vifaa na zana bora za kisasa, na kuzihifadhi, kuzitunza, kuzitengeneza na kukarabati zilizopo ili ziweze kutumika katika majukumu ya ulinzi wa nchi.
- (c) Kuboresha na kuendeleza shughuli za utafiti na maendeleo ya teknolojia ya kijeshi.

(d) Kujenga mazingira bora ya kufanya kazi na ya makazi kwa wanajeshi na vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa.

(e) Kuwapatia wanajeshi na vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa huduma na mahitaji muhimu katika viwango vinavyostahili na kwa wakati.

(f) Kuendeleza ushirikiano wa kijeshi na kiulinzi kati ya Tanzania na nchi mbalimbali duniani.

(g) Kutoa mafunzo ya uzalendo, ukakamavu, ufundi stadi, kilimo na taaluma nyinginezo kwa vijana wanaojiunga na Jeshi la Kujenga Taifa.

(h) Kuboresha utendaji kazi wa watumishi wa umma ndani ya vyombo veya ulinzi, kwa kuwapatia huduma na stahili zao mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha utekelezaji wa mambo hayo, katika mwaka 2007/2008 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ilijiwekea malengo ya Bajeti yafuatayo:-

(a) Kununua vifaa na vitende kazi kwa ajili ya Jeshi la Wananchi na kuwapatia wanajeshi na askari wa mgambo mafunzo ya kijeshi ya kinadharia na vitendo.

(b) Kulipia huduma muhimu za maji, umeme, simu na mahitaji mengine kama vile mafuta, vilainisho, vipuri na matengenezo ya magari, mitambo na vifaa mbalimbali.

(c) Kuwapatia wanajeshi, watumishi wa umma, vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa stahili zao kwa wakati.

(d) Kuendeleza ushirikiano wa kijeshi na kiulinzi kati ya nchi yetu na nchi mbalimbali duniani kupitia nchi moja moja, ushirikiano wa kikanda na kimataifa na kutekeleza makubaliano yaliyofikiwa katika ushirikiano huo.

(e) Kuboresha mazingira ya kufanya kazi na makazi kwa wanajeshi na vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa.

(f) Kuendeleza shughuli za utafiti na maendeleo ya teknolojia ya kijeshi katika viwanda veya mashirika ya Mzinga na Nyumbu.

(g) Kuendeleza juhudzi za kuzuia maambukizi mapya ya UKIMWI kwa wanajeshi na familia zao, watumishi wa umma na vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa na kutoa huduma ya dawa na lishe kwa waathirika.

(h) Kuendeleza mafunzo ya uzalendo, ukakamavu, ufundi stadi, kilimo na taaluma nyinginezo kwa vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa.

(i) Kuboresha utendaji kazi wa watumishi wa umma kwa kuwapatia mafunzo ya kuongeza ujuzi pamoja na kuboresha mazingira ya kazi.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa malengo hayo katika mwaka 2007/2008 ulikuwa kama ifuatavyo, kwanza ni kuhusu mafunzo na Mazoezi ya Kijeshi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni wajibu wa Serikali kuhakikisha wanajeshi na wananchi wanapatiwa mafunzo yanayostahili ili wawe na uwezo wa kulinda uhuru na usalama wa nchi yetu na kushiriki katika majukumu mengine ya ulinzi wa nchi kama nilivyoeleza hapo awali. Hivyo, katika mwaka 2007/2008, Jeshi la Wananchi limetoa mafunzo mbalimbali kwa maafisa na askari wake ndani na nje ya nchi kulingana na kipaumbele na mahitaji. (*Makofi*)

Aidha, Jeshi limeendelea kuweka mazingira mazuri ya maafisa na askari wake kupatiwa mafunzo ili wawe na utaalam na ujuzi wa hali ya juu katika fani zao. Hii ikiwa ni pamoja na kuviweka vyuo vyake mbalimbali katika hali nzuri. Vile vile Jeshi la Wananchi liliendelea kuandaa umma wa Watanzania katika jukumu la ulinzi wa Taifa kuitia mafunzo ya mgambo sehemu mbalimbali nchini. Mafunzo hayo ni pamoja na mafunzo ya awali, kozi za uongozi, uundaji wa kombania za vijijini na ukamilishaji wa mazoezi ya kivita katika kanda nne za ulinzi nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia katika mwaka huo Jeshi la Wananchi kwa msaada wa majeshi ya nchi rafiki liliendesha mafunzo maalum yafuatayo kwa maafisa na askari wake:-

(i) Mafunzo ya *Marine Special Force* yaliyoendeshwa na wanajeshi toka Jamhuri ya Watu wa China.

(ii) Mafunzo ya Polisi Jeshi kwa maafisa na askari waliokwenda Lebanon yaliyoendeshwa na wanajeshi toka Marekani.

(iii) Mafunzo ya kikosi cha Ulinzi wa Amani kwa maafisa na askari watakaokwenda Darfur nchini Sudan yaliyoendeshwa na wanajeshi toka Marekani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupatiwa mafunzo ya kinadharia ni muhimu kwa wanajeshi kuwezeshwa kufanya mafunzo kwa vitendo yaani mazoezi. Katika mwaka 2007/2008 maafisa na askari wa Jeshi la Wananchi katika ngazi za kikosi, brigedi na kamandi wamewezeshwa kufanya mazoezi katika kiwango cha kuridhisha.

Aidha, katika mwaka huo Jeshi la Wananchi liliendesha mazoezi mbalimbali ya medani na ya Kituo cha Uamrishaji yaliyojulikana kama Linda Jiji, Songa Mbele, Rudisha Imani, *Brain Storm, Transfer Flight*, Mivumo Mingi na Nguvu Mpya. Mazoezi ya Mivumo Mingi yaliyofanyika mkoa wa Tanga na Nguvu Mpya yaliyofanyika Kanda ya Kusini yote yalifanywa na mgambo chini ya usimamizi wa Jeshi la Wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mafunzo na mazoezi hayo yameendelea kuwaimarisha na kuwaandaa wanajeshi wetu na umma wa Watanzania katika utayari kivita kulinda nchi

yetu dhidi ya adui. Aidha, mafunzo na mazoezi hayo yameendelea kujenga wanajeshi wetu umahiri na kujiweka tayari kushiriki operesheni za kulinda amani katika nchi zenye migogoro watakapohitajika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili ni kuhusu vifaa na vitendea kazi. Kiutendaji, baada ya mafunzo kitu kingine muhimu kwa jeshi ni vifaa na vitendea kazi vitakavyoliwezesha kutekeleza majukumu yake. Changamoto kubwa kuliko zote inayoikabili Serikali kwa sasa kuhusu ulinzi wa Taifa letu ni kulinunulia Jeshi la Wananchi vifaa na vitendea kazi bora vyta kisasa kwa ajili ya ulinzi wa nchi. Serikali imeendelea kulipatia Jeshi letu mahitaji haya muhimu, hatua kwa hatua, kulingana na uwezo uliopo, kwa kuzingatia vipaumbele katika mpango wa muda mrefu wa kulijenga Jeshi kivifaa na kimafunzo na bila kuathiri vipaumbele vingine vyta Kitaifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia haya, katika mwaka 2007/2008, Serikali imenunua baadhi ya vifaa na vitendea kazi muhimu ambavyo vimesaidia kuboresha utendaji wa Jeshi. Lakini eneo lililokuwa na kishindo (*impact*) kikubwa ni usafiri na usafirishaji ambapo ununuzi wa magari, kwa kiwango cha kuridhisha, umeboresha uwezo wa Jeshi na wanajeshi kwa ujumla kusafiri kutoka sehemu moja kwenda nyingine kwa haraka na kwa urahisi. Serikali itaendelea kuimarisha mafanikio yanayopatika katika nyanja hii kadri uwezo kifedha unavyoimarika ili kero ya usafiri na usafirishaji iliyolikabili Jeshi kwa muda mrefu ibaki kuwa historia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kuwa uwezo wa Serikali kifedha kununua vifaa na vitendea kazi vipyta ni mdogo, Jeshi la Wananchi limeendelea kutekeleza mpango wa kukarabati baadhi ya vifaa na vitendea kazi vyake vilivyoharibika na kuweza kuvitumia katika majukumu yake. Hii ikiwa ni pamoja na kutengeneza vipuri vyta vifaa na vitendea kazi hivyo. Wakati huo huo, Jeshi la Wananchi limeendelea kufanya utafiti baadhi ya vifaa vilivyopo kuona uwezekano wa kuvikarabati na kuviongezea uwezo ili kuvitumia katika mazingira ya sasa na baadae. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatu ni kuhusu mahitaji na huduma muhimu kwa Wanajeshi na Vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwapatia wanajeshi na vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa, mahitaji na huduma muhimu na iliyobora, hususan chakula, maji, umeme, usafiri na mawasiliano ili kuhamasisha utendaji wao. Hivyo, pamoja na changamoto ya upungufu wa fedha, Serikali imetoea kipaumbele cha kwanza kwa mahitaji na huduma hizi katika upangaji wa Bajeti. Hatua hii pamoja na zingine za kiutawala zinazochukuliwa kurekebisha kasoro zilizopo, zimeboresha utowaji wa mahitaji na huduma hizi. Hata hivyo, katika mwaka 2007/2008 mafanikio hayo, kwa kiasi kikubwa, yaliathiriwa na mfumuko wa bei, jambo lililosababisha kupanda kwa gharama kuzidi uwezo wa kibajeti. Hali hii imefanya wazabuni, wakati mwingine, kutishia kusitisha kutoa huduma hizo na hata wanajeshi na vijana kupatiwa mahitaji na huduma zilizo chini ya viwango vinavyostahili, mambo yanayozusha kero. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ufumbuzi wa msingi wa kero hizi ni kuboresha viwango vya Bajeti, jambo ambalo Serikali imekuwa ikilifanya kila mwaka kulingana na uwezo wa kifedha unavyoongezeka. Sambamba na hatua hii ni kudhibiti matumizi ya mahitaji na huduma hizi ili kujiridhisha na uhalali wa matumizi hayo kabla ya kufanya malipo. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kupitia Jeshi la Wananchi na Jeshi la Kujenga Taifa yamejizatiti katika hili ili kuhakikisha wanajeshi na vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa wanapata mahitaji na huduma bora.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Wananchi linafanya utafiti ili kuona uwezekano wa kutumia nishati ya umeme wa mionzi ya juu, mabaki ya chakula na taka za mimea. Hatua hii mbali na kuliwezesha Jeshi la Wananchi na Jeshi la Kujenga Taifa kupunguza gharama za uendeshaji, pia itayawezesha majeshi haya kuyapatia umeme makambi yasiyopata umeme kutoka kwenye gridi ya Taifa. Pia hatua hii itasaidia kupunguza matumizi makubwa ya kuni na hivyo kuimarisha uhifadhi wa mazingira. Eneo lingine linalofanyiwa utafiti ni mradi wa kuvuna maji ya mvua kwa matumizi ya makambi ya jeshi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hospitali na zahanati za Jeshi na Jeshi la Kujenga Taifa zimeendelea kutoa huduma mbalimbali za kinga na matibabu kwa wanajeshi, na familia zao, vijana na raia, hii ikiwa ni pamoja na huduma za afya kwa mama na mtoto. Baadhi ya hospitali na zahanati hizi zimepanuliwa kwa kufanyiwa ukarabati mkubwa na kuziimarisha kivifaa na wataalamu ili kuziwezesha kutoa huduma zaidi na iliyo bora. Hospitali na zahanati hizo ni pamoja na hospitali Kuu ya Jeshi Lugalo, Mbeya, Mwanza, *TMA* - Monduli, Mazao - Morogoro na Bububu - Zanzibar ambayo ujenzi wake umekamilika mwishoni mwa mwaka 2007. Ukarabati wa Hospitali ya Bububu ulifanywa kwa ufadhilli wa nchi ya Ujerumani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya umekubali kusajili baadhi ya hospitali na zahanati za Jeshi la Wananchi kwa ajili ya kutoa huduma ya tiba kwa wanachama wa mfuko huo. Huduma hiyo imeanza kutolewa katika hospitali na zahanati za Mazao- Morogoro, Mbeya, Mwanza, *TMA*-Monduli, Nyumbu- Kibaha, Hospitali Kuu ya ya Jeshi Lugalo na *Navy*-Dar es Salaam, Mirambo-Tabora, Luhuwiko - Songea, Ngerengere-Morogoro na Nachingwea-Lindi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na ufinyu wa Bajeti, huduma ya sare kwa wanajeshi na vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kutolewa katika viwango vinavyoridhisha na kwa wakati. Juhudi zinafanywa ili kuboresha upatikanaji wa huduma hii. Hii ikiwa ni pamoja na kuimarisha na kuvitumia viwanda vya Jeshi na Jeshi la Kujenga Taifa katika kushona sare hizo badala ya kuagiza nje kupitia kwa wazabuni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nne ni kuhusu ushirikiano wa kiulinzi na kijeshi baina ya Tanzania na nchi nyingine duniani. Katika mwaka 2007/2008, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendeleza juhudhi za kuimarisha ushirikiano wa kijeshi na kiulinzi baina ya Tanzania na nchi nyingine duniani. Wizara imetekeleza majukumu mbalimbali

kupitia uhusiano na nchi moja moja, ushirikiano wa Kikanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Ushirikiano wa Kimataifa kupitia Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa. Hii ikiwa ni pamoja na kuwa na ziara za kubadilishana za viongozi na maafisa wa Kiserikali na kijeshi, kuhudhuria mikutano ya ngazi mbalimbali na kutekeleza wajibu wetu kulingana na makubaliano na mikataba ambayo Tanzania imesaini na kuridhia katika ushirikiano mbalimbali. Makubaliano muhimu ni Jeshi la Wananchi kushiriki operesheni za kulinda amani katika nchi zenyenye migogoro. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tano, ni kuhusu mazingira ya kufanya kazi na ya makazi kwa Wanajeshi na vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kujenga mazingira bora na nadhifu ya kufanya kazi na kuishi kwa wanajeshi na vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa katika makambi na kwingineko ni moja ya vipaumbele vya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Hii inahusu ujenzi mpya na ukarabati wa nyumba za kuishi, mabweni, miundombinu, huduma za majisafi, majitaka, umeme na mawasiliano, majengo ya kufanya kazi na mafunzo na maeneo salama ya kufanya mafunzo kwa vitendo katika makambi na kwingineko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa iliyopo katika jukumu hili ni kujenga nyumba za kutosha ili kuwarejesha katika makambi wanajeshi wanaoishi uraiani, hatua itakayoimarisha Jeshi kiutendaji. Kwa kuwa fedha zinazohitajika ni nyingi na uwezo ni mdogo, mkakati uliopo ni kutekeleza jukumu hili kwa kuzingatia vipaumbele na kwa awamu. Hivyo katika mwaka 2007/2008, yafuatayo yametekeleza ili kufanikisha dhamira hiyo.

Mheshimiwa Spika, ukarabati wa majengo na miundombinu mingine. katika eneo hili kazi zilizofanyika ni zifuatazo:-

- (i) Kuimarisha mazingira ya Makao Makuu ya Jeshi na Hospitali Kuu ya Jeshi Lugalo.
- (ii) Kukarabati mifumo ya maji safi na majitaka – Lugalo, Dar es Salaam.
- (iii) Kukarabati baadhi ya majengo katika maeneo ya Lugalo, Kisarawe, Pangawe, Kibaha na baadhi ya majengo ya vikosi vya Zanzibar na Nachingwea.
- (iv) Ukarabati wa vifaa vya kuzimia moto kwenye makambi.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa nyumba mpya na ukamilishaji wa viporo vya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, nyumba mpya za kuishi familia 242 za wanajeshi ikiwa ni pamoja na mabwalo mawili zimejengwa kwenye makambi yaliyoko Arusha na Dar es Salaam kwa kutumia mkopo toka Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*). Hii ikiwa ni pamoja na kuunganisha nyumba hizo kwenye mitandao ya huduma za majisafi, majitaka na umeme na karibu zitakabidhiwa kwa watumiaji. Kutokana na gharama za

ujenzi huo kupanda, ilibidi kupunguza idadi ya nyumba kutoka 270, zilizotolewa taarifa hapa Bungeni mwaka jana, hadi nyumba 242.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana tulitoa taarifa hapa Bungeni kuhusu ununuzi wa mtambo wa kujenga nyumba za kuishi kwa gharama nafuu pamoja na malighafi ya ujenzi wa nyumba hizo. Tulieleza pia kwamba majaribio ya ujenzi wa nyumba hizo yangefanyika mwezi Agosti, 2007. Hata hivyo, kutokana na matatizo ya kiufundi na kilogistiki, hatukuweza kufanya hivyo. Matatizo hayo yameshashughulikiwa na majaribio hayo yatafanyika mwaka huu muda wowote kuanzia sasa.

Mheshimiwa Spika, vile vile katika mwaka 2007/2008 maandalizi yamefanywa ili kumalizia ujenzi katika Hospitali ya Bububu, Zanzibar, kukarabati mifumo ya majisafi na majitaka Mirambo - Tabora, Hospitali ya Jeshi Lugalo na Keko - Dar es Salaam, na kuendeleza ujenzi wa jengo la ofisi Makao Makuu ya Wizara, Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu upimaji, umiliki na utunzaji wa maeneo ya Jeshi, kazi ya kuyapima, kuyalipia fidia na kisha kuyamiliki kisheria maeneo yote ya Jeshi haikuwa na mafanikio makubwa kutokana na ufinyu wa Bajeti. Fedha kidogo zilizopatikana zilitumika katika kulipia fidia kwa wenze maeneo yaliyochukuliwa huko Masange, Tabora na Tondoroni, Pwani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sita ni kuhusu viwanda, utafiti na uendelezaji wa tekinolojia ya Kijeshi. Changamoto nyagine inayoikabili Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni kuendeleza utafiti na maendeleo ya teknolojia ya kijeshi katika viwanda vya kijeshi vya mashirika ya Mzinga na Nyumbu. Lengo la jukumu hili ni kujenga uwezo wa kujitegemea katika vifaa vya kijeshi lakini lengo hili halijafikiwa kutokana na ukosefu wa mtaji wa kuwekeza katika mitambo na wataalam. Hata hivyo, juhudhi mbalimbali zimeendelea kufanyika ili kujikwamua na tatizo hili. Hii ikiwa ni pamoja na kuongeza ufanisi katika matumizi ya Bajeti inayotengwa, kuhamasisha na kutumia ubunifu wa wataalam katika shughuli za viwanda na kutafuta wawekezaji wenze uwezo kimtaji wa kushirikiana nao kuendesha viwanda hivyo. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana kutokana na juhudhi hizo ni yafuatayo, kwanza, Shirika la Mzinga, katika mwaka 2007/2008, shirika limeanza utekelezaji wa mradi wa kukarabati na kuboresha mitambo na majengo ya kiwanda chake. Mradi huu wa miaka mitatu utakapokamilika utaboresha na kuimarisha uzalishaji wa bidhaa zinazozalishwa katika kiwanda hicho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia ubunifu wa wataalam wake shirika hili limefanikiwa kufufua na kukarabati baadhi ya vifaa vyake vilivyokuwa vimeharibika kiwandani na kuweza kuvitumia katika uzalishaji. Aidha, shirika hili limekarabati vifaa vilivyoaribika na kuongeza uwezo baadhi ya bidhaa na vifaa vya zamani vya Jeshi la Wananchi. Pia, shirika hili limefanya utafiti na kubuni teknolojia kwa ajili ya matumizi ya kiraia kama vile kutengeneza breki za gari moshi, mashine za kupasulia, kuranda na kukereza mbao na mashine za kukoboa na kusaga nafaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Shirika la Nyumbu, shirika hili limeendelea kufanya utafiti wa kuboresha teknolojia ya gari la aina ya Nyumbu kwa kufanya majaribio

magari yaliyozalishwa katika miaka ya nyuma. Aidha, shirika hili limeendeleza utafiti na ubunifu wa teknolojia kwa ajili ya matumizi ya kiraia katika ujenzi wa nyumba za gharama nafuu na matumizi mbadala ya zao la mkonge katika kuzalisha nishati ya umeme.

Saba, ni kuhusu mkakati wa kupambana na UKIMWI. Wanajeshi na watumishi wa umma ndani ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kama sehemu ya Watanzania wameendelea kuathiriwa na UKIMWI. Ili kukabiliana na hali hiyo elimu ya kinga kuzuia maambukizi mapya na elimu rika imetolewa kwa wanajeshi na watumishi raia hadi ngazi ya Brigadi. Aidha, Kamati za kuratibu shughuli za utoaji wa elimu hiyo hadi ngazi za kikosi zimeundwa. **Kulingana na uwezo kifedha, wanajeshi na watumishi wa umma waliopimwa kwa hiari na kugundulika kuwa wameathirika wamepatiwa dawa za kurefusha maisha na msaada wa lishe.** Vile vile, wanajeshi na familia zao, watumishi wa umma na vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa wameendelea kuelimishwa kuhusu janga la UKIMWI na jinsi ya kujikinga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa Vijana wa Kitanzania. Mafunzo ya ukakamavu, uimarishaji wa umoja wa Kitaifa na kuwajengea vijana uzalendo wa nchi yao yameendelea kutolewa katika makambi mbalimbali ya Jeshi la Kujenga Taifa. Aidha, vijana hao walipatiwa mafunzo ya stadi za kazi na uzalishaji mali katika fani za kilimo, ufugaji bora wa wanyama na kuku, uvuvi na utunzaji wa mazingira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, idadi ya vijana waliochukuliwa katika makambi na kupatiwa mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa na walioandikishwa kujiunga na vyombo vya ulinzi na usalama baada ya kumaliza hatua mbalimbali za mafunzo hayo ni kama ifuatavyo:-

(i) Vijana 2,454 (wakiwemo wasichana 479 na wavulana 1,975) wa operesheni kasi mpya waliojiunga na mafunzo hayo mwezi Machi, 2006 walimaliza mafunzo yao ya miaka miwili mwezi Machi, 2008. Vijana 518 kati ya waliomaliza mafunzo hayo, waliandikishwa kujiunga na Jeshi la Wananchi na vijana 31 waliandikishwa kujiunga na Magereza.

(ii) Vijana 3,902 (wakiwemo wasichana 662 na wavulana 3,240) wa operesheni maisha bora walianza mafunzo yao ya miaka miwili mwezi Juni, 2007 katika makambi mbalimbali. Baada ya kumaliza mafunzo ya awali ya ukakamavu na uzalendo ya miezi sita, vijana 1,501 kati yao waliandikishwa kujiunga na Jeshi la Wananchi na waliobakia kwa sasa wanaendelea na awamu ya pili ya mafunzo ya stadi za kazi na uzalishaji mali.

(iii) Vijana 4,223 (wakiwemo wasichana 691 na wavulana 3,522) wa operesheni uadilifu walianza mafunzo yao ya miaka miwili mwezi Juni, 2008 katika makambi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu shughuli za Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA JKT).

Mheshimiwa Spika, SUMA JKT inapaswa kuendesha kibiashara miradi ya uzalishaji mali ili kuzalisha faida. Faida inayopatikana inategemewa kutumika katika kusaidia Serikali kugharamia uendeshaji wa Jeshi la Kujenga Taifa. Hata hivyo, kutokana na uwezo mdogo kimtaji, ukosefu wa utaalamu na matumizi ya ufugaji na kilimo cha asili, SUMA JKT haijaweza kukidhi matarajio hayo. Kwa kiasi kikubwa shughuli nyingi za uzalishaji mali zinazofanyika sasa, hasa zile za kilimo na mifugo, ni za mafunzo kwa vitendo kwa vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa. Juhudi za kutafuta wawekezaji wenye uwezo kimtaji ili kushirikiana nao katika uzalishaji wa kibiashara bado hazijawa na mafanikio makubwa. Wawekezaji wachache waliojitokeza wamekuwa wakitoa masharti magumu ya kushirikiana nao kama vile kumilikishwa ardhi. Shughuli za SUMA JKT zimegawanywa katika sekta za kilimo, viwanda na ujenzi na utekelezaji wake kisekta ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu sekta ya kilimo na ufugaji, katika mwaka 2007/2008 miradi ya kilimo iliendelea kutekelezwa katika makambi mbalimbali kwa kulima mazao ya muda mfupi na mrefu ya chakula, biashara na bustani. Baadhi ya mazao yaliyozalishwa ni mahindi, mpunga, kahawa, kokoa, zabibu, alizeti, machungwa na korosho. Hadi kufikia mwezi Machi, 2008 baadhi ya mazao yalivunwa na kuuzwa na kuiingizia SUMA JKT shilingi 244,700,000/=. Mazao mengine yalikuwa bado hayajavunwa na kuuzwa. Pia miradi ya ufugaji wa ng'ombe wa maziwa na nyama, mbuzi, kondoo, nguruwe, kuku wa mayai na nyama iliendelea kutekelezwa katika makambi na kuiingizia SUMA JKT shilingi 220,415,000/=. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, sekta ya viwanda, katika sekta ya viwanda SUMA JKT imefanikiwa kupata wabia wa kushirikiana nao katika baadhi ya viwanda vyake ambavyo kwa sasa viro katika hatua za awali za uzalishaji. Katika mwaka 2007/2008 SUMA JKT ilipata mafanikio yafuatayo katika sekta hii:-

(i) Kwanza kiwanda cha ushonaji cha *CAMISUMA* kilishona sare zenye thamani ya shilingi 286,800,252/= kwa ajili ya majeshi mbalimbali.

(ii) Kiwanda cha Ushonaji cha JKT Ruvu kilishona sare za Jeshi la Kujenga Taifa zenye thamani ya shilingi 484,239,000/= na sare za Jeshi la Ulinzi zenye thamani ya shilingi 398,000,000/=.

(iii) Kiwanda cha samani cha Chang'ombe kilitengeneza samani za watu binafsi na taasisi mbalimbali zenye thamani ya shilingi 308,560,444/=.

(iv) Kiwanda cha *TANZANSINO* kiliboresha shughuli zake kwa kubadili mbia wa awali *Shanxi Provincial Technical Renovation and Equipment Corporation* na kushirikiana na mbia mpya *Holley Industry Group Company Ltd.*, mwenye uwezo wa mtaji na teknolojia ili kukiwezesha kiwanda kuongeza aina ya dawa zinazozalishwa. (*Makofit*)

Sekta ya Ujenzi, sekta hii ndiyo yenyeye kuonyesha mwelekeo wa mafanikio kulingana na majukumu ya SUMA JKT. Katika mwaka 2007/2008 SUMA JKT ilitekeleza na kukamilisha mradi wa ujenzi wa nyumba za kuishi wanajeshi katika makambi ya Jeshi la Wananchi na Jeshi la Kujenga Taifa katika maeneo ya Lugalo na Mtoni Kijichi mkoani Dar es Salaam (nyumba za kuishi familia 142 na mabwalo mawili kwa ajili ya maafisa na askari) na Oljoro mkoani Arusha (nyumba za kuishi familia 94). Thamani ya mradi huo ni shilingi 5,100,000,000/=. Vile vile katika mwaka huo SUMA JKT ilipewa miradi mbalimbali ya ujenzi ifuatayo:-

Shirika la TANAPA (miradi minne), Wizara ya Miundombinu (miradi miwili), Wizara ya Kilimo na Chakula (miradi miwili) na Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo (mradi mmoja). Thamani ya miradi yote hii ni shilingi 2,479,021,192/=. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, utawala bora. Wizara imeendelea kuzingatia na kutoa msukumo zaidi katika udhibiti wa matumizi bora ya rasilimali zake. Aidha, watumishi kumi na mbili wamehudhuria mafunzo mbalimbali ndani na nje ya nchi yanayohusu uzingatiaji wa taratibu, sheria, kanuni na miongozo mbalimbali ya matumizi ya fedha za Serikali. Vile vile vituo vyote ya malipo vya Jeshi mkoani vimeunganishwa na mtandao wa Makao Makuu ya Jeshi ili kurahisisha malipo na kuongeza udhibiti na uwajibikaji. Hatua hii pia imeimarisha utoaji wa taarifa za matumizi ya fedha zilizo sahihi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha dhana ya Utawala Bora na ushirikishwaji, katika mwaka 2007/2008 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendesha mikutano miwili ya Baraza la Wafanyakazi na imewawezesha wafanyakazi wake kushiriki kwenye sherehe za Mei Mosi na siku ya Wanawake Duniani.

Aidha, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeshiriki katika Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma mwaka 2008 ambapo ilitoa elimu kwa umma kuhusu majukumu iliyonayo na utekelezaji wake pamoja na huduma mbalimbali zinazotolewa na taasisi zake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua athari za rushwa, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kusisitiza umuhimu wa kufanya kazi kwa uwazi na uaminifu ili kudhibiti mianya ya rushwa. Katika kutekeleza suala hili kila Idara na Vitengo na hasa vile vinavyohusika na utoaji na usimamiaji wa huduma na zabuni zimetakiwa kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia taratibu, kanuni na sheria.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto ya upungufu wa Bajeti, katika mwaka 2007/2008, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, imetoa stahili mbalimbali kwa wanajeshi na watumishi wa umma. Stahili hizo ni pamoja na malipo ya likizo, mishahara na posho mbalimbali, vifaa vya malazi, mavazi na sare za kazi kwa watumishi wa umma na huduma ya maziko. Aidha, madai ya malimbikizo ya mishahara kwa watumishi waliopandishwa vyeo, waajiriwa wapya na watumishi waliobadilishwa vyeo yameendelea kulipwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia kuhusu maendeleo ya Watumishi wa Umma. Jukumu lingine lililoteklezwa na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa katika mwaka

2007/2008 ni kusimamia maendeleo ya watumishi. Katika mwaka huo Wizara imeajiri jumla ya watumishi 67, imethibitisha kazini watumishi 87, kupandisha vyeo watumishi 491 na kubadilisha vyeo watumishi 36 waliopata sifa kwa mujibu wa muundo wa utumishi. Aidha, Wizara imeweza kupeleka watumishi 46 katika mafunzo ya muda mrefu na watumishi 19 katika mafunzo ya muda mfupi.

Kuhusu michezo, kwa kutambua kuwa michezo husaidia kuwajenga wanajeshi na watumishi wa umma ukakamavu, kiafya na kiakili, katika mwaka 2007/2008 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeshiriki katika mashindano ya Shirikisho la Michezo la Wizara (*SHIMIWI*) yaliyofanyika mjini Tanga tarehe 14 Novemba, 2007 hadi 02 Desemba, 2007, katika mashindano hayo timu yetu ya mpira wa miguu na mpira wa pete zilishiriki na kufanya vizuri kwa kufikia robo fainali. Kwa upande wa majeshi, timu za Jeshi la Wananchi zilishiriki katika mashindano mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa, ikiwa ni pamoja na mashindano ya majeshi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yaliyofanyika Kampala Uganda tarehe 22 Juni, 2008 hadi 03 Julai, 2008. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008 Jeshi la Kujenga Taifa limeshiriki katika michezo mbalimbali kwa ngazi za mikoa, Taifa, Kimataifa na kwa mashindano maalum. Vile vile, wachezaji kutoka jeshi hilo wamechaguliwa kuunda timu za Mikoa au Taifa katika michezo mbalimbali. Haya ni mafanikio makubwa kwani ni sehemu ya majukumu ya jeshi hili ya kufunza vijana na kuibua vipaji vya michezo nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mafanikio muhimu ya utekelezaji wa malengo ya Bajeti ya mwaka 2007/2008 utekelezaji wa malengo ya Bajeti ya mwaka 2007/2008 ulikuwa na kishindo (*impact*) cha mafanikio katika maeneo yafuatayo ya shabaha kuu za ulinzi wa Taifa kwanza ni ulinzi wa uhuru na usalama wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mafanikio muhimu ya utekelezaji wa malengo ya Bajeti ya mwaka 2007/2008 ni Jeshi letu kuweza kudhibiti ipasavyo ulinzi wa mipaka yetu na hivyo kuhakikisha uhuru na usalama wa Tanzania. Kutokana na hatua hiyo hali ya ulinzi na usalama wa mipaka ya nchi yetu na nchi jirani kwa ujumla ilikuwa shwari. Hata hivyo, yapo matukio yanayosababisha amani na utulivu kuzorota katika maeneo ya baadhi ya mipaka. Matukio hayo na maeneo ya mipaka yalikutokea ni haya yafuatayo: -

Kwanza ni eneo la mpaka kati ya Tanzania na Kenya. Eneo hili limekabiliwa na tatizo la wahamiaji haramu wenye asili ya Kiethopia na Kisomali wanaoingia nchini toka Kenya ambao baadhi yao wameshiriki katika vitendo vya uhalifu. Pia katika kijiji cha Jasini mkoani Tanga lipo tatizo la ujenzi holela usiozingatia sheria za mipaka ambapo baadhi ya wananchi wa pande zote mbili wamejenga makazi katika maeneo yasiyoruhusiwa, kuharibu mazingira kwa kukata miti ovyo na kuendesha shughuli za kilimo na ufugaji. Vile vile, mapigano kati ya koo za Waanchari na Waryanchoka katika vijiji vya mpakani wilayani Tarime, Mkoa wa Mara yamesababisha vurugu zinazotoa mianya kwa watu wasio wema toka Kenya kuingia nchini kinyemela na kufanya uhalifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo la mpaka kati ya Tanzania na Uganda. Katika eneo hili lipo tatizo la baadhi ya alama za mpaka kuharibiwa na mvua na pia wanyama kutokana na wahamiaji haramu kuendesha shughuli za ufugaji katika maeneo yasiyoruhusiwa ya mpakani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni la mpaka kati ya Tanzania na Rwanda. Katika eneo hili lipo tatizo la uhalifu wa kutumia silaha, wizi wa mifugo na utekaji wa magari unaofanywa na wahamiaji haramu wanaoshirikiana na raia wasio wema. Hali hiyo ni sugu katika barabara zinazopita pori la Kimisi lililopo katika Wilaya za Muleba, Karagwe, Biharamulo na Ngara.

Mheshimiwa Spika, eneo la mpaka kati ya Tanzania na Burundi. Eneo hili limekabiliwa na matukio ya ujambazi na wizi wa kutumia silaha yanayofanywa na wahamiaji haramu wanaoshirikiana na raia wasio wema. Pia eneo la mpaka kati ya Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (*DRC*), eneo hili limeathiriwa na vitendo vya ujambazi na uharamia hasa kwenye Ziwa Tanganyika unaofanywa na watu wenye silaha ambao baadhi yao ni wahamiaji haramu toka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Mheshimiwa Spika, eneo la mpaka kati ya Tanzania na Malawi. Katika eneo hili utata wa mpaka kati ya Tanzania na Malawi katika Mto Songwe na Ziwa Nyasa bado haujapatiwa ufumbuzi. Pia eneo la mpaka katika Bahari ya Hindi. Eneo la mpaka katika Bahari ya Hindi limekuwa shwari isipokuwa kwa vitendo vya kihalifu vya uvuvi wa kutumia baruti na vyombo vya uvuvi vya kigeni vinavyoingia kuvua bila vibali, pamoja na eneo hilo kutumiwa kupitisha/kusafirisha binadamu isivyo halali (*illegal immigrants and human trafficking*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, matukio haya ni changamoto kwa jukumu letu la kuhakikisha amani na utulivu katika maeneo ya mipaka yetu. Hivyo, Jeshi la Wananchi kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za nchi na wananchi kwa ujumla, limeendesha operesheni mbalimbali kwa lengo la kudhibiti matukio hayo ya kihalifu dhidi ya raia wetu. Katika operesheni hizo silaha mbalimbali, risasi na baadhi ya wahamiaji haramu wamekamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vinavyohusika. Hatua hiyo kwa kiasi fulani imesadia kurejesha amani na utulivu katika baadhi ya maeneo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kulihakikishia Bunge lako Tukufu na wananchi kwa ujumla kwamba Jeshi la Wananchi limejiandaa na lipo imara kukabiliana na matukio yanayohatarisha usalama wa nchi yetu na raia wake. Aidha, Jeshi la Wananchi lipo makini, linafuutilia na kuchukua tahadhari dhidi ya matukio hayo, hususan nyendo na harakati za wahamiaji haramu na watu wengine waovu katika mipaka yetu na maeneo yanayozunguka mipaka hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali haipo tayari kuona usalama wa nchi yetu unahujumiwa. Hivyo, itaendelea kulisaidia Jeshi la Wananchi kuimarisha uwezo wake wa kudhibiti ulinzi wa mipaka yetu. Naomba kutoa rai kwa wananchi, hasa wale waishio katika maeneo ya mipakani, kuacha kushirikiana au kuwapatia hifadhi wahamiaji haramu

na watu wengine wenye nia mbaya dhidi ya usalama wetu. Jamii itambue kuwa kushirikiana au kuwahifadhi watu wa aina hiyo ni kosa la jinai licha ya kitendo hicho kuhatarisha amani na utulivu wetu. Waheshimiwa Wabunge na mamlaka za Tawala za Mikoa na Wilaya wanaombwa kutoa ushirikiano katika kuwaelimisha wananchi kuhusu suala hili. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hatua hizo, Serikali imeendelea kuchukua hatua za kidiplomasia kuomba serikali za nchi jirani kutoa ushirikiano katika kuhakikisha amani na utulivu katika maeneo ya mipaka yetu. Hatua hizo zimehusisha pia juhudzi za kulipatia ufumbuzi tatizo la utata wa mpaka kati ya Tanzania na Malawi katika Mto Songwe na Ziwa Nyasa. Wakati huo huo, juhudzi za Serikali kuandaa umma wa Watanzania katika jukumu la ulinzi wa Taifa letu dhidi ya adui, zimendelea kuzaa matunda. Idadi na ubora wa askari wa mgambo wanaoandalishi kwa ajili ya jukumu hilo, imeendelea kuongezeka katika mikoa yote ya Tanzania. Kwa vile askari wa mgambo ndiyo nguvu kuu ya ulinzi wa Taifa letu, ongezeko hili ni hatua muhimu katika kuhakikisha uhuru na usalama wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kukua na kuenea kwa teknolojia, utandawazi na mwingiliano mkubwa wa kijamii vimeendelea kuleta changamoto mpya za kiusalama duniani. Changamoto hizo ambazo uasilia na maumbile yake siyo hasa ya kijeshi bali ni ya kisiasa, kijamii na kiuchumi, ni pamoja na itikadi kali, ugaidi, uhalifu wa kimataifa, biashara ya dawa za kulevyia, usambaaji wa silaha ndogo ndogo, uasi au kujitenga na dola halali za nchi na vita vya wenyewe kwa wenyewe vinavyosababisha wimbi la wakimbizi, ndani na nje ya nchi zao, utelekezaji wa mabaki ya sumu ya kemikali, uchafuzi wa maji na hewa, pamoja na uharibifu wa mazingira. Nchi mbalimbali duniani; tajiri na maskini, zimeathiriwa na changamoto hizi na kuzisababishia ukosefu wa amani na utulivu na kudhoofishwa uhuru na maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, nchi nyingi duniani hivi sasa zinashirikiana kijeshi na kiulinzi ili kuwa na nguvu za pamoja kudhibiti ueneaji wa changamoto hizi. Ni vigumu kwa nchi moja pekee, kuweza kuzidhibiti kikamilifu changamoto hizi kwa vile zina uwezo wa kuvuka mipaka ya nchi moja hadi nyingine bila kugundulika. Kwa hakika kila nchi duniani, hivi sasa inakabiliwa na chaguo la kushirikiana na nchi nyingine au kuhatarisha usalama wake. Kwa vile hakuna nchi yenye kinga dhidi ya changamoto hizi, ushirikiano kijeshi na kiulinzi na nchi nyingine ni jambo lisiloepukika. Hivyo, ili kujimarishia amani na utulivu, nchi ya Tanzania imeshirikiana na nchi mbalimbali duniani katika jukumu hili, lakini katika misingi ya usawa, kutambua na kuheshimu hadhi na uhuru wa nchi nyingine.

Aidha, kupitia ushirikiano huo, Tanzania imeimarisha maelewano na urafiki na nchi mbalimbali katika nyanja za kijeshi na kiulinzi. Sambamba na juhudzi hizo, nchi yetu imeshirikiana kijeshi na kiulinzi na nchi jirani katika Jumuiya za kikanda ili kujenga mazingira ya maelewano na kuishi kwa amani na utulivu.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, mafanikio yaliyopatikana katika eneo hili ni pamoja na haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ushirikiano na nchi moja moja (*Bilateral Cooperation*): Baadhi ya Serikali za nchi rafiki zimeipatia Tanzania misaada ya mafunzo, vifaa na teknolojia ya kijeshi na misaada mingine ya kihuduma, kwa ajili ya Jeshi la Wananchi. Serikali hizo na misaada zilizotoa ni zifuatazo:-

(i) Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China imelipatia Jeshi la Wananchi misaada ya zana na vifaa mbalimbali, pamoja na mafunzo ya kijeshi kwa maafisa na askari.

(ii) Serikali ya Jamhruri ya Shirikisho la Ujerumani imelipatia Jeshi la Wananchi vifaa vya hospitali, utaalamu wa aina mbalimbali ikiwa ni pamoja na mafunzo kwa baadhi ya maafisa na askari.

(iii) Serikali ya India imetua nafasi za kozi za kijeshi kwa maafisa na askari wa Jeshi la Wananchi.

(iv) Serikali ya Uingereza imetua nafasi za mafunzo kwa kozi mbalimbali kwa maafisa wa Jeshi la Wananchi.

(v) Serikali ya Marekani imetua vifaa na mafunzo kwa ajili ya kuendesha kozi mbalimbali za kijeshi kwa maafisa na askari wa Jeshi la Ulinzi. Aidha, Serikali ya Marekani kupitia Jeshi lake, imetua mafunzo ya ulinzi wa amani kwa kikosi cha Jeshi la Wananchi kinachojiandaa kwenda katika operesheni ya kulinda amani nchini Sudan, chini ya *United Nations and African Mission In Darfur (UNAMID)*.

(vi) Serikali ya Umoja wa Falme za Kiarabu imeendelea kusaidia ujenzi wa Chuo cha Ukamanda na Unadhimu cha Jeshi la Wananchi Mkoani Arusha.

(vii) Serikali ya Kanada imetua mafunzo ya lugha ya Kifaransa na sheria za kijeshi kwa wanasheria wa Jeshi la Wananchi, ulinzi wa amani, ukamanda na unadhimu kwa maafisa na askari.

(viii) Serikali ya Ufaransa imetua nafasi za mafunzo ya ulinzi wa amani. Aidha, imetua mafunzo ya lugha ya kifaransa kwa wakufunzi wa lugha hiyo katika shule za Jeshi la Wananchi.

Mheshimiwa Spika, Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC*), kupitia ushirikiano katika Jumuiya ya Afrika Mashariki; Jeshi la Wananchi limetua nafasi za kuhuduria kozi za ukamanda na unadhimu na nafasi za mafunzo ya awali ya maafisa kwa wanajeshi kutoka nchi za Kenya, Uganda na Rwanda. Aidha, maafisa wetu wamepata nafasi za kuhuduria mafunzo ya ukamanda na unadhimu katika nchi za Kenya na Uganda.

**Mheshimiwa Spika, kupitia ushirikiano katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (*SADC*), Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, imeshiriki kikamilifu katika vikao vya Jumuiya vya ngazi ya Mawaziri, Wakuu wa Majeshi na**

**Wataalamu, kwa lengo la kuimarisha urafiki na maelewano. Vile vile majeshi ya nchi za Jumuiya hii, yameendelea kushirikiana katika nyanja mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutoa nafasi za mafunzo katika vyuo vya kijeshi vya nchi wanachama. Vile vile Jeshi la Wananchi lilisimamia na kukamilisha Mpango wa Uundaji wa Brigade ya Pamoja ya nchi za Jumuiya ya SADC, iliyozinduliwa rasmi Lusaka, Zambia tarehe 17 Agosti, 2007 wakati wa Kikao cha Kumi na Saba cha Wakuu wa Nchi za Jumuiya hiyo. Kupitia ushirikiano katika Umoja wa Afrika, Jeshi la Wananchi limeshiriki na kufanikisha Operesheni ya Kurejesha Demokrasia Nchini Comoro (*Operation Democracy Comoro*), kwa kumng'oa madarakani Kiongozi Muasi wa Kisiwa cha Anjuani, Kanali Mohamed Bakari.**

Mheshimiwa Spika, kupitia Umoja wa Mataifa, kikosi cha Jeshi la Wananchi, kimeshiriki katika operesheni ya kulinda amani huko Lebanon. Aidha, Jeshi la Wananchi kwa sasa linajiaandaa na Operesheni ya Kulinda Amani huko Darfur na tayari kikosi kimoja kimeshapata mafunzo. Pamoja na kutokuwa na uzoefu wa muda mrefu katika jukumu hili, wanajeshi wetu wameonyesha uhodari na nidhamu ya hali ya juu katika kulitekeleza kwake.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuhakikisha uhuru na usalama wa Tanzania, jukumu lingine la kiulinzi la Jeshi la Wananchi ni kusaidia mamlaka za kiraia hapa nchini katika kuokoa maisha na mali za wananchi wakati wa maafa. Katika kutimiza wajibu huo, mwaka 2007/2008, Jeshi la Wananchi, pamoja na kukabiliwa na changamoto ya upungufu wa vifaa, limeshiriki kikamilifu katika matukio yafuatayo:-

(i) Uopoaji wa maiti katika Migodi ya Mererani. Kuanzia tarehe 29 Machi, 2008 hadi 30 Mei, 2008, Jeshi la Wananchi lilishiriki katika shughuli za kuopoa maiti waliofukiwa na mafuriko ya mvua katika mgodi wa madini huko Mererani, Mkoa wa Manyara.

(ii) Kuanzia tarehe 13 April, 2008 hadi 27 Mei, 2008, Jeshi la Wananchi lilishiriki katika ujenzi wa daraja la muda katika Mto Lufilyo uliopo katika Kijiji cha Lusungo, Wilaya ya Kyela, Mkoa wa Mbeya, ili kuwawezesha wananchi wa maeneo hayo kupita na kuvuka mto huo kwa urahisi na kwa usalama.

(iii) Kuanzia tarehe 26 Mei, 2008 hadi 9 Juni, 2008, Jeshi la Wananchi lilishiriki katika kudhibiti ulinzi na usalama wakati wa Mkutano wa Name wa Leon Sullivan uliofanyika katika Mkoa wa Arusha.

(iv) Kuanzia tarehe 27 Mei, 2008 hadi tarehe 30 Mei, 2008, Jeshi la Wananchi lilishiriki katika operesheni iliyoendeshwa na Polisi, Usalama wa Taifa, Mahakama na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ya kudhibiti uvuvi haramu katika Mwambao wa Bahari katika Mikoa ya Dar es Salaam na Tanga.

(v) Kuanzia mwezi Novemba, 2007, Jeshi la Wananchi limeendelea kushiriki katika utafutaji wa mabomu kwenye viwanda vinavyojihusisha na ununuzi wa vyuma chakavu.

(vi) Tarehe 21 Juni, 2008 Jeshi la Wananchi lilishiriki katika uokoaji wa watu kufuatia kuporomoka kwa jengo la ghorofa kumi Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, malengo ya bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2008/2009, yamezingatia utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Wizara wa kipindi cha 2007/2008 – 2009/2010 katika kufikia shabaha kuu za ulinzi wa Taifa nilizoeleza mwanzoni mwa Hotuba hii. Kwa hiyo, kazi zitakazofanyika katika mwaka huu ni:-

(a) Kununua vifaa kwa ajili ya Jeshi la Wananchi na kuwapatia wanajeshi mafunzo ya kijeshi ya kinadharia na vitendo kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya ulinzi wa nchi na kutoa mafunzo kwa askari wa mgambo.

(b) Kulipia huduma muhimu za maji, umeme na simu na mahitaji mengine kama vile mafuta, vilainisho na vipuri kwa ajili ya magari, mitambo na vifaa mbalimbali.

(c) Kuwapatia wanajeshi na watumishi wa umma, vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa.

(d) Kuboresha mazingira ya kufanya kazi kwa wanajeshi, watumishi wa umma na vijana watakaojiunga na Jeshi la Kujenga Taifa.

(e) Kuboresha huduma ya makazi kwa kukamilisha viporo vyta ujenzi wa majengo mbalimbali katika Makambi ya Jeshi la Wananchi zikiwemo nyumba za kuishi familia 80 huko Makambako na Pemba, baadhi ya majengo katika Shule ya Kijeshi ya Ulinzi wa Anga - Tanga, Hanga la kuegesha ndege – Dar es Salaam na mabweni ya askari 83 Regiment huko Kiluvya, Kibaha. Vile vile kukarabati Hospitali ya Bububu, Zanzibar, mabweni ya askari huko 302 KV na 671 KJ, Dar es Salaam, bwalo la askari huko Pemba, zahanati na maghala ya silaha huko Kaboya na baadhi ya majengo katika Kambi la Mirambo, Tabora.

(f) Kukamilisha viporo vyta ujenzi wa majengo mbalimbali katika makambi ya Jeshi la Kujenga Taifa ya Bulumbora, Chita, Mafinga, Mlale na Ruvu, zikiwemo nyumba za kuishi familia 16, zahanati tatu, pamoja na bafu na vyoo vitatu. Vile vile kukarabati nyumba za kuishi familia 222, mabweni ya vijana 52, mabwalo 2 na zahanati moja pamoja na mahabusu moja na mtandao wa maji mmoja katika makambi haya.

(g) Kutoa huduma ya tiba na kinga kwa wanajeshi na familia zao, vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa na watumishi wa umma, ikiwa ni pamoja na kuendeleza juhudhi za kuzuia maambukizi mapya ya Ugonjwa wa UKIMWI na kutoa huduma ya dawa kwa waathirika wa Ugonjwa huu.

(h) Kuendeleza ushirikiano wa kijeshi na kiulinzi kati ya nchi yetu na nchi mbalimbali duniani kupitia nchi moja moja, ushirikiano wa kikanda na kimataifa na kutekeleza makubaliano yatakayofikiwa katika ushirikiano huo.

(i) Kuendeleza tafiti na kuboresha uzalishaji wa bidhaa mbalimbali toka mashirika ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa ajili ya matumizi ya Jeshi la Wananchi.

(j) Kuendeleza mafunzo ya uzalendo na ukakamavu, ufundi stadi, kilimo na taaluma nyinginezo kwa vijana wanaojiungu na Jeshi la Kujenga Taifa.

(k) Kuboresha utendaji wa watumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kumaliza Hotuba yangu, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru wote walioniwezesha kufanikisha na kutekeleza jukumu la kuiongoza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, tangu niteuliwe kushika wadhifa huu mwezi Februari, 2008. Kwanza, naomba kumshukuru Rais na Amiri Jeshi Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa imani aliyonayo juu yangu ya kunateua kuiongoza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Hii ni changamoto kubwa kwangu, lakini kwa ushirikiano mzuri ninaoendelea kuupata kutoka kwa wafanyakazi wenzangu katika Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na kwingineko, naamini nitafanikisha matarajio aliyonayo juu yangu. Hivyo, kwa niaba ya Makamanda, Maafisa, Wapiganaji na Watumishi wote wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, naomba kumshukuru tena kwa kuendelea kuliimarishe Jeshi la Wananchi kihuduma na kivifaa ili liweze kutimiza wajibu wake wa kuhakikisha uhuru na usalama wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba kumshukuru Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Amani Abeid Karume, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda na Mawaziri wote, kwa msaada walionipatia katika kutekeleza majukumu yangu. Pia kwa mara nyingine tena, napenda kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Wilson Masilingi na Wajumbe wa Kamati hiyo, kwa msaada wao walioutoa kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Waziri aliyenitangulia, Mheshimiwa Alhaj Prof. Juma Athuman Kapuya, Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, pamoja na aliyekuwa Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, Naibu Waziri wa Fedha na Uchumi, kwa kuniachia misingi mizuri ya kutekeleza majukumu yangu. Aidha, natoa shukrani za pekee kwa wafanyakazi wenzangu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, nikianzia na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Emmanuel Nchimbi, Katibu Mkuu, Bwana Abel W. R. Mwaisumo, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Davis A. Mwamunyang'e, Mnadhimu Mkuu wa Jeshi, Luteni Jenerali Abdulrahaman A. Shimbo, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, Meja Jenerali M. Madata, Makamanda, Maafisa, Wapiganaji na Watumishi wa Umma wote. Wote nawashukuru kwa ushirikiano mkubwa walionipa na kwa ushauri wao ulio makini na wenye uaminifu.

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Kwahani, kwa ushirikiano wao wanaonipa. Matumaini yangu ni kuwa, tutaendelea kushirikiana zaidi kwa manufaa ya jimbo letu na Taifa kwa ujumla. Kwa niaba ya Serikali, naomba pia kutoa shukrani zangu kwa Serikali za nchi mbalimbali kwa ushirikiano wao na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Napenda pia kumshukuru Mpigachapa Mkuu wa Serikali na Watumishi waliopo chini yake, kwa kuichapa na kuikamilisha Hotuba hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, ili Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iweze kutekeleza majukumu yake kama ilivyoolezwa katika Hotuba hii; kwa mwaka 2008/2009, naliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 383,557,338,000; ambazo kati yake shilingi 299,467,220,000 zitatumika kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 84,090,118,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo; ambazo kati yake shilingi 82,860,118,000 ni fedha za ndani na shilingi 1,230,000,000 ni fedha za nje. Fedha hizi zimegawanywa katika Mafungu matatu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kama ifuatavyo: -

(a) Fungu 38 - Jeshi la Wananchi wa Tanzania: Bajeti ya Matumizi ya Kawaida shilingi 236,405,175,000; Bajeti ya Matumizi ya Maendeleo shilingi 5,300,000,000, ambazo kati yake shilingi 5,000,000,000 ni fedha za ndani na shilingi 300,000,000 ni fedha za nje.

(b) Fungu 39 - Jeshi la Kujenga Taifa: Bajeti ya Matumizi ya Kawaida shilingi 52,247,006,000; Bajeti ya Matumizi ya Maendeleo shilingi 3,650,000,000, ambazo kati yake shilingi 3,500,000,000 ni fedha za ndani na shilingi 150,000,000 ni fedha za nje.

(c) Fungu 57 - Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa: Bajeti ya Matumizi ya Kawaida shilingi 10,815,039,000; Bajeti ya Matumizi ya Maendeleo shilingi 75,140,118,000, ambazo kati yake shilingi 74,360,118,000 ni fedha za ndani na shilingi 780,000,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**SPIKA:** Asante sana Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Nadhani mnashuhudia wenyewe ile nidhamu ya jeshi inajitokeza hata kwa Waziri hapa. Yeye haki yake ni dakika zisizozidi 60, lakini katumia 40 tu na hotuba ni safi, mambo muhimu yote yamo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea nilikuwa nataka kuchukua fursa hii kuwatambulisha baadhi ya wageni muhimu wa Wizara hii.

Nikianza na Kaimu Katibu Mkoo, Bwana Elias Warishanga Shayo, yule pale, asante sana. Naomba Waheshimiwa Wabunge, mtambue kuwepo kwa Mkoo wa Majeshi ya Ulinzi ya Jamhuri ya Muungano, Jenerali Davis Mwamunyange, yule pale, ahsante sana. Pia mtambue uwepo wa Mnadhimu Mkoo wa Majeshi yetu, Luteni Jenerali Abrahman Shimbo, yule pale na Mkoo wa Jeshi la Kujenga Taifa, Meja Jenerali M. E. Madata, yule pale. (*Makofi*)

Sasa wapo wengine wazito tu pale, lakini kwa kuwa orodha haijakamilika basi kesho baada ya maswali, nitapata fursa ya kuweza kuwatambua wapiganaji wetu hawa na makamanda; ni watu muhimu sana kwetu. Tunatulia humu Bungeni kwa sababu ya kazi yao. Kuna mwaka fulani lilitokea tetemeko tu kidogo, watu walitafuta pa kutokea. Sasa tunashukuru kwa sababu hawa wanahakikisha mipaka yetu ni salama na Bunge linafanya kazi yake bila wasiwasi. Asanteni sana Jenerali Mwamunyange na wapiganaji wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Dr. Hussein Mwinyi, Waziri wetu wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, anao wageni wengine ambaa ni muhimu na hao wanatoka jimboni kwake Kwahani kule Zanzibar. Kwanza ni Mheshimiwa Ali Salum, Diwani wa Kwahani. Mheshimiwa Ali Salum, yule pale, ahsante sana karibu sana. Pia yupo Bwana Idrisa Kitwana, huyu hakutajwa hasa shughuli yake lakini labda nadhani ndio mpambe huyu. Waziri wa Ulinzi ana wapambe wa kijeshi na wengine wa kiraia. (*Makofi*)

Halafu wapo vijana watano toka Maskani kule Jimbo la Kwahani, Maskani hiyo inaitwa Maskani Dodoma. Kwa hiyo, vijana simameni.

(*Hapa wageni waliotajwa walismama*)

**SPIKA:** Ahsante sana, tunashukuru sana mnamsaidia Waziri wetu na mumfikishie salamu kule Zanzibar, mtakaporejea. (*Makofi*)

Wageni wa Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Emmanuel Nchimbi ni kama ifuatavyo: Yupo mdogo wake Mheshimiwa Naibu Waziri, anaitwa Alex Nchimbi, aah! Wanakuja kesho? Basi wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri, tutawatambulisha kesho.

Baada ya hapo basi naomba sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, ili aweze kutoa maoni ya Kamati; Mheshimiwa Wilson Masilingi. (*Makofi*)

**MHE. WILSON M. MASILINGI - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii, kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuwasilisha taarifa ya Kamati. Kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7), Kanuni za Bunge Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu, lipokee na kujadili maoni haya na kuidhinisha bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa taarifa kuhusu makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii, kwa niaba ya Kamati, kwanza kabisa, napenda kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkoo, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika na kushirikiana vyema na viongozi wa nchi za Umoja wa Afrika, kuongoza kwa mafanikio Operesheni Maalum ya Kijeshi Kisiwani Comoro, ambako hali imeendelea kuimarika tangu kutolewa madarakani Kiongozi Muasi Kanali Mohamed Bakari. Mheshimiwa Rais wetu mpPENDWA, ameonyesha uwezo mkubwa katika uongozi wake, kwani msimamo na hekima zake zinaheshimika na kukubalika kwa viongozi wenzake na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kamati yetu kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, ina jukumu la kuimarisha ushirikiano na Mabunge ya nchi nyingine, tumepokea kwa furaha heshima iliyopewa nchi yetu kutokana na mchango wa Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete na wewe, kwa kuzingatia uongozi wako bora ukachaguliwa kuwa Rais wa Umoja wa Mabunge wa Jumuiya ya Madola (*Commonwealth Parliamentary Association – CPA*). Hongera sana. Aidha, nawashukuru Mheshimiwa Dr. Hussein Mwinyi, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dr. Emmanuel J. Nchimbi, Naibu Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Ndugu Abel Mwaisumo, Katibu Mkoo Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Wataalamu wote wa Wizara hiyo, kwa maelezo mazuri na ufanuzi makini wakati Kamati ilipokuwa ikichambua Bajeti ya Wizara hii. Tunaendelea kumwombea ndugu Abel Mwaisumo, apone haraka maradhi yanayomsumbu. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwapongeza Jenerali Davis A. Mwamunyange, Mkoo wa Majeshi ya Ulinzi, Luteni Jenerali Abdulrahman A. Shimbo, Mnadhimu Mkoo wa Jeshi na Meja Jenerali Martin Madata, Mkoo wa Jeshi la Kujenga Taifa, pamoja na Makamanda, Maafisa na Wapiganaji wote, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuilinda na kuiletea heshima nchi yetu. Makamanda na Wapiganaji katika vikosi vyetu vya Kijeshi vilivyopo nchini Lebanon na wachache waliobaki katika Kisiwa cha Comoro, wanaendelea kuiletea nchi yetu heshima kubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati na mimi binafsi, natoa salamu za rambirambi kwa Amiri Jeshi Mkoo, Mkoo wa Majeshi, familia na ndugu wa Marehemu Brigedia Jenerali Januari Nyambibo, aliyekuwa Mkoo wa Chuo cha Kijeshi Monduli, Arusha aliyefariki juzi. Pia tunatoa rambirambi kwa wale wote waliofariki katika ajali ya helikopta huko Arusha na Makamanda na Askari mashujaa wetu wote waliofariki kipindi kifupi kilichopita. Mwenyezi Mungu, azilaze roho za marehemu wote hao mahali pema peponi, amina.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kwa michango yao ya kina katika kuchambua bajeti na kukamilisha Taarifa hii ili iwasilishwe mbele ya Bunge lako Tukufu. Naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Wilson M. Masilingi, Mwenyekiti, Mheshimiwa Mussa A. Zungu, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Anna M. Abdallah, Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mheshimiwa Col. Mstaafu Saleh Ali Farrah, Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Hassan C. Kigwalilo, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa William J. Kusila, Mheshimiwa Edward N. Lowassa, Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mheshimiwa Dr. John S. Malecela, Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, Mheshimiwa Col. Mstaafu Feteh S. Mgeni, Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed, Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. Msabaha, Mheshimiwa Balozi Abdi H. Mshangama, Mheshimiwa Thomas A. Mwang'onda, Mheshimiwa Brig. Jen. Mstaafu Hassan A. Ngwilizi, Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Muhammad I. Sanya, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo na Mheshimiwa Magalle J. Shibuda.

Mheshimiwa Spika, pia natoa shukrani za dhati kwa wananchi wote wa Jimbo la Muleba Kusini, kwa ushirikiano wanaonipa kama Mbunge wao kwa kipindi chote ninapoendelea na kazi hii ya Ubunge.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, tarehe 04 Juni, 2008, Kamati ilikutana Jijini Dar es Salaam, kupitia na kuchambua Taarifa ya Wizara hii kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2007/2008 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2008/2009, kama ilivyowasilishwa na Mheshimiwa Dr. Hussein Mwinyi, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Tarehe 24 Juni, Kamati, ilifanya tena kikao hapa Mjini Dodoma na kupata maelezo zaidi kuhusu Makadirio ya Matumizi na kazi zilizopangwa kufanywa kwa Mwaka wa Fedha wa 2008/2009. Katika vikao hivyo, Kamati ilielezwa kuhusu yafuatayo:-

- (i) Hali ya Ulinzi na Usalama nchini na Utekelezaji wa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati katika vikao vilivyopita.
- (ii) Dira, makusudio na majukumu ya Wizara ya Ulinzi na JKT.
- (iii) Malengo ya Bajeti ya Mwaka 2007/2008, pamoja na utekelezaji wake.
- (iv) Malengo ya Bajeti kwa mwaka 2008/2009 na makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kupitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2006/2007 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa 2007/2008, Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama wakati huo ilitoa ushauri na mapendekezo kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008. Mheshimiwa Waziri, alieleza Kamati kuwa kupitia utekelezaji wa malengo ya bajeti mwaka 2007/2008, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, imejitahidi kuzingatia ushauri wa Kamati kwa kiasi kikubwa. Hata hivyo, kutohana na uwezo mdogo kifedha, baadhi ya maoni na mapendekezo ya Kamati hayajatekelezwa kikamilifu. Pamoja na kuelezwa juu ya utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kwa mwaka wa fedha uliopita, vile vile tulielezwa kuwa utekelezaji wa

malengo ya bajeti ya mwaka 2007/2008, ulipata mafanikio makubwa katika maeneo mbalimbali. Kamati inaipongeza Wizara kwa mafanikio iliyoyapata kwa kipindi cha mwaka wa fedha wa 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuelezwu kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha wa 2008/2009, Kamati ilielezwa kuhusu malengo ya bajeti kwa mwaka 2008/2009. Vile vile Kamati ilielezwa kuwa katika mwaka wa fedha wa 2008/2009, kipaumbele kitawekwa kwenye kumalizia utekelezaji wa programu na kazi zilizoanza katika mwaka 2006/2007 na 2007/2008, pamoja na kutekeleza programu mapya. Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, alieleza Kamati kuwa kazi kuu zilizopangwa kutekelezwa ni kama ifuatavyo:-

(i) Kununua vifaa kwa ajili ya Jeshi la Wananchi na kuwapatia wanajeshi mafunzo ya kinadharia na vitendo ili kuimarisha ulinzi wa nchi.

(ii) Kulipa huduma muhimu za maji, umeme na simu na mahitaji mengine kama vile mafuta, vilainisho na vipuri kwa ajili ya magari, mitambo na vifaa mbalimbali.

(iii) Kuboresha mazingira ya kufanya kazi, kuishi, mafunzo, upatikanaji wa vitendea kazi, huduma na mahitaji muhimu kwa wanajeshi, watumishi wa umma na vijana watakaojiunga na Jeshi la Kujenga Taifa.

(iv) Kuwapatia wanajeshi, watumishi wa umma, vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa na Majenerali wastaa fu stahili zao kikamilifu.

(v) Kutoa huduma ya tiba na kinga kwa wanajeshi na familia zao, vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa na watumishi wa umma, ikiwa ni pamoja na kuendeleza juhudzi za kuzuia maambukizi mapya ya Ugonjwa wa UKIMWI na kutoa huduma ya dawa kwa waathirika wa Ugonjwa huu.

(vi) Kuendeleza ushirikiano wa kiulinzi kati yetu na nchi mbalimbali duniani kupitia nchi moja moja, ushirikiano wa kikanda na kimataifa na kutekeleza makubaliano yatakayofikiwa katika ushirikiano huo.

(vii) Kuendeleza tafiti na kuboresha uzalishaji wa bidhaa mbalimbali toka mashirika ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa ajili ya matumizi ya Jeshi la kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza vyema majukumu yaliyopangwa kwa mwaka wa fedha wa 2008/2009, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 383,557,338,000; kati ya hizo shilingi 299, 467,220, 000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 84,090,118,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Kamati ilijadili kwa undani taarifa ya utekelezaji wa majukumu na mpango wa Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2008/2009. Baada ya kupitia kifungu kwa kifungu katika mafungu yote matatu, Kamati inaunga mkono maombi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa. Tunaomba na Waheshimiwa Wabunge, muiunge mkono Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Dira na Majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2008/2009, kwa mafungu yote matatu; Fungu 38 – Ngome; Fungu 39 – Jeshi la Kujenga Taifa; na Fungu 59 – Wizara na Utawala kama ifuatavyo:-

(i) Serikali iendelee kuupa kipaumbele ulinzi wa nchi yetu kwa kutenga fedha za kutosha ili majeshi yetu yatekeleze majukumu yake ya msingi. (*Makofi*)

(ii) Serikali iweke utaratibu wa kulipia huduma za maji, umeme na simu zinazotumiwa na Jeshi la Wananchi na Jeshi la Kujenga Taifa bila watoa huduma hizo kufika kwenye maeneo ya Jeshi. (*Makofi*)

(iii) Vikosi vya Ujenzi na Ufundı vya Jeshi la Wananchi na Jeshi la Kujenga Taifa, vipewe fursa ya pekee kuchukua ukandarasi katika miradi ya serikali; barabara, madaraja na nyumba ili kupunguza gharama na kuongeza ufanisi katika kutekeleza miradi hiyo.

Jeshi la Wananchi na Jeshi la Polisi washirikiane kulimaliza kabisa tatizo la ujambazi na utekaji wa magari katika kanda ya ziwa hususan Mikoa ya Shinyanga, Kagera, Mwanza na Mara na maeneo mengine ya nchi yetu yenye matatizo hayo. (*Makofi*)

Serikali iandae Mpango Maalum na Endelevu kuhusu ujenzi wa Nyumba za Makazi ya Askari kwa kutumia nguvu kazi na uwezo uliomo ndani ya Jeshi.

Sheria ya Ulinzi wa Taifa na Sheria ya Jeshi la Kujenga Taifa, zipitiwe ili zifanyiwe marekebisho yanayohitajika haraka iwezekanavyo katika kipindi cha mwaka huu wa fedha 2008/2009.

Kamati ilibaini kwamba, wanajeshi wanaotumikia Jeshi kisheria kwa zaidi ya miaka thelathini na sita lakini wakaamriwa kuendelea kutumikia Jeshi kwa manufaa ya nchi, hulipwa mafao yao ya kustaaful kwa miaka thelathini na sita tu; na kwamba, miaka ilioongezeka kwa amri halali huwa hawalipwi mafao yao. Kamati inaelekeza kuwa, Kanuni iliyo katika Kanuni za Pensheni za Majeshi ya Ulinzi (*The Defense Force Service Pensions and Gratuities Regulations*), inayoweka ukomo wa malipo ya pensheni, irekebishwe ili wanajeshi walipwe mafao yao yote kwa muda wote waliotumikia Jeshi kihalali, sambamba na kuwapa haki zao wote walioathiriwa na Kanuni hiyo kwa sababu ni kinyume cha haki. (*Makofi*)

Kamati ilifahamishwa kwamba, fedha kwa ajili ya mafao na huduma ya makamanda wastaafu, hupelekwa kwenye Bajeti ya Jeshi na kusababisha bajeti ya Wizara ionekane kubwa. Kamati inashauri kuwa, mtindo huu urekebishwe mara moja.

Kamati inapendekeza ianzishwe Tume ya Huduma za Jeshi (*Military Service Commission*), inayojitegemea itakayoshughulikia ajira na kuboresha huduma kwa Makamanda na Askari, kwa sababu ajira ya Kijeshi ni tofauti na sheria za ajira za kiraia.

Ili kuendelea kuboresha hali ya ulinzi na usalama katika mipaka yote nchini, serikali izipe kipaumbele barabara za mipakani ili zifanyiwe matengenezo ya mara kwa mara.

Serikali iongeze bajeti ya ujenzi kwa makambi yote nchini na kuongeza juhudii katika kuweka uzio kwenye mipaka ya makambi ya Jeshi. Aidha, jitihada ziongezwe katika kupanda miti kuzunguka maeneo ya Jeshi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuhitimisha kwa kuwashukuru Dr. Thomas D. Kashilillah, Kaimu Katibu wa Bunge na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge, wakiwemo Makatibu wa Kamati hii; Ndugu Athuman Hussein na Ndugu Neema Kiula, kwa kuratibu vyema na kufanikisha shughuli za Kamati kama zilivyopangwa.

Baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kama yalivyowasilishwa muda mfupi uliopita na mtoa hoja, Mheshimiwa Dr. Hussein Mwinyi, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Wilson M Masilingi, Mwenyekiti wa Kamati ya Nje, Ulinzi na Usalama. Waheshimiwa Wabunge, mnivumilie kidogo kwa sababu nimepata orodha sasa ya baadhi ya wale Wakuu wa Sehemu mbalimbali na vitengo Jeshini kama ifuatavyo: Bwana E. E. Mrema, Kamishna wa Viwanda, Ujenzi na Kilimo; Major General Ally Mboge, Kamishna wa Maendeleo ya Jeshi; Bwana N. Alute Kamishna Msaidizi wa Viwanda, Ujenzi na Kilimo; Brig. Gen. S. L. Makakala, Mkuu wa Utumishi Jeshini; Brig. Jen. L. E. Mndeme, Chief of Logistics and Engineering; Col. M. S. Masanja, Msaidizi Kijeshi wa Mnadhimu Mkuu; Col. Ame Mwakang'ata Mkuu wa Shirika la JKT linaloitwa SUMA, Brig. Gen. M. B. Mashauri, Mkuu wa Shirika la Utafiti Kuhusu Nyumbu; na Brig. Gen. C. Muzanila, Mkuu wa Shirika la Mzinga. Karibuni sana. (*Makofi*)

Basi wale wengine kwa kesho tutapata nafasi kuwatambulisha. Sasa ni zamu ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani, aje atoe maoni ya Kambi ya Upinzani.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM - MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, aliyenijalia uzima na afya njema, kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 99(7), Toleo la Mwaka 2007, kuhusiana na Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na JKT kwa mwaka wa fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchache wa fadhila kama sitakishukuru Chama changu cha *CUF*, kwa uongozi wake makini chini ya Mwenyekiti Prof. Ibrahim Haruna Lipumba, Makamu wake Ndugu Machano Khamis Ali na Katibu Mkuu, Ndugu Maalim Seif Sharif Hamad, kwa imani yao ya kuelimisha na kuwatetea wananchi kujua haki zao katika dhana nzima ya kuboresha maisha ya Watanzania.

Nachukua fursa hii, kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Mtambile, kwa msaada na imani walionayo kwangu katika kutekeleza majukumu yangu ndani ya Jimbo la Mtambile na hata nikiwa Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, itakuwa sikuwatendea haki hata kidogo kama sikuwashukuru Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Naibu wake, Mheshimiwa Dr. Slaa, pamoja na Wabunge wote wa Upinzani, kwa ushirikiano walionipa katika kufanya kazi zangu kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu, Sera na Sheria ya Ulinzi wa Taifa ni ya zamani (tangu mwaka 1966), huku dunia ikishuhudia mabadiliko makubwa ya kiuchumi, kisiasa, kijamii, kisayansi na kadhalika. Hivyo, pamoja na mabadiliko madogo katika Sheria na Sera hizo, bado kuna haja ya kuziangalia kwa upeo Sheria za Jeshi ili ziendane na wakati huu wa maendeleo ya Sayansi na Teknolojia. Sambamba na hilo ni imani ya Kambi ya Upinzani kuwa ni vyema Sera na Sheria za Ulinzi wa Taifa kuangaliwa upya ili kuweza kuboresha mazingira ya Kijeshi zaidi. Aidha, mfumo wa Mahakama ya Kijeshi na viwango vya adhabu zinazotolewa, uangaliwe upya kwa lengo la kuboresha nidhamu.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imeingia kwenye mikataba mbalimbali ya Kimataifa na ili mikataba hiyo iweze kutekelezwa ni sharti ijumuishwe katika Sheria ya Ulinzi, jambo ambalo halijafanyika; hivyo, Kambi ya Upinzani imeona si vyema kuridhia jambo ambalo huwezi kuliingiza kwenye sheria na kulitekeleza.

Mheshimiwa Spika, mbali na shughuli zinazofanywa na sekta ya ulinzi nchini za kuimarisha usalama wa taifa, lakini bado sekta hii haijaleta tija inayotakiwa na kuweza kunyanya uchumi wa nchi hii, kama inavyotegemewa na wananchi walio wengi na hasa kwa kuzingatia wanavyofanya majeshi na askari wa nchi nyingine duniani. Sekta hii inatakikana iwe mstari wa mbele katika kuleta maendeleo na hasa katika shughuli za uvumbuzi wa kila siku, wao wawe ndio chachu ya maendeleo na sekta nyingine ziwe zinafuatia kama vile wanavyofanya taasisi za ulinzi za nchi nyingine. (*Makofi*)

Mfano mzuri, mnamo mwaka 1740 na 1805, Majeshi ya Ulinzi ya Ulaya mbali na shughuli nyingine za kiulinzi na usalama, lakini walifanya utafiti na kugundua mfumo mpya wa kijeshi ambao umewapelekea mafanikio makubwa katika kuleta maendeleo kiuchumi na utulivu nchini mwao. Hata nchi ya *United Kingdom*, wanajeshi wao walichangia kwa kiasi kikubwa, uvumbuzi wa kutumia ndege katika vita na *submarine* ambayo ilitumika kwa kubebea, kutulia na kurukia ndege za kivita, pia walichangia kwa

kiasi kikubwa katika uvumbuzi wa rada ambayo inawasaidia sana katika kuleta na kulinda usalama nchini mwao.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa shirika la kutengeneza magari Nyumbu bado halijafikia kiwango kinachotakikana katika uzalishaji; Kambi ya Upinzani inalishauri jeshi letu ni vyema wabuni magari ambayo yataendana na mazingira halisi ya barabara za Tanzania, ambayo yatatumia gharama nafuu, badala ya kutumia fedha nyingi kutengeneza gari la kisasa ambalo lina gharama kubwa. Ni vyema kutumia rasilimali zetu chache kwa kuongeza tija. Isitoshe, Serikali nayo itenge fedha za kutosha au kuwawekea utaratibu bora wa magari hayo kuzalishwa kibashara (*Assembly Line of Production*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mbali na shughuli za kiulinzi, Askari na Wanajeshi wa Marekani wanaoshughulikia Kitengo cha Afya, huwa mara kwa mara wanafanya tafiti za kisayansi kuhusiana na afya ya wanajeshi na jamii kwa ujumla. Kama hiyo haitoshi, *Military Infection Diseases Research Programme (MIDRP)*, iliendelea kufanya tafiti kwa ajili ya kuwalinda askari na wananchi na kutokomeza kabisa maradhi ya malaria na maradhi ya ngozi kwa wafanyakazi wake. Sambamba na hilo, wamefanikiwa kuanzisha *Army Research Institute (ARI)*, ambayo wameweka maabara ambayo inashughulika na shughuli za kutoa mafunzo ya utafiti.

Mheshimiwa Spika, katika kuonyesha majeshi na askari wa wenzetu wamepiga hatua kubwa kimaendeleo, Majeshi ya Marekani wameanzisha tovuti, *Deploy Med Research LINK*, kwa ajili ya kusambaza taarifa za kiserikali zinazohusiana na utafiti wa kisayansi, ambao una lengo la kuboresha upatikanaji wa habari za kiutawala, idara na huduma za kifaya na huduma nyingine za kijamii. Hii ni hatua kubwa kimaendeleo. Kambi ya Upinzani, inataka kujua mbali ya kuwa na tovuti ya jeshi; je, Serikali yetu imewaandaa vipi wanajeshi wetu kutumia huduma za mtandao kwa ufanisi?

Mheshimiwa Spika, ili taasisi zetu za ulinzi zifanikiwe zinahitaji kuwa wazi, kuwa wavumbuzi na kukubali kubadilika na kuendena na maendeleo ya kisayansi na teknolojia. Mtaalamu wa *Physics*, Rutherford alinukuliwa akisema kwamba: “*We have short of money so we must think.*” Wanajeshi wetu wafahamu kuwa tuna tatizo la umaskini; hivyo, inatalazimu kila wakati kufikiri kwani uvumbuzi unahitaji zaidi vipaji binafsi (*talented military personnel*).

Mheshimiwa Spika, nchi kama Canada, Sekta ya Ulinzi haikufanikiwa tu katika kuchangia maendeleo ya nchi yao ila taasisi husika zilijiuliza masula mengi kwa mfano: Kitu gani tunaweza kukifanya na kuleta maendeleo? Sisi tuna uwezo kiasi gani ili kuleta mageuzi ya kimaendeleo? Na tutafanya nini?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inalitaka jeshi letu lifikirie kwa kina namna ya kuongeza kasi ya kuleta mapinduzi ya maendeleo katika nchi yetu, kama wanavyofanya wenzetu kwa ajili ya kunyanya uchumi wa nchi zao, jambo litakalosa idia kupatikana kwa fedha za kutosha kwa bajeti ya jeshi letu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, ilikwishashauri jinsi ya kupata vijana wenyе vipaji maalum, ambao tunaamini kama vipaji hivyo vikitumiwa vizuri, jeshi letu litakuwa ndiyo hazina kubwa ya chimbuko la teknolojia mpya na rahisi kwa maendeleo ya Watanzania. Jeshi waanze kuwatafuta vijana wenyе vipaji tangu wakiwa mashulen; *primary na secondary*.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Ulinzi Israel, limeisaidia sana nchi hiyo katika kupiga hatua mbele za kimaendeleo. Serikali ya Israel ilipanga mikakati madhubuti ya kuhakikisha kuwa, sayansi inapewa kipaumbele kwa kila sekta kwa kuzisaidia kifedha na kuwaunga mkono kisera, kwa mfano, Sekta ya Biashara ilichangia Pato la Taifa kwa asilimia tano mwaka 1990 hadi asilimia 14 mwaka 2000. Si hivyo tu, lakini leo hii Israel ina makampuni 68 ya kibiashara, ambayo ni ya tatu baada ya Marekani na Canada na huku ikiwa na makampuni ya technoloji yaliyotoa ajira kwa watu zaidi ya wastani wa 120,000 mwaka 2005. Kubwa zaidi, leo hii Israel wana wanasyansi na wahandisi 140 kila penye wafanyakazi 10,000, ukilinganisha na 83 Marekani na 60 Ujerumani. Kwa mantiki hiyo ni vyema vyombo vyetu vya ulinzi vikajifunza katika kuleta maendeleo na mapinduzi ya kweli ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, *Kigali Institute of Science, Technology and Management (KISTM)*, imeonyesha jinsi gani taasisi za kielimu zinavyoweza kutumika kuibadilisha jamii kimaendeleo kutoka hatua ilipo. Taasisi hii muhimu ilianzishwa na kufanyakazi chini ya Jeshi la Rwanda na kuleta maendeleo makubwa kiuchumi kabla ya mauaji ya 1990. Hili ni somo kwa nchi yetu, kuona umuhimu wa kubadilisha mfumo na kulifanya jeshi kuwa ndio kituo kikuu cha maendeleo kwa kutoa wasomi na wa wataalamu wa fani mbalimbali kama vile marubani, madereva wa magari, madaktari, watafiti, wakandarasi na walimu wa vyuo vikuu; na hii ingesaidia hata kuweza kukabiliana na ufisadi ambao unaathiri uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa posho ya nyumba na chakula cha Wanajeshi uliowekwa kwa Askari wa Jeshi la Tanzania ni kwamba, ambaye yuko nje ya Kambi analipwa 10% ya mshahara wake kama posho ya nyumba. Inasikitisha kuona kwamba, Askari wa JWTZ anapewa Sh. 9,000 kwa mwezi kama posho ya nyumba au ya makazi. Tujiulize hivi kuna chumba gani cha Sh.9,000, ambacho kinastahili chenye umeme na chenye hadhi inayotakiwa. Je, hivi kweli ni busara kwa mila, desturi na haki za kibinadamu Askari kuweza kuishi kwenye chumba kimoja na watoto wote hatuoni kwamba tunawadhalilisha na hatuwatendei haki; hivi Sh.9,000 posho ya nyumba ni kwa mshahara wa mwaka gani? Ninaishauri Serikali kuongeza posho ya nyumba kwa angalau asilimia 20 ya mshahara wa Mwanajeshi kwani itawapelekea wanajeshi wetu kupata vyumba vya kutosha kwa kuishi kwa kuridhika, kwa kutenganisha vyumba vya wazazi na vile vya watoto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, posho ya chakula cha Askari ya Sh. 75,000 kwa mwezi ni kiwango kidogo sana, kwani ni wastani wa Sh. 2,500 kwa siku, fedha ambayo hawezi kujikimu kwa milo mitatu na kuna malalamiko kwamba, ikiwa upo kazini fedha zako zinapunguzwa kwa sababu umekula Kambini. Je, hivi askari kupata chakula chake kambini unapunguza nini, hatuoni mlo huo ni sehemu ya motisha na sio kumpunguza

posho yake? Tunaitaka Serikali kuwapatia posho ya chakula wanajeshi angalau 10,000 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka kujua kigezo gani kinatumika kuwanyima posho ya chakula ya Sh. 75,000 wanajeshi wetu wanaopata nafasi ya kupangiwa mikoa hiyo ya mipakani? Ndio maana wamekuwa na msamiati mpya unaojulikana kwa jina la KUJILA, kwa mfano, unaenda Kigoma utalazimika kutumia fedha za mshahara wako bila posho ya chakula. Kambi ya Upinzani inataka kufahamu fedha hizo za posho za chakula wanazonyimwa wanajeshi, ambazo tayari huwa zipo kwenye bajeti, zinapelekwa wapi na ni lini KUJILA kwa wanajeshi wanaopelekwa mikoa ya mipakani kutapatiwa ufumbuzi?

Mheshimiwa Spika, vijana wetu wenyewe elimu ya juu na hata wenyewe elimu inayomfanya mwombaji aweze kujiunga na jeshi, wana kigugumizi na kujiunga na jeshi baada ya kuona sheria kuwa mwanajeshi anapoajiriwa hawezi kuoa na kuolewa hadi ifikie miaka sita; yaani kipindi cha mkataba. La kusikitisha ni kwamba, hata wale wanajeshi waliomaliza mkataba wa miaka sita; bado wengi wao hawajaruhusiwa kuoa na kuolewa. Je, tatizo ni nini? Kambi ya Upinzani inataka kufahamu hivi tunaposhauri na kuhimiza kupambana na UKIMWI, huku tukitaka wanajeshi wetu kuwa waaminifu, wasijiingize katika vitendo viovu, lakini unamtungia sheria asioe wala asirolewe kwa muda wa miaka sita, ni kweli tunawatendea haki na ni kweli tumedhamiria kuwalinda na UKIMWI; hivi ni kweli mwanajeshi unapokuwa unamnyima haki ya msingi ya ndoa unamtarajia aishi vipi? Kambi ya Upinzani, inaishauri Serikali; sheria hii irekebishwe na iondolewe ili wanajeshi waweze kuoa na kuolewa na kuwafanya wale vijana wenyewe hofu juu ya sheria hii waweze kujiunga na jeshi hili.

Mheshimiwa Spika, Wizara bado haijaangalia Mavazi kwa Askari wa JWTZ kwa undani zaidi. Imedhihirika kwamba, mpaka sasa hakuna utaratibu wa kipindi maalum kwa mwajeshi anaweza akabadilisha Sare za Jeshi, bila kufikia kiwango cha sare hizo kupauka/kuchakaa. Kambi ya Upinzani, ina mashaka na umadhubuti wa baadhi ya sare za wanajeshi, kwani inaonekana vitambaa vinavyotengenezwa sare hizo haviko katika viwango vinavyotakiwa; hivyo, Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kuwabana kikalifu wazabuni wote wa sare za wanajeshi wetu. Aidha, Kambi ya Upinzani inataka kujua sare za wanajeshi wetu zinatoka ndani ya nchi au nje ya nchi na kama zinatoka nje ya nchi kama inavyosadikiwa; hivi viwanda vyetu vya ndani ya nchi havina uwezo wa kutengeneza sare za wanajeshi wetu, hasa JKT na Magereza?

Hivi hatuoni kuvipatia viwanda vyetu zabuni ya sare za wanajeshi wetu wa JWTZ tutaongeza ajira kwa Watanzania, kwani Kambi ya Upinzani inapata mashaka kuelewa uhafifu wa vitambaa vinavyotengenezwa sare za wanajeshi; tunatumia fedha zetu kiasi gani; kwa maana hiyo Kambi inataka kueleweshwa na Serikali kila pea moja ya Sare ya wanajeshi inagharimu fedha kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, kuna malalamiko mionganoni mwa wanajeshi kuchelewa kupandishwa vyeo, hali ambayo imeathiri sana maslahi ya wanajeshi na hadhi zao huku wengine umri wao ukiendelea kuwa mkubwa. Haipendezi hata kidogo, askari ambaye

analitumikia jeshi mpaka anastaafu akiwa na cheo cha Lansi-Coplo, hali hii inazusha maswali mengi sana katika mfumo mzima wa maslahi ya kuinua mgongo na pensheni yake na nikweli mtu amelitumikia jeshi kwa miaka zaidi ya 20 anastaafu akiwa koplo? Kambi ya Upinzani inataka kujua ni vigezo gani vingine vinavyowapelekea baadhi ya wanajeshi kupandishwa vyeo haraka haraka zaidi na wengine wakisota taratibu mno, ukiachia mbali elimu ya muda aliyoingia Jeshini na ukakamavu wake sambamba na nidhamu ya mwanajeshi.

Kambi ya Upinzani inayasema haya ili kuweka bayana kwamba, sasa umefika wakati wa kuandaa mazingira mazuri ya kupandishwa vyeo wanajeshi wetu, kwani kuchelewa kuwapandisha vyeo si tu tunawavunja moyo kisaikolojia, lakini pia kwa namna nyingine tunawaathiri maslahi yao wakati wanapostaaful. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inaiomba Serikali kuliangalia suala hili na kulipatia ufumbuzi wa kudumu ili kuondoa kabisa manung'uniko kwa wanajeshi wetu.

Mheshimiwa Spika, moja kati ya kazi za wanajeshi wetu ni kuhakikisha mipaka yetu inakuwa salama wakati wote; kwa kuwa raia wote wa Jamhuri ya Muungano nao wawe salama. Vituo teule vilivyowekwa mipakani, vinafanya kazi vizuri katika kuhakikisha wananchi wapo salama, lakini vitendo vinavyofanywa na wahalifu wanaosadikiwa toka nchi jirani baina ya Mkoa wa Kagera na Tanzania, kwa Wilaya za Karagwe na Ngara, haviwezi tena kuvumiliwa na Wananchi wa Tanzania, huku tukiwaelekea na kuwatupia mzigo Jeshi la Polisi peke yake.

Haiwezekani, Wananchi wa Kagera waishi kwa wasiwasi ndani ya nchi yao, huku mikoa mingine ikilala kwa usingizi mnono, kwani Tanzania ni moja na wote wana haki sawa mbele ya Sheria. Kambi ya Upinzani inataka kujua vitendo vinavyoripotiwa vyakuuawa, kutekwa na kuporwa mali katika mapori na misitu kadhaa ya Mkoa wa Kagera, vitaendelea kulalamikiwa na Wabunge hadi lini bila kupatiwa ufumbuzi huku tukijua kwamba sasa wakati umefika kwa JWTZ kukomesha kabisa uovu huu katika Mkoa wa Kagera? Kambi ya Upinzani inasikitishwa sana na kitendo kinachofanywa na majambazi toka nchi jirani, kwa wavuvi wetu wa Kigoma kuwanyang'anya vyombo vyao na wengine kuuawa; hivi kweli kama Ziwa hili ni letu sote; kwa nini wanaendelea kuwatesa wavuvi wetu wa Kigoma?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka kujua Vituo Teule vilivyoko katika Vijiji vya Kagunga, Mtanga, Karago, Igunga, Herembe, Kalya, Mwakisega, Kasege na Katonga, ambavyo vimetanda kandokando ya Ziwa Tanganyika Kigoma, vinawasaidiaje wavuvi wa Kigoma wanaonyanyaswa na wahalifu ambapo wanaendelea kudhalilishwa huku wavuvi hao wakijiuliza ni lini wanaweza kuvua wakiwa na uhakika wa usalama wao? Sambamba na hilo wavuvi katika Ziwa Victoria na wao bado wanaendelea kuteseka kwa kuporwa vifaa vyao vya uvuvi na kupigwa na wahalifu, huku wakiendelea na kilio kwa Serikali yao kukomesha kero hii ambayo imekuwa sugu. Kambi ya Upinzani inataka kujua ni matukio mangapi ya uhalifu yameripotiwa katika Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria na wananchi wangapi wamepoteza mali na maisha kati ya Julai, 2007 hadi Julai, 2008 na ni kwa kiasi gani JWTZ imewasaidia wavuvi wa Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria kutokana na wahalifu wa nchi jirani?

Mheshimiwa Spika, mwezi uliopita Serikali ilifanikisha vyema Maadhimisho ya Siku ya Mashujaa, chini ya Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano. Kumbukumbu ya siku hii ni ya kipekee, kutokana na kuwakumbuka mashujaa wetu waliolinda nchi yetu na wale waliotumwa na Serikali, kuzikomboa nchi mbalimbali Kusini mwa Jangwa la Sahara. Kuna malalamiko makubwa kwa mashujaa wetu walioshiriki Vita vya Kagera mwaka 1978/79 na walioshiriki Vita Msumbiji, ambapo wengi wao sasa ni wastaa fu na wenyewe ulemavu na wengine wameshafariki dunia huku familia zao zikiendelea kuteseka.

Mheshimiwa Spika, mashujaa hawa niliowataja ambao wengi wao ni walemavu, wanaishi maisha ya kubahatisha, wakiwa wanyonge na ikionekana Serikali imewatelekeza muda mrefu. Wanajiuliza; hivi kulitumikia taifa na kupata ulemavu ni adhabu na kama si adhabu kwa nini Serikali badala ya kuwaenzi wanawatelekeza wao na familia zao?

Mashujaa wetu baada ya Uhuru wanajiuliza; inakuwaje mashujaa walioshiriki Vita ya Pili ya Dunia, wanapatiwa fedha kwa msaada toka Serikali ya Uingereza, lakini Mashujaa wetu walioshiriki Vita vya Kagera 1978/79, Vita vya Msumbiji na Renamo, mbona wameachwa mayatima, wakitangatanga mitaani na wakilia muda wote bila kunyamazishwa na Serikali yao?

Kambi ya Upinzani inataka Serikali kulieleza Bunge hili Tukufu, wapo mashujaa wangapi walioshiriki Vita vya Kagera na Msumbiji; na je, Serikali inajua wanavyoishi na Serikali inafuatilia hali za maisha yao? Ninayaleta haya kwa sababu ni huzuni kubwa, simanzi na majonzi unapowaona mashujaa hawa hawana viungo, huku wakiendelea kulalamika bila ufumbuzi wa kuboreshewa maisha yao na wanajiuliza maswali kadhaa yasiyo na majibu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inapata kigugumizi kuelewa kwa nini tumeweza kuondosha mabaki ya mifupa ya Mashujaa wa Tanzania kule Msumbiji na kuleta mifupa hiyo kuijika kwa heshima Tanzania, kule Mtwara. Hivi Serikali inafahamu familia za Mashujaa ziko wapi; na maisha ya familia hizo yakoje? Ndio kusema, kuchimba mifupa ya marehemu mashujaa waliouawa Msumbiji ni hatua ya kwanza, lakini Serikali ina mkakati gani wa kuenzi na kuzitunza familia za mashujaa hao ambazo zinateseka kwa maisha magumu, huku wakijiuliza kwa nini wazazi wao wameuawa katika ushujaa lakini familia zinatarajiwa kufa kwa mawazo na njaa? Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali, kutenga fungu maalum katika bajeti kwa Mashujaa na familia za Marehemu Mashujaa wetu, kwa lengo la kuwaenzi kwa dhati kabisa.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, inaendelea na utaratibu wa upimaji wa maeneo ya JWTZ na JKT, sambamba na kuyapatia maeneo hayo hatimiliki na hatimaye kutolewa fidia kwa yale maeneo ambayo JWTZ na JKT walijachukua kwa wananchi kwa manufaa ya kijeshi. Kambi ya Upinzani inataka kujua, maeneo yaliyopimwa; je, tayari Serikali imeshatoa hatimiliki; na je, fidia imetolewa kwa wananchi?

Mheshimiwa Spika, tunaomba ufanuzi kuhusu maeneo yafuatayo:-

- |        |                      |               |
|--------|----------------------|---------------|
| (i)    | Oldonyo Sambu JWTZ   | Arusha        |
| (ii)   | Kunduchi Rifle Range | Dar es Salaam |
| (iii)  | Bulombora JKT        | Kigoma        |
| (iv)   | Kiabakari (253 KJ)   | Mara          |
| (v)    | Buhemba JKT          | Mara          |
| (vi)   | Chita JKT            | Morogoro      |
| (vii)  | Umoja Camp JWTZ      | Mtwara        |
| (viii) | Kasanga TPDF Det     | Rukwa         |
| (ix)   | Mgambo JKT           | Tanga         |

Mheshimiwa Spika, Pia Kambi ya Upinzani inataka kuelewa ni maeneo gani ya wananchi, yaliyochukuliwa na Jeshi la Ulinzi wa Taifa na ambayo hadi leo hayajapimwa na ni mangapi yana mgogoro na wananchi; na ni hatua zipo Serikali itachukua?

Mheshimiwa Spika, wastaifu wetu wa JWTZ wamegubikwa na giza nene la maisha magumu, kutokana na kiwango kidogo cha pensheni wanachopata huku bidhaa zikipanda kila kukicha, ambapo wastaifu wengine wanafanya kazi zisizostahili kulingana na vyeo walivyokuwa navyo. Hiyo ndio hali halisi ya wastaifu kuendelea kuteseka huku umri wao ukiwa mkubwa na utegemezi wa familia; hivyo, Kambi ya Upinzani inaiomba Serikali kuandaa maisha yao tofauti na ilivyo sasa. Kuna malalamiko kati ya wastaifu wa zamani kupata pensheni ndogo, ukilinganisha na wastaifu wa hivi karibuni, hali ambayo si kwa Majenerali wastaifu, lakini hata maafisa wastaifu na askari wastaifu wa kawaida wa zamani kulinganisha na kiwango cha mshahara wa wastaifu wa sasa. Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kuwapatia pensheni wastaifu wa zamani kulingana na vyeo vya sasa. Kambi ya Upinzani inasikitishwa na kitendo cha Serikali cha kuwapatia Sh. 21600- wastaifu wa zamani yaani wastani wa Sh. 720 kwa siku.

Kambi ya Upinzani inahoji hivi wastaifu hawa waliokuwa chimbuko la Jeshi imara na kurithisha jeshi shupavu la sasa; unawapa Sh. 720 kwa siku; huku si kuwadharau na kuwakejeli? Hivi Serikali inatambua Sh. 720 kwa mwanajeshi aliye na familia kwa mahitaji ya siku moja akanunue nini; je, ni kweli atamudu hata chai ya asubuhi? Hivi Serikali hailewi hili ama haitaki kuwarekebishiwa kiwango hiki cha fedha kinachostahili au hayo ndio malipo yanayostahili baada ya kazi ngumu ya kulinda nchi hii katika mazingira magumu?

Mapema mwezi huu, wastaifu wa JWTZ walichanganyikiwa pale walipokwenda chukua pensheni yao ya miezi sita na kukuta fedha za mwezi mmoja tu. Je, tatizo hasa ni nini; mbona Serikali haitoi jibu sahihi kwa wastaifu hawa? Mnawaacha wakiwa na madeni madukani huku wengine wakiadhiria kwa kutolipa madeni ya vyakula katika sehemu wanazokopeshwa! Kambi ya Upinzani, inaiomba Serikali kulipatia ufumbuzi tatizo hili haraka iwezekanavyo, pia tunawaomba wafanyabiashara wote waliowakopesha wastaifu hawa, waendelee kuvuta subira kwani hawakutegemea kama watakumbwa na mkasa huo.

Mheshimiwa Spika, kuna malalamiko makubwa kwa wanajeshi wanaofikia muda wa kustaaafu na kuongezewa muda kwa utaalamu wao kwa miaka miwili miwili. Akimaliza muda alioongezewa, anapochukua kiinua mgongo chake kinapungua tofauti kama angelichukua muda wa miaka iliyopita, sababu anaambiwa ametumia chakula na mshahara, hivyo zimekatwa. Ikumbukwe kuwa, kila mwanajeshi hivi sasa ni msaafu mtarajiwa; je, Serikali mnalishughulikia vipi tatizo hili? Kambi ya Upinzani inataka kujua ni wastaaafu wangapi wa aina hii, wamekumbwa na mkasa huu kuanzia mwaka 2006 hadi leo 2008. Mpango huu wa kuwapunja askari mafao yao; je, Serikali mmeiga utaratibu huu toka Serikali ya nchi gani kwani hiki ni kichekesho cha kusadikika?

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ripoti ya Mdhhibit na Makaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2007, inabainisha upungufu kadhaa katika Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; hivyo, Kambi ya Upinzani inataka ufanuzi wa matumizi yafuatayo:-

(1) Je, vifaa vilivyolipiwa vyenye thamani ya Sh. 15,174,000 ambavyo havikupelekwa kwenye Mradi wa Malindi na Mbweni; vimepelekwa wapi?

(2) Je, kwa nini taarifa ya matumizi ya jumla ya Sh.24,172,373 haikutolewa?

(3) Malipo yenyeye shaka ya Sh.530,107,528 kwa Jeshi la Kujenga Taifa, ambapo taarifa ya manunuzi haikuwekwa bayana hivyo Kambi ya Upinzani inauliza tatizo ni nini?

(4) Malipo yaliyofanywa bila ya kuwa na hati za malipo kuwa jumla ya Sh.291,509,765. Je, Wizara inajua kufanya hivyo inatia shaka?

(5) Malipo yenyeye nyaraka pungufu Ulinzi – Ngome kiasi cha Sh.381,532,247, vile vile malipo yenyeye nyaraka pungufu; Jeshi la Kujenga Taifa jumla ya 3,045,290,483 hivi Wizara inalionaje upungufu huu?

(i) Fungu 39 - Jeshi la Kujenga Taifa, taswira ya matumizi haitoi picha nzuri, mfano, malipo yaliyofanywa bila ya kuwa na nyaraka ya Sh. 3,336,800,248 hili ni tatizo lingine. Maduhuli ambayo hayajapelekwa benki Sh.45,892,280; je, fedha hizi zilipelekwa wapi?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka kujua Serikali ina mkakati gani kwa Wizara husika kuhakikisha fedha zitatumika vizuri na kuachana na upungufu uliojitokeza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Kujenga Taifa, JKT limekuwa chachu kwa vijana kupata mafunzo ya kijeshi na kiufundi katika kujenga nidhamu, uzalendo na uwajibikaji wa siku hadi siku kwa lengo la maslahi ya Taifa kwa ujumla. Hivyo, stadi mbalimbali wanazopata JKT; mfano, ujenzi, kilimo, ufugaji na useremala ni kwa kiasi gani vijana hawa wanaendelezwa kwa kuwawezesha kuijendezea kimaisha mara tu wamalizapo

mafunzo yao na kutobahatika kupata ajira Serikalini? Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili Tukufu; ni vijana wangapi wameshajiunga na JKT tangu 2006 hadi leo na wangapi wamepata ajira Serikalini?

Tunayasema haya kwa kuwa na wasiwasi kwamba, idadi kubwa ya vijana wa JKT ambao wamepata mafunzo ya matumizi ya silaha na kuachwa mitaani wakitangatanga bila kutafutiwa namna ya kuendelezwa kimaisha. Je, Serikali haioni kuna uwezekano wa vijana hawa kuijingiza katika vitendo vya uhalifu? Hivyo, Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kufanya tathmini kuwatambua vijana ambao wamepitia JKT na hawajaajiriwa ili watafutiwe namna ya kuendelezwa kimaisha.

Mheshimiwa Spika, SUMA JKT limekuwa mfano bora hivi sasa katika uzalishaji mali hasa ujenzi wa nyumba bora za kisasa katika maeneo mbalimbali. Kambi ya Upinzani inataka kujua SUMA JKT wamepata faida kiasi gani kuanzia mwaka 2006 hadi 2008? Pamoja na sifa walizonazo SUMA JKT, Kambi ya Upinzani inataka ufanuzi kwa nini halijaunda Kamati ya Ukagazi kinyume na Kanuni Na. 30, 31 na 32(2) ya Kanuni za Fedha za Umma kama Ripoti ya Mdhhibit na Mkagazi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2007 ilivyobainisha. Sambamba na hilo; kwa nini Shirika la SUMA JKT halijaanzisha Kitengo cha Manunuvi kinyume na kifungu cha 44 cha Sheria ya Manunuvi ya Umma? Kambi ya Upinzani inataka kujua ni lini SUMA JKT itaunda Kamati ya Ukagazi na ni lini SUMA JKT litaanzisha Kitengo cha Manunuvi kwa mujibu wa Sheria?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka kuelewa kiwanda cha kutengeneza dawa za Binadamu cha TANZANSINO, kinachoendeshwa kwa ubia kati ya SUMA JKT na China, kimefanikiwa kutengeneza dawa ya aina gani na kimepata faida kiasi gani kuanzia mwaka 2006 hadi 2008? Sambamba na hilo, Kambi ya Upinzani pia inataka kujua ni kiasi gani cha fedha kimepatikana kwa mwaka 2006 hadi 2008 kutoka kiwanda cha kushona nguo cha CAMISUMA?

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, kwa hotuba yako. Waheshimiwa Wabunge, nimepokea maombi ya Wabunge kumi na moja kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Kwa jinsi muda ulivyo, watakaopata nafasi nadhani ni wanane, watano, kwa jioni hii na watatu asubuhi. Ndivyo ninavyoona, lakini kama michango itakuwa si mirefu sana, basi pengine walioomba wanaweza kupata nafasi ya kuchangia. Kwa tangazo hili ni dhahiri kwamba, wanaojaribu kuomba kuongea katika Wizara hii wamechelewa, orodha imefungwa kwa sababu nitakuwa najenga matumaini ya kusadikika ambayo hayapo.

Sasa walioomba ambao hawajachangia kabisa ni Mheshimiwa Yahya Kassim Issa. Halafu waliochangia mara moja ni Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Issa Kassim Issa, Mheshimiwa Anna Margareth Abdallah, Mheshimiwa Tatu Ntimizi na Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa. Kwa hiyo, kwa orodha yangu

sasa watatu wa kwanza ni Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, atafuatiwa na Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, halafu Mheshimiwa Issa Kassim Issa.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii nikiwa mchangiaji wa kwanza katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, sina tatizo na hotuba hii; ni nzuri na ina mwelekeo mzuri, sina wasiwasi nayo. Wasiwasi wangu ni kawaida yetu kuweka maneno mazuri, mengi na ya kufurahisha lakini utendaji ndiyo nina wasiwasi nao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niliwhi kuuliza swal hapa kuhusu wanajeshi ambao wameathirika katika Vita vya Idd Amin Dada. Niliuliza hivyo kwa sababu wapo wengi ambao hivi sasa hali zao haziridhishi na bado tupo katika mapambano. Nasema tupo katika mapambano kwa sababu hata ukiambiwa kwamba, kalinde usalama, uhakikishe hujui kitatokea nini. Tumeambiwa hapa kwamba, kuna vijana wetu huko Lebanon, wapo waliokwenda Comoro na wapo wenye matumaini ya kwenda Darfur.

Mheshimiwa Spika, sasa tunawapa matumaini gani kwa sababu askari hawa wana watoto, wana familia na familia zile zinataka kuendelezwa na wazee wao na wanakwenda mstari wa mbele wakati mwengine. Sasa wapo wengine toka mwaka 1978, mpaka leo hali zao ni mbaya kabisa. Hawa hawakuumia wenyewe tu, bali mpaka familia zao zimeumia na sisi tumekaa hapa kwa sababu ya kazi zao na ndiyo maana leo tunazungumza katika Bunge hili huku kila mmoja akiwa hana wasiwasi, usalama huu wanaujenga wao.

Mheshimiwa Spika, sasa ni wakati wa kufikiria kwamba, ikiwa hatuwasaidii askari hawa tunawavunja moyo katika maisha yao na tunaua familia zao. Waziri Mkuu, alisimama hapa na akasema kwamba, kutakuwa na utaratibu maalum ambao watu hawa watalipwa pesa. Sasa Waziri mhusika, kama amesimama Waziri Mkuu kujibu na siyo msaada kama wanaosaidiwa watoto wadogo au wazee, kwa sababu katika swal langu nililouliza hapa mwanzo nilijibiwa hivyo, nami nikasema haiwezi kuwa, hawa watu ndiyo waliotukomboa mpaka tukawa hapa. Kwa hiyo, wanastahili kupata malipo maalum ili wahakikishe familia zao zinapata elimu. Tunaona wazee wapo hai na bado watoto wanapata tabu kimasomo.

Mheshimiwa Spika, ikiwa hatukufanya hivyo, watu hawa tujue tutakuwa tumewatendea vibaya. Kwa hiyo, hili wakati Serikali imesema italitekeleza, kwanza, nataka kupata jibu kwamba ni kweli utaratibu wa bajeti hii umekwishatengenezwa au la?

Mheshimiwa Spika, la pili, mambo yangu mawili tu kuhusu muundo na mwenendo wa Jeshi. Kwa kweli tunaelewa kwamba, Jeshi letu ni la Muungano na kabla ya hapo ikiwa Zanzibar, Tanzania Bara kote kulikuwa na majeshi yake. Kule Zanzibar tulikuwa tunaita Jeshi la Ukombozi (JLU), kwa sababu sisi tumeipata nchi kwa vita. Kwa bahati tumefanya uchaguzi lakini walikuwa hawataki kutoa, tukaona tuna haki tukachukua, ndiyo maana likaitwa Jeshi la Ukombozi, maana yake tumejikomboa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wazee wetu wakaona busara kuunganisha. Kwa kweli ni jambo zuri kabisa, kwa sababu mkataa wingi mchawi. Tujiulize nini dhamira ya Muungano huu? Ina maana kuweza kuweka jeshi letu kuwa imara, lakini pia kujenga umoja na kujenga undugu katika Muungano wetu. Hizo ndiyo dhamira zetu, lakini sura inakwenda vipi katika shughuli hizi za Muungano? Niliwahi kuuliza swali langu hapa, Waziri mhusika akasema kwamba, matatizo yataondoka kwa sababu hivi sasa tunataka kufanya JKU, JKT lakini suala halikuwa hivyo. Tunataka sehemu zote mbili za Muungano, tuhakikishe watoto wanaajiriwa ndani ya Jeshi. Hili nalisema sana.

Mheshimiwa Spika, kuna matatizo hivi sasa yanajitokeza, sio la kuajiri JKU au JKT; hili si tatizo. Tatizo; hivi sasa hali ya uongozi umeelemea upande mmoja wa Muungano. Muungano huu tuhakikishe kwamba, hakuna atakayesema maneno kwamba, kuna nchi mbili kwamba, tumeungana nchi mbili na kujenga Taifa lenye nguvu na hili ndilo lengo la wazee wetu walioamua hivyo.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna mpango wakati wanaajiriwa wanajeshi na kwa kuwa hivi sasa maeneo yote yamedhibitiwa na upande mmoja wa Muungano, Wazanzibari vijana hawapati nafasi. Nipo Dunga na ndiko wanakopima katika Wilaya ya Kati, wapo vijana wenu walipotea wakaja Dunga, tukawaauliza vipi ninyi? Ahaa! Sisi tumeambiwa tunapimwa Jeshini, alaa hivyo! Enhee tumeambiwa tuje. Katika jibu lake alisema kila mkoa zinapelekwa nafasi na nasema Serikali ndiyo itakuwa imesema hivyo. Sidhani kama mtu wa Mtwara anakwenda Arusha, *Wallah* sifirkirii hivyo kwa sababu ni hii hii Tanzania Bara. Kule kuna taratibu maalum na hata hapo nyuma nilikuwa ni mmoja katika shughuli hizi za kuwahoji vijana amba wanataka harakati hizi, lakini linalofanyika sasa ni kwamba, nafasi zetu zinakuwa finyu kwa kuwa maeneo yote ya uongozi wanaleta watu wao; sasa sura hii ya Muungano itakuwa vipi?

Mheshimiwa Spika, baya zaidi, umefika wakati hivi sasa wengine wanaauza ng'ombe kwa kupata Jeshi. Kitu kibaya kabisa, kama mtoto anakwenda jeshini kwa kutoa chochote; kweli jeshi hilo ni zuri na huyo aliyefanya hivyo kweli ni vizuri? Leo anauza nafasi, kesho na kutwa si atauza nchi! Mambo haya yanawajibika yafuatiliwe tena vizuri kabisa. Ukiangalia Katiba yetu katika Ibara ya 13(4) inasema: "Ni marufuku kwa mtu ye yote kubaguliwa na mtu au mamlaka yoyote inayotekeleza madaraka yake chini ya Sheria yoyote au katika utekelezaji wa kazi au shughuli yoyote ya mamlaka ya nchi."

Mheshimiwa Spika, sasa mna kauli moja mnasema, wale watu si wasomi, kuna kauli hiyo inazungumzwa. Nilikuwa Mwalimu kwa miaka ishirini na mbili na sifirkirii kwamba, watoto waliopo jeshini hawanijui; si kweli hasa kwa Zanzibar ile, lakini wanalamika hata hizi nafasi za kwenda *Cadet* si rahisi, kamaliza *depot* yupo hapa Bara, kafanya *interview* apate nafasi madhali ya Ame na Makame *Wallah* si rahisi haipati nafasi. Anangojea tena aanzie Koplo, umri umeshapita; tunakwenda wapi? Hii si hali nzuri hata kidogo; wazee wameasisi kufanya Muungano ili tuwe pamoja.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka vita vya Idd Amin nilikuwa kambini watu wanapambana. Namkumbuka Marehemu Hamada Mshamba, mwenzake mmoja tena

kijana wa Bbara, ule mkamatano anamwambia nitajiua, anamwambia hapana tutarudi, twende tatarudi, umoja ule kama si hivyo angeshapotea mtu yule. Kwa uthibitisho zaidi, kama miaka miwili nyuma waliandikishwa vijana na vijana wanne wakaachwa; sijui nafasi zile alikuwa apewe nani baada ya kuachwa nafasi zile tumezunguka pale kwa sababu ndiyo haya tunayosema kila ukisogelea matatizo, hatukufanikiwa, nikapiga simu Ngome.

Mheshimiwa Spika, kupiga simu najibiwa kwamba, hao ndiyo wameshakosa; tazama kauli, watu wameshapima na kufunga funga pointi, maana yake nini, huo ni ushahidi kwamba hapo watu wanataka kuperyeza watu wao. Hatuwezi kwenda hivyo, hebu tuache haya matabaka, tuondokeni huko, kuungana huku tuhakikishe kwamba, tunakudumisha na hakuna kitu cha kusaidia kuliko kuungana sisi. Matokeo yake imekuja Ngome, namshukuru yule askari, sikulijua jina lake kwa kweli lakini ni kijana aliyeonyesha uungwana wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, tulifuatana na yule kijana mguu kwa mguu, tukaenda kunakohusika, matokeo yake ndiyo tukafanikiwa. Namshukuru sana kijana yule, kwa bahati ni mmoja wa wanajeshi, alikuwa chini ya Waitara; ni kijana mdogo kabisa, alionyesha uungwana. Kwa hiyo, mambo kama haya na pia ibara ya 148 kwa kweli tunajua kwamba, Amiri Jeshi wetu ni Rais, sasa tusimpake matope. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Yahya Kassim Issa. Sauti yako kali kidogo, nadhani ndiyo hivyo tuko kila aina. Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, wakati huo huo ajiandae mdogo wake Mheshimiwa Yahya; Mheshimiwa Issa Kassim Issa.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kusema machache katika Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Nasema machache kwa sababu kimsingi mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama na ni mionganoni mwa waliowasikitikia sana ndugu zetu hawa, kwa bajeti ndogo kulingana na mahitaji yao. Hata hivyo, kuna mambo lazima tuyazungumze kwa sababu kimsingi hatuizungumzi Wizara tu, lakini tunazungumza mbele ya Serikali ili kama kuna namna ya kusaidia Wizara hii, waweze kupata msaada hasa kwa wakati tulionao au siku zinazokuja.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kulipongeza sana Jeshi la Wananchi la Tanzania, kwa kazi kubwa wanayoifanya hasa wakati ambapo nchi yetu inakumbwa na majanga mbalimbali. Wanafanya kazi ya kizalendo bila malipo na wanafanya kazi ngumu inayostahili kuonewa huruma lakini kwa sababu wao ni Wazalendo kweli kweli, hilo wala hawajali.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuitia kwa Waziri, kwa kazi anayoifanya ya kudumisha nidhamu na uongozi bora ndani ya Jeshi letu. Jeshi hili ni mionganoni mwa majeshi machache sana katika Bara la Afrika, ambalo toka limeasiswa halijaonyesha

namna yoyote au tamaa ya madaraka. Tumeshuhudia majeshi mbalimbali katika Bara letu, wanazozana na viongozi wa kisiasa mara wanakwenda wao *State House*, ni kutamu lakini wao wanajua kuwa wajibu wao ni kulinda mipaka ya nchi yetu na wanaifanya kwa uangalifu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo sasa, wenzangu wamesema hapa kuhusu mafao; napata tabu kidogo ninaposikia kuwa askari mstaafu ambaye pengine alikuwa na cheo kikubwa lakini kwa sababu kastaafu miaka ya nyuma anapewa Sh. 21,000. Jamani Sh. 21,000 kwa mwezi ni pesa kidogo sana, pamoja na kuwa nchi yetu ina ukata, lakini naomba Serikali iliangularie sana jambo hili. Sh. 750 kwa vyovoyote vile, mlo mmoja tu hauwezi kutimia. Naomba Mheshimiwa Waziri, atakapokuwa anahitimisha, atuelimishe askari wa jeshi anatakiwa ale chakula kiasi gani kwa siku akiwa peke yake bila kuwa na familia? Nafikiri hii itatusaidia kuelewa na labda watu wa Serikali watassaidia kuona huruma kwa sababu jambo hili linahusu binadamu.

Mheshimiwa Spika, katika msingi huo basi, askari hawa wanaostaafu wengi wao wanakimbilia nchi jirani. Wataalam wa uchumi zamani walikuwa na lugha wanaita *comparative advantage*, sasa wameondoka huko wanasema *competitive advantage*, wanakwenda nchi jirani kwa sababu ya kutafuta ajira. Sasa napata mashaka kwa sababu katika vita ukimteka askari mgeni kama mnapambana moja katika kitu muhimu unachotafuta kwake ni taarifa pengine ya Jeshi lake au pengine ya nchi yake. Sasa sijui mtu anayeondoka kwa hiari yake ambaye umemfanya awe na maisha magumu, anakwenda nchi nyingine anatumwiwa, anafanya kazi, sijui katika hali ya kawaida huogopi pia anaweza kutoa taarifa ambazo zinaweza kuathiri nchi yetu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nafikiri hawa watu tuwatunze sana ili wasipate ule utashi wa kuondoka kwao wakaenda kutumika katika sehemu nyingine. Wanafaidika, kwa sababu tuna taarifa kwamba, wanaokwenda huko muda mfupi tu wakirudi wanajenga nyumba na kufanya mambo mengine ya maana. Sasa sijui, kwa sababu wenzetu wanaenzi sana majeshi na sisi tuna hali mbaya ya uchumi kiasi hicho au ni kwa sababu hatujawapa kipaumbele askari. Usipompa kipaumbele mtu anayelinda usalama na utulivu wa nchi yako, hivi utampa nani? Nauliza swali hili.

Mheshimiwa Spika, wanajeshi wana malalamiko mengi, nilibahatika kushiriki kwenye Mkutano wa Sullivan kule Arusha, askari hawa wa jeshi walikuwepo na walifanya kazi ya ziada, lakini mwisho katika malipo waliyolipwa ikaonekana kuna tofauti kubwa; askari wa jeshi aliyelipwa sana alipewa Sh. 10,000, vikundi vingine vyatilizaji vilivyokuwepo pale pale walipata Sh. 30,000, Sh. 34,000 au Sh. 40,000.

Mheshimiwa Spika, tofauti hii inamfanya askari avunjike moyo kwa sababu kazi aliyoifanya ndiyo ile ile ya kulinda mkutano, usalama wa wajumbe, lakini inapokuja katika suala la malipo wengine wanafaidika zaidi. Ningombaa mambo kama haya yatazamwe, kwa sababu ni vitu vidogo vidogo lakini vinajenga sura ya kuchukia ambayo si nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu Mererani. Askari wetu wa Jeshi, wameshiriki katika uokoaji wa janga lile kubwa la kusikitisha sana, vilevile vikundi vingine vimelipwa, lakini majeshi labda ni kwa sababu ya huo ujeshi wao hawakulipwa. Labda kwa sababu wanajeshi wana makombati makubwa na wakienda pale huwa na mikazo mingi, nafikiri huwa wanadhaniwa kuwa hawali; na wao wanakula, kwa hiyo, wanahitaji waangaliwe sana.

Serikali lazima iitazame sana Wizara hii. Askari huwa wanapata Sh. 75,000, lakini Sh. 5,000 nayo ni pesa ndogo kwa sababu wana familia, wanapanga nyumba nje ya kambi, inabidi mtu alipe kodi ya nyumba na apate chakula.

Mheshimiwa Spika, sasa ukiangalia Sh. 5,000 ya chakula na Sh. 10,000 za nyumba anazopata ni kidogo sana, ambazo hata sisi wenyewe, maana yake kuna baadhi ya vitu hata usihitaji mtu kutoka mbali akwambie; mkikaa tu watu mliopo Serikalini, mnapopanga hizi *sealing*, mzipange kweli kulingana na sungura mdogo tuliyenaye, lakini iangaliwe katika sungura huyu unachukua kiasi gani kupeleka mahali ambako ni nyeti. Hata nyumbani tu katika mila za Kiafrika, chakula akinamama wakipika wanawawekea chakula kingi kidogo akina baba kwa sababu wao ndiyo wanaohangaika.

**MBUNGE FULANI:** Sasa hivi hakuna.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mpaka leo yapo kwa watu ambao wanaangalia umuhimu wa baba.

Mheshimiwa Spika, sitaki kusema kuwa majeshi ndiyo baba wa nchi, lakini wao wana jukumu ambalo tunapaswa kuliangalia sana.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kuhusu mashujaa. Napenda nimwulize Mheshimiwa Waziri; hivi kuna fungu maalum la mashujaa katika nchi yetu ambalo wanalipwa mashujaa, maana yake isiwe tu tunatumia fedha nyingi tunakwenda kuwakumbuka kwa mambo ya ngao, sime na magwaride makubwa; lakini wakiondoka pale hawapati kitu, hiyo itakuwa haitusaidii sana? Katika bajeti ya Wizara hii au ya Serikali ni vizuri kukawa na fungu maalum japo kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali, kuwe na fungu la mashujaa ambao watakuwa wanaangaliwa katika maisha yao ya kila siku. Vinginevyo, ushujaa wao unaokumbukwa kwa kupigwa tarumbeta na saluti kubwa haitasaidia sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maisha ni magumu sana, watu wenye nguvu zao hawawezi kujikimu; je, mtu mzima ambaye ameshapigana vita huko inakuwaje? Hiki kitu kinasikitisha sana. Nafikiri hilo ni lazima tuliangalie.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nije katika hoja ambayo ni nzito kidogo. Kuna vijana wetu wengine wapo katika sehemu za kati, yote ni Tanzania lakini tukubali kuwa kuna sehemu tunaweza kuziita ni za mazingira magumu kulingana na mambo yanayofanyika. Tumeambiwa sasa hivi kwamba, katika maeneo ya Kanda ya Ziwa ni namna gani askari wanavyokabiliana na majambazi na hatari nyingi. Ni tofauti sana na askari aliye Lugalo na yule anayefanya kazi kule Biharamulo.

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, kwa mawasiliano ya karibu na Mkuu wa Majeshi, wawaangalie hawa vijana ambao wamekaa katika mazingira yale labda kwa miaka saba mpaka kumi au zaidi; sio tu kuwapatia namna ya kuwahamisha na kuwapeleka sehemu nyingine, lakini pia kuwapatia labda nitumie neno la Kiingereza; *incentives* ambazo zitaweza kuwapa moyo katika kufanya kazi zao, kwa sababu katika lugha ya kawaida wanasesma mcheza kwao hutunzwa. Sasa kwao ni hapa ndani ya nchi yetu, kwao ni pale ambapo wamekwenda kufanya kazi kwa imani na uaminifu wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nataka nilalamikie suala ambalo Mheshimiwa Yahya amelisema. Sina hakika tatizo liko wapi, kwa sababu ndiyo Utanzania huo. Zanzibar kuna mchanganyiko wa watu kutoka pande zote mbili, Pemba kuna mchanganyiko wa watu kutoka pande zote mbili, Bara huku kuna mchanganyiko wa watu kutoka pande zote mbili na tunawatumia hawa kwa sababu ni wenzetu. Kwenye kura hatugombani, kwenye chaguzi mbalimbali hatugombani, kwa nini tunagombana katika kutafuta nafasi za kijeshi? Kama hili ni tatizo, basi ni vizuri liangaliwe lakini nafikiri hii ndiyo *integrity* iliyotakiwa katika nchi yetu na tunapaswa kuiunga mkono na sio kuilaumu sana.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri aangalie kama kuna nafasi zetu ambazo ni za Unguja na Pemba hatuzipati, wanapata wengine; hilo ni jambo dogo kwa sababu kuweza kupata taarifa kama hizi ni kazi ndogo kabisa wala hailazimu tuje kusimama hapa kusema, kwa sababu si kila kitu tunatakiwa kukisema humu ndani. Mengine ni yetu ya ndani na ni aibu zetu wenyewe; ni vizuri tukazihifadhi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa na nimtakie mafanikio Mheshimiwa Waziri, hapo atakapoomba kupitishiwa mafungu. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. ISSA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini vilevile napenda kukueleza kwamba, nami sauti yangu kali kidogo kwa sehemu hii ya jeshini na aliyezungumza kwa sauti kali ni ndugu yangu baba mmoja, mama mmoja. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, la pili, napenda kuipongeza Wizara ya Ulinzi, Waziri, pamoja na Mkuu wa Majeshi na kwa kuzingatia hasa Waziri wa Ulinzi ni mwenzangu sana. Vilevile mimi ni mdau, natoka jeshini. Sasa nitazungumza kulingana na hali halisi ya jeshini tuliyokuwa nayo. Jamani wataalam mnaotoa fedha katika Wizara ya Ulinzi, mnaangalia kwa ufinyu sana na mnawaumiza wanajeshi, kwa sababu hii ni Wizara ngumu sana, ni nyeti na imegawanyika makundi mawili; kuna Wizara na Ngome yenye ambayo ina wanajeshi. Sasa tukikaa hapa kila siku tunazungumza kuhusu habari za Wizara hii, matatizo ya Wizara hii na matatizo wanayopata wanajeshi wetu lakini hakuna kinachoendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu habari ya wazabuni Jeshini. Kwanza, huduma ya wanajeshi, shilingi 2,500 nataka waniambie *this scale* ya chakula

anachotakiwa kula askari; mchele gramu 270, nyama gramu 240, sembe gramu 240 mbali ya vidokezo vingine, mnamlipa shilingi 2,500 lengo lenu ni nini? Wakati wanafunzi wanapiga kelele mnawapandishia fedha, wanajeshi wanaotulinda sisi tukawa hapa kwa usalama kama Mheshimiwa Spika alivyosema, lilitokea tetemeko la ardhi Waheshimiwa Wabunge mlitafutana; je, ukilia mzinga tutakuwaje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *scale* ya maaskari wanayolipwa kwa ajili ya *ration allowance* wazabuni watagoma. Mimi nilikuwa mzabuni na-*declare interest*. Wazabuni ni wazalendo na wanajeshi kwa sababu hali ya maisha imepanda. Leo umekwishawaambia wasipande magari bure wanakaa shamba, Kambi wanaifuata maili 25 au kilomita 40; watajihadumia vipi na pale Kambi hakuna nyumba? Tegemeo lenu huyu askari afanye nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naishauri sana Serikali na Wataalam na hasa ile Wizara ya Fedha na Uchumi, nina masikitiko sana. Naibu Waziri wa Fedha, ametoka Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, leo basi angalau asiwatetee wanajeshi *ration allowance* angalau ya shilingi 5,000 iweze kukidhi angalau kidogo na ukali wa maisha.

Mheshimiwa Spika, leo tunakaa hapa tunaambizana sungura mdogo; sungura mdogo maisha yote miaka 44 anakuwa mdogo tu! Sasa hivi tutumie kondoo, sungura hafai tena na hasa kwa Wizara hii. Tusidanganyane bwana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, leo tatizo lolote likitokeza mnawatumia wanajeshi, hapa juzi tu Watumishi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, walikuwa wanataka kugoma mkawapeleka wanajeshi; daraja limebomoka, Waziri vidole vilikuwa havichoki vinaumia kwa kupiga simu Kyela kunatakiwa daraja, walipelekwa wanajeshi, wamepewa nini? Wamepelekwa sawa ni wajibu wao kufanya kazi, lakini na sisi tusiwasifu tu, maslahi yao ni madogo; unapomsifu mtu na maslahi yake mtengenezee. (*Makofi*)

### **MBUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MHE. ISSA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, la pili, nyumba wanazoishi askari. Waheshimiwa Wabunge, wamesema ni aibu tupu. Mimi ni Mbunge wa Jimbo la Mpenda, Makao Makuu ya Nyuki, Brigedi ipo kwenye Jimbo langu. Lazima ninapoenda kwenye mazoezi ninapita Nyuki Brigedi, nikitoka nyumbani kwangu kwenda mazoezini ni lazima nipte Nyuki Brigedi; ni aibu tupu. Ikinyesha mvua uweke ndoo panapokuwa na kitanda, nyumba zile ni mbovu hazistahili kukaa wanajeshi. Kama kuna tatizo wapeni *NSSF* wajenge nyumba na viwanja vipo; kwa nini tusiwajengee nyumba; kama tunatakiwa tuwapatie maisha bora wanajeshi; kwa nini hatuwatunzi, tunawapa kazi nzito tu, tunawasifu kila siku hapa wanajeshi, wanajeshi? Mtoto unapomsifu hata zawadi humpi, hata danganya toto basi hakuna. Sisi tunapofika hapa tunakula pipi! (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, hongera, sasa kwa nini wanajeshi hatuwatunzwi?

Mheshimiwa Spika, kuhusu huduma ya usafiri, kweli kwenye kitabu chake cha hotuba Mheshimiwa Waziri ameeleza huduma ya usafiri, lakini mimi ninakubaliana na

maelezo yake; ni mazuri lakini hakuna kinachofanyika. Ushahidi kamili ninao, Askari wa Dunga anakotoka Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, wanapanda magari ya mawe, usafiri hakuna. Magari yanayochukua mawe wanajeshi ndiyo wanayopanda; si aibu hii!

Mheshimiwa Spika, tuna miaka 45 tunaendelea mwanajeshi apande *tipper* juu kuna mawe, usafiri hakuna, inanitia uchungu sana na mnistahimili kwa sauti ninayoitoa kwa sababu mimi nilikuwa Askari Koplo; askari wa chini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Jeshi halijabadilika ni lile lile ingawa kuna wataalam, *scale* wanatumia ile ile mpaka leo, *ration allowance* ile ile, lakini tatizo lililokuwepo fedha wanazopewa wanajeshi hazitoshi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukienda Kambi ya Dunga ni aibu na ipo barabarani, lile banda la ulinzi limeliwa na mchwa, nenda Chukwani, Mwenyezi Mungu Askari anawasitiri. Namwomba Mkuu wa Majeshi apite Chukwani aone hali ya askari ilivyo; Mwenyezi Mungu anawanusuru tu. Waziri ni shahidi, nadhani amekwenda Chukwani ambako Askari wanafanya kambi kuna aibu ya vyoo. Nilipiga kelele mwaka jana hapa, kama kitatokea kipindupindu askari watakufa, lakini Mungu anawasitiri askari wetu matumbo yao ni ya madhubuti. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, wamezungumza mengi hapa, lakini ndugu yangu Davis Mwamunyange, afande wangu, watu wana imani sana na ye. Vilevile askari wamepata matumaini sana kwa ye ye kuchukuliwa kuwa Mkuu wa Majeshi.

Mheshimiwa Spika, lakini namwomba sana Mkuu wa Majeshi, aangalie utaratibu mzima anaokwenda nao hivi sasa; wanadhimu wake baadhi ya wengine wanampotosha. Kwa nini nimezungumza wanampotosha?

Mheshimiwa Spika, leo hili Jeshi jamani kweli ni la Muungano, lakini nenda Makao Makuu; katika nafasi za Wakurugenzi tisa hakuna Mzanzibari hata mmoja na wengine wanakwenda kujipendekeza kwao ili wapate kukaa pale, wengine hawaondoki. Basi Wazanzibari kama hakuna wasomi, lakini wapo kwa sababu mpaka sasa hivi katika Jeshi letu hili walio na vyeo vya juu ni Wazanzibari watano tu kuanzia Brigedia yupo mmoja, Makanali sijui wapo watatu peke yao; mmoja yupo Egypt na mmoja yupo India. Maluteni Kanali ni wawili tu. Jamani hakuna wengine wa kuweza kuwapandisha vyeo, tukaona na sisi kama kweli hili Jeshi la Muungano lipo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninamwomba sana Mkuu wa Majeshi aangalie upandishaji vyeo, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa alisema. Ni dhahiri vijana wanaotoka Zanzibar wanaomaliza *form six*, kupelekwa *cadet* jambo hilo ni gumu. Tunao vijana wamemaliza *form six* mwaka wa kumi huu, wengine wapo tayari kuacha kazi, hawajawapeleka hata ile *cadet* kwamba, wamefeli na wanafaulu katika mitihani. Tunakwenda wapi namna hii?

Mheshimiwa Spika, Mkuu wa Majeshi aangalie sana washauri wake, wengine wanampotosha kwa faida zao; Wazanzibari wasomi mimi ninajua wapo, lakini inabidi

tuweze kulisema hili suala na ninajua atalichukulia hatua. Sina wasiwasi na yeze kwa sababu yeze ni msikivu na mtamaduni wa kuweza kufahamu anayoelezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika haya niliyoweza kuzungumza na niliyoweza kuchangia, naomba tena sana na nitarudia kusema kuhusu matatizo ya Maaskari wa Makambi yote yanayohitajika. Jeshini kuna demokrasia, lakini si kweli kwamba kuna demokrasia; kwa sababu askari akisema ole wake! Najua na ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri anapotembelea makambi, anapofanya vikao vyake awaite maaskari.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii. (*Makofi/Kicheko*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Issa Kassim Issa, kwa utetezi wako. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Anna Abdallah na kama nilivyosema, atafuatiwa na Mheshimiwa Tatu Mussa Ntimizi.

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Lakini awali ya yote, naomba kuunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watu wote wanaomsaidia katika kazi hii kubwa ya ulinzi wa Taifa letu. Aidha, napenda kumpongeza Jenerali Davis Mwamunyange, ambaye ni Mkuu wa Majeshi, Afisa Mnadhimu Mkuu wa Jeshi, Luteni Jenerali Abdulrahaman Shimbo na vilevile Meja Jenerali Madata, Mkuu wa *JKT* na Wasaidizi wao wote wanaowasaidia katika kazi hii nzito. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuishukuru sana na kulipongeza Jeshi letu kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kulinda na kutunza amani ya nchi yetu. Wamefanya kazi nzuri sana vijana wetu wa Jeshi kule Comoro na kule kote walikotajwa kwamba, wamefanya kazi. Napenda kuwapongeza sana, kwa kazi nzuri waliyoifanya kule Mererani na hivi karibuni kule Kyela, wamefanya kazi nzuri sana. Bila wao, ninadhani mpaka leo pengine tungekuwa tunahangaika na daraja lile kule. Kwa hiyo, tunawapongeza sana kwa kazi hiyo. Hii yote inadhihirisha kwamba, katika Jeshi tuna mafundi wakubwa sana na wa kila aina. Jeshi na ndani ya *JKT* kote kuna mafundi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, cha kwanza, ninaiomba Serikali na tunawaomba wananchi kwamba, nchi yetu inaitwa ni Kisiwa cha Amani, lakini tusiichezee amani hii; hajji hivi, kazi inafanyika. Jeshi letu linasemekana ni dogo, lakini ni la kitaalam. Jeshi dogo la kitaalam linahitaji kuimarishwa, kusaidiwa na kupewa vitendea kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu, waliokwisha kusemea juu ya posho na juu ya kusaidia jeshi kuwa na vifaa vya kisasa. Sasa hivi ni wakati wa Sayansi na Teknolojia na Jeshi nalo lazima liende kwenye teknolojia hiyo ya kisasa. Kwa hiyo, hizi ni kazi ambazo zinahitaji fedha, lakini kwa bahati mbaya sana, ukiona fedha wanazopewa hazitoshelezi. Fedha hizo hizo kidogo watafanya kazi nzuri, lakini tusichukulie kwamba, kwa kuwa wanafanya kazi nzuri, basi hawastahili nyongeza; tunahitaji sana Jeshi liimarishwe na lipewe fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisi tuliopo kwenye Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, tunashukuru kwamba, tumepitia vipengele vyote vinavyotakiwa katika bajeti yao. Katika kila kipengele, kuna upungufu mkubwa sana wa mahitaji. Kwa hiyo, tunasisitiza kwamba, si vyema hayo mambo yaletwe hapa katika Bunge, lakini kwa kupitia Kamati basi ni vizuri Serikali isikilize Kamati inasema nini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaunga mkono kabisa yale yote yaliyosemwa mbele ya Bunge hili na Mwenyekiti wa Kamati. Kwanza, suala la kuhuisha Sheria ya Ulinzi wa Taifa, Sheria ile inatakiwa kuhuishwa siyo mbaya, lakini kuna vipengele vinahitaji kuhuishwa sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, tunaomba hivi; wakingoja mpaka baada ya Uchaguzi wa mwaka 2010, Waheshimiwa Wabunge watakuwa wapya. Sasa mpaka waanze kwenda kuwaeleza tena matatizo na nini kuja kubadilisha itachukua muda. Kwa kuwa sisi tumekwishakuelewa, tunahitaji Sheria hii ihuishwe kabisa katika kipindi hiki na ifanywe mapema. Tunajua maeneo ya kuhuisha wakiileta tutayasemea, kama haitaletwa mimi nitaiomba Kamati yangu iilete na hili siyo jambo jema sana. Kwa hili ni Sheria ya Ulinzi wa Taifa, kwa nini sisi ndiyo tuone ina upungufu? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namwomba Waziri na ninaiomba Serikali na wengine wote wanaohusika, wahakikishie kwamba, kama tulivyowashauri waihuishe ile sheria na wailete humu ndani ya Bunge katika kipindi hiki na tingesema hata mwezi Oktoba, 2008 mbona bado kuna nafasi kubwa sana. Kwa hiyo, wafanye hivyo.

Mheshimiwa Spika, pili, suala la kuanzisha *military service*, hili jambo tusilione kama ni la mchezo. Wenzetu wanajeshi wanazo sheria; ni kweli wanazo taratibu, lakini ni vizuri haya mambo yote ya maslahi na nini yanahitaji kuwe na *military service* ambayo imepitishwa na Bunge hili?

Mheshimiwa Spika, kuna mambo ambayo tumeyaona ambayo Kamati imesema, lakini naomba niyatilie mkazo. Kwanza, kama tunavyofahamu kwamba, sheria za ndani ya jeshi ni tofauti sana na sheria za kiraia. Hili suala la miaka sita mimi nasema ni sehemu ya sheria ya jeshi. Haiwezekani sheria ya jeshi ikawa sawa sawa na sheria ya mwalimu, daktari na ya kila mtu. Hili ni jeshi tuwaacie, lakini haya mambo yahuishwe vizuri ndani ya *military service*.

Mheshimiwa Spika, kuna mambo ambayo yanafanyika; kuna sheria ingawa wanayo kwenye jeshi kuna hii *service pensions and gratuities regulations*, utakuta kwamba masharti yale ingawa ni ya jeshi wameiga ile ya utumishi wa umma. Kwa mfano, tunao wanajeshi ambao wamemaliza muda wao, wamefikia umri wa kustaafu lakini ni watalaam, wanajua mambo fulani fulani wameombwa, siyo kwamba wanaombwa wanaamriwa kuendelea na kazi. Inasikitisha kwamba, baada ya muda wanaambiwa ninyi, sasa sheria ya umma inasema lazima wapewe sijui *contract*, sijui waandikiwe na nani ili wakubaliwe.

Mheshimiwa Spika, sasa huku jeshini ni tofauti anapewa amri hawezi kubisha anaendelea na kazi. Kwa hiyo, ama hii *service pensions and gratuities regulations* kwa kuwa ni *regulation* ibadilishwe haihitaji kuja humu ndani ya Bunge. Tunataka katika Bunge lijalo, sisi kwenye Kamati tuambiwe kwamba imebadilishwa. Hawa wanajeshi wanaoendelea na kazi baada ya muda wao wa kustaafu, walipwe pamoja na muda wao ule walioendelea. Si hilo tu, wale wote ambao wamekumbwa na haya masahibu walipwe mara moja, kwa sababu wameitumikia nchi. Haifai kuwasifia hapa kuwa wanafanya kazi nzuri, halafu inafika katika jambo hili ambalo tunawaona wao kama ni watu wa kawaida ama ni *civil service* tu ya kawaida; hili jambo halifai. Tukiwa na *military service* yao peke yao, mimi nina hakika wataweza kuyaweka haya na kuyahuisha yakawa tofauti na taratibu za kawaida za utumishi wa umma. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, tuna wastaafu wengi sana katika nchi yetu; walimu na madaktari wengi; lakini fedha zao za pensheni hazikuwekwa katika Wizara walizokuwa wanazitumikia. Fedha zao za pensheni zipo kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali, zinatoka huko ndiyo wanalipwa. Kwa mshangao mkubwa, tumegundua kwamba, pensheni za wanajeshi anapewa Waziri, yaani katika Makadirio ya Matumizi ya Wizara hii tutakayopitisha ni pamoja na fedha za pensheni za hao wanajeshi wastaafu. Sasa ukiona hata shilingi bilioni nane; karibu nusu nzima inakwenda kwenye pensheni. Kwa hiyo, jeshi lenyewe hawana fedha za kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi ninaiuliza Serikali; kwa nini Wanajeshi tu ndiyo pensheni zao wanapewa Wizara na kama ndiyo hivyo basi kila Wizara ichukue pensheni za wafanyakazi wake wote ambao wamestaafu? Kwa kupeleka fedha hizo kule halafu Wizara inaonekana ina fedha nyingi, tunawapa matatizo yasiyokuwa na msingi. Wao wanawenza kufuatilia matatizo ya hao wastaafu wa jeshi na kila kitu.

Mheshimiwa Spika, nafikiri Kamati imependekeza hapa kwamba, inaitaka Serikali ihakikishe kwamba, fedha za pensheni haziwekwi katika bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Fedha za bajeti ziwekwe katika Mfuko Mkuu wa jumla wa Serikali. Hilo ndilo ombi lingine, mimi nadhani Serikali hii inasikia.

Mheshimiwa Spika, katika Sherehe za Nane Nane mwaka huu, Kaulimbiu ilikuwa Mapinduzi ya Kijani, wengine wakasema ni mkombozi wa mkulima, wengine wakasema watasababisha Tanzania isiwe na njaa na mambo mengine. Mapinduzi ya Kijani katika vikosi vya JKT hasa SUMA JKT hawa ni watu ambao katika vikosi ambavyo vina mashamba makubwa na mazuri, ndiyo walimu watakaoleta mapinduzi ya kijani kupitia wale vijana wanaokwenda katika makambi haya kujifunza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, wakulima wetu wengi huko vijijini hao tunaowaita *peasant farmers*, wana kazi kubwa sana ya kupeleka sijui Afisa Ugani na wa kufanya nini. Kwenye JKT wanao Maafisa Ugani na wanafundishwa kwa nidhamu. Katika kipindi cha miaka miwili, wale wanaomaliza wakirudi vijijini wanaweza kuwa walimu wazuri sana. Sasa mimi nataka kuuliza; je, katika Mipango ya Kilimo ya Wilaya (*DADPS*), mashamba haya ya JKT na Magereza yapo katika mipango hiyo? Je, mashamba hayo ya kilimo na mifugo yanapataje msaada huo wa miradi ya kilimo? Kwa sababu bila hivyo, eti wao

ndio watafute fedha kutoka Wizarani tuwaone kwa sababu wanazalisha. Kwa hiyo, tunaomba wawe *integrated* na mimi ningependa kujua kama wanahesabiwa katika hizo *DADPS* ili na wao waweze kunufaika na hizo fedha za kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nina hakika kabisa tunaweza. Kwa mfano, hapa Dodoma, Kiwanda cha kutengeneza mvinyo Hombolo kinahitaji tani 400,000 za zabibu, sasa hivi Dodoma inatoa tani 400 tu. Mimi nina hakika, Makutopora inaweza ikatoa mpaka tani 100,000, kwa kuwa kuna vijana pale wana mashamba na wana utaalal hebu muwafikishe huko. Waziri amesema hakuna fedha za kutosha, lakini tutakuwa tunafanya jambo la ajabu, tuwaambie wajitegemee halafu hatuwekezi nya kutosha.

Mheshimiwa Spika, lingine ninalotaka kulizungumzia ni suala la vikosi nya ujenzi vilivyo ndani ya Jeshi la Kujenga Taifa. Vikosi hivyo vina uwezo mkubwa sana na kwa mujibu wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kazi walizozipata katika mwaka wa fedha uliopita ni kidogo sana na ni kazi ya Serikali. Kwa hiyo, tunaomba hao mnawaachia sijui kurekebisha hiki na kile kwenye Makambi yao na nini, kuna vitu vingine ambavyo hatulazimiki kuwapa makandarasi wa nje; ni vitu ambavyo ramani zake na kila kitu tunatakiwa tuijue sisi humu ndani tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi ninasema hiyo Sheria sijui ya Manunuzi hebu wairekebishe, kuna kazi za lazima za kufanywa na majeshi yetu; Jeshi la Kujenga Taifa, Wanajeshi wenyewe, kuna vikosi nya ujenzi kwenye magereza na kadhalika. Hivi sisi tuna aibu gani wanasema haki za binadamu. Mimi ninaambiwa kabisa katika hao tunaosema kuna makandarasi kutoka nchi za nje rahisi sana tunawapa miradi yetu yote wanatumia *engineers* wengine amba ni wafungwa tu, wanakuja kuwafanyisha kazi huku wanawapa fedha na kila kitu. Sasa sisi tuna watu wengi, tuna *labour* hii ambayo hatuitumii sisi, nafasi hii ni kujijengea uwezo. Sasa tusipowapa sisi kazi; nani atakayewapa kazi wanajeshi, kazi mbili kwa mwaka sijui nani? Wizara ya Miundombinu kazi zote walizonazo wamewapa miradi miwili tu ni aibu sana. Kwa hiyo, tufanye hii kazi ili waweze kujitegemea. Sasa kuna wengine wanasema kuna *research* zinafanywa; sijui wanafanya hivi Jeshi la Israel; sasa sisi tusipowapa hizi kazi nani atakayewapa? Mimi nasema, tuwe wanamapinduzi tuwape kazi kama tunataka wajitegemee.

La mwisho, mimi nilisikitishwa sana niliposikia tangazo hivi karibuni na sijui limetoka kwa Mkuu wa Majeshi ama limetoka kwenye Wizara; Katibu Mkuu anatutangazia umma kwamba, wanajeshi wote lazima walipe nauli kwenye daladala; hivi ni utawala bora huu, hawa wanajeshi hawana makamanda wao wa kuwaambia hayo? Sisemi wasafiri bure, lakini ni sahihi kutangaza wanajeshi wote mkiwaona humo ndani ya madaladala wamevaa *uniform*, msiwaogope watoe nauli; jamani kwa nini watoe nauli, tunawadhalilisha vijana hawa! Isingewezekana kupeleka *circular* hii kwenye makambi yao huko wanakokaa, kuwaambia haya kila mtu wakastukia kwenye daladala mwanajeshi anatoa nauli.

Mheshimiwa Spika, sasa tunawatangazia umma, jana tena nilisikia, wanalamika huko kwenye daladala wanajeshi hawatoi nauli wanawakomalia; mimi nasema afadhali wakati mwingine. Lazima tuwe na utawala bora jamani, siyo kutangaza kila kitu tu hata

kama nchi hii ni ya utandawazi, sijui mnasema ya uwazi na nini; yapo mambo mengine ya ndani waambieni hawa vijana ndani lakini sasa mmekwisha kuharibu. Mimi hili sikulipenda sana, tena si ajabu waliootoa hii *circular* wenyewe wana magari tena makubwa kabisa, wanatembea peke yao. Sasa mimi nasema hili siyo zuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Anna M. Abdallah. Namuita sasa Mheshimiwa Tatu Musa Ntimizi, hayupo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa.

**MHE. MASOLWA C. MASOLWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nizungumze machache japo kwa dakika tano. Awali ya yote, ningempongeza Waziri, Naibu Waziri, pamoja wapiganaji wa Kambi ya Wanajeshi, kwa kazi nzuri wanayoifanya kama wenzangu walivyotangulia kusema. Ninawaomba kwa kuwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wamechukua nyadhifa zao hivi karibuni, basi wazitembelee kambi zetu ili wakutane na wanajeshi wetu, wasikilize matatizo yao na sisi Wabunge tukiwepo ni vyema kama watuarifu.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Bububu limebahatika kuwa na kambi mbili za kijeshi ambazo ni za kihistoria. Moja ni Kambi ya Mwanyanya na sina shaka askari waliotangulia miaka ya nyuma, ambao walikuwa makomandoo wamatokea kambi ile. Sasa imehashiwa kambi sehemu nyingine. Bububu pia ni kambi ambayo kuna hospitali ya kisasa kabisa, ambayo naipongeza Serikali kwa kutupatia hiyo hospitali, ambayo inasaidia hata raia; zaidi raia ndiyo wanaopata tiba pale ukilinganisha na askari wake.

Mheshimiwa Spika, sasa nikianzia na Kambi hiyo ya Bububu, pamoja na pongezi hizo, lakini ningeomba sana Serikali hiyo hospitali ikamilishwe kama ilivyokusudiwa mwaka huu. Kuna mashine ambazo ni za kisasa kabisa zilishawekwa pale, lakini inasemekana kuna aina fulani ya gesi ambazo zinahitaji ili *zi-operate* vizuri hazipo. Sasa itakuwa si vyema kuweka mashine hizo bila kutumika kwa ukosefu wa gesi tu na ndiyo maana nikasema Mheshimiwa Waziri, atembelee pale ili ajionee mwenyewe.

Askari wetu ambao ni wataalam wanajishughulisha na tiba katika kambi ile wanastaafu lakini hakuna uendelevu (*sustainability training*), kwa ajili ya *ku-cover* ambao watastaafu. Sasa ningeomba sana Wizara iweke programu maalum kwa hospitali ya Bububu na nyingine nasikia iko Tabora, ambazo zimepata msaada kutokana na GTZ, Serikali ya Ujerumani, kuwe na *training* maalum kwa ajili ya kuendeleza hawa wataalam wetu. Anapostaafu mtu mwingine *ana-cover*, kuliko ilivyo sasa hivi, kwa sababu nilivyoona takwimu ya pale Bububu kama atastaafu ina maana kazi hazitakwenda.

Mheshimiwa Spika, lakini suala lingine ni suala zima la hati miliki za maeneo. Pamoja na kwamba, Waziri amesema wana ufinyu wa bajeti na mwaka jana walilazimika kulipia baadhi ya maeneo waliyoyataja, lakini Zanzibar ni visiwa ambavyo eneo lake ni

dogo sana na kama Kambi za Jeshi zitakuwa hazina hati miliki, watu wanavamia maeneo. Watu tunazaliana kwa wingi, lakini pia wanavamia maeneo. Sasa naiomba sana Serikali, kwa Kambi za Zanzibar na Pemba, zipatiwe hati miliki. Kumejitokeza migogoro mgingi sana kwa upande wa Zanzibar, inayopelekea kutokuwa na maelewano na nchi.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie Kambi ya Mwanyanya. mwaka jana au mwaka juzi kama sikosei, kulikuwa na matatizo ambayo baadhi yamekuwa *solved*. Ninaishukuru Serikali, nimeona gari pale linahudumia wanajeshi wetu, lakini bado kuna matatizo ya maji, pamoja na kuwa na hodhi la kukusanya maji, lakini kuna wakati mwingine umeme unakatika maji yanakuwa shida, inabidi sasa yaende kubanana na raia kule. Eneo letu bado lina shida ya maji.

Sasa ningeomba Serikali au Wizara husika, wachimbiwe kisima, maji yanapatikana chini ya mita tatu na *water table* ipo *very high*. Kwa hiyo, shilingi milioni mbili sio pesa nyingi, naomba wachimbiwe kisima pale angalau tatizo hilo litakuwa limepungua. Pia nyumba za kuishi, najua kweli kuna upungufu wa fedha lakini Kambi ya Mwanyanya kuna vikosi viwili pale. Ofisi ni moja ndogo kabisa na ya kizamani, haifanyiwi *maintenance* na nyumba za kulala hakuna. Ningeomba sana Wizara japo hayo maturubai au hizo *full suit ziwekwe* pale.

Mheshimiwa Spika, nizidi kusema tu kwamba, Kambi ya Mwanyanya ni Kambi ambayo imevamiwa na raia. Kwa hiyo, hata lile eneo lake lipo wazi kabisa; mtu akiwa anapika jikoni unamwona kabisa yule pale. Pamoja na kwamba, agizo limetolewa kupanda miti, lakini miti inachukua muda mrefu; kuna haja ya kujenga ukuta japo kidogo kidogo kwa awamu ili kuwahifadhi, vinginevyo ile Kambi itafutiwe eneo. Eneo silioni, kwa maeneo yetu ya Zanzibar kama unavyosema, ardhi haitoshelezi, lakini kuna Kambi nyingi hali kadhalika Mtoni, Welezo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, niungane na wenzangu wanaosema kuna haja sasa hivi ya kujenga Kambi japo za muda katika maeneo ambayo yana matatizo na hao majambazi. Mkoa wa Kagera umetajwa, lakini pia na Wilaya ya Bukombe. Mimi nilikwenda mwaka jana, ikifika saa mbili watu wameshalala, majambazi yanaweza yakaja yakashambulia karibu na Kituo cha Polisi. Polisi watalala kwa sababu wanasiliza mlion wa risasi wanajua hiyo bunduki ya aina fulani sisi hatuna au wanasiliza mlion wa risasi hizo wanajua hiyo ni bunduki ya aina fulani sisi hatuna, watafanya hujuma wataondoka. Sasa kwa Mtanzania inakuwa ndani ya nchi yake ananyanyaswa, sasa kuna shida gani japo ya muda tu kwamba, pajengwe Kambi katika maeneo hayo yenye matatizo; itasaidia sana kwa wananchi wetu na wao watembee kwa kujitanua.

Mheshimiwa Spika, mwaka juzi Kamati ya Miundombinu ilitembelea Wilaya ya Chato, kwenda kuangalia barabara na tuliambiwa kama wiki moja iliyopita yule msimamizi wa barabara gari lao likikuwa limevamiwa na majambazi, likapigwa likatbolewa matundu kama saba au manane ya risasi. Tulikwenda kule roho juu; kuna msitu ukitoka Geita unaelekea Chato, pale ndio kuna eneo la majambazi. Kwa hiyo,

pakiwa na Kambi hizi ndogo za muda mpaka hali itakapokuwa shwari, nafikiri itasaidia sana.

Mheshimiwa Spika, nisingependa kurudia maneno waliyozungumza Waheshimiwa Wabunge, hasa kutoka Zanzibar. Upande wa ajira kwa vijana wetu tunapata shida. Vijana wamemaliza Kidato cha Nne wana sifa zote, lakini waki-*apply* kule majina hayarudi; watapata watu wawili, mmoja au hawapati kabisa. Sasa na sisi tumeahidi kwamba, ajira kwa kila kijana wa Mtanzania, lakini pia tunatoa pesa kwa baadhi yetu tunasomesha vijana, tunatoa pesa kwa ajili ya *tuition* na wanajiedeleza mpaka Kidato cha Nne na anafaulu anaweza akawa na *Division Four* au *Three*. Aki-*apply* nafasi ya Jeshi na Polisi inakuwa ni shida kwa upande wa Zanzibar.

Hilo namwomba sana Mkuu wa Majeshi, asione labda tunanung'unika tu Zanzibar na nini. Zanzibar pia kuna vijana wana uwezo wa kuwa na askari na wana-*qualify* kwa hilo. Kwa hiyo, ni *very serious issue* ambayo inaweza ikaonekana ni kero za Muungano, lakini sio kero. Labda tuseme ni kupuuza tu, sifa zipo sasa kinachokosekana hapa sijui ni nini, *seriousness*? Namwomba sana kwa mara nyingine, Mkuu wa Majeshi, aliangalie na hilo.

Mheshimiwa Spika, kama ninavyosema, sina mengi ya kuchangia lakini *concern* yangu ilikuwa ni hiyo, lakini kwa kuwa muda upo niongeze kidogo kuhusu Shirika la Nyumbu. Mimi nikiwa Shule ya Msingi nilisikia Shirika hili linatengeneza magari, lakini katika hotuba hii inaonyesha kama *improvement* yake ni ndogo sana. Magari yaliyotengenezwa sijui mangapi, lakini *performance* yake ni ndogo kwa sababu mimi nafikiri hawapewi fedha ya kutosha ili kuendeleza ule utafiti wao. Tafiti zao zinataka kuwa nyingi sana; wanatafiti mpaka ujenzi wa nyumba za bei nafuu. Wangejikita kwenye eneo moja na Serikali ikatoa pesa katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia ni vyema sasa Jeshi liwapeleke vijana wetu hawa askari katika Shule kama za DIT, Vyuo Vikuu katika Sekta ya Uhandisi wanapomaliza hiyo ya Nyumbu kama ni *centre* ya majaribio wanaweza waka-*produce* kitu ambacho kitasaidia sana nchi yetu, badala ya kununuliwa magari ya bei kubwa. Kwa hiyo, wataweza kutengeneza magari ya bei nafuu. Nalipongeza sana Shirika la Nyumbu, lakini niongezee uwezo wa fedha isiwe kama Kambi ya watu tu wapo pale, lakini nafikiri iwe ni Kambi yenye watu wenye *profession* zao lakini na fedha wapatiwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante, mniwie radhi nitumie Kanuni ya 28(5), kuongeza muda kidogo ili nimpate mchangiaji mwingine ili nipunguze katika orodha yangu. Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa sijui yupo; ndio mse maji wangu wa mwisho kwa jioni hii. Ahsante sana.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na kwamba, nilikuwa nimekata tamaa lakini Mungu atasaidia.

**SPIKA:** Ndiyo Mungu amekwishesaidia hivyo, sio atasaidia. (*Makofī/Kicheko*)

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nipende tu kuchukua nafasi hii, kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nipate kuzungumza mawili, matatu, kuhusu Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, pamoja na vyombo vyake vyote ambavyo alivitumia kwa maana ya maandalizi mazuri ya hotuba ambayo tumeshaipokea na nianze kwa kuiunga mkono hoja. (*Makofī*)

Mheshimiwa Spika, tunaposema Jeshi la Ulinzi tunazungumzia maisha yetu, unaposema ulinzi ina maana ya kwamba, upo uwoga fulani ambapo unatangaza kisirisiri ili uweze kuendelea kuishi na unatafuta chombo. Kwa hiyo, hiki chombo ndio hawa maaskari ambao nadhani hoja yao leo ipo hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kipindi kilichopita nilikuwa ndani ya Kamati hiyo; Kamati ya Ulinzi na Usalama ilikuwa inaitwa hivyo wakati huo, sasa hivi imeongezewa na Kamati nyine. Ilikuwa ni mara yangu ya kwanza kuwa ndani ya Kamati hiyo.

Niliona mazuri, ukweli niliona mazuri na Serikali yetu inajitahidi kufanya mazuri kwa uwezo wake, lakini tukubali tusikubali kilichonisikitisha kabisa mpaka nikawa nazungumza mwenyewe kirohoroho, nikasema hivi kweli naweza nasahihishwa naambiwa eti ni kimoyomoyo haya. Mimi kama nina mtoto wangu na bahati nzuri nina watoto wa kiume tuseme wote, nina mtoto mmoja tu wa kike.

Nikasema hivi kweli naweza nikamshawishi mwanangu aingie kwenye Jeshi hili; nilipoona nyumba tu, ukweli nilichoka nikasema hapana. Mtoto utamsomesha muda wowote mpaka amalize hiyo *Form Six* tunayozungumza, halafu anakwambia mama mimi nataka kujiunga na Jeshi, unasema sawa nenda mwanangu; sidhani kama atakuja akualike katika maisha yake yote kwamba mama njoo ugenini na mimi leo uje ugeni nyumbani kwangu hawezi. Tuseme tu iliyo kweli, hana mahali pa kukwambia kwamba mama ukija atakulaza mahali, yaani hata wewe mzazi utanza kutafuta hivi ni wapi ninapokwenda?

Mheshimiwa Spika, kifupi nilipoona kwamba, wamejenga nyumba 200 hivi, lakini zikawa na upungufu nimefanya hesabu hapa kama nyumba 28 tu eti na zenyewe tukashindwa kuzimalizia. Hapana, kitu cha kweli hebu tuwfikirie kuwajengea nyumba hawa maaskari jamani. Mpaka anaweka uzio nyumba yake kwa khanga. Wanaweka yale mavirago mle ndani, siwezi hata kueleza inatisha. Wanakaa kwenye magodauni, inatisha ukiingia mle wewe dakika tano au sita tu unatoka jasho; je, anayelala humo na kutafuta watoto humo? (*Makofī*)

Mheshimiwa Spika, niombe jamani Wizara iwafikirie, kama wana hoja ya nyumba hebu tuwajengee nyumba hawa Wanajeshi wetu ili waweze kujisikia na wao kwamba kweli Jeshi tunalijali. Jeshi tunalipenda na kweli wanatulinda, hili ndilo lilikuwa ombi langu la kwanza.

Lingine ni suala la hiki chakula ambapowanapewa posho wakiwa nje. Mimi nilikuwa nanong'ona na jirani yangu hapa, nasema inawezekana nakula kuliko wenyewe. Maana shilingi 3,000 sijui chai anakunywa hela ngapi; shilingi 500, halafu chakula cha mchana shilingi elfu moja sijui na jioni; halafu unamkabidhi bunduki; hivi ni kweli jamani? Hata Mbunge mwenzangu amesema shilingi tano, nasema hata hiyo haitoshi, hebu tukae tuwfikirie jamani. Tukae tukiwa na nia ya kuwajali hawa Wanajeshi wetu kwamba, wanahitaji kula ili wafanye kazi inayostahili maana kazi zao zinahitaji nguvu au bunduki jamani ni kusimama tu basi; anatumia akili ya kulenga, anatumia akili ya kuiweka vizuri begani, anatumia akili nzuri ili hiyo risasi ilindwe; leo unamlisha kwa lelemama si ataruka na hiyo bunduki wataanguka wote huko mbele au wengine humu hamkupita Jeshi la Kujenga Taifa ili baadae ujiunge na Jeshi? Tukubali jamani tutoke, mimi hiyo tano hapana, kama mtanikatalia kumi basi, lakini tuwe katikati ya tano na kumi wapate kupata chakula kinachostahili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu maandalizi yao baada ya kusttafu. Watumishi wengi walianzisha *system* ya kutafuta viwanja kabla hawajastaifu wanatafutiwa maeneo. Niliisikia hiyo sera kwa walimu, nikasikia tena kwenye Wizara fulani; kitu kama hicho. Wanatafuta maeneo ya kukaa kabla hawajastaifu, Wizara mbalimbali zilifanya hivyo. Sasa hawa hata pamoja na kukaa kwenye hayo Makambi, ajabu na kweli leo hata anapostaifu hivi anakuwa ameandaliwa vipi?

Mimi niiombe sasa Wizara, hebu iwafikirie na hilo pia. Mwanza palijitokeza wakati fulani miaka ya nyuma, mimi nikiwa Naibu Meya, ilinihangasha hasa Wanajeshi hawa nao wanahitaji maisha baada ya shughuli za kazi za kutumikia Serikali. Wakawa wanavamia maeneo wanasema na sisi hapa tukitoka kazini baadae nitajenga wapi?

Sasa katika hili, hawa maaskari nao wa aina zote, wanahitaji kupata maeneo baada ya kusttafu kwao; je, Wizara inazungumzia nini maana yake miji inaendelea kupanuka? Tuwfikirie na wao na tuwaingizie hoja ili wawe na wazo la kuomba viwanja. Inawezekana basi wao wenyewe wakishawekwa Kambini na mtu akishawekwa Kambini, Mheshimiwa mmoja amesema hata ile kuzungumza hawesi, mimi sijauonja huo uaskari wa hivyo. Lakini aandaliwe basi ujumbe ufile, wapewe wazo la kuwa wajiandae na kupata viwanja ili baada ya kusttafu kwao, wakipata mafao wajue pa kuyapeleka, wasiende kutangatanga. Ndiyo maana wanakwenda kwanza kuendeleza maisha pengine halafu wanarudi; wakirudi ndio wanakuja kutafuta waweze kujenga. Nilikuwa ninashauri hivyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, hawa watoto wetu wa Kujenga Taifa, humu nikiwaliza wangapi mmepitia huko hakuna hata mmoja.

**WABUNGE FULANI:** Tumo sote.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Sote; mkiombwa vyeti mtaleta? Nikiuliza humu wewe ulikuwa Jeshi la Kujenga Taifa operesheni gani hapa mtasema?

**WABUNGE FULANI:** Ndio.

**SPIKA:** Mheshimiwa ongea na Spika.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Naongea na wewe Mheshimiwa Spika, naogopa hata wewe kukuuliza. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Kujenga Taifa lilikuwa linajenga kweli, yaani ni kujenga hasa. Kuna Naibu Waziri wa kipindi kilichopita, aliniambia Mama Hewa mbona unanenepa, tukupeleke Jeshi la Kujenga Taifa.

Nikamwambia ninao uzoefu wewe ulienda, nikasema ndiyo maana nakwambia, lakini basi nikanyamaza, lakini kule ndiko kweli kuna mwanzo wa kuwekwa *u-fit* na uzalendo. Huko hakuna mtu wa kusema huyu hapa ni Waziri, huyu ni nani; wote ni sawa. Naomba siku moja labda tujaribu hata mara moja tu kwa wiki mtakubali?

Sasa katika hili maana yangu ni nini? Linaleta ukakamavu wa aina fulani wa kuipenda nchi yako na kuweza kujua nchi yako unatakiwa ufanye nini. Kuna maeneo kule unajifunza uzalishaji, kuna ufundi kule mwili wako unakuwa *fit* na nini, yaani unajisikia kweli niko Tanzania na Tanzania ina raha zake.

Sasa katika hili, niombe kama kweli tunakubali kurejesha Jeshi la Kujenga Taifa, nafahamu lipo lakini lisisimama, baadae likarudi. Sasa turudishe ile heshima ya mwanzo, tusiwapeleke hawa vijana, turudi tena tukaone jinsi gani kama kweli Kambi hizo ndizo zilivyokuwa hapo mwanzo.

Mimi wakati fulani nilikwenda kutembelea na penyewe nimekuta yaani unasema hivi humu kesho kutakucha; nyumba zimepasuka, naomba na wao tuwajali katika hili. Makambi hayo yaimarishwe, turudishe ile heshima na kazi tulivyokuwa tukiifanya na nidhamu iliyokuweko.

Labda ndiyo maana wakati mwingine tunapotoka kinidhamu kwa sababu tumeacha maadili yetu ambayo tulifundwa kutoka Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, basi niendelee kuunga mkono hoja na niwapongeze Mawaziri hawa, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Tuwape matumaini Wanajeshi wetu kwamba, Bunge hili lipo sambamba nao, likiongozwa na Spika mwenye viwango.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Maria Hewa. Waheshimiwa Wabunge, muda nilioongeza umekuwa kama kiasi cha dakika tano, lakini ni kwa sababu nzuri tu; wanapoomba kuchangia Waheshimiwa Wabunge, halafu orodha tunaifupisha mno, huwa inaleta kidogo manung'uniko. Ni kwa sababu hiyo hiyo basi, kesho nitawapatia nafasi Wabunge watatu kati ya wafuatao; Mheshimiwa Castor Raphael Ligallama, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir na kama kutakuwa na muda, basi Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, kutegemea na muda utakavyokuwa na urefu wa matangazo. Hiyo itatufikisha kwenye saa 5.00 asubuhi, basi kwa namna yoyote, Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi atakavyokuwa amepanga, yeye na Naibu wake, watakuwa na dakika 75; itatufikisha saa 6.15.

Kwa maana hiyo basi, Kamati ambayo sidhani kama ina magumu sana, kwa sababu mlionchangia wote mnalitakia Jeshi letu mambo mazuri. Kwa hiyo, hakuna ubishi sana, nimetoa dakika 45 kwa Kamati ya Matumizi tufikie saa 7.00 kesho tukijaliwa.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaahirisha Shughuli za Bunge kwa leo, ningependa mtambue kwamba, tumetawanya ratiba hapa ya mpangilio wa shughuli zetu kwa kipindi kinachotukabili cha wiki takriban mbili. Lakini ya umuhimu ni kwamba, Alhamisi tarehe 21; Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, atakuja Bungeni humu kutuhutubia. Kwa hiyo, naomba mzingatie hilo katika safari zenu ili aukute Ukumbi katika hali ambayo wawakilishi wote tumetulia katika viti vyetu. Muda hasa tumeponga kwa sasa ni mara baada ya kipindi cha maswali, lakini huwezi kujua. Kwa hiyo, tutaendelea kuwathibitishia hiyo ni Alhamisi tarehe 21. Jumatatu tarehe 25 Agosti, 2008, Rais wa Comoro atakuja kulihutubia Bunge, siku hiyo nayo tunapanga ni mara baada ya maswali, huo ndio wakati mzuri; tunapata kama saa moja hivi ya Rais kuweza kuingia hapa na kuweza kutuhutubia. Niliomba haya myaweke katika ratiba zenu na hasa Wenyeviti wa Kamati, msichague nyakati hizi tena au tarehe hizi kuwa na vikao, tutakuwa tumeponga tena kwa hiyo tuwepo.

Baada ya kusema hayo, tutaendelea kesho. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge mlionchangia leo. Michango mizuri sana, inaonyesha uzalendo wa kulipenda Jeshi letu. Nawashukuru sana na sasa naahirisha Bunge hili hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.54 Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumanne,  
Tarehe 19 Agosti, 2008 Saa Tatu Asubuhi)*